

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 20 Aprili, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae. Katibu!

NDG. ATHUMAN HUSSEIN – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:-

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

NAIBU SPIKA: Katibu!

NDG. ATHUMAN HUSSEIN – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Maswali Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Deo Ngalawa, sasa aulize swali lake

Na. 109

**Wastaafu wa Shirika la Posta na Simu la Iliyokuwa
Jumuiya ya Afrika Mashariki**

MHE. DEO F. NGALAWA aliuliza:-

Serikali iliamua pamoja na mambo mengine ya kulinusuru Shirika la Posta kuhakikisha jukumu la kulipa pensheni za wastaafu liliokwuwa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki kwenye mojawapo ya Mifuko ya Pensheni:-

Je, Serikali itakuwa tayari kuhamisha jukumu hili kwenye mojawapo ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deo Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na jukumu la kuwalipa pensheni ya kila mwezi wastaafu wa liliokwuwa Shirika la Posta na Simu la Iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa sasa wastaafu hao wanalipwa pensheni ya kila mwezi na Shirika la Posta na kwamba Serikali hurejesha fedha hizo baada ya shirika kuwasilisha madai yake hazina kupitia kwa Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali haiwezi kuhamisha jukumu la kulipa pensheni wastaafu wa Shirika la Posta na Simu wa Iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki

kwenda kwenye mojawapo ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa kuwa zoezi la kuunganisha Mifuko ya Pensheni halijakamilika. Ni rai ya Serikali kwamba, uamuzi wa kuhamisha au kuendelea kwa sasa utaratibu wa sasa utatolewa baada ya zoezi la kuunganisha Mifuko ya Pensheni kukamilika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Deo Ngalawa, swali la nyongeza.

MHE. DEO F. NGALAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, Shirika hili la Posta na Simu limekuwa likijiendesha kwa kusuasua sana na moja kati ya mambo ambayo yanaifanya shirika hili lisuesue ni hela za pensheni inayolipa wale waliokuwa wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Je, Serikali haloni sasa umeshafika wakati kulitua mzigo shirika hili ili iweze kulichukua hilo jukumu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, malipo ya pensheni kwa hawa wafanyakazi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki inalipwa kama kawaida, lakini kuna mabadiliko ambayo yalifanya Julai, 2015 kupanda kwa pensheni kutoka Sh.50,000 kwenda Sh.100,000, lakini kuna baadhi ya hao wastaifu hawajabadilishiwa hizo pensheni zao, mfano, Mr Mbalamwezi. Je, ni lini Serikali itawabadilishia pensheni hizo ili ziwe sawa na wenzao? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali yetu inafanya jitihada zote na kwa sasa tunapoongea na namshukuru Mheshimiwa Mbunge amekiri kwamba kwa sasa wastaifu hao wanalipwa inavyotakiwa na pale tu wanapokuwa wameshalipwa na Shirika la Posta, Shirika la Posta linapowasilisha madai hayo Hazina walikuwa wakiliipwa na hakuna madai mengine yoyote ambayo yamebaki. Kwa

hiyo, tupo *current* kila mwezi wanapokuwa wamelipa wanaleta madai na Hazina imekuwa ikifanya malipo hayo kwa Shirika letu la Posta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyo sema kwenye jibu langu la msingi kwamba kwa sasa tusubiri mfumo huu wa kiutaratibu wa kuunganisha Mifuko utakapokamilika *then* Serikali itafanya maamuzi ya aidha, wastaafu hawa wahamishiwe kwenye moja ya Mifuko hii au wahamishiwe hazina moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, kwamba ni lini watalipwa, nimekuwa nikilarifu Bunge lako Tukufu hapa kwamba Mifuko yetu yote ilishaanza kulipa ongezeko lile la pensheni na wastaafu waliobaki kama alivyotaja ni mmoja mmoja na tumekuwa tukishughulika na kila kesi ya mstaafu anapokuja, kila mstaafu ana mambo yake tofauti ambayo yamesababisha kwa nini wasiongezewe pensheni hii na sisi tumekuwa tukishughulika nao. Kwa huyu aliyemtaja kama kweli hajaanza kulipwa tunamwomba afike Hazina na hili tutaweza kulishughulikia. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Pauline Gekul, swali la nyongeza.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Waziri kwa muda mrefu wafanyakazi wamekuwa hawapandishwi madaraja yao kwa kigezo cha uhakiki wa vyeti feki, jambo ambalo linakwenda kuathiri pensheni zao. Naomba nipate kauli ya Serikali kwa nini hawamalizi zoezi hili ili wafanyakazi hususan Walimu wawzeze kupandishwa madaraja na pensheni zao zisiende kuathirika baadaye?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri swali hili ni jipya wala halihusiani

na swali la msingi ambalo nimelijibu. Hili ni suala la kiutumishi na naamini Waziri wa Utumishi wakati alipowasilisha bajeti yake hapa alilisema hili suala vizuri kabisa nini kimefanyika, uhakiki ulishakamilika, zipo kasoro zillizonekana ndio maana wanamalizia uhakiki huu na ni imani yangu watakamilisha muda sio mrefu, lakini siamini kwamba imekuwa ikizuia watumishi kupanda madaraja yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema Mheshimiwa Waziri wa Utumishi atalitolea ufanuzi mzuri na alishalisemea, kwa hiyo nimwombe kwa kauli ya Serikali sitoweza kuitoa hapa kwa sababu swali hili ni jipya.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelelea na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 110

Kufungua Benki ya Kilimo Ruvuma

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI aliuliza:-

Benki ya Kilimo ipo kwa ajii ya kumwezesha mkulima wa Tanzania aweze kufanya uwekezaji wenye tija katika kilimo:-

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka Benki ya Kilimo katika Mkoa wa Ruvuma ili wananchi wawewe kukopeshwa?

(b) Je, Serikali ipo tayari kupunguza riba kwa pesa anayokopeshwa mkulima kutoka benki hiyo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mpango Kazi wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania wa miaka mitano (2017 – 2021), benki inakusudia kuanzisha Ofisi za kikanda katika Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Kusini, Kanda ya Kati, Kanda ya Ziwa, Nyanda za Juu Kusini pamoja na Zanzibar. Kutokana na ufinyu wa rasilimali fedha, benki itatekeleza mpango wake wa kusogeza huduma karibu na wateja wa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia 30 Juni, 2018, Ofisi ya Kanda ya Kati itakuwa imefunguliwa ambayo pia itakuwa ni Makao Makuu ya Benki ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ufunguzi wa Ofisi ya Kanda ya Kati kukamilika, benki itafanya uchambuzi wa fursa zilizopo kikanda na hivyo kuchukua hatua na taratibu za kufungua Ofisi nyingine kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania inatoa mikopo kwa kutumia mfumo wa makundi:-

(i) Kundi la kwanza ni wakulima wadogo wadogo kwa riba ya 8% – 12% kwa mwaka;

(ii) Kundi la pili ni la miradi mikubwa ya kilimo kwa 12% – 16% kwa mwaka;

(iii) Kundi la tatu ni wanunuzi wa mazao kwa 15% – 18%;na

(iv) Kundi la mwisho ni mikopo ya ushirika ambapo riba yake inaendana na hali ya soko na matumizi ya mkopo huo. Hata hivyo, majadiliano kuhusu kiwango cha riba yanaweza kufanyika kulingana na historia ya mkopaji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, swalii la nyongeza.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Fedha, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa Mkoa wa Ruvuma ni mionganini wa mikoa ambayo ni *food basket* nchini Tanzania, je, Serikali inachukua hatua gani za makusudi za kuweka benki hii kila mkoa badala ya kuweka benki hii kikanda? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ili kuboresha uchumi wa viwanda tunaoutarajia ambao kimsingi malighafi zinatokana na kilimo asilimia 75. Je, Serikali ipo tayari kuongeza ruzuku ya mbolea ili mbolea iuzwe Sh.10,000 kwa kila mfuko wa kilo 50 badala ya mfuko ambao unauzwa sasa Sh.60,000 mpaka Sh.65,000? (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi ili niweze kufafanua swali la Mheshimiwa Mbunge, Jacqueline Msongozi wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Ruvuma, hususan katika kile kipengele chake cha (b) kuhusu ruzuku katika suala zima la mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara ya Kilimo, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wangu siku chache zilizopita ni kwamba tupo katika mkakati na mpango maalum katika Bunge hili la bajeti kuhakikisha kwamba ule mfumo wa ununuzi wa mbolea ya pamoja, tutawaletea semina Waheshimiwa Wabunge wote ili waweze kujua nini maana ya bei elekezi ya mbolea ili waweze kuwa na uelewa mpana nini maana ya kutoka kule kwenye ruzuku na sasa hivi tupo katika mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja. Nakushukuru. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Suzan Kiwanga, swali la nyongeza.

MHE. SUZAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa Naibu Waziri wa Fedha amesema

kwamba wana mpango wa kufungua Benki ya Kilimo kwenye ngazi ya kanda na kwa kuwa Mkoa wa Morogoro hususan Wilaya ya Kilombero hasa Jimbo la Mlimba sasa hivi tupo kwenye ujenzi kwa kutumia mkopo katika Halmashauri yetu tunajenga Benki ya *NMB* Mlimba. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kupeleka dirisha katika mabenki haya ya *NMB* na *CRDB* kwa ajili ya kusogeza huduma kwa wananchi wakulima ambao wanateseka sana katika kupata pesa za kuendeleza kilimo chao badala ya kusubiri mpaka Benki ya Kilimo ikawa Kanda ya Kati?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kufungua matawi haya kikanda ni kuwasogezea wakulima huduma kule walipo na hiyo kama nilliyosema lko kwenye mpango mkakati wa Benki ya Kilimo. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba *tuu-support* mpango huu ili benki yetu iweze kuwasogelea wakulima wetu kule walipo katika kanda zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la kufungua dirisha katika mabenki mengine ya kibiashara ni wazo jipya, kama Serikali tunalichukua tuone kama linawenza kufanyiwa kazi na tuweze kuli-*implement*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipayende kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika benki ambazo huwafuata wakulima kule walipo ni Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania. Kwa hiyo, popote pale wakulima walipo wanapokuwa wametuma maombi kwa ajili ya mkopo, Benki ya Kilimo huwatembelea wakulima hawa kule walipo. Kwa hiyo, tuendelee kuipa *support* Benki ya Maendeleo ya Kilimo iweze kuendelea kuwafikia wakulima wetu kwa ajili ya kuwashudumia. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa tunaendele na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi,

Mheshimiwa Twahir Awesu Mohamed, Mbunge wa Mkoani,
sasa aulize swali lake.

Na. 111

Usalama wa Raia na Mali Zao

MHE. TWAHIR AWESU MOHAMED aliuliza:-

Jeshi la Polisi lina dhamana kubwa ya kulinda usalama
wa raia na mali zao na ni msimamizi mkuu katika haki za
binadamu:-

(a) Je, ni lini Jeshi hilo litafanya kazi zake kisayansi zaidi
na kuondokana na kutumia nguvu zisizo za lazima wakati wa
kutekeleza majukumu yake?

(b) Je, suala la weledi kwa watendaji wa polisi
linasimamiwa vipi ili polisi waweze kupambana na uhalifu
unaokua kitalaam kila siku?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa
Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la
Mheshimiwa Twahir Awesu Mohamed, Mbunge wa Mkoani
lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi ni chombo
kilichoanzishwa kwa mujibu wa Katiba kusimamia usalama
wa raia na mali zao na katika utendaji wake linaongozwa
na sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali. Aidha,
Jeshi la Polisi limejiwekea kanuni za kudumu (*PGO*) ambazo
zimetafsiri na kutoa mwongozo wa utekelezaji wa sheria zote
zinazoongoza utendaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa kazi
zake askari anaruhusiwa kutumia nguvu inayoendana na
mazingira ya tukio. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai
kifungu namba 11(2) kinamruhusu askari kutumia nguvu katika

ukamataji iwapo mkamatwaji atakaidi. Pia *PGO* 274 inaeleza mazingira ya matumizi ya nguvu na aina ya nguvu inayopaswa kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiwajengea uwezo wa kiutendaji askari kwa kutoa mafunzo mbalimbali sehemu za kazi yenye lengo la kuwakumbusha taratibu za kazi, pia limekuwa likitoa mafunzo ya weledi ya ndani na nje ya nchi ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha linafanya kazi zake kwa weledi Jeshi la Polisi limekuwa likiajiri wasomi wenyewe taaluma mbalimbali kama vile TEHAMA, maabara, uchunguzi wa nyaraka na taaluma zingine zinazohusiana na makosa yanayosababishwa na ukuaji wa teknolojia.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Twahir Awesu Mohamed, swali la nyongeza.

MHE. TWAHIR AWESU MOHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, imekuwa ni kawaida sasa katika nchi yetu watu kutekwa, kupigwa, kuumizwa na hata kuuliwa. Kumekuwa na dhana kwamba Jeshi la Polisi linafahamu fika tendo hili, lakini wamelinyamazia. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anataka kuwaambia nini Watanzania ili isije ikafika hatua wakajichukulia sheria mikononi mwao? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kumekuwa na katazo la kufanya mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa. Siku ya tarehe 8 Aprili, 2018, CCM mikoa miwili ya Pemba waliandamana chini ya ulinzi mkali wa Jeshi la Polisi wakiwa wamebeba mabango wakiimba nyimbo za kuhatarisha amani, za uchochezi. Mheshimiwa Naibu Waziri nataka aniambie, hili katazo linahusu Vyama vya Siasa vya Upinzani pekee au ni kwa vyama vyote vya siasa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sikubaliani na maoni ya Mheshimiwa Mbunge maana maoni yoyote yanahitaji yathibitishwe, yahalalishwe, yalinganishwe. Kwa takwimu ambazo ninazo zinaonesha hali ya uhalifu nchini inaendelea kupungua. Sasa anaponiambia kwamba sasa hivi kuna ongezeko la mambo ya uhalifu, akataja mengi tu, ninachoweza kusema ni kwamba tuna Jeshi la Polisi kwa sababu ya hulka ya baadhi ya binadamu kufanya au kufikiria kufanya uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi zote majeshi ya polisi au vyombo vy'a dola vipo kuzuia himo hali, kwa hiyo hatuwezi kusema kwamba kuna Taifa duniani ambalo litakuwa halina *element* yoyote ya uhalifu. Ninachoweza kumhakikishia ni kwamba Jeshi la Polisi linafanya kazi yake nzuri na ndiyo maana hali ya uhalifu imepungua nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusiana na wananchi, kwamba wachukue sheria mkononi, naomba tu nimsisitize Mheshimiwa Mbunge kwa wananchi wake na wananchi wengine ambao wanansikiliza hapa kwamba tunaendelea kusisitiza kwamba wausijaribu kuchukua sheria mkononi. Mamlaka za dola zipo kwa ajili yao na pale ambapo wanaona kwamba kuna tatizo lolote la uhalifu basi wawasilishe malalamiko yao katika vyombo husika na sheria itachukua mkondo wake. Kitendo cha kuchukua mkononi hakihalalishi aliyechukua sheria mkononi asichukuliwe hatua na yeye za kisheria pindi atakapokuwa amevunja sheria, hata kama atakuwa ametendewa kosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ametoa mfano wa tarehe fulani ambayo CCM waliandamana, bahati mbaya sina taarifa himo, lakini ninachoweza kusema ni kwamba suala la kuandamana, suala la kufanya mikutano na kadhalika linapotokezea ni lazima Jeshi la Polisi litoe ulinzi ili shughuli ile kama ni maandamano au mikutano, kama

umeruhusiwa lakini kwa mujibu wa sheria na taratibu zimefautwa, lazima Jeshi la Polisi liwepo kutoa ulinzi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sisi tunachowenza kusema ni kwamba kipindi hiki ambapo Serikali yetu ya Awamu ya Tano ina shughuli nyingi za mafanikio makubwa kiuchumi na ninyi mnaona, ni mashahidi, kwamba Taifa letu linaendelea kupiga hatua kwa kasi kabisa na uchumi wetu unainuka na kero nyingi zimetatuliwa, Jeshi la Polisi lina jukumu la kuhakikisha nchi inaendelea kuwa salama. Hatuwezi kuendekeza kutoa ulinzi kwa maandamano, mikutano, hatuna askari wa kutosha kuweza kufanya shughuli hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana tunasema kwamba kwa taasisi yoyote au chombo chochote ambacho kitahitaji kufanya maandamano na mikutano isiyokuwa na tija, Jeshi la Polisi halina muda huo, lina muda wa kulinda maisha ya wananchi na usalama wao katika kipindi hiki ambapo Serikali yetu inapiga hatua kubwa ya maendeleo. Kwa hiyo, hii si kwa chama chochote, si kwa mtu ye yoyote haibagui mtu, ni sheria msumeno inakata pande zote mbili. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalı lake.

Na. 112

Kushuka kwa Uzalishaji wa Pamba – Mwanza

MHE. KITETO Z. KOSHUMA aliuliza:-

Uzalishaji wa pamba Mkoani Mwanza umepungua kutoka tani 350,000 kwa mwaka 2009 hadi tani 120,000 kwa mwaka 2016:-

Je, Serikali inachukua hatua gani za makusudi ili kulifufua zao hilo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa pamba umekuwa ukishuka katika miaka ya hivi karibuni, sio kwa Mkoa wa Mwanza tu, bali pia katika maeneo yote yanayozalisha pamba nchini. Miongoni mwa sababu ambazo zilichangia kushuka kwa uzalishaji ni bei ndogo ya pamba kwa wakulima, kukosekana kwa mfumo bora wa usimamizi wa ununuzi wa pamba ambao ulisababisha baadhi ya wakulima kukopwa, matumizi madogo ya pembejeo hususan viuadudu, mbegu bora na mbolea. Aidha, kutozingatiwa kwa kanuni bora za kilimo cha pamba na matumizi madogo ya zana bora za kilimo vimeathiri uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekusudia kuinua kilimo cha zao la pamba kwa kuimarisha usimamizi kuanzia ngazi ya kijiji hadi ngazi ya kitaifa. Katika usimamizi huo, mkazo umewekwa katika upatikanaji wa taarifa na takwimu sahihi za wakulima, eneo wanadolima, kiasi cha pembejeo hususan viuadudu, mbegu bora na mbolea. Aidha, Serikali inasimamia kikamilifu vyama vya msingi ili viwe imara na pale ambapo havipo vianzishwe ili huduma za pembejeo na masoko zipatikane kupitia vyama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uhamasishaji na usimamizi imara, msimu wa 2017/2018, uzalishaji wa pamba unategemewa kuwa zaidi ya tani 600,000. Hii ni kutokana na wakulima kuhamasika na Serikali kupeleka pembejeo hususan viuadudu ambapo chupa milioni 7.3 zenye thamani ya shilingi bilioni 29.2 zimenunuliwa na kupelekwa kwa wakulima ikilinganishwa na chupa 700,000 katika msimu uliopita. Aidha, vinyunyizi 16,500 vyenye thamani ya shilingi milioni 495 vimenunuliwa. Pia vinyunyizi vibovu 6,000 vilivyokuwa kwa wakulima vimekarabatiwa bila malipo pamoja na wakulima kufundishwa namna ya kupulizia viuadudu hivyo ili kudhibiti visumbufu vya zao hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa muda wa kati na mrefu kuongeza uzalishaji wa pamba kutoka tani 121,639 mwaka 2016/2017 hadi kufikia tani milioni moja ifikapo mwaka 2020. Lengo hilo litafikiwa kwa kuongeza matumizi ya mbegu bora ambapo katika msimu wa 2018/2019, bodi itazalisha tani 40,000 za mbegu aina ya UKM08 ambayo ni zaidi ya mahitaji ya tani 25,000 kwa mwaka. Mbegu mpya aina ya UKM08 ina sifa za kipekee ikiwemo tija kubwa ya uzalishaji ikilinganishwa na mbegu ya zamani aina ya UK91.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati mwingine ni kuongeza uzalishaji wa mbegu mpya aina mbili zilizothibitishwa kwa ajili ya kuzipeleka kwa wakulima na kutenga maeneo maalum ya kuzalisha mbegu bora. Aidha, maeneo yaliyoainishwa na Serikali kupitia Bodi ya Pamba katika kutekeleza mpango wa uzalishaji wa mbegu bora aina ya UKM08 ni Wilaya za Igunga, Uyui, Urambo, Nzega na Meatu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma, swali la nyongeza.

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini wakulima wa pamba katika mikoa ambayo inahusika kulima pamba kama vile Mikoa ya Shinyanga, Simiyu na kwingineko bado ni wakulima wadogowadogo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wakulima hawa wanakuwa wakulima wakubwa ili kuleta tija katika zao hili la pamba ambalo ni zao la kibiaresha linalotegemewa hapa nchini Tanzania ili kuongeza Pato la Taifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu alifika Mkoa wa Mwanza na kufanya kikao na wadau wa pamba na kuwaahidi kwamba atarudi tena mwezi Mei ili kuweza kupanga bei ya pamba kwa msimu huu ambaeo unakuja; naomba kuiuliza Wizara, je, ni kwa nini isione kwamba waweze kupandisha bei ya pamba kutoka Sh.1,200 kwa msimu uliopita hadi Sh.2,000 kwa msimu ambaeo

unakuja kwa sababu zao hili la pamba ndiyo dhahabu ya Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Simiyu na mikoa mingineyo? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge, mdogo wangu Mheshimiwa Kiteto Koshuma kwa maswali yake mawili mazuri ya nyongeza na vilevile kwa jinsi ambavyo anaafuatilia zao hili la kimkakati Tanzania, zao la pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na swali lake la kwanza; ni kweli kwamba uzalishaji wa pamba ulikuwa ukishuka na kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, Serikali tumejipanga kwamba sasa hivi tutakuwa na mfumo bora wa uzalishaji wa zao la pamba kwa maana ya uzalishaji wa mbegu ile niliyoisema kwenye jibu langu la msingi, UKM08 na vilevile tuweze kuzalisha pamba zaidi kwa kuzingatia kwamba kitakuwa ni kilimo chakisasa na ni mfumo bora wa mbegu hii ambayo tumeianzisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye swali lake la pili, naomba niseme kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu amekuwa ni *champion* kabisa katika zao hili la pamba na mpaka sasa hivi ameshafanya mikutano na wadau mbalimbali kuhusu zao la pamba; mikutano zaidi ya sitana leo hii pia tunakutana na wadau wengine wa pamba, jana pia Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya tena mkutano mwingine na *ginners* wote wa pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie mdogo wangu, Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali tumejipanga safari hii kuhakikisha kabisa kwamba zao la pamba litakuwa pia ni zao bora na litaendelea katika uzalishaji, ukizingatia tumeshaanzisha hii mbegu nyingine mpya niliyoisema ya UKM08.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tarehe 26, mwezi huu wa Nne, wadau wote wa pamba tutakusanyika kwa ajili ya kuangalia *indicative price* ya zao la pamba itakuwa ni shilingi ngapi. Kwa maana hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge mwezi huu kabla ya mwisho wa mwezi tutakuwa tumeshajua bei ya zao la pamba itakuwa ni shilingi ngapi.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi, sasa aulize swali lake.

Na. 113

Umuhimu wa Kupima Ardhi Yote Nchini

MHE. QAMBALO W. QULWI aliuliza:-

Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kuwa ardhi yote ya Tanzania inapangwa, inapimwa na kumilikishwa kisheria kama namna mojawapo ya kuondoa migogoro hususan ya wakulima na wafugaji nchini?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI aliijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kupanga na kupima ardhi yote nchini kama namna mojawapo ya kupunguza migogoro baina ya watumiaji wa ardhi, hususan wakulima na wafugaji na watumiaji wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Na. 6 ya Mwaka 2007, uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ni jukumu la mamlaka ya upangaji ambazo ni halmashauri za wilaya na viji. Aidha, kifungu cha 7(1) cha Sheria ya Mipangomiji Na. 8 ya Mwaka 2007 kinaelekeza kuwa jukumu la upangaji na uendelezaji

miji lipo chini ya mamlaka za upangaji ambazo ni Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji, Wilaya na Mamlaka za Miji Midogo. Wizara yangu imekuwa ikizhamasisha na kuzijengea uwezo mamlaka za upangaji katika kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi na kuandaa mipango kabambe ambayo ndiyo dira ya kuongoza uendelezaji wa ardhi katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeweka mikakati mbalimbali ya kuhakikisha kuwa ardhi yote ya Tanzania inapangwa, inapimwa na kumilikishwa kisheria. Mikakati hiyo ni pamoja na kuandaa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha kila Kipande cha Ardhi Nchini ambayo itahusisha halmashauri zote nchini; kusajili makampuni binafsi ya kupanga na kupima ardhi yenye weledi wa kufanya kazi hizo kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo na kununua vifaa vya kisasa vya upimaji vitakavyosambazwa kwenye kanda nane za usimamizi wa ardhi kwa lengo la kuharakisha upimaji wa ardhi katika wilaya mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la upimaji wa ardhi ni endelevu, natoa rai kwa halmashauri zote nchini kutenga fedha za kutosha katika bajeti zao kila mwaka kwa ajili ya kurahisisha na kuharakisha zoezi la kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi na mipango kabambe na hivyo kuwezesha kukamilika kwa azma ya kupanga, kupima na kumilikisha kila kipande cha ardhi nchini kwa wakati.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Qambalo Qulwi, swali la nyongeza.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Niulize maswali mawili madogo ya nyongeza; kama ambavyo Serikali imekiri katika majibu yake juu ya umuhimu wa zoezi hili la kupanga, kupima na hatimaye kumilikisha ardhi kisheria, lakini nakumbuka katika hotuba ya Waziri ya mwaka 2016/2017 aliliambia Bunge hili kwamba ni 15% tu ya ardhi ya nchi hii ndiyo imefanyiwa upangaji, upimaji na umilikishaji na nydingi ya hizo utazikuta ziko maeneo ya mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuliachia zoezi hili muhimu sana kama ambavyo Serikali imekiri kwa halmashauri zetu za wilaya na vijiji ni zoezi ambalo lina gharama kubwa na halmashauri nyingi hazitaweza kabisa. Je, kama Serikali inatambua umuhimu wa zoezi hili, kwa nini Serikali Kuu sasa isiingilie katи ikazisaidia mamlaka hizo za wilaya na vijiji kuhakikisha ardhi yote ya nchi hii inapimwa, inapangwa na pia kumilikishwa kisheria? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya Mwaka 1999 kifungu cha saba (7) kinamtaka Kamishna wa Ardhi kutoa cheti cha ardhi ya kijiji kwa vile vijiji ambavyo mipaka yake imetambulika na imekubalika lakini viko vijiji ambavyo vina sifa hiyo na havijapata hati hiyo. Nini kauli ya Serikali kwa Makamishna na Maafisa wa Ardhi wa Wilaya ili vijiji vipate hati hiyo muhimu sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali Kuu imekuwa inasaidia zoezi la upangaji, upimaji na hata kuanda matumizi bora ya ardhi katika vijiji na *master plan*. Hata hivyo, kimsingi kwa mujibu wa sheria, zoezi hili lazima lisimamiwe na ni jukumu la halmashauri husika na vijiji. Ni kweli, kazi ya vijiji kupanga matumizi bora ya ardhi unaweza ukasema ni gharama, lakini viko vijiji ambavyo vimesimamia na vimepanga matumizi bora ya ardhi katika vijiji vyao na maisha yanaendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za upangaji wa matumizi bora katika kijiji kimoja haizidi shilingi milioni 22. Sasa kama wananchi wote wataona ni busara kutoa shilingi milioni 22 ili kila mmoja mwananchi wa kijiji kile awe na uhakika wa ardhi yake, wafanye hivyo, kwa sababu si gharama kwa sababu unapanga na kupima mara moja katika maisha yenu yote. Kwa hiyo, bado nahamasisha kwamba pamoja na

Serikali Kuu kuendelea kusaidia, lakini jukumu hili lazima liwe ni jukumu la msingi, kwa mujibu wa sheria, la mamlaka za vijiji na wilaya husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa, kama nilivyosema, Serikali inaandaa mpango wa jumla wa kupanga na kupima nchi nzima. Mpango huu tutaueleza vizuri kwenye *budget speech* nitakayosoma mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, ni kweli kwamba ni jukumu la Kamishna kutoa cheti cha vijiji. Sasa kama ana taarifa juu ya vijiji ambavyo anahitaji na ambavyo havina vyeti nya vijiji, tuwasiliane ili tujue kwa nini imetokea hivyo tuweze kurekebisha tuwapatie hivyo vyeti.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mbunge wa Itilima sasa aulize swali lake.

Na. 114

Shirika la Nyumba Kujenga Nyumba – Mkoa wa Simiyu

MHE. NJALU D. SILANGA aliuliza:-

Shirika la Nyumba lilianzishwa kwa ajili ya kusaidia watumishi wa umma pamoja na wananchi wenyewe maisha ya chini na Mkoa wa Simiyu ni mpya ambapo tayari kuna watumishi wengi ambao hawana nyumba za kuishi ikiwemo Wilaya za Itilima na Busega:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba katika Mkoa mpya wa Simiyu pamoja na wilaya zake kwa kutumia Shirika la Nyumba?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mbunge wa Itilima, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Taifa lilipokea maombi ya ujenzi wa nyumba kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Itilima mwaka 2014. Baada ya kupokea maombi hayo shirika liliendelea na hatua nyingine za maandalizi ikiwa ni pamoja na kuandaa mpango wa kina wa matumizi ya ardhi, kuandaa michoro ya nyumba na kukadiria gharama za nyumba husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika liliingia makubaliano na Halmashauri ya Wilaya ya Itilima ya kujenga jumla ya nyumba 14 tarehe 2 Julai, 2005. Kati ya nyumba hizo 13 za Wakuu wa Idara na moja ni ya Mkurugenzi wa halmashauri. Utekelezaji mradi huu ulipangwa kuanza mara moja baada ya halmashauri kulipa kiasi cha shilingi bilioni 400 ikiwa ni awamu ya kwanza ya malipo ya nyumba husika. Hata hivyo, Halmashauri ya Itilima haijafanya malipo hayo hadi sasa na hivyo kuchelewesha kuanza kwa mrai huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzipongeza Halmashauri za Momba, Busekelo, Mlele, Mvomero, Monduli, Uyui, Kongwa na Geita na nyingine kwa ushirikiano ambao umewezesha watumishi wao kujengewa nyumba na Shirika la Nyumba la Taifa. Natoa wito kwa halmashauri zote uhitaji wa nyumba kuwasilisha maombi ya kujengewa nyumba na Shirika la Nyumba ili maombi hayo yaweze kufanyiwa kazi na kuwapatia makadirio ya gharama za ujenzi ili kazi hiyo iweze kufanywa na Shirika la Nyumba.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Njalu Silanga, swali la nyongeza.

MHE. NJALU D. SILANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ni kweli kulingana na uchache Halmashauri ya Wilaya ya Itilima haukuweza kupata shilingi milioni 400 kwa wakati. Tuliweza kujenga nyumba nne kwa kutumia utaratibu kwa kutumia mikataba ya halmashauri na Naibu Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Kandege alikuja kufungua hizo nyumba. Je Waziri atakubaliana nami kuangalia utaratibu mpya na wa masharti ya ujenzi wa nyumba za watumishi hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, miji mingi nchini imekuwa ikikua kwa kasi bila mpangilio. Je, Wizara iko tayari kushirikiana na halmashauri hapa nchini ili kuweka upimaji ikiwemo Wilaya ya Itilima na Mkoa wa Simiyu kwa ujumla?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu kwa maswali hayo.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Njalu tukutane huko nje tufahamishane namna gani mahitaji yake namna gani anaweza tukajenga hizo nyumba, lakini ajue Shirika la Nyumba limewekwa kwa mujibu wa sheria lazima lifanye biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama tullvyokubaliana kwamba wangekuwa wanatenga pesa halafu tunawajengea nyumba. Shirika la Nyumba ujenzi wake wa gharama za ujenzi ni nafuu kuliko *contractor* yoyote, Shirika la Nyumba ni *contractor* wa daraja la kwanza. Hata hivyo, kwa kujua ni Shirika la Nyumba la Serikali gharama za ujenzi ni nafuu na ubora wa nyumba zake ni mzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, labda tujadiliane huko nje kitu gani wamekwama badala ya kujenga nyumba 13 wanataka wajenge ngapi halafu tujue namna ya kushirikiana. Kwa kweli hatuwezi kujenga nyumba bila kupewa pesa Shirika la Nyumba haliwezi kwa sababu itabidi likope fedha benki liende kujenga nyumba zao. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Njalu kwa hili la nyumba tuwasiliane baadaye ili tuone jambo gani wamekwama, tuweze kushirikiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili upimaji kabla ya kupima Mji wa Itilima lazima ifanywe *master plan* na bahati nzuri Bariadi wameshafanya *master plan*. Kama tatizo ni utaalam, sisi tuko tayari kuwaazima Wataalam wa Mipango Mji wawasadie Itilima namna ya kuandaa *master plan*, halafu baada ya *master plan then sasa lije zoezi lingine* la upimaji na upangaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kama halmashauri yoyote haina Wataalam wa Serikali wa upangaji na upimaji wasipate tatizo. Serikali imeshasajili makampuni ya upangaji na ya upimaji ya Wataalam wabobezi ambao tumewasajili na tumewapa ruksa ya kufanya kazi hizi kama wenzao wa ujenzi wanavyofanya kazi nyingine za ujenzi wa barabara na majengo.

Mheshimiwa Naibu Spka, kwa hiyo, halmashauri kama haina Wataalam isikae ikitabu Wataalam wa Serikali tunayo makampuni ambayo yanaweza kuwasaida wananchi wa Itilima kupanga mji wao, kupima hadi umilikishaji. Kwa hiyo, tunaweza tukawasaidia Wataalam, lakini pia halmashauri inaweza ku-*engage* Wataalam binafsi kampuni binafsi wakafanya kazi hiyo. Kwa hiyo, yote mawili yanawezakana kufanya kwa Itilima.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge maswali yaliyosalia yatapangiwa utarabu mwininge nimejulishwa hapa, Katibu.

NDG. ATHUMAN HUSSEIN – KATIBU MEZANI:

KAULI ZA MAWAZIRI

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango na kwa mujibu wa Kanuni ya 49 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Kauli ya Serikali juu ya madai ya kutoonekana kwa matumizi ya shilingi trilioni 1.51 kwenye matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013 hadi 2016/2017, Serikali kuititia Wizara ya Fedha na Mipango ilikuwa kwenye kipindi cha mpito cha miaka mitano ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa kuandaa

hesabu za Serikali kwa kutumia mfumo wa viwango vya kimataifa vya uhasibu katika sekta ya umma yaani *International Public-Sector Accounting Standards - IPSAS Accrual*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho, Serikali iliendelea kukusanya taarifa mbalimbali kwa kutumia mfumo huu ili kutuwezesha kutambua kikamilifu hesabu za mali, madeni pamoja na mapato yanayotokana na kodi. *IPSAS Accrual* ni mfumo wa kiuhasibu ambapo mapato yanatambuliwa baada ya muamala husika kukamilika na sio wakati fedha taslimu inapopokelewa na matumizi yanatambuliwa wakati muamala wa matumizi umekamilika na sio wakati fedha inalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huu ni mzuri na una faida nyingi ikiwa ni pamoja na miamala ya mapato na matumizi kutambuliwa wakati husika na siyo wakati wa fedha taslimu inapopokelewa au kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya utekelezaji wa mpango mkakati wa uandaaji wa hesabu kwa mfumo wa *IPSAS Accrual* umeiwezesha Serikali na taasisi zake kutoa taarifa za kina na zinazoonesha uwazi na uwajibikaji wa taasisi husika, hususan katika usimamizi wa mali na madeni ya taasisi. Kuongezeka kwa uwazi, kumewawezesha watumiaji wa hesabu kupata taarifa zinazowasaidia kufanya maamuzi sahihi na kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na matumizi ya mfumo huu wa viwango vya kimataifa vya uhasibu katika sekta ya umma, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kwamba hakuna fedha taslimu ya shilingi triliioni 1.51 iliyopotea au kutumika kwenye matumizi ambayo hayakuidhinishwa na Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kurudia, kutokana na matumizi ya mfumo huu wa viwango vya kimataifa vya uhasibu katika sekta ya umma, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, hakuna fedha taslimu ya shilingi triliioni 1.51

iliyopotea au kutumika kwenye matumizi ambayo hayakuidhinishwa na Bunge lako Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, madai ya baadhi ya watu wasilitakia mema Taifa letu na Serikali yetu ya Awamu ya Tano hayana msingi wowote wenyewe mantiki. Haya yanadhihirishwa na aya zifuatazo kwenye tamko hili la Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) imemeleza jumla ya mapato yote ya Serikali kwa mwaka 2016/2017 yalikuwa shilingi trilioni 25.3 ambapo fedha hizi zinajumuisha mapato ya kodi, mapato yasiyo ya kodi, mikopo ya ndani na nje pamoja na misaada na mikopo nafuu kwa washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kuanzia mwaka 2016/2017, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilianza rasmi kuyatambua mapato kwa mfumo wa *Accrual* ambao nimeueleza kwenye aya zilizotangulia. Hivyo basi, kati ya mapato haya ya shilingi trilioni 25.3, yalikuwemo pia mapato tarajiwa yaani *receivables* kama mapato ya kodi yenye jumla ya shilingi bilioni 687.3 pamoja na mapato ya kodi yaliyokusanywa kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya jumla ya shilingi bilioni 203.92 yaani *transfer to Zanzibar*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uandishi wa taarifa ya ukaguzi, CAG alitumia taarifa za hesabu na nyaraka mbalimbali ikiwa ni pamoja na Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti yaani *Budget Execution Report* ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2017, mapato yalikuwa jumla ya shilingi trilioni 25.3 na matumizi yalikuwa shilingi trilioni 23.79. Matumizi haya hayakujumuisha shilingi bilioni 697.85 zilizotumika kulipa dhamana na hati fungani za Serikali zilizoiva.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi haya yalikuwa hayajafanyiwa uhamisho yaani *re-allocation* wakati ukaguzi unakamilika. Hivyo basi, baada ya kufanya uhamisho jumla

ya matumizi yote kwa kutumia ridhaa za matumizi yaani *exchequer issues* yalikuwa shilingi trilioni 24.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ufanuzi huo, shilingi trilioni 1.51 zilizodaiwa kutoonekana kwenye matumizi ya Serikali zilitokana na mchanganuo ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyoonekana kwenye *screen*, kwanza kabisa kulikuwa na matumizi ya dhamana na hati fungani zilizoiva za shilingi trilioni 0.6979; mbili, mapato tarajiwa yaani *receivables* ya shilingi trilioni 0.6873; tatu, mapato ya kodi yaliyokusanya kwa niaba ya Serikali ya Zanzibar shilingi trilioni 0.2039, ambapo jumla ya yake ni shilingi trilioni 1.5891.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha iliyotolewa kutokana na mchanganuo huu kulikuwa na fedha pia iliyotolewa zaidi ya mapato yaani *Bank Overdraft* ya shilingi trilioni 0.0791, tukitoa hii ya *bank overdraft* ndiyo tunapata fedha zinazodaiwa kutoonekana kwenye matumizi ya Serikali ya shilingi trilioni 1.51. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inamaanisha kwamba baada ya kupunguza mapato ya Zanzibar ya shilingi bilioni 203.92 na kupunguza mapato tarajiwa ya shilingi bilioni 687.3, mapato halisi kwa mwaka 2016/2017, yalikuwa shilingi trilioni 24.41. Aidha, baada ya kujumlisha matumizi ya dhamana na hati fungani zilizoiva za kiasi cha shilingi bilioni 697.85 kwenye matumizi ya shilingi trilioni 23.79 yaliyooneshwa katika Taarifa ya CAG, ridhaa za matumizi zilizotolewa zilikuwa shilingi trilioni 24.49 na kuleta ziada ya matumizi ya shilingi bilioni 79.07 ikilinganishwa na mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mchanganuo huu, ni dhahiri kwamba kwa mwaka 2016/2017 matumizi ya Serikali yalikuwa makubwa kuliko mapato kwa shilingi bilioni 79.09 ambazo ni *overdraft* kutoka Benki Kuu ya Tanzania. Utaratibu wa kutoa fedha zaidi ya mapato yaani *overdraft facility* upo kwa mujibu wa kifungu cha 34 cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2006. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuhitimisha kwa kusema kwamba Serikali kuititia Wizara ya Fedha na Mipango imepata mafanikio makubwa sana katika uandaaji wa Hesabu za Serikali kwa kutumia mfumo huu wa viwango vya kimataifa vya uhasibu katika sekta ya umma (*IPSAS Accrual*). Itakumbukwa kwamba katika Afrika, Tanzania ndio nchi pekee iliyofanikiwa kwa kiwango kikubwa kuandaa hesabu kwa kuzingatia matakwa ya *IPSAS* na kufanikisha kuandaa hesabu za majumuisho kwa kuzingatia mfumo huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maelezo haya ya Serikali, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kuwa Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, ipo makini na haiwezi kuruhusu upotevu wa aina yoyote wa fedha za umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira na vitendo vya Serikali ya Awamu ya Tano ambavyo Watanzania ni mashahidi ni kuona kwamba kila mapato yanakusanywa na kila mapato yanayokusanywa yanatumika ipasavyo na kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika!

NAIBU SPIKA: Ahsanteni sana. Waheshimiwa Wabunge nitaleta kwenu matangazo niliyonayo, tangazo la kwanza ni tangazo la wageni waliopo ukumbini leo, tutaanza na wageni walioko jukwaa la Mheshimiwa Spika na hawa ni wageni 16, Waheshimiwa Madiwani kutoka Jiji la Mbeya, karibuni sana Waheshimiwa. Wanaongozwa na Mheshimiwa Nyembele. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge na wale ambao wamekuja kwa ajili ya mafunzo. Tunaanza na wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Tunao wageni 11 wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, ambaye ni Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambao ni Kamati ya Siasa na Sekretarieti ya CCM kutoka Wilaya ya Kigamboni, Mkoani Dar es Salaam, karibuni sana. (*Makofii*)

Tunaye pia Mgeni wa Mheshimiwa Jumaa Awesso ambaye ni Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambaye ni mpiga kura wake kutoka Wilaya ya Pangani, Mkoa wa Tanga. Karibu sana, huyu anaitwa Ndugu Daffa Jumbe. (*Makofii*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambao ni wafanyabiashara kutoka Wilaya ya Kilolo, Mkoa wa Iringa. Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni 12 wa Mheshimiwa Angelina Malembeka ambao ni wahamasishaji wa utalii kutoka utalii 225 group. Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni 20 wa Mheshimiwa Injinia Edwin Ngonyani ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni 135 wa Mheshimiwa Munira Khatib ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo cha Mipango ya Maendeleo ya Vijijini cha Dodoma. Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Oscar Mukasa ambao ni waratibu wa mradi wa kuimarisha uwajibikaji katika upatikanaji wa huduma bora za afya pamoja na wawakilishi wa wananchi kwenye huduma ya upimaji wa VVU na uzazi salama. Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni Walimu kutoka Iringa Mjini. Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao vile vile wageni 50 wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa ambaye ni Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na

Mawasiliano ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni sana. (*Makof*)

Vile vile tunao wageni ambao wamelitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, tutaanza na wanafunzi 45 na wanafunzi watano kutoka *Black chool of Linguistics and Literature* ya hapa Dodoma wakiongozwa na Mwalimu wao Ndugu Peter Frank. Karibuni sana. (*Makof*)

Tuna pia wageni 30 ambao ni viongozi kutoka Taasisi ya *Star Women* ya Jijini Dar es salaam inayojihusisha na kuinua vikundi vyaa akinamama nchini. Karibuni sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge hao ndiyo wageni tulionao, wageni wetu karibuni sana mjifunze namna tunavyofanya kazi hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo lingine, hili ni tangazo linatoka kwa Katibu wa Bunge, kuna mabadiliko madogo ya ratiba ya Mkutano wa 11 wa Bunge. Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba Mheshimiwa Spika amefanya mabadiliko madogo kwenye ratiba ya uwasilishaji wa bajeti za Wizara kama ifuatavyo:-

Hotuba ya bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itawasilishwa na kujadiliwa tarehe 30 Aprili na tarehe 2 Mei, 2018 badala ya tarehe 3 Mei, mpaka tarehe 4 Mei, 2018.

Hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, itawasilishwa na kujadiliwa tarehe 3 mpaka 4 Mei, 2018 badala ya tarehe 30 na tarehe 2 Mei, 2018. Ratiba mpya inayoonyesha mabadiliko hayo Waheshimiwa Wabunge mttagawiwa kwenye viti vyenu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

MWONGOZO WA SPIKA

WABUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge mnaoomba miongozo nimewaona, lakini niwakumbushe tena kwamba Kanuni inataka mambo yaliyotokea Bungeni leo.

MHE. DAVID E. SILINDE: Yaliyotokea eeh! Ndiyo.

NAIBU SPIKA: Kwa hiyo, Mbunge yoyote atakayezungumza nje ya hapo tutakuwa nadhani tumeelewana vizuri Kikanuni. Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. LYIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimesimama kuomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 43, naomba niisome:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 43 bahati mbaya macho yangu, lakini niseme tu kwamba kuwa nimeshaeleweka kuhusiana na muda wa maswali hapa Bungeni, inasema hivi: "Muda wa maswali Bungeni utakuwa dakika tisini (90) isipokuwa katika Mkutano wa Bunge la Bajeti ambapo muda utakuwa dakika sitini (60)"

Mheshimiwa Naibu Spika, na jambo hili limekuwa sababu mara nyingi hata maswali hamna ya nyongeza ili kuweza kukamilisha muda huo. Hata ukiangalia *order paper* ile ya mwanzo ilikuwa haioneshi chochote kuhusu Kauli za Mawaziri lakini baadaye tuliletewa Kauli za Mawaziri nikitegemea kwamba kwa kawaida ya Bunge hili Kauli za Mawaziri huwa zinakuja baada ya kipindi cha maswali na majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo imekuwa ni jambo la ajabu kwamba umekatisha kipindi cha maswali na majibu ukaléta kauli ya Mawaziri labda kwa sababu kipindi hiki kinaoneshwa *live* cha maswali labda ili wananchi waweze kuona.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wangu, ni kwa nini kitii chako kimekatiksha kipindi cha maswali ambapo yapo Kikanuni ni *one hourna* ukaleta kauli ya Mawaziri wakati jambo hilo wala halina udharura wowote na kikawaida linakuja baada ya maswali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mlinga

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wangu naomba kwa Kanuni ya 68(7) ambapo jambo limetokea mapema leo Bungeni.

Mheshimiwa Naibu spika, mwongozo wangu naomba kupitia kanuni ya 68(7) ambapo jambo limetokea mapema leo Bungeni. Mwongozo wangu ulikuwa unahusiana na Kauli ambayo ametoka kuitoa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, hizi kauli zinazotolewa Bungeni huwa zinabaki kwenye *record* kwa maana ya *Hansard*, lakini tumeshuhudia hivi karibuni kuna baadhi ya Wabunge wameongea kauli zinazohusiana na hii kauli ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambazo zinakinzana. Wamesema kuwa Serikali yetu imepiga fedha 1.5 trillion akiwemo Mheshimiwa Zitto.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Kanuni ya 64(1)(a) inasema "Mbunge hatatoa taarifa ambazo hazina ukweli Bungeni" na kwa kuwa leo tumethibitisha kuwa kauli ambayo alitoa Mheshimiwa Zitto ni ya uongo. Sasa mwongozo wangu nikuombe kuwa Mheshimiwa Zitto aje afute kauli yake humu Bungeni na aombe radhi kwa kuwadanganya Wabunge na kwa kulidanganya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. DAVID E. SILINDE: Mwongozo, bado kuna miongozo.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tusikilizane kidogo, naomba ukae Mhesimiwa Slinde nimesimama.

Waheshimiwa Wabunge, kanuni zetu hizi kabla sijaijibu hii miongozo miwili, mtu ambaye akisimama ni lazima asikilizwe ni yule anayezungumza kuhusu utaratibu. Kuhusu miongozo, taarifa na vitu vingine ni kiti kinavyoona inafaa kwa hivyo leo nimechukua miongozo miwili na hiyo ndiyo nitakayoshughulika nayo.

WABUNGE: Aaaaah!

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nimeombwa mwongozo na Mheshimiwa Susan Lyimo lakini pia Mheshimiwa Mlinga, nitaanza na mwongozo wa Mheshimiwa Susan Lyimo ambaye ametupeleka...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tuwe tunasikilizana kwa sababu hizi kanuni mnazo miaka miwili na nusu sasa, naamini mnazifahamu vizuri, kwa hiyo, tuwe tunasikilizana.

Mheshimiwa Susan Lyimo ameomba mwongozo kupitia Kanuni ya 68(7) akitupeleka kwenye Kanuni ya 43 kwamba muda wa maswali umekatishwa na yeye ametoa maeleo marefu ambayo kwa sababu ya muda sina haja ya kuyarejea lakini swai lake alilouliza ni kwamba, kwa nini tumekatisha kipindi.

Waheshimiwa Wabunge, hii Kanuni ya 43, Mheshimiwa Susan Lyimo ameshaisoma kwa hivyo sina haja ya kuirejea. Tumekomea kwenye swalii la sita liliolulizwa na Mheshimiwa Njalu Silanga na amepewa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza na nimewapa taarifa kwamba tutakomea swalii hilo kwa sababu hayo maswali mawili yatawekewa utaratibu mwingine kwa taarifa nilizopata mimi kwenye kiti. (*Makof!*)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge muwe mnaskiliza ili siku nyingine msirudie kuuliza jambo hilo hilo. Kama hamsikilizi maana yake mngemsikiliza *Chief whip* wenu hapo halafu mkanyamaza, mkamjibu wenyewe baadaye.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Njalu Silanga amepewa nafasi yake ya Kikanuni ya kuuliza maswali yake ya nyongeza, maswali ya ziada ya hapo ni kiti kinavyoona inafaa. Kwa hivyo hakuna kipindi chochote kilichokatishwa isipokuwa maswali mawili yatawekewa utaratibu mwengine. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa mwongozo mwengine na Mheshimiwa Goodluck Mlinga ambaye ametumia pia Kanuni ya 68(7) akieleza kuhusu jambo ambalo yeye amelihuisha na kauli illyotolewa hapo na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwamba Mheshimiwa Zitto alikuwa ametoa taarifa ambayo inakinzana na taarifa hii aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye kauli yake.

Hata hivyo, Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mlinga ametupeleka kwenye Kanuni ya 64(1)(a) ambayo inakataza kutoa taarifa ambazo hazina ukweli Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Zitto hakutoa taarifa yake Bungeni, kwa hiyo hii Kanuni hapa ya kumtaka aje afute kauli yake haihusiki, hakutoa taarifa yake Bungeni na kwa hivyo yeye...

*(Hapa Mheshimiwa Suzan Kiwanga aliongea
bila ruhusu ya Kiti)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kiwanga!

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Zitto hakutoa kauli yake hapa, kwa hiyo mwongozo wangu ni kwamba hiyo habari ya yeye kuja kufuta kauli haipo, yeye atatoa maelezo huko huko alikokuwa ametoa kama ataona inafaa. Kwa hiyo, huo ndiyo muongozo wangu, tutaendelea.

MHE. DAVID E. SILINDE: Kuhusu utaratibu!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Slinde ukisema kuhusu utaratibu maana yake unataka kunipa mimi utaratibu. Sasa kaa nikueleze vizuri, kaa chini nikueleze vizuri. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tena wengine ni wazoefu hizi kanuni mzisome sawa sawa, Kanuni ya tano (5) Mheshimiwa Silinde fungua Kanuni ya tano (5) twende sawa sawa.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 5(4) inasema hivi "Mtu yejote ambaye hataridhika na uamuzi wa Spika, anaweza kuwasilisha sababu za kutokuridhika kwake kwa Katibu wa Bunge ambaye atawasilisha malalamiko hayo kwa Spika". (*Makofii*)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

NAIBU SPIKA: Nisikilzeni Waheshimiwa Wabunge wa upande wa kushoto, mkipiga kelele ndiyo maana hamuelewi mnapoelekezwa, msipige kelele nisikilzeni. Nisikilzeni niwafundishe Kanuni. (*Makofii*)

WABUNGE FULANI: Aaaah!

NAIBU SPIKA: Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, kuhusu utaratibu anapewa Mbunge mwengine na siyo kitu, kitu hakipewi utaratibu. Kwa hivyo ukiona kuna jambo ambalo Kiti kimefanya ambalo wewe huridhiki nalo, Kanuni ya 5(4) unapeleka malalamiko kwa Katibu ili ampelekee Spika. Someni Kanuni vizuri Waheshimiwa Wabunge...

MHE. JOHN W. HECHE: Punguza ubabe basi!

NAIBU SPIKA: ...maana humu ndani tunao wageni wanaona ambavyo sisi wenyewe hatujui utaratibu kwa hiyo, someni vizuri Kanuni.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MHE. JOHN W. HECHE: Punguza ubabe Bwana!

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

NAIBU SPIKA: Naomba ukae Mheshimiwa Gekul!

MHE. PAULINE P. GEKUL: Kuhusu utaratibu!

NAIBU SPIKA: Kaa chini, kaa chini Mheshimiwa Gekul. Katibu.

NDG. HUSSEIN ATHUMAN-KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kubenea humu ndani usipokuwepo huwatunatulia sana naona umekuja na vurugu leo.

Waheshimiwa Wabunge nimeletewa orodha ya majina ya Waheshimiwa Wabunge watakaoanza mjadala asubuhi ya leo kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na tutaanza na Mheshimiwa Riziki Lulida atafuatiwa na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza na Mheshimiwa Susan Mgonokulima ajindae.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa rehema kwa kunijaalia nami kuchangia hoja iliyopo mbele yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Ummy Mwalimu na Naibu waziri na Dkt. Mseru

na Dkt. Mgassa. Mnamo mwezi Machi, kulikuwa na mtoto anaumwa *sickle cell* akawa na damu mbili nikapigwa simu saa tano kwamba hali ya mtoto yule ni mbaya na huyo mtoto ni Rais wa ugonjwa wa *sickle cell Africa*. Nilimpigia Mheshimiwa Ummy usiku saa sita akanijibu na alitumia uwezo wake na huruma yake na yule mtoto aliongezwa damu, sasa hivi yule mtoto anaendelea salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dkt. Mgassa alikuwa nje ya nchi, baada ya kupata taratibu zile alimtafuta Dokta. mwininge ambaye alikuwa yuko Dar es Salaam mpaka saa 7.30 usiku yule mtoto ameweza kuongezewa damu lita kama nne hivi nafikiri na yule mtoto anatoa shukurani za dhati kwa niaba ya familia yake, Mheshimiwa Ummy na wote wahusika Mwenyezi Mungu awabariki sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa mzima nikilwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano, nikapata ajali, sasa hivi mimi ni mlemavu. Mtu ambaye amenisaidia sana ni Dkt. Mseru Mwenyezi Mungu ambariki sana. Hivyo, kwa niaba ya Madaktari wote, naomba Dkt. Mseru anifikishie salamu zangu za dhati, Mwenyezi Mungu awajaalie Madaktari wote Tanzania kwa huruma na kazi ngumu wanazofanya kwa kuwasaidia Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mwenyekiti wa kupambana na *malaria* ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mimi Riziki Said Lulida niko tayari kutokomeza malaria Tanzania wewe je? Twende zetu Kasulu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tuna ugonjwa hatari wa malaria na malaria inaua, lakini nataka nitoe kitu kimoja ambacho nimekiona kwa muda mrefu kutohana na uzoefu niliokuwa nao. Malaria ni ugonjwa hatari lakini kuna wafadhili wanasema wao wanatoa fedha kwa ajili ya kusaidia malaria, hizi pesa hazionekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri Mkuu kwa vile ye ye ndio mdau katika Bunge la Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania, Mheshimiwa Ummy Mwalimu na wenzake nataka watujibu hizi pesa za malaria zinakwenda wapi? Nimeweza kuhudhuria mikutano mingi ya mararia ikiongozwa na USAIDna Taasisi nyingine wanasema tumepeleka Tanzania bilioni 600 zinakwenda wapi hizo pesa. Mimi sijajua mpaka leo na nimejaribu kumuuliza Naibu Waziri ananiambia hata na mimi vilevile Mheshimiwa Riziki hatujui pesa za malaria zinakwenda wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, malaria kama hizi pesa ambazo wanasema wanatuletea hazijulikani zinakwenda wapi, mimi napata kigugumizi na kujiuliza kuna nini na hizi pesa za malaria. Kwa mfano, pesa za UKIMWI zinaonekana ndani ya halmashauri, katika halmashauri tunaweza tukazikagua zile pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuna hela za *Global Fund*, kuna hela za *TAC AIDS*, kuna hela za Bill Clinton, Kuna hela za *Foundation* ya Benjamini Mkapa zinaingia ndani ya halmashauri na zinawenza kukaguliwa. Hizi pesa za malaria naomba Waziri mwenye dhamana aniambie ziko wapi ili tuweze kuzifanya kazi na Watanzania waweze kuzitumia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, malaria yalikuwa yamepotea lakini sasa hivi malaria imeongezeka kwa kiasi kikubwa. Mikoa ambayo ina malaria ni mikoa ya kanda ya ziwa ikiwemo Geita, Simiyu, Mara, Kigoma na Lindi na Mtwara. Sababu za msingi za kuwepo maeneo hayo malaria ni kwa ajili ya migodi mikubwa ambayo iko katika hiyo mikoa wameacha mahandaki makubwa, lakini mahandaki haya yalisababishwa na mikataba mibovu ambayo *EIA* haikufuatwa, hivyo baada ya kumaliza machimbo wameacha machimbo yakiwa wazi na mbu wamezaliana kwa wingi hiyo mikoa sasa hivi iko katika hatari kutokana na malaria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba suala hili la malaria lisimamiwe kwa kikamilifu ili wananchi wa Mikoa hiyo Geita , Simiyu, Mtwara, Lindi, Kigoma, Katavi tutakuwa tumepoteza

watu wengi hasa wanawake na watoto, wajawazito ndio walengwa wakubwa wa malaria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia suala la NHIF bima ya afya ni mkombozi kwa Watanzania na ilichukuliwa bima ya afya bima ikawa ni kwa ajili ya wafanyakazi wa Serikali na taasisi zake, lakini walishahau kama kuna wakulima wanauzua mazao na hao wakulima wanapouza korosho wanapata pesa kama milioni 50 wengine milioni 20, naomba watu wa bima ya afya itengeneze mikakati maalum ya kuhakikisha hata wakulima na sekta binafsi ziwe zinatoa msaada na kuweza kulipia bima ya afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nazungumza hivyo Wabunge kila siku unapigiwa simu, mimi naumwa nataka kwenda Dar es Salaam lakini kama angetengenezewa mazingira mazuri ya korosho zake, kuwa unapouza korosho unatoa bima ya familia ya milioni 1,500,000, matatizo haya yangeweza kwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wavuvi wanavua kanda ya ziwa dagaa, Zanzibar wanavua kila kitu, wanapata pesa, je, ni mikakati gani wametengeneza ili watu wale wanawatembelea na kuweza kujunga na bima ya afya. Mambo ya kuwa tegemezi kutegemea wafadhili, wafadhili sasa hivi wamekuwa kama wanatubabaisha, wanatunyanyasa leo nitatoa kesho sitoi. Mazingira haya ya kutegemea wafadhili ni aibu kwa Taifa tutumie njia ya sisi wenyewe kuweza kujitegemea na sio kutegemea watu wa nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona tunaweza kutokomeza malaria kwa kutumia pesa zetu za ndani. Hatukatai kuchukua pesa za nje, lakini pesa za nje sasa hivi zina masharti ambayo yanatufanya tunakwazika, tunakuwa na madeni mengi ambayo tukijiuliza hela hizi kama hazisimamiwi, ni mzigo mkubwa kwa Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia damu salama kwanza nataka nilete hamasa kwa Wabunge

tuchangie damu salama. Ugonjwa wowote ni utarajiwa hautegemei wakati wowote, unaweza kupata ajali ukategemea upewe damu, unaweza ukajikuta mwanaao anaumwa, familia yako inaumwa ,hivyo suala la damu salama lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niwashukuru sana. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Riziki. Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Suzan Mgonukulima dakika tano.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwa dakika tano. Naomba nianze na kitu kilichotokea hapa wakati Waziri anatoa kauli. Mimi naona mnatu-*confuse* kwa sababu gani? Tulitegemea kwamba majibu aliyoyatoa Waziri angeyapeleka kwa CAG afute hoja. Mnachotaka kutuaminisha hapa, mimi naaminai kwamba CAG anafanya kazi kwa kupewa vielelezo, kama hakupewa vielelezo Naibu Spika ataandika kitu alichokiona. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa nikusaidie kwa kuwa una dakika tano tu Kauli za Mawaziri kikanuni hazijadiliwi. Kwa hiyo kama unataka kujadili hoja zilizoko kwenye ripoti ya CAG ile ni taarifa ya wazi, nenda huko usije kwenye ile kauli ya Waziri kwa sababu kanuni zetu haziruhusu.

Waheshimiwa nimewakumbusha kuna watu miaka miwili na nusu na bado kanuni hamzijui na mkielezwa mnapiga kelele, mnashangaza sana na wengine ni Wabunge wa siku nyingi na huko nikiwatazama mnachecha na watu wanawaangalia hapa.

Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza endelea.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Naibu Spika, ujumbe umefika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nijadili sasa mambo machache kwa sababu ni dakika tano kwanza nianze na utoaji dawa katika hospitali. Dawa zipo, ninachotaka kuongelea ni namna wale Wafamasia wanavyotoa dawa kwa wagonjwa. Wafamasia wanatoa dawa kwa wagonjwa bila kutoa maelekezo ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko dawa ambazo ukisoma *leaflet* yake ukishapewa dawa wanakwambia kwamba labda hii dawa unapaswa uiyeyushe kwenye maji kabla ya kumeza au utumie hiyo dawa kabla ya kula au masaa fulani kabla ya kula au hizi dawa zinaendana na chakula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotokea Wafamasia wetu wamekuwa wakitoa dawa hizo kwa kuonesha kwamba unatumia moja mara moja, mbili mara tatu na kadhalika bila kutoa maelekezo ya kutosha kwa wagonjwa. Kwa hiyo, unakuta wakati mwininge mtu anakwenda kumeza dawa ambavyo haitakiwi na kwa kweli haileti tija katika matibabu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kuhusu uzazi wa mpango, Mheshimiwa Waziri nimepitia kitabu chake hicho ameandika maneno mazuri na anafanya kazi sio mbaya, lakini hakuna mahali alipogusa kuhusu uzazi wa mpango. Huku nyuma kulikuwa na kitengo wakati wa Awamu ya Kwanza kulikuwa na kitengo kinaitwa UMAT (Uzazi na Malezi Bora Tanzania).

Mheshimiwa Naibu Spika, kitengo hiki kilikuwa kinafundisha mambo mengi kutumia dawa ya kinga ya kuzaa, kufundisha wanawake namna ya kujitunza, namna ya kulea watoto wao na namna ya *ku-space* ili wasizae watoto wengi na kwa wakati muafaka. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Waziri, kitengo hiki hata kama hakitarejeshwa kama kilivyokuwa, lakini wkiangalie ili kiweze kwenda kutoa elimu ya kutosha kule chini kwa wanawake wa vijiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije sasa kwenye lishe, ukienda kwenye ukurasa wa 89 wa kitabu chake,

Mheshimiwa Waziri ameongea kuhusu lishe, ameongea mambo mazuri ambayo yanahuus mashirika mbalimbali namna ya kurutubisha vyakula ambavyo tunakula, kuweka madini ya joto na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshauri Waziri kwamba lishe ndio msingi wa maisha ya mtu katika kukua kwake kimwili na kiakili. Kwa hiyo, ni vyema hiki kitengo cha lishe na taasisi hii iwe mtambuka, washirikiane na Wizara ya Kilimo pia na Idara ya Maendeleo ya Jamii . (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wako hawa *Social Workers* ambao kazi yao ni wataalam wazuri kabisa wa kutoa ushauri kuhusu mambo hayo lakini hawaajiriwi, wanafundisha watu kila siku lakini hawapewi ajira na hawa watu wa muhimu sana katika maendeleo ya nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Susan Mgonukulima atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mheshimiwa Joseph Haule ajiandae dakika tano tano wote.

MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kunipa nafasi niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze na pale nikikumbuka bajeti ya mwaka jana nilimwomba Waziri kuhusu hospitali ya rufaa ya mkoa wa Iringa, ina upungufu wa Madaktari Bingwa sita. Kutokana na msongamano wa wagonjwa wanaopata ajali kutokana na njia kuu inayounganisha nchi yetu ya Tanzania na nchi jirani Zambia, Msumbiji, Malawi na Kusini. Hata hivyo, hadi tunafikia bajeti hii ya mwaka 2018/2019, sikuweza kusaidiwa hata kupata Daktari mmoja Bingwa wakati aliniahidi hapa. Naomba atakapokuja kuhitimisha aweze kunipa hilo jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, imeonekana katika Taifa letu saratani ya shingo ya kizazi imekuwa ni tatizo kubwa sana.

Kwa taarifa ya yeye mwenyewe Waziri ameliambia Taifa kwamba katika wanawake wanaopimwa kwa mwaka wanawake 670 hupatikana na tatizo hilo. Hilo tatizo limeonekana ni kubwa na limeonekana kisababishi ni wanaume ambao hawajatahiriwa, lakini sikuona kwenye kitabu chake mkakati ambao ameuweka wa makusudi kutoa elimu kwa kundi la wanaume kutoruka njia mbili ili tatizo hili liweze kupungua kwenye Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Waziri anapokuja kuhitimisha hoja hii aniambie Wizara imejipangaje kufanya utafiti wa kujuu chanzo kikuu kabisa cha kusababisha hili tatizo likue kwa kasi katika Taifa letu kwa maana najua huwezi kutoa tiba kwenye tatizo ambalo chanzo chake hukijui. Ukiilinganisha na taarifa ya wataalam hebu turudi miaka ya nyuma tulikuwa na wanaume wengi sana ambao hawajatahiriwa lakini hili tatizo halikuwa kwa kiasi kama ambaccho tunakiona kwa sasa. Hivyo, niiombe Serikali tatizo hili walilogundua ni sehemu moja ndogo tu, sehemu kuu ipo, hivyo Wizara ijpange kufanya utafiti wa kina ili tuweze kutatua tatizo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuja kwenye mabadiliko ya tabianchi, sasa hivi katika Taifa letu kumekuwa na magojwa mengisana ya mlipuko ambayo yanapelekea Taifa letu liweze kutafuta dawa katika nchi mbalimbali kuokoa maisha ya Watanzania. Hata hivyo, inasikitisha sana katika Taifa letu la Tanzania hadi sasa tunapozungumza *asprin* tunaagiza Kenya, nchi yetu ya Tanzania Wizara ya Afya asilimia 50 inatumia fedha hizi kuagiza dawa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu hiki hakuna mkakati wa Wizara ya Afya ulioonesha kuwa tunakuja na mpango mbadala kutafuta wadau waweze kujenga kiwanda cha dawa katika nchi yetu ili kulipunguzia Taifa kutumia gharama kubwa sana kuagiza dawa nje ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonekana kwenye Wizara hii kuna 1.5 imepotea, sasa hili ni jambo la kushangaza sana

na linasikitisha pale tunapokwenda kwenye hospitali zetu za rufaa kukosa vifaa wakati kuna hela zinazopotea bila kuelewa kitu chochote. Naomba Waziri mwenye dhamana wakati wa... (*Makof*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joseph Mkundi, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Haule, Mheshimiwa Allan Kiula ajiandae.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana. Kwa kuanza nitambue jitihada za Mawaziri na timu zao kwenye Wizara hii kwa kazi wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu kwa leo kwanza niongelee juu ya magonjwa yasiyo ya kuambukizwa ambayo yamekuwa *common* sana kwenye jamii yetu na kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri sikuona kama kuna eneo yamepewa msisitizo sana. Kuna magonjwa kama kisukari, shinikizo la damu na kadhalika kama hayo, yamekuwa ni ya kawaida sana kwenye jamii yetu na yamekuwa yanapoteza maisha ya watu wengi sana kwenye maeneo hasa ya vijijiini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ushauri wangu kwenye eneo hili, niombe Serikali kupitia Wizara kama ambavyo imekuwa inafanya kwenye matatizo ya UKIMWI, zahanati zetu vituo vya afya na hospitali viwe na dawa hizi na ikiwezekana kusiwe na gharama wakati wa kupata dawa hizi ili watu wetu waweze kupata madawa haya na huduma kwa urahisi kwenye maeneo yetu ya vijijiini na kwa hivyo kuweza kuokoa maisha ya watu wetu wengi sana wanaopoteza maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nafikiri nilichangie, nimeona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kaongelea namna ambavyo kumekuwa na mkakati wa

kuimarisha hospitali za rufaa na hospitali za mikoa. Nikizungumzia kwenye Jimbo langu ya Ukerewe, sisi hospitali yetu ya rufaa ni hospitali ya wilaya hasa kutokana na jiografia yetu na kwa maana hiyo msaada mkubwa ambao tungeweza kuupata kwenye Visiwa vyta ya Ukerewe na akatusaidia sana ni kuimarisha hospitali yetu ya Wilaya Hospitali ya Nansio.

Mheshimiwa Naibu Spika, sawa tumekuwa na maboresho ya wakati fulani lakini bado tuna tatizo kubwa sana la wataalam kwenye hospitali yetu ya Wilaya. Kama mnavyojua jiografia ya ukerewe ni ya visiwa, sasa yanapotokea matatizo ya dharura kwa mfano wagonjwa wanaohitaji kupata rufaa na wakati huo usaifiri wetu una *limited time*, ikifika jioni hakuna usafiri wa kuvusha wagonjwa kwenda maeneo mengine. Tunashukuru kwamba tumepata shilingi milioni 200 kwa ajili ya kununua boti, lakini bado haiondoi umuhimu wa kuongeza wataalam na Madaktari kwenye hospitali yetu ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri, tunashukuru kwamba tumepata shilingi milioni 200 kwa ajili ya kuboresha Kituo cha Afya cha Bwisya ambayo itasaidia sana. Kituo kile kinahudumia zaidi ya watu 30,000 kwenye Kisiba cha Ukala, lakini wakati tunakamilisha ujenzi wa kituo kile cha afya Mheshimiwa Waziri niombe sana sambamba na kukamilisha kituo kile Wizara basi ione uwezekano, kama jambo la muhimu sana kufanya maandalizi ya wataalam kwa ajili ya kuhudumu kwenye vituo hivi ambavyo tumekuwa tunaviboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kile ni kituo kikubwa, kinakamilika lakini mpaka sasa kina watumishi sita pekee, jambo ambalo kama litaendelea kuwa namna ile hata kama kitakamilika hakitakuwa na tija. Kwa hiyo, niombe sana kwa Mheshimiwa Waziri, hiki Kituo cha Afya cha Bwisya kinaelekea kukamilika, basi tupatiwe wataalam wa upasuaji lakini na Madaktari kwa ajili ya kutoa huduma, sambamba na upatikanaji wa gari la wagonjwa kwa ajili ya kuhudumia kwenye kituo kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo kutokana na jiografia yetu tuna matatizo makubwa ya afya na ningefurahi sana kama wakati wa kuhitimisha Mheshimiwa Waziri angeongelea maeneo tata hasa kimazingira kama Ukerewe, Serikali ina mkakati gani kuweza kuboresha huduma za afya ili kuweza kuokoa maisha ya akinamama na watoto ambaeo mara kwa mara wamekuwa wanapoteza maisha kutokana na jiografia au mazingira kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Visiwa vyetu vya Ukerewe bahati nzuri Mheshimiwa Waziri, tumekuwa mara kwa mara tunabadilishana mawazo juu ya kutusaidia kwenye visiwa vyetu vya Ukerewe. Kisiwa cha Ilugwa, kutoka Kisiwa cha Ilugwa kuja Wilayani kuna karibu saa tano ambazo mgonjwa anatakiwa asafiri na kule tuna zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ili kuweza kuwasaidia wananchi wale ambapo Ilugwa ile zahanati inahudumia zaidi ya visiwa vitano, inahudumia watu zaidi ya 20,000, tuombe basi zahanati hii iweze kusaidiwa kupandishwa kuwa kituo cha afya ili iweze kutoa huduma zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Joseph Haule atafuatiwa na Mheshimiwa Allan Kiula na Mheshimiwa Joseph Mbatia ajiandae.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwa dakika hizi tano ulizoni katika Wizara hii nyeti Wizara muhimu sana kwa maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wizara hii tumeona kuna changamoto kubwa sana za miradi mbalimbali kuweza kufika kwa wakati katika maeneo ambayo yanastahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni-*declare interest*, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Kitu kikubwa ambacho naweza nikakizungumza kwa haraka, baada ya lile zoezi la kutumbua wafanyakazi wa vyeti *fake*, tumekuwa na athari kubwa sana ya watumishi katika maeneo yetu hasa Mkao wa Morogoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Wilaya yetu ya Kilosa uhitaji wa watumishi ulikuwa ni 1,025 kwenye kada mbalimbali kama Wauguzi, Madaktari, Wafamasia, Ustawi wa Jamii na Maafisa Afya, lakini waliopo ni 474 tu, sawa na asilimia 46. Pia tuna upungufu wa watumishi 551 sawa na asilimia 54. Unaweza ukaona jinsi ambavyo Wilaya ya Kilosa imekuwa nyuma sana katika sekta hii ya afya na watu wamekuwa wakitaabika sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wito wangu kwa Serikali, tunaomba itusaidie sana watumishi hawa waweze kufika katika Wilaya yetu ya Kilosa lakini pia tuweze kuokoa maisha ya mama na mtoto ukizingatia jiografia ya Wilaya ya Kilosa imekuwa iko mbali mbali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiukweli kabisa tumeona kwamba kuna upungufu mkubwa wa vituo vya afya ambapo sasa hivi Serikali imetoa shilingi milioni 400 pale kwenye Kituo cha Afya cha Kidodi, tunashukuru sana. Pia kituo hiki ni muhimu kwa sababu kinaenda kuhudumia wananchi wa Kata ya Ruaha, Vidunda, Kidodi pamoja na Rwembe. Kwa jiografia iliyoko pale tunaona pia kuna umuhimu wa kusisitiza na kuiomba Serikali iweze kutupatia gari ili liweze kusaidia wananchi wa Jimbo la Mikumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika upungufu huu wa Madaktari Bingwa katika Wilaya yetu ya Kilosa, mwaka 2017 tulisikia Serikali inataka kupeleka Kenya Madaktari 500, basi kwa upungufu huu tunadhani mngetudondoshea pale Mikumi kidogo Madaktari Bingwa kadhaa ili waweze kutusaidia katika Wilaya yetu ya Kilosa, hii ingeweza kusaidia sana. Pia dawa zimekuwa zinafika chini ya kiwango; dawa zimekuwa chache. Unaposikia kuna shilingi trilioni 1.5

hazieleweki zimekwenda wapi kwa kueleweka, nadhani zingeweza kuwa zimepangiwa mkakati maalum katika kitengo hiki cha afya na kuweza kuwasaidia mama na mtoto, tungeweza kupata hesabu nzuri sana na Serikali ingeweza kutimiza malengo ya kuwasaidia Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini pia kuna kitu ambacho Serikali inabidi iongeze nguvu. Katika Maafisa Maendeleo wa Jamii wamekuwa pungufu sana. Kwa nchi nzima tunaona kwamba uhitaji ni watumishi 4,000 Iakini waliopo ni 1,700. Kwa hiyo, unaona kwamba asilimia 57.5 kuna upungufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maafisa Maendeleo ya Jamii ndio wahamasishaji wakubwa katika Wilaya zetu, katika maeneo yetu kuwahamasisha wananchi waweze kujiletea maendeleo yao. Unapokuwa huongezi msisitizo katika kada hii na kufanya upungufu katika watumishi wa Maafisa Maendeleo ya Jamii inakuwa inashindwa kuwa-*connect* Watanzania na wananchi katika kujiletea maendeleo yao katika maeneo yao. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali iongeze nguvu katika kuongeza Maafisa Maendeleo ya Jamii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo tumevitembelea, bajeti haziendi kwa wakati na vyuo vimekuwa katika hali mbaya. Namuomba sana dada yangu, Mheshimiwa Ummy, waongeze nguvu kwa kuongeza Maafisa Maendeleo ya Jamii ili waweze kuwa chachu na kuwakusanya wananchi pamoja, waweze kujadiliana nao ili kujiletea maendeleo katika maeneo yao. Maana huwezi ukaongelea maendeleo katika Jimbo, Wilaya na katika Mkoa bila kuwahusisha Maendeleo ya Jamii. Hao ndio wanaoweza ku-*connect* Serikali na wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunapokuja kuongelea suala la barabara, suala la wananchi kulima, watu kufanya programu mbalimbali katika nchi yetu, Maafisa Maendeleo ya Jamii ni watu wa muhimu sana. Naiomba sana Serikali iongeze nguvu zake katika kuajiri watu hawa. Asilimia

57, unaweza ukaona upungufu huo ni mkubwa sana na inatia *damage* kubwa sana kwa Serikali.

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Allan Kiula atafuatiwa na Mheshimiwa James Mbatia na Mheshimiwa Agnes Marwa ajiandae.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuweza kunipatia nafasi nami kuchangia Wizara hii muhimu kabisa, na mimi niseme niweze kusikika na Mheshimiwa Waziri aweze kuona namna ya kusaidia mambo mengine.

Kwanza kabisa, nampongeza Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayofanya katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Afya kwa sababu pamoja na kwamba tunapitisha, bajeti lakini Serikali ndiyo inatoa pesa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, naipongeza Wizara, Waziri, Naibu na Watendaji wake Wakuu. Ile sera ya kuboresha vituo vya afya; Kituo cha Kinyambuli tulipata shilingi milioni 400 na kinaendelea vizuri kabisa. Pia tangu niingie Bungeni nimekuwa nikijadili sana suala la Wilaya mpya kutokuwa na Hospitali za Wilaya. Kwa hiyo, nashukuru sana tumeweza kupata shilingi bilioni 1.5 mwaka huu na tunaenda kujenga Hospitali ya Wilaya. Huo ni ukombozi mkubwa sana kwa wana Mkalama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea, yako mambo ambayo pia ni muhimu ukisimama uweze kusema. Kama liko jambo lina *trend* kwenye mtandao halifu unakaa kimya na unaona linaharibu sura ya Serikali, hatuwezi kukaa kimya.

MBUNGE FULANI: Mmh!

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana tunaona kwamba hapa na pale watu wanajaribu kutoa ufanuzi wa baadhi ya mambo. Sisi sote kama Waheshimiwa Wabunge tunajua kwamba Ripoti ya CAG inapotolewa, hizi *oversight committees* pia kama PAC, LAAC na PIC tutakaa na tutaleta ripoti Bungeni na ripoti hiyo itajadiliwa. Kwa hiyo, ni vyema watu wakatambua hilo. Huwezi ukamnyooshea mtu kidole au unamtukana halafu akawa amekaa kimya. Kwa hiyo, Kauli ya Serikali imekuja muda muafaka kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza, kama watu wameona kwamba ulivyopunguza muda wa maswali halafu karuhusu Kauli ya Waziri ili wananchi waone, kama wao wameenda kwenye mitandao, sasa umefanya kitu gani cha ajabu? Hilo ni jambo la lazima. Unajua watu wanasesma mkuki kwa nguruwe... (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Mmh! (*Makofi*)

MHE. ALLAN J. KIULA: Sasa jambo hilo ni muhimu na uendelee kufanya hivyo hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiendelea na uchangiaji katika hoja ya Wizara, Mheshimiwa Waziri lipo suala la Hospitali ya Kansa ya *Ocean Road*. Hospitali hiyo ni muhimu sana na wananchi wetu wanapata huduma muhimu.

T A A R I F A

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Allan Kiula, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa taarifa kwa mzungumzaji kwamba ni lazima ajue

kwamba tumeambiwa kwamba Taarifa ya Serikali huwa hajadiliwi. Nilikuwa nampa taarifa. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo taarifa yake siipokei.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kiula subiri kidogo.

Mheshimiwa Mwakagenda, nafahamu unajua tofauti ya Taarifa ya Serikali na wewe unayo nakala yake hapo. Maelezo ya Mheshimiwa Kiula hayahu Tuarifa ya Serikali, yanahu jambo ambalo limesababisha mchakato. Wewe umesikia anasema anamsifu Naibu Spika au ni hicho kina taabu? Kwa sababu yeye anazungumzia ratiba iliyosababisha yule mtu kusoma, sasa utasemaje hiyo ni Tuarifa ya Serikali Mheshimiwa?

Mheshimiwa Kiula.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, hata hivyo, taarifa hiyo siipokei kwa sababu wao wanapenda kusema halafu sisi tusiseme. Sasa tutasema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya *Ocean Road* inatoa huduma, nzuri lakini wananchi wetu wanapata shida sana. Mheshimiwa Waziri umekiri kwenye ripoti yako kwamba *waiting time* ni wiki sita watu kupata huduma pale, mnataka *m-reduce* mpaka wiki mbili. Sasa kuna *mitigation* gani inafanyika hapo ndani ya wiki sita na watu wanapoteza maisha? Mheshimiwa Waziri unajua kabisa nimeshapoteza wananchi wangu wa Mkalama kwa kusubiri huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la dawa. Mheshimiwa Waziri umezungumza suala la duka la dawa kuwa na dawa toshelevu. Tunaomba jambo hilo liwekewe mkakati, bajeti iwekwe ya kutosha kwa sababu

yako maduka nje ya Muhimbili ambayo yanauza hizo dawa kwa bei ghali na wananchi hawawezi kumudu gharama hizo. Sasa jambo hilo linachafua taswira ya *Ocean Road* na inaonekana kama ni jambo la makusudi na kwa bahati mbaya daktari hawezi kusubiri mgonjwa afe anamwambia nenda mahali fulani utapata dawa. Picha wanayopata wananchi ni kwamba hayo maduka ni ya madaktari husika. Kwa hiyo, tunawapaka matope madaktari wetu na jibu sahihi ni hospitali yetu kuwa na dawa za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri natambua kabisa kwamba TAMISEMI wanaweza kutupatia gari na labda Halmashauri inaweza kununua. Nimekuwa nikizungumza sana suala la *ambulance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi juzi tu ametokea Diwani wangu mmoja amepata *stroke*, amecheleweshwa hospitali kwenda Singida kwa sababu hakuna usafiri, na mimi ni Mbunge. Sasa tunaomba jambo hilo kwa vyanzo vyovyote vile tuweze kupata gari la wagonjwa. Mkalama hatuna gari la waonjwa. Lile ambalo lilijibiwa na TAMISEMI ni gari lililochoka, Wilaya ilivyogawiwa tulipewa, linatugharimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuokoe maisha ya wananchi. Tunaomba tufikiriwe kwa jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la hoja za watumishi wa afya...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

MHE. ALLAN J. KIULA: Mimi nina dakika kumi. Hoja za watumishi...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Allan Kiula, kwa majina yaliyoletwa na chama chako, kila Mbunge wa CCM anachangia dakika tano. Ni kwa mujibu wa majina yaliyoko hapa mbele. Kwa hiyo, muda wako umekwisha Mheshimiwa.

Mheshimiwa James Mbatia, atafuatiwa na Mheshimiwa Agnes Marwa na Mheshimiwa Getrude Rwakatare, ajiandae.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Ninaamini nina dakika kumi za kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza kabisa nianze na maswali kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujuu tu, Serikali uwekezaji wake katika sekta ya afya ni asilimia ngapi? Sekta binafsi uwekezaji wake katika afya kwa ujumla wake ni kiasi gani na ndani ya sekta binafsi, mashirika ya dini yanachangia huduma ya afya kwa kiasi gani? Ni kiasi gani kuna ubia kati ya Serikali na sekta binafsi? Kuna ubia kiasi gani kati ya mashirika ya dini na Serikali? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu lengo la nne la Malengo Endelevu ya Dunia inazungumzia afya bora kwa wote ifikapo mwaka 2030. Nawapongeza wataalam wetu katika sekta ya afya, Waziri, Katibu Mkuu Dkt. Mpoki, wataalam; akina Profesa Mseru, akina Dkt. Janabi na wenzao, KCMC, Bugando na wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwe wakweli tu, katika Taifa letu, sekta ya afya japo wanafanya kazi kubwa na juhudii kubwa hatujawawezesha sekta hii kibajeti waweze wakatekeleza majukumu yao inavyotakiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali yetu iko kwenye hali hii, basi inabidi kuweka vivutio rafiki, mazingira rafiki, hata tukaangalia motisha kwa sekta binafsi tuweze kupata wawekezaji wakubwa wanaoaminika waweze wakasaidiana na Serikali katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kufanya utafiti nimeona ni Aga Khan peke yake ambayo imeweza kuwekeza zaidi ya shilingi bilioni 200 kwa sasa kwenye sekta ya afya.

Wako wapi wawekezaji wakubwa kama Aga Khan wawekeze ili afya ya Mtanzania, utu wa Mtanzania ukaweza kupata nafasi yake? Duniani kukojie, nikiangalia namna gani tunaweza tukafanya *a medical tourism* katika maeneo fulani hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natoka Vunjo, pale Vunjo tuna Hospitali ya Kilema ya Kanisa Katoliki, ubia na Serikali; tuna Hospitali ya Marangu ya KKKT; Kirueni wanaanzisha hospitali yao kule Mwika ambapo wana vifaa vya kisasa; wana *MR/na CT Scan*, lakini hawana majengo ya kutosha. Vifaa hivi wamepata Canada, Serikali ishirikiane nao ili hata watu waweze kutoka nje kuja kutiba Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale kuna kupanda Mlima Kilimanjaro; hali ya uokoaji wa wapanda Mlima Kilimanjaro, miundombinu rafiki tunailfanyaje? KCMC iko pale, tunatokaje ndani ya *box* ili tuweze kusema eneo fulani tunatengeneza *a medical tourism* na *facilities* za kutosha zipo na tukaacha *ku-export* au kwenda kutafuta huduma za afya nje ya Watanzania? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hayo kwa sababu ukiangalia huduma zinazotolewa hapa kwetu Tanzania, na mimi ni mhanga, Mheshimiwa Waziri unajua hilo. Ni kwamba inabidi tujitoe na tufikiri kwa mapana kwamba namna gani uhai wa mwanadamu; nimesoma kitabu cha Biblia Takatifu leo asubuhi Yoshua bin Sira ule mstari wa 16:30 inasema: "Hakuna utajiri ulio bora kuliko afya ya mwili na hakuna furaha iliyo bora kuliko furaha moyoni." (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia Tanzania leo hii tumewekwa wapi kwenye *happiness index*? Tumewekwa pamoja na Yemen, Syria na Burundi. Tumeshika nafasi ya 153 kati ya nchi 156. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa lazima tutoke tufikiri kwamba kwa nini hatuna furaha moyoni kwenye mambo ya ustawi na kwenye afya zetu? Tukiangalia, Watanzania ni wagonjwa kiasi gani kwenye utafiti? Wataalam wetu

tunawasaidia kiasi gani? Kama huyu ni daktari, unamwezesha namna gani? *On call allowance, risk allowance*, huduma nyinginezo ambazo madaktari wetu hawazipati, waka-concentrate kwenye kutibu tu na masomo yao ya sayansi yalivyo magumu? Unakuta daktari wetu huyu ana fuga kuku, huyu ana *bar*, huyu ana enda kutafuta *income* nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni namna gani tunawaheshimu madaktari wetu? Kwa mfano, daktari ana kitambulisho chake, akipita polisi anamsimamisha, umeongeza *speed*, amwambie ninawahi kwenda kutibu, polisi anamwachia. Huwezi ukamweka daktari kwenye kundi moja na walevi. *You cannot do things like that.* (*Makofii*)

Mjeshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lazima tufikiri kwa mapana, ni namna gani tunawapa *incentives* madaktari wetu waweze kufanya *research*. Wizara yako inatuonesha, kuna upungufu wa wataalam zaidi ya asilimia 50 katika sekta ya afya. Wauguzi, Manesi, Madaktari wenyewe, Madaktari Bingwa na kwingineko. Namna gani tunafanya *in training* na *out training*? Nitoe mfano, *think globally*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi uliopita nilikuwa *Zydus Hospital*; imeajiri watu wauguzi wake pamoja na madaktari zaidi ya 1,200; lakini wanaotibwa pale kila siku, wanaoingia na kutoka pamoja na waliolazwa na madaktari wote kwa pamoja ni zaidi ya watu 5,000 kwa siku. Ni shirika kubwa ambalo limewekeza kweli kweli. Serikali ya India imeshirikiana nao namna ya kutoa huduma iliyo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kuna mtaalam mmoja anaitwa Dkt. Daria Singh, anaweza akafanya operesheni nne kwa siku moja ya *knee replacement* na *accuracy* asilimia 100. Anafanyaje? Ni kwamba huyu amewezeshwa vizuri, amefikiri vizuri, anajua kazi yake anaifanyaje. Sasa hebu tujulize hapa kwetu, kulikoni? Kuna nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni vyema Mheshimiwa Waziri tukafanya...

(Kengele ya kwanza ililia)

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Naibu Spika, niliomba dakika kumi, siyo dakika tano.

MBUNGE FULANI: Endelea.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema tukafanya *in training na out training*, yaani tukaomba wataalam kama hawa wa *Zydus Hospital*/wakaja kutusaidia kufundisha humu ndani, na sisi tukaenda tukasoma kule kwao. Wataalam wetu tukafanya programu ambazo ni *exchange program* na tukaweka mazingira yaliyo rafiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuje kwenye vitendea kazi. Kwa mfano, Waheshimiwa Wabunge hapa leo hii wanazungumzia *X-Ray* kwenye mikoa. Kweli hii ni karne ya kuzungumzia *X-Ray, CT Scan na MRI?* (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulizungumzia na Serikali imeahidi miaka nenda rudi kuhusu *linear accelerator* kwa ajili ya wagonjwa wa kansa; mpaka leo hii hakuna *linear accelerator* nchi hii. Tulikuwa tunamsifia sana Dkt. Janabi na wenzake hapa, mambo ya *Cardiac Cath. Lab.*; Tanzania tunazo tatu tu, ambapo tuna *population* ya watu zaidi ya milioni 50 *compared* na wenzetu wa Kenya wanazo *Cardiac Cath. Lab.* zaidi ya tisa. Wako kwenye hali bora kuliko sisi katika mazingira haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukimsoma Yoshua bin Sira sura ya 30:17 inasema: "Afadhalii kifo kuliko maisha ya taabu na pumziko la milele kuliko ugonjwa wa kudumu." Ukijaribu kuangalia ni kwa nini anasema hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tujiulize kweli afya zetu, ilivyotokea kikombe cha kwa babu kinatibu, karibu nusu ya

Serikali yote ilikimbilia kwa babu kwa sababu unaweza kuona afya yako siyo nzuri. Sasa tunafanyaje? Miundombinu ile tuliyopeleka kule, tunaiwezeshejaje sekta hii ya afya ili afya za Watanzania ziwe bora? Tuwe wakweli kwamba afya za Watanzania ziko hoi bin taabani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bima ya Afya hospitali nyininge zinakataa, hasa hospitali za watu binafsi kwa sababu haitoshelezi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nayapongeza sana mashirika ya dini. Niwe mkweli kabisa! Nawapongeza sana KKKT, Wakatoliki pamoja na BAKWATA kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuwekeza kwenye sekta ya afya. Sasa tuwape lugha nzuri, tushirikiane nao vizuri; wao wana mtandao mkubwa duniani waweze kuleta ile *technology* na ile misaada tukashirikiana kwa pamoja, kwa kuwa dunia yetu hii ni kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba chonde chonde, inaonesha hata kwenye kitabu chako na kitabu cha Kamati kuhusu lishe, hali ya Tanzania lishe siyo nzuri. Hili tatizo la lishe lilianza tangu miaka ya 1978 pale...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa atafuatiwa na Mheshimiwa Getrude Rwakatare na Mheshimiwa Selemani Zedi ajiandae.

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Afya. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri wanazozifanya. Kwa kweli suala la afya sasa Tanzania tumefika mbali sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Ummy, wewe ni Jembe. Kwa kweli unatosha. Hukuchaguliwa kimakosa katika nafasi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwa kuipongeza na kuishukuru sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kusikiliza maoni ya Wabunge wao na hasa kwa kunisikiliza mimi Mbunge wa Wanawake wa Mkoa wa Mara na Mbunge ambaye ni Rais wa Wabunge wote wa Mkoa wa Mara. Kwa kuwa niliongelea suala la Hospitali ya Rufaa ambayo ni Hospitali ya Kwangwa, kwa kweli nilipoingia tu Bungeni niliongelea na baada ya kuongelea sasa tupo kwenye bajeti. Kwa kweli nami katika Mkoa wa Mara nitaandikwa kwenye wino wa dhahabu. Nashukuru sana kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniamini, ananiona ni Mbunge ninayefaa na kutosha ndiyo maana nakuwa mwakilishi mzuri Mkoa wa Mara, amekuwa akinipa vifaa ambavyo nimekwishapeleka katika Wilaya za Bunda, Tarime, Serengeti, Rorya na Wilaya nyingine. Kwa kuwa wale wananchi wanaponitura mimi nafanya kweli, ndiyo maana Mheshimiwa Rais ananiona kupitia kwa Mheshimiwa Ummy. Kwa kweli ninajisifia kwamba ninatosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba suala lingine, namwomba Mheshimiwa Waziri Ummy aangalie sana sasa suala la zahanati zilizopo kwa Mheshimiwa Getere ambaye sasa naye anatakiwa apate huduma hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali yangu kwa sababu inawahudumia sana Wapinzani. Majimbo yote iliyopeleka vifaa ni ya Wapinzani. Sasa na hili Jimbo la Mheshimiwa Getere jamani ambalo halina kitu chochote ambalo ndiyo la CCM, chama kilichopo madarakani sasa na lenyewe lipelekewe vifaa kwa sababu halina vifaa katika zahanati zake zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kuna zahanati ya Hunyali ambayo aliifungua Waziri Mkuu, haina vitanda, mashuka na kadhalika, ambapo vyote hivyo Mheshimiwa Rais alinipa kupitia Mheshimiwa Waziri Ummy na nikavipeleka kwenye Majimbo ya Wapinzani ambayo ni Bunda, Tarime na Serengeti. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye hiyo zahanati ya kwa Mheshimiwa Getere katika Kata ya Kihumbu kuna hospitali ambayo inatakiwa *finishing* ambayo ni madirisha na milango. Mheshimiwa Ummy nakuomba uandike tafadhali, nina imani unanisikiliza. Pia kuna *dispensary* ya Hunyali, kipekee naomba Mheshimiwa Waziri aichukulie kwa umuhimu zaidi kwa sababu jiwe la msingi aliweka Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu ambaye ametoka kule siku siyo nydingi sana. Sasa Mheshimiwa Ummy akimaliza tu kwenye hili Wizara yake, nina imani kabisa nitapeleka hayo mashuka na vitanda kwa maana sasa hivi bajeti imekaa sawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naishukuru sana Serikali yangu kwa kweli iko vizuri inafanya kazi nzuri. Kwa kweli tumetoka kwenye asilimia 50 mpaka sasa hivi tuko kwenye asilimia 98, anayebisha simuoni wala. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri wanazofanya na hasa Mheshimiwa wetu Dkt. John Pombe Magufuli kupitia jembe lake la ukweli Mheshimiwa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Agness. Mheshimiwa Dkt. Getrude Rwakatare atafuatiwa na Mheshimiwa Seleman Zedi na Mheshimiwa Salma Kikwete ajiandae.

MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi. Naomba awali ya yote nimshukuru Mungu, Baba yetu wa Mbinguni ambaye ametuazima uhai, anatupa afya njema na tuko Bungeni kwa furaha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa niwadhibitishie kwamba ndani ya Bunge mna *Bishop*, ndani ya Bunge mna Mchungaji ambaye haachi kuomba kwa ajili ya Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wote na Bunge zima; wa CCM na hata Wapinzani, wote ninawaombea Mungu awape kibali kwenye Majimbo yenu kwa jina la Yesu.

WABUNGE FULANI: Amen.

MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE: Namwomba Mungu awape afya njema katika Jina la Yesu.

WABUNGE FULANI: Amen.

MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE: Naomba Mungu awape maneno matamu, kila mnalolisema liwe sukari masikioni mwa wasilizaji.

MBUNGE FULANI: Na mabarabara.

MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE: Yaani mwende kifua mbele kwa kibali kwa wanaume na wanawake.

WABUNGE FULANI: Amen! (*Makofi/Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Washa *microphone*.

MBUNGE FULANI: Muda umeisha. (*Kicheko*)

MHE. MCH. GETRUDE P. LWAKATARE: Ahsante. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa napenda nitoe shukrani za dhati kwa Rais wangu kipenzi, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ambaye ameniteua na leo niko Bungeni pamoja nanyi. Mungu ambariki, ampe maisha marefu. Tunapongeza kazi anazozifanya mpaka nchi jirani wanatetemeka. Kwa kweli ni mtu mwema, ni jembe, ye ye hakika ni *bulldozer*, anafanya vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwa mwenye dhamana ya Wizara hii. Namshukuru kipekee kabisa na nimpe pongezi nyingi Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwa kazi nzuri unayoifanya. Wanawake wenzako tunajivunia. Kwa kweli hujatuaibisha. Kila kitu unafanya kwa umakini.

T A A R I F A

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rwakatare kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Bungara.

MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Naibu Spika, hata kwenye maombi jamani! (*Kicheko*)

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anayezungumza sasa hivi, kuna lugha ya maudhi ameitumia kusema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni *bulldozer*. Ni kauli ya maudhi kusema kweli. Haiwezekani Rais wetu kuitwa *bulldozer*. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bungara hiyo sasa siyo taarifa, kwa sababu hiyo maana yake nimuulize, anakubali au anakataa? Wewe ungeenda zako kwenye Kanuni ya 64 pale, sasa hujaenda kule.

MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE: Na yeye namwombea.

NAIBU SPIKA: Kwa hiyo, Mheshimiwa Rwakatare unaikubali taarifa hiyo?

MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Naibu Spika, naikataa ila namwombea, Mungu amsaidie. (*Makofii*)

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimeshaombewa. (*Kicheko*)

MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kipekee kabisa nimshukuru Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na wasaidizi wake wote. Tunasema mabadiliko makubwa tunayaona, asiyekuwa na macho shauri yake. Ukweli tumeona kwamba huduma zilizokuwa zinapatikana nchi za nje, sasa hivi zinapatikana hapa hapa Tanzania, umejitahidi. Siyo hivyo tu, upatikanaji wa dawa sasa hivi ni 85% na bado unasema utaongeza zaidi. Jamani, uimarishaji wa huduma katika vituo vyetu vya afya na hospitali, tumeona huduma za afya zimeimarika kwa kiwango kikubwa sana, tunashukuru na kwa sababu muda wangu ni mfupi, ningependa tu niende moja kwa moja kwa kile ambacho ningependa kuchangia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kuhusu kinga, tiba bila malipo. Magonjwa mengi yanayotupata Watanzania kwa sababu wengi wanakosa elimu ya kutosha. Nilikuwa naomba tuongeze, kwa mfano, UKIMWI; UKIMWI ni ugonjwa ambao unaweza kuepukika. Tuombe viongozi hata wa dini kwenye mahubiri yao waongeze juhudii ya kuweza kuwaambia watu, wanandoa waweze ku-stick na rafiki au na mke mmoja ambaye atawenza kumsaidia, yaani kama Waembrania 13:4 inasema: "Ndoa iheshimiwe na watu wote, malazi yawe safi."

TAARIFA

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rwakatare, kuna taarifa. Mheshimiwa Cecil Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu Mama Rwakatare ni mchungaji na inaaminika kwamba kuna watu ambao wanaombea hata watu wenye

UKIMWI wanapona. Sasa sijui Kanisani kwake haya maombi yapo kwa ajili ya kuisaidia Serikali kupunguza matumizi? (*Kicheko/Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwambe hilo sijui atakujibuje. Mheshimiwa ulikuwa unapewa taarifa. Je, taarifa hiyo unaipokea ama unaikataa?

MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea. Ni nzuri na ninaombea. Awalete wengi niwaombee wapone, Mungu yupo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasema kwa habari ya kitabu cha Waebrania 13:4, "Ndoa na iheshimiwe na watu wote, malazi na yawe safi, washerati na wazinzi Mungu atawahukumia adhabu ya magonjwa yasiyotibika." Magonjwa yasiyotibika ni UKIMWI na mwengine. Kwa hiyo, kama mtu akiweza kukaa na mke wake bila kwenda mchepuko au nyumba ndogo, uhakika watampendeza Mungu, lakini zaidi sana watajikinga na magonjwa. Watalea watoto wao, kifo ndiyo kitawatenganisha. (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mchungaji Rwakatare kwa mchango huo. Mheshimiwa Selemani Zedi atafuatiwa na Mheshimiwa Salma Kikwete na Mheshimiwa Amina Makilagi, ajiandae.

MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia (*Kicheko/Makofi*)

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nachangia kwa niaba ya Mheshimiwa Selemani Zedi na jina langu lipo huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia Wizara hii ya Afya, napenda kuishukuru sana Serikali kwa Mkoa

wangu wa Mwanza, wametupa shilingi bilioni tatu na tumeweza kufanya ukarabati Vituo vyta Afya zaidi ya saba kikiwemo Kituo cha Kahangara (Magu); Karume (Itemela), Kome (Buchosa); Kagunga (Serengema), Mallya (Kwimba), Lugeye (Magu) pamoja na Misungwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali kwa kuweza kutoa fedha hizi ili kuweza kuboresha huduma ya afya katika Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena kuchangia katika suala la saratani ya shingo ya uzazi. Ni jambo jema kwamba Serikali sasa imeleta chanjo ili kuwachanja watoto wenyе umri wa miaka 14. Naomba kuishauri Serikali kwamba sasa iangalie kwenda kwenye *phase II* ambayo ni ya watoto wa kike wenyе umri wa kuanzia miaka 15 mpaka miaka 25. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kuishauri Serikali kuangalia ni namna gani wanaweza wakaanza pia na watoto wenyе umri wa miaka tisa, kumi na kuendelea mpaka hiyo 14. Kwa sababu gani naishauri Serikali kufanya hivyo? Umri wa miaka tisa mpaka 14 watoto wetu sasa hivi wameanza kungia katika masuala ya kujamiihana mapema sana. Ni vyema sana kuwakinga ili kuwaepusha kupata saratani ya shingo ya uzazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, saratani ya shingo ya uzazi inaambukizwa kwa magonjwa ya kujamiihana. Kwa hiyo, nashauri sana watoto wetu kuanzia miaka 9 hadi 14 na wao pia Serikali iwaangalie ni namna gani wanaweza wakawapatia chanjo. Pia watoto wa kiume wanaweza wakapatiwa chanjo ya *Gardasil* pamoja na *Gardasil 9* ambayo inaweza ikawasaidia kuwakinga watoto wa kike wasipate maambukizi ya kujamiihana na hatimaye kupata saratani ya shingo ya uzazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuongelea suala la ugonjwa wa *myoma*. Ugonjwa wa *myoma* ni ugonjwa ambao unawapata akina mama, wanapata uvimbe katika

kizazi na inapelekea wanawake kutolewa kizazi na hatimaye kukosa watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali kuweza kusaidia kufanya utafiti wa ugonjwa huu kwamba upo kwa ukubwa kiasi gani? Kuna siku utakumbuka katika Bunge hili wanawake wote walismamia kuchachamaa kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya wa kipindi hicho alisema ugonjwa huu siyo mkubwa na siyo hatarishi. Wanawake wote humu ndani walishangaa na wakanyanya. Ninaomba Serikali iweze kufanya utafiti wa ugonjwa huu wa myoma kwa sababu ni ugonjwa ambao unawamaliza sana wanawake, wanakosa watoto katika umri mdogo sana kuanzia miaka 25 hadi 35. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuongelea suala la utoaji huduma wa afya kwa akina mama wajawazito kuhusiana na suala la *delivery packs*. Serikali ilizitoa *delivery packs* bure kwa mwaka mmoja tu na baada ya hapo wanawake wengi tumekuwa tukiuliza maswali ndani ya Bunge na kujibiwa kwamba *delivery packs* zinakuja. Serikali cha kusikitisha sana *delivery packs* sasa tumeambiwa kwamba zinauzwa na bahati mbaya sana zinauzwa shilingi 21,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake huko vijijini hawana uwezo wa kununua hizi *delivery packs* kwa bei hiyo. Niniomba Serikali irudie kuangalia upya gharama za bei ya *delivery packs* angalau basi zishuke bei hadi kufikia shilingi 10,000. Kwa sababu kwenye *pharmacy* nyingine huko mjini wanauza shilingi 10,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *delivery packs* siyo la muhimu sana. Tunatarajia mama mjamzito anapofika hospitali, kuna *delivery kit* ambapo *nurse* anapotoka kwenda kumhudumia huyu mama wakati anajifungua, anapoenda kufanya ile *procedure*, anaondoa vifaa vinavyohotajika kutoka kwenye *delivery kit* ili apate *delivery pack* aende kumsaidia yule mama aweze kujifungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, utaona hili suala la *delivery packs* sio la lazima sana Serikali kutoa bure, lakini waangalie ni namna gani wanaweza wakapunguza bei ili wale wanaoweza kununua waweze kununua.

Mheshimiwa Naibu naunga mkono hoja. Nashukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Salma Kikwete atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Makilagi na Mheshimiwa Mariam Kisangi ajiandae.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Hatimaye nikushukuru wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye Wizara hii ya Afya ambayo ni muhimu sana kwa ustawi na maendeleo ya mwanadamu katika muktadha ufuataao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, usipokuwa na afya njema huwezi kwenda shule; usipokuwa na afya njema maendeleo hayawezi kufanyika; usipokuwa na afya njema kitu kitakachojitokeza hata uchumi wa Taifa letu utapungua kwa ajili ya kukosa nguvu kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaifanya katika Taifa letu. Sambamba na hilo namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Afya pamoja na Naibu wake na watendaji wote wa Wizara hii bila kuwasahau madereva na wahudumu ambao wanafanya kazi nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii kwa kutupatia fedha kiasi cha shilingi 1,200,000,000 katika Jimbo la Lindi Mjini. Shilingi milioni 400 zimetolewa kwa ajili ya Hospitali ya Kituo cha Afya cha Mingoyo, lakini shilingi milioni 700 zimetolewa kwa ajili ya

Kituo cha Afya cha Mnazi Mmoja. Tunaishukuru sana Serikali.
(Makofî)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, pamoja na mazuri ambayo yameweza kujitokeza, lakini Lindi tuna mambo yafuatayo; hatujajua hatma yetu ya Mkoa wa Lindi kuwa na Hospitali ya Mkoa na Hospitali ya Wilaya. Ukiuliza hivi, unaambiwa Sokoine ni Hospitali ya Mkoa. Wakati mwингine unaambiwa Sokoine ni Hospitali ya Wilaya. Mheshimiwa Waziri, naomba utakapokuja hapa utupe ufanuzi juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kama Mkoa wa Lindi na kama ambavyo Hospitali ya Sokoine iko pale, lakini kikubwa Mganga Mkuu wa Hospitali ya Mkoa hana gari la kufanya huduma. Sizungumzii *ambulance*, tunazungumzia gari la kufanya huduma, anatumla gari binafsi kuendeshea shughuli za Serikali. *(Makofî)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 28 tu ndiyo ya wahudumu waliopo ndani ya Mkoa wa Lindi. Tuna upungufu wa asilimia 72. Naomba hili liangaliwe kwa jicho la huruma. *(Makofî)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya UKIMWI nchini Tanzania kwa mujibu wa *Tanzania HIV Impact Survey* ya mwaka 2016/2017, maambukizi ya wanawake ni asilimia 6.5 na wanaume ni asilimia 3.5. Hii hufanya maambukizi Kitaifa ni 5%. Sasa ndani ya Mkoa wa Lindi ni asilimia 0.3. Nawapongeza sana watu wa Mkoa wa Lindi kwa kupunguza kiasi kikubwa cha maambukizi. *(Makofî)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maambukizi ya UKIMWI yana vitu mbalimbali ambavyo vinasababisha. Kwa hiyo, tuna wajibu sisi kama Watanzania kuepuka vitu vile ambavyo vinaambukiza ili pesa hizi zitakazopatikana baada ya kutumika kununua madawa na vitu vingine, zitumike katika mazingira ya kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo katika nchi yetu. *(Makofî)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia ARVs ndiyo dawa zinazotumika kufubaisha virusi vya UKIMWI. Sasa hizi dawa ziende kwa wakati kwa kunusuru maisha ya watu hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vifo vya akina mama na watoto; haikubaliki nchi kama Tanzania, mwanamke kufa wakati analeta kiumbe kingine duniani. Tunajua kuna mipango na mikakati mizuri sana iliyowekwa, lakini ni lazima itekelezwe na iwekwe kwa wakati. Kuna magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama figo, *pressure* na kisukari. Ni lazima yawekewe mikakati madhubutili kuhakikisha mazingira haya yanakuwa salama katika nchi yetu. Yote haya yanawezekana tu kama bajeti iliyopangwa na Serikali itapelekwa kwenye maeneo husika kwa wakati na ikiwa timilifi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Amina Makilagi atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Kisangi na Mheshimiwa Kuchauka ajiandae.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niungane na wenzangu kuchangia hoja iliyombele yetu. Kwa kuwa leo nina dakika tano, nitaenda kwa haraka kama ifuatavyo; Mungu anisaidie niweze kuzitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ya kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kunipa afya. Namshukuru yeye kwa sababu bila yeye nisingeweza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee niendeleee kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa uthubutu wake na kwa dhamira yake na

kuhakikisha sekta ya afya inakwenda kuleta tija kwa wananchi kwa kuhakikisha anapeleka fedha za dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika nchi yetu ni 5% zinakwenda kwa wananchi. Kwa utayari wake sasa, Mheshimiwa Rais wetu anaboresha vituo vya afya, hospitali za wilaya na hospitali za rufaa. Nani kama Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachowezza kusema ni kwamba awasamehe ambao hawajui watendalo, kwa sababu waswahili wanasema, akutukanaye hakuchagulii tusi. Ukiwa kwenye maji unaoga, akija mwendawazimu, humfukuzi. Hata waliosema kuna fedha zilipotea na wenyewe pia awasamehe kwa sababu leo ufanuzi umetolewa mzuri na ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya utangulizi huo, namshukuru sana Waziri na timu yake. Mwenyewe Mheshimiwa Ummy na Katibu Mkuu. Kusema kweli unapoona mambo mazuri, ujue kuna Watendaji na viongozi wazuri. Taarifa imeandaliwa vizuri na kazi inaendelea vizuri, hongera sana. Endeleeni kuchapa kazi, nchi yetu iweze kufika pale tunapohitaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na Mheshimiwa Agness Marwa kuleta shukrani za wananchi wa Mkoa wa Mara kwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kujenga Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara, *Mwalimu Nyerere Memorial Centre*. Hospitali hii kwa muda mrefu tangu ukoloni imejengwa kwa nguvu za wananchi. Wananchi wa Mkoa wa Mara walichanga fedha nydingi na kilikuwa ni kilio cha muda mrefu. Kwa uongozi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, sasa hospitali inajengwa na fedha zinakuja. Tunamshukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachokiomba sasa aendelee kutenga fedha, mahesabu yameshafanyika, zinahitajika shilingi bilioni 24. Fedha zipelekwe ili Hospitali ya

Rufaa *Memorial* kwa ajili ya wananchi wa Mkoa wa Mara iweze kujengwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivyo kwa sababu katika Kanda ya Ziwa Hospitali ya Bugando imelemewa. Hospitali ya Bugando inahudumia mikoa zaidi ya tisa. *Population* ya watu kwa mujibu wa sensa ni watu zaidi ya shilingi milioni 15 ni pamoja na Kanda ya Magharibi. Hospitali ya Bugando inapokea watu wa ugonjwa wa kansa. Kwa mujibu wa utafiti uliofanyika Kanda ya Ziwa ndiyo watu wanaathirika sana. Hospitali ya Bugando kwa siku inapokea wagonjwa zaidi ya 50 kwa siku wanaokuja kwa ajili ya mionzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Bugando haina hospitali hata ya kulaza wagonjwa wa kansa. Pamoja na kuishukuru Serikali kwa kuboresha Hospitali yetu ya Bugando ambayo inahudumia wananchi wa Kanda ya Ziwa wakiwemo na wa Magharibi na hata wa nje ya nchi, ninaomba sasa fedha zipelekwe ili hiki kituo cha kulaza wagonjwa wa kansa kiweze kupatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naishukuru sana Serikali kwa kupeleka fedha kwa ajili ya kujenga vituo vya afya hapa nchini. Ni ukweli usiopingika kwamba kazi imefanyika vizuri, ushauri wangu sasa, katika bajeti inayoendelea na itakayokuja baadae, ninatoa ushauri kwa sababu nimekuwa nikitembea nchi nzima, ninaomba muwe mnaangalia na maeneo ya pembezoni. Mfano, Wilaya ya Nyasa, Wilaya mpya, ina kituo kimoja cha afya cha Serikali. Wananchi wote wanahudumiwa pale. Hospitali ile haina hata gari la kubeba wagonjwa na vilevile Wilaya ya Nyasa haina hata barabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mtakapokuwa mkipeleka magari ya kubebea wagonjwa na hata kupeleka vipaumbele vya hizi fedha kwa ajili ya kujenga Hospitali za Wilaya, na Vituo vya Afya, angalieni hapa ikiwemo na Musoma Vijijini imekuwa ni Wilaya ambayo imekuwa inaitii sana Serikali. Tumejenga shule nyngi kwa nguvu za wananchi,

kuanzia msingi mpaka lenta; kila kata tumejenga. Sasa kwenye wilaya kama hizi ambazo tulijielekeza kwenye elimu, nilikuwa naomba na kwenye vituo vya afya, hebu angalieni na Musoma Vijijiini. Tuna Kituo kimoja cha Mlangi ambacho kinahudumia kama Wilaya nzima ya Halmashauri ya Musoma. Musoma ina Hospitali ya Rufaa, lakini *population* ya watu wamekuwa ni wengi, haiwezi kuhudumia katika maeneo mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie upungufu wa wataalam katika sekta ya afya. Kwa mujibu wa taarifa zilizowasilishwa, hali ni mbaya. Madaktari hasa mabingwa hakuna, hata huko Bugando kuna upungufu mkubwa sana. Hata Hospitali ya Mkoa wa Mara tuna madaktari wawili tu. Siyo Mara peke yake kwa sababu, mimi Jimbo langu ni Tanzania nzima. Katika hospitali zote nilizozitembelea na hata Vwawa juzi nillikuwa Mbozi, hali ni mbaya. Tunaomba Serikali itenge fedha kwa ajili ya kuwapeleka wataalam katika hospitali zetu na hasa Madaktari Bingwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nitoe ushauri, nendeni mkaongee na Watanzania walioko Botswana. Mimi nilishaanza kufanya nao mazungumzo; wako tayari kurudi nyumbani kwa manufaa ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, muda ni mfupi, naomba kuunga mkono na mambo mengine nitayaleta kwa maandishi. (*Makofi*)

Mhesimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mariam Kisangi, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Toufiq, halafu Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka salama na kuweza kuwa na afya njema kwa siku ya leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa umuhimu mkubwa napenda nimpungeze Mheshimiwa Rais wangu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa utendaji wao mwema uliotukuka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe shukrani za dhati kwa Chama cha Mapinduzi - Mkoa wa Dar es Salaam kwa jinsi walivyopata shida, walivyohangaika na uchaguzi na hatimaye tukampata Mbunge mahiri, Mheshimiwa Mtulia wa Kinondoni. Kwa kweli ni jambo la kutukuka katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam. Chama cha Mapinduzi kimepata nyongeza ya Mbunge, sasa tuko *fifty-fifty*. Ahsanteni sana akina mama wote wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa jinsi mlivyowajibika katika kupata nyongeza ya Mbunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nlende kwenye Wizara ya Afya. Napo napenda nimpungeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara ya Afya kwa kazi kubwa wanayoifanya kuwahudumia wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika huduma za afya katika Mkoa wa Dar es Salaam zimeimarika kwa kiwango kikubwa sana. Napenda niipongeze Serikali kwa jinsi ilivyoimarisha huduma ya afya ya mama na mtoto katika Mkoa wa Dar es Salaam. Nawapongeze sana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, timu yake, Wakurugenzi na Wakuu wa Wilaya zote za Mkoa wa Dar es Salaam jinsi wanavyoshirikiana katika kuhakikisha wanaboresha huduma za afya ya mama na mtoto katika Mkoa wa Dar es Salaam. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe shukrani za kipekee kwa Kampuni ya *Arms Groups* ambayo imeweza kutujengea Hospitali za Afya ya Mama na Mtoto katika Hospitali ya Amana, lakini wanatarajia kwenda Mwananyamala na Temeke pia. Nampongeza sana mfadili huyu na ninamwambia fungu lako utoalikuta kesho kwa Mwenyezi Mungu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nizungumzie juu ya huduma hizi zinazotolewa na Serikali, zizingatie idadi ya watu. Jimbo la Mbagala lina takribani idadi ya watu 1,100,000 lakini mpaka sasa hivi hospitali iliyopo ya Zakiem imezidiwa. Najua juhudzi za Serikali wanataka kuboresha Hospitali ya Maji Matitu, lakini naiomba Serikali iiongezee pesa iwe hospitali kubwa. Idadi ya watu imezidi Mbagala na watu wanaongezeka kila siku. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naiomba Serikali iangalie eneo la Mbande. Kama ilivyo wanafunzi wa shule, madarasa hayatoshi kila siku, lakini na idadi ya watu inakuwa ni wengi, akina mama ni wengi, huduma inayotakiwa ya afya kule ni kubwa. Wakati tunaangalia maeneo gani tupeleke huduma tuzingatie na idadi ya watu. Akina mama wa Mbande na wananchi wa Mbande ambako wanakutana na Mkoa wa Pwani na Wilaya ya Ilala, pamoja na kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya kuweka ile Hospitali ya Chanika, lakini bado hawa watu wa Mbande wanakuja Zakhiem na Temeke hivyo. Naiomba Serikali iangalie hilo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niende kwenye Hospitali ya Mloganzila. Hospitali hii ni kubwa na nzuri, naipongeza sana Serikali, lakini bado ina upungufu wa madaktari na wauguzi. Wale ukifika pale unaambiwa mgonjwa wako huruhusiwi kumhudumia. Weka uji, weka maziwa hapo, lakini unakuta wodi nzima ina ma-nurse watatu, wagonjwa 50. Watawanyweshaje huo uji? Hata iweje, lazima kuna wengine watakosa huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachonishangaza, lengo la Serikali katika kuanzisha ile Hospitali ya Mloganzila ni kwenda wanafunzi wanaojifunza udaktari na wanaojifunza uuguzi, wakajifunzie. Sasa wale wanafunzi, hivi hakuna wanafunzi wa *practical?* Wanafanya nini? Kwa nini wasiungane na wale ma-nurse na madaktari katika kusaidia wagonjwa? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli madaktari wale na wauguzi wana kazi. Kunywesha kila mmoja umnyweshe

na haruhusiwi ndugu yejote kubaki pale, hili ni tatizo. Naiomba Serikali iangalie, kama imeshindwa kabisa, waache hata ndugu mmoja aweze kutoa huduma kwa mgonjwa wake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Serikali nayo iimarishe vitengo vya mifupa katika hospitali za wilaya na mikoa ili kusaidia mzigo mztio utakaoenda *MOI* - Muhimbili. Naomba Hospitali ya Muhimbili wangalie gharama... (*Makof*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mariam Kisangi, muda wako umekwisha.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la ucheleweshwaji wa bili kwa wagonjwa. Hilo ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, mengine nitayaleta kwa maandishi. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Fatma Toufiq atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka na Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji ajiandae.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa nami kuchangia katika bajeti hii. Naomba nichukue fursa hii pia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo naomba nichukue fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote kwa kuandaa hotuba hii. Naomba nichukue fursa hii pia kuipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Rais kwa kutoa kipaumbele kwa afya katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 21 wa hotuba hii Serikali imebainisha ongezeko la maboresho ya vituo vya afya ili kuweza kutoa huduma za dharura. Pia naipongeza sana Serikali lila napenda kufahamu, pamoja na kutoa huduma za dharura; je, Serikali imejipangaje kwa ajili ya kupata vifaa mbalimbali ikiwemo vifaa vya *Ultra Sound*, *X-Ray* sambamba na hilo pamoja na wataalam? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuipongeza Serikali kwa kujitahidi kuongeza uwezo kwa baadhi ya Watendaji wa Idara ya Afya. Naomba niishauri Serikali pia iweke mkakati wa muda mrefu wa kuweza kupata wataalam wa afya zaidi. Kwa sababu wenzangu wengi wamelizungumzia, tuna upungufu mkubwa sana wa wataalam wa afya.

Kwa hiyo, nillikuwa naomba niishauri Serikali, iandae mkakati wa muda mrefu wa kuhakikisha kwamba wanapatikana watendaji wa afya wengi zaidi kwa kupewa elimu na kutoa kipaumbele ili kusudi waweze kupatikana hawa Watendaji katika Idara ya Afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Dodoma, pia na sisi tuna upungufu mkubwa sana wa rasilimali watu na tuna karibu 60%. Kwa hiyo, naomba nitoe shime kwa sababu Mkoa wa Dodoma ni Makao Makuu, hebu Serikali ione iiangalie Mkoa wa Dodoma kwa jicho la kipekee kwa kuwapatia watendaji. Naishukuru tena Serikali ya Awamu ya Tano kwa kutenga shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali za Wilaya katika baadhi ya Wilaya za Mkoa wa Dodoma ikiwemo Wilaya ya Chemba, Wilaya ya Chamwino, pamoja na Wilaya ya Bahi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Dodoma imeonekana kwamba kuna ongezeko sasa hivi la maambukizi ya VVU kutoka asilimia 2.9 mwaka 2014/2015 imekwenda kwenye ongezeko la 5% mwaka 2016/2017 wakati kiwango cha Kitaifa kimepungua kutoka asilimia 5.1 kwenda asilimia 4.7. Hii *it is alarming* kwamba kwa kuwa Dodoma ni Makao Makuu na watu wengi sasa wameanza kuja hapa, hebu

Serikali ione umuhimu wa kuwa na mkakati kabambe wa kuhakikisha kwamba maambukizi haya hayaendelei tena. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda ni mfupi, naomba pia nizungumze kuhusu suala la ukatili ambalo linaendelea kwa kasi sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 97 wa hotuba hii imebainisha kwamba matukio ya ukatili katika mwaka 2016 yalikuwa ni 31,996 wakati mwaka 2017 yamekuwa 41,416. Maana yake ni kwamba matukio ya ukatili yameongezeka kwa matukio 9,420. Hii kwa kweli siyo hali nzuri, ipo sababu sasa jamii pamoja na familia waone jinsi gani ya kulea watoto wetu katika malezi mazuri ili kusudi wasiwe na tabia ya ukatili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, nawaomba viongozi wa dini wajaribu kuendelea kuwahubiria wananchi wetu ili kusudi wawewe kuwa na miyo ya uwoga na kumwogopa Mungu ili kusudi kuweza kupunguza huu ukatili. Sambamba na hilo, nilikuwa naomba pia, Serikali ione jinsi gani itafanya kuzuia ukatili badala ya kutoa takwimu nyingi ambazo zinaendelea kila siku. (*Makof*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie pia Sera ya Wazee ya mwaka 2003, kwa kweli bado haijatungiwa sheria. Kwa hiyo, nilikuwa...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Naunga mkono hoja, ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji na Mheshimiwa Aisharose Matembe ajiandae.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi mchana huu wa leo na mimi nichangie kwenye hoja iliyio mbele yetu.

Awali ya yote kama ilivyo ada na mimi nitoe shukrani zangu za dhati kwa wahudumu wanaohudumu kwenye Wizara hii hasa Mawaziri, lakini siyo Mawaziri peke yao kwa sababu hizi sifa ambazo Mawaziri wanazipata ni kwa sababu ya wale wanaowa-*support*. Kwa hiyo, nao wanastahili sifa nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Wizara hii wanaitendea haki, nami nawaombea kwa Mwenyezi Mungu waendelee kuifanya hii kazi kama ambavyo Mwenyezi Mungu atawajalia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba tu Serikali ya Awamu ya Tano, mara zote ninapoanza kuchangia pengine naweza kuonekana kama mlalamishi, lakini ni lazima ukweli usemwe. Nini Kanda ya Kusini tunaikosea nchi hii? Kwa sababu kila ninaposimama kwenye bajeti, ukiangalia Kanda ya Kusini inavyotendewa na kanda nyingine ni tofauti. Kwa nini nasema hivyo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Kanda ya Kusini hatuna Hospitali ya Kanda ya Kusini, lakini kuna Kanda nyingine tayari zina Hospitali za Kanda. Kanda ya Kusini ukiangalia kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri, pesa iliyotengwa haina tofauti na pesa ambazo zimetengwa kwenye Hospitali za Wilaya nyingine, kwenye sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Kanda ya Kusini tumetengewa shilingi bilioni moja, lakini iko mikoa au wilaya zimetengwa zaidi ya shilingi bilioni mbili mpaka shilingi bilioni nne kwenye Hospitali za Mikoa. Kwa nini Kanda ya Kusini mnatushau kwa kiwango hicho? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ukiangalia hospitali yetu ya kanda yenye kwanza haipo na wanasema ile Hospitali ya Ligula ndiyo ambayo wanaiandaa kuwa Hospitali

ya Kanda, lakini hizi shilingi bilioni moja kwanza hatuna uhakika kama zitafika. Tunaomba Serikali ya Awamu ya Tano mwiangalie Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri tu, maana nikisema lazima nitoe mifano. Kuna huu Mkoa wa Geita umetengewa zaidi ya shilingi bilioni nne, lakini Mkoa wa Geita uko Kanda ya Ziwa. Kanda ya Ziwa wana Bugando, Kanda ya Kaskazini wana KCMC; sisi Kanda ya Kusini hatuna Hospitali ya Kanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri unayehudumu kwenye hii Wizara uiangalie sana Kanda ya Kusini. Sasa naomba nirejee kwenye nafasi ya utumishi.

T A A R I F A

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kuchauka leo Mheshimiwa Bungara ana taarifa nydingi sana. Mheshimiwa Bungara.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampa taarifa, siyo Mkoa wa Geita tu umepewa hela hizo. Geita kuna Wilaya ya Chato; Chato imepewa fedha shilingi bilioni nne na Geita shilingi bilioni nne. Tunaomba hela za Chato hizo ziende Kusini. Taarifa hiyo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Geita na Chato ni Mkoa huo huo mmoja, basi hiyo ya Chato iende Kusini. Upendeleo hatutaki katika nchi hii. Ahsante sana. (*Kicheko/ Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kuchauka, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naipokea taarifa hii *hundred percent*. Nafkiri

hata mimi nili-over/look tu pale. Kwa hiyo, Geita ni shilingi bilioni tano. Kanda ya Kusini shilingi bilioni moja. (*Kicheko/Makofi*)

T A A R I F A

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kuchauka kuna taarifa nyingine.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Suala la utumishi ni jambo...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kuchauka kuna taarifa nyingine. Mheshimiwa Musukuma.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, muda wangu.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani juzi Mheshimiwa Spika alitoa mfano mzuri sana wakati Mheshimiwa Lema akimtolea mfano moja kwa moja Spika kuhusu matibabu kwamba unajua hivi vitu vinavyoongeleta vinakuwa kama mizaha, lakini humu ndani tuko watu wa Geita, tunaumia sana haya maneno mnayozungumza. Ni bora mtu unapojenga hoja, ukajenga hoja ya kutetea mkoa wako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukianza kulinganisha Geita na Kusini, tutazungumza maneno humu mtatoka hatuongei. Ukichukua *population* ya Geita na Kusini ni vitu viwili tofauti. Kwa hiyo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa ajenge hoja yake siyo kutoa mifano kwa watu ambaeo na sisi tuko huku ndani. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kuchauka unaipokea taarifa hiyo?

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, hapana. Taarifa hii haiwezi kupokelewa kwa sababu mimi nimetoa mfano. Ningeweza kutoa mfano mkoaa wowote ule, lakini kwa sababu Mkoaa wa Geita ni Mkoaa wa watani zangu, ni watoto wangu na wajukuu zangu, nikautolea mfano huo.

MBUNGE FULANI: Hapana, hatukubaliani na hilo.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naongelea suala la wahudumu. Suala hili naweza kuliona kama ni janga la kitaifa kwa sababu tatizo hili ni kubwa sana. Pamoja na juhudu kubwa ya Serikali ya kujenga miundombinu ya afya, lakini kama hatujaliangalia suala la watumishi, itakuwa hizi juhudu zote tunazozifanya haziwezi kutuzalia matunda yaliyotegemewa. Kwa mfano, nataka niwaambie kwamba jambo hili kwanza linaweza likapunguza hata ufanisi wa wale watumishi wachache na vilevile kuweza kuwaletea madhara mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kuna hospitali moja, *nurse* mmoja alipigwa makofi na mgonjwa. Sababu ilikuwa ni nini? Yule *nurse* alikuwa peke yake kwenye wodi, kuna akina mama wawili wanajifungua, mmoja akajifungua mapema kuliko yule mwingine. Wakati anamhudumia yule mama, hajamaliza hata kufunga kitovu, yule mama mwingine na mtoto ameshatoka anataka kudondoka. Sasa yule *nurse* alichokifanya, kuogopa yule mtoto asije akadondoka akafa, mama akapoteza mtoto, aliamua kumwacha yule mwingine kabla hajamfunga kitovu akamhudumia yule mwingine bila kubadilisha *gloves*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa yule mama kwa sababu aliona kile kitendo cha kumpokelea mwanae mama ambaye hajabadilisha *gloves* zenyenye damu za mama mwingine kwa kuogopa maambukizi ya UKIMWI, akamzaba makofi. Hata hivyo yule *nurse* alikuwa na mambo mawili ya kuamua, amwache mtoto aanguke afe au ampokee mtoto apate maambukizi aweze kutibiwa. Kwa hiyo, hili suala tunaweza kuliona dogo, lakini ni kubwa sana. Uhaba wa ma-*nurse* na madaktari ni mkubwa sana. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri ulichukulie katika muktadha huo kwamba hili jambo ni la muhimu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nilitaka niongelee kwenye hospitali yangu ya Wilaya ya Liwale. Hospitali ya Wilaya ya Liwale ina wodi tano kama juzi nilivyosema. Wodi moja ya wazazi, moja ya wanaume na nydingine ya watoto. Pia kuna wodi mbili za *grade II*, lakini kwa *night shift* panaingia *nurse* mmoja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu *just imagine nurse* mmoja anahudumia wodi tano, ufanisi wake utakuwa wapi? Siyo kwamba anakwenda *night atapata off*, hakuna *off* kwa sababu ya uhaba wa watumishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, niko chini ya miguu yake aiangalie Hospitali ya Wilaya ya Liwale, hali ni mbaya sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba nijielekeze kwenye upande wa lishe. Na mimi nitoe utaalam wangu kidogo, ni-*declare interest*, mimi ni msindikaji wa nafaka kwa taaluma. Tanzania hatuna Sera ya Ulaji na ndiyo maana ulaji wetu unakuwa wa hovyo hovyo na ndiyo maana tunapata magonjwa hayo yasiyoambukiza na mengine yanayoambukiza kama vile kisukari, kwa sababu tunakula hovyo hovyo. Nitolee mfano kwenye nafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, *National Milling* wakati ule tunasindika nafaka tulikuwa tunakoboaa mahindi asilimia 80, tunatoa unga kwa asilimia 80, lakini leo hii Tanzania tunatoa kwenye hizi *coat meal*/tunatoa asilimia 55 mpaka 60. Maana yake ni nini? Tunakoboaa mpaka vitamini zote tunaziondoa, baadaye sasa tukirejea kwenye mahospitali, mtu akipata sukari akienda hospitali ndiyo anaenda kuambwa kwamba ukale dona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Serikali isiweke sera tukajua kwamba *standard* ya sembe ni *standard*

inayokobolewa kwa kiwango gani au mchele, unakobolewa, unapiqwa *polish* mpaka unakuwa mweupe unapoteza kila kitu. Kwa nini Tanzania hatuna sera? Ukienda kwa wenzetu hapo Nairobi *maximum rate percent* kwamba kukoboa ngano, kwanza tunapoteza nafaka. Kwa mfano, kama asilimia 60 ndiyo *flourambayo* inatumika, ina maana asilimia 40 zote unawaachia mifugo. Sasa hata nafaka yenyewe tunapunguza. Ina maana kwamba hata njaa nayo tunaiendekeza sisi wenyewe kwa sababu ya ulaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukiingia kwenye suala hili la lishe, naomba Serikali waje na sera, ijlilikane *standard* ya ulaji kwamba chakula gani kinaliwa kwenye *standard* gani na *TBS* wawe wanafuatilia hizi *standard* ili kuhakikisha watu wetu wananzaika na masuala haya ya lishe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba niongelee kwenye hii Taasisi ya JK na ya *MOI*. Ukiangalia kwenye jedwali hapa, kamati walishasema hapa kwamba mwaka 2017 wametengewa fedha lakini zilizoenda ni zero. Kwenye Taasisi ya JK ni zero, kwenye Taasisi hii ya *MOI* ni zero. Sasa pamoja na sifa kubwa, Mheshimiwa Rais juzi alikwenda kwenye Taasisi akawasifia, lakini kwa *trend* hii ya kutowapelekea pesa mnataka wafanye nini? Kwa nini basi tunatenga hizi fedha wakati hamko tayari kuzipeleka?

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo nalisema kwenye Wizara hii, lakini linahusu sana Wizara ya Fedha. Kwa sababu Kamati zote zinazokuja mbele yetu hapa, malalamiko makubwa kwenye fedha za maendeleohaziendi. Sasa Taifa gani hili ambalo tunataka kulijenga kwamba tunakusanya pesa kwa ajili ya kulipa mishahara tu, lakini hatutengi fedha za maendeleo? Tunakusudia nini? Hivi tunataka kujenga Taifa la namna gani? Kwa sababu kila Wizara itakayokuja hapa, kila Mwenyekiti anayekuja hapa anasema fedha za maendeleohaziendi.

Mheshimiwa Naibu Spika, afya, fedha za maendeleohaziendi; Taasisi hizi, fedha ya maendeleo haiendi. Sasa ina

maana pamoja na kujinasibu kwamba Serikali ya Awamu ya Tano makusanyo yamepanda, hivi tunakusanya kwa ajili ya kulipa mishahara? Kama hatutaki kuwekeza kwenye hizi taasisi kwa kutoa fedha za maendeleo, sidhani kama tunaweza tukafanya kile tunachokusudia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba niende kwenye sera za wazee. Hapa tumeshaweka sheria nyingi sana; kuna dirisha la wazee, sijui kufanyaje wazee, kuna matibabu sugu ya wazee, lakini hawa wazee ni wapi? Kwa sababu hatujapata sheria hapa inayowatambua wazee. Ikiletwa sheria hapa, itaweza kuainisha hawa wazee tunaowakusudia ni wazee wa namna gani?

Mheshimiwa Waziri, kila mwaka tunakuomba utuletee sera hii ya wazee ili hawa wazee tuweze kuwatambua.

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Nini tatizo? Kigugumizi ni cha nini cha kuwaletea sheria hawa wazee ili watambuliwe? Mpaka leo hii tunaongelea wazee, lakini wazee wenyewe tunaowaambia tunawatengea madirisha, tunawatibu bure, bado hatujawatambua kwa mujibu wa sheria ni wazee wa aina gani?

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kichauka, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Aisharose Matembe na Mheshimiwa Innocent Bilakwate ajiandae.

MHE. MWANTUMU DAU HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia siku hii leo, Ijumaa ndiyo siku yangu adhimu aliyonikeea kipindi hiki ili niweze kuchangia Wizara hii ya Afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake.

Mheshimiwa Waziri, Mama Ummy, mwanangu nakushukuru sana na nakushukuru kwa jitihada zako unazozitendea Wizara hii ya Afya na ninakushukuru kwa jitahada zako kwamba umefika pia nami kunisaidia kufika *Ocean Road* kumpeleka ndugu na akapata uzima kuhusu *cancer*. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, dakika zangu tano, kwanza niingie suala la ukatili dhidi ya watoto na wanawake nchini. Ukatili wa watoto na akina mama umezidi hapa nchini kwetu. Umezidi mno, umekithiri, maana yake sijui mtu afanye nini hasa! Nataka kuishauri Serikali, hili suala wasilitizame kwa jicho tu hivi, waangalie kwa kina ili hili suala la udhalilishaji wa watoto na akina mama lifanyiwe kazi ili liondoke katika nchi hii. Inawezekana kwa nchi yetu hii ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mama na mtoto katika kuimarisha huduma ya afya, lazima aimarishe kwa jitihada zake na uwezo wake ambao anao. Mama anakwenda hospitali hana mbele wala nyuma, ana mtoto wake anaumwa, pengine naye pia anaumwa, anakwenda pale, hana hata shilingi. Bima ya afya pia hana, anafika pale anaandikiwa madawa anakwenda akahangaike nje ili apate pesa zimsaidie mtoto. Kuimarisha huko ndiyo kunaendelea? Hakuna. Kwa hiyo, jitihada ya Serikali itazame vilevile kwa jicho la huruma mama na mtoto waweze kusaidiwa waweze kuimarisha afya zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee na uboreshaji wa huduma ya vituo vya afya; vituo vya huduma ya afya hapa nchini niseme Wizara imejitahidi sana, lakini kwa kuingilia ndani ukaitazama katika huduma zetu za afya ndani ya madaktari wengine wanakuwa madaktari, maana yake ni kama wanawanyanya wale wanaohitaji huduma, wanaokwenda pale kutibiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu ashakwenda pale anaumwa, lakini daktari anajifanya kama yeye ni daktari, amesoma na uwezo wake, basi kumhudumia yule mtu aliyelewenda pale, mnyonge, maskini, anamnyanyapaa.

Anaona kama hakwenda mgonjwa pale. Anapiga simu au kama ana kikaratasi chake, anaendelea kusoma. Wengine utakuta wanachukua simu wanachapa zile karata katika ile simu, mna zile karata wanacheza. Mtu hajui huku kama kaja mgonjwa anaumwa amhudumie. Hilo limo katika vituo vyetu, nakuomba uliangalie kwa kina katika vituo vyako hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unapokwenda kutembelea uangalie vizuri madaktari wetu. Sisemi kama hawafanyi vizuri, wanafanya vizuri, tumewapongeza humu sana, lakini suala hilo madaktari wengine wanafanya. Jitahidi katika kutembelea vituo vyako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, kuna ukurasa wa 14 aya 22 - afya na usafi wa mazingira. Kuna mazingira mengine katika vituo vyetu ambavyo tunakwenda kulingilia kama vituo vya mabasi, huduma za vyoo sio nzuri. Huduma ni mbaya, hazina usafi, utoke huku uende ukachukue maji uingize ndani ndipo uende ukafanye huduma yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara izingatie suala hili na hivi vyoo vitembee hasa ili kwenda kutizama juu ya huduma zilizokuwepo.

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Shukrani sana Mheshimiwa.

MHE. MWANTUMU D. HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja Wizara ya Afya. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Aisharose Matembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Bilakwate na Mheshimiwa Taska Mbogo ajiandae.

MHE. AISHAROSE N. MATEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Awali ya yote nianze kwa

kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia uzima na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu. Naishukuru Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa na nzuri wanayoendelea kuifanya ya kuwaaletea wananchi maendeleo ya haraka na yenye tija. (*Makofii*)

Pili, nampongeza sana Waziri wa Afya na timu yake kwa juhudni kubwa wanayofanya kuboresha huduma za afya na upatikanaji wa dawa ambapo hapo awali iili kuwa ni changamoto kubwa na kero kubwa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na bajeti iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako tukufu, bado kuna changamoto kubwa eneo la afya la mama na mtoto. Takwimu zinaonesha kwa mwaka 2004/2005 vifo vya mama wajawazito vilikuwa 578 katи ya vizazi hai 100,000; mwaka 2009/2010 vilishuka na kufikia 434 katи ya vizazi hai 100,000; lakini mwaka 2015/2016 vifo vya akina mama wajawazito vilipanda hadi kufikia 556 kutoka vizazi hai 100,000. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu hizi, bado tuna kazi kubwa ya kufanya ili kupunguza vifo vya wakina mama wajawazito. Ikumbukwe kwamba tulijiwekea malengo ifikapo mwaka 2020 tuwe tumepunguza vifo hivi viwe vimefikia 292 katika vizazi hai 100,000. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iongeze nguvu katika kuajiri wataalam hasa katika Kitengo cha Afya ya Mama na Mtoto lakini pia katika kada zote za afya, kwani kwa Mkoa wetu wa Singida tuna uhaba mkubwa sana wa watumishi katika kada ya afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuajiri wataalam hao, tuende sambamba na kuleta vifaa tiba katika wodi zetu za wazazi, kwani vilivyopo ni chakavu na havitoshelezi mahitaji. Katika Mkoa wa Singida jiografia yake ni ngumu sana na inahitaji *ambulance* nyingi za kutosha ili kuepuka vifo vya akina mama na watoto na kuwafikia haraka sehemu za kutolea huduma kwa wakati. Inasikitisha sana,

baadhi ya Hospitali za Wilaya na Vituo vya Afya vya Ikungi, Manyoni na Itigi havina kabisa magari ya kubebear wagonjwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tutarajie nini kwa mama ambaye tayari ameshashikwa na uchungu wakati hakuna usafiri wa kumfikisha katika kituo cha kutolea huduma? Mheshimiwa Ummy dada yangu mpendwa najua wewe ni msikivu na ni mama wa wanawake wanyonge na suala hili nimekuwa nikikuletea mara kwa mara kwamba Hospitali yetu ya Mkao wa Singida haina kabisa gari ya kubebear wagonjwa, hivyo nakuomba unisaidie ili tuweze kupata magari ya kubebear wagonjwa na pia tuweze kusaidia kuokoa vifo vya akina mama wajawazito na watoto. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie Hospitali yetu ya Rufaa ya Mkao wa Singida. Hospitali hii imejengwa takribani miaka kumi iliyopita, lakini mpaka sasa haitoi huduma. Vitengo vinavyotoa huduma ni vitengo vitatu tu; Kliniki ya Uzazi na Mtoto, Kliniki ya Ngozi na Kliniki ya Wagonjwa wa Kisukari. Sasa inawezekana vipi hospitali yenye hadhi ya kuitwa Hospitali ya Rufaa ya Mkao iweze kuhudumia vitengo vitatu tu? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana hata baadhi ya majengo yameshaanza kuchakaa. Sasa ni kwa nini Serikali haitoi fedha za kutosha ili Hospitali hii ya Rufaa iweze kukamilika na kuanza kutoa huduma na hata hatimaye kupunguza msongamano katika hospitali zetu za Wilaya na vituo vyetu vya afya? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba wakati Waziri wa Afya atakapokuja kufanya majumuisho, anipe *commitment* ya Serikali ni lini Hospitali hii ya Rufaa itakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hospitali yetu ya mkoa haina Madaktari Bingwa wa kutosha; madaktari waliopo ni sita tu, wakati ikama inahitaji kuwa na madaktari 33. Naomba Serikali iwaonee huruma...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

MHE. AISHAROSE N. MATEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na mengine nitayaleta kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Bilakwate atafuatiwa na Mheshimiwa Taska Mbogo, Mheshimiwa Kunti Majala ajiandae.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa afya na nguvu kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuendelea kumpongeza Jemedari wetu Mheshimiwa John Pombe Magufuli pamoja na Waziri Mheshimiwa Ummu Mwalimu, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara ya Afya kwa kazi nzuri wanayoifanya, hakika Serikali yetu imejipanga kuhakikisha inaboresha huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wako watu wengi wanabeza mara hakuna kilichofanyika sasa mimi ngoja niwaambie baada ya kuwasemea wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa ni nini kimefanyika Kyerwa. Wakati naingia hapa Bungeni nilikuwa nina kituo cha afya kimoja ambacho huduma zake hazikuwa nzuri kituo cha Nkwenda leo kimeboreshwa akina mama wanapata huduma ya upasuaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nimepokea shilingi milioni 700 kwa ajili ya Kituo cha Afya Mlongo, hiyo ni

kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya John Pombe Magufuli. Mwaka huu kwenye bajeti ya TAMISEMI nimepokea bilioni moja na milioni mia tano (1,500,000,000) kwa ajili ya hospitali ya Wilaya, nani kama John Pombe Magufuli?

MBUNGE FULANI: Hakuna.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ni kazi nzuri zinazofanywa na Serikali ya John Pombe Magufuli, wenge macho wanaona na wenge masikio wanasi. Pamoja na kazi hizi zinazofanyika bado tunazo changamoto za watumishi, niendelee kuiomba sana Serikali yetu, Kyerwa watumishi wa afya ni wachache sana, ninaomba tunapotoa mgao kama Serikali na Kyerwa muiangalie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilpongeze Serikali kwa ajili ya huduma za matibabu ya kibingwa, kwa kweli tumepiga hatua nzuri sana. Mimi nimefika pale Muhimbili kwenye Hospitali ya Jakaya Mrisho Kikwete ya Moyo, kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana inatia moyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo haya tulikuwa tunasikia yanafanyika nje, lakini leo tunaona yanafanyika Tanzania, nilpongeze Daktari wetu Profesa Janabi, lakini na madaktari wengine ambao wanaboresha huduma za afya. Ninachoiomba Serikali yangu siku tujitalidi kama tunavyofanya maamuzi magumu kwenye mambo mengine, hebu tufanye maamuzi magumu kuboresha huduma za afya kwa upande wa matibabu ya kibingwa ili tuweze kuokoa pesa nyngi zinazoenda nje ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu nilimpeleka Mzee wangu India, Watanzania ni wengi wanaotibiwa India na wanatumia gharama kubwa sana. Kama mtu mmoja tuliweza kutumia zaidi ya milioni 30 kuna mama mmoja alikuwa anafanyiwa upasuaji pale Hospitali ya Apollo anahitaji zaidi ya dola 30,000 hizi pesa zote tukiboresha huduma za afya zitaingia Tanzania na tutaongeza kipato cha Wizara ya Afya. Ninaiomba sana Serikali iongeze vifaa,

iongeze nguvu ninaamini tunao wataalam wengi sana lakini tatizo bado vifaa havitoshii kuweza kuboresha huduma hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala la upatikanaji wa madawa. Kwa kweli Serikali inafanya kazi nzuri, tumetoka bilioni 30 leo tunaongelea bilioni 200, ni kazi kubwa inayofanyika kwa kweli tuna kila sababu ya kuipongeza Serikali yetu kwa kuhakikisha inaboresha huduma za afya na Watanzania wanakaa sawa. Ninachoomba Mheshimiwa Ummy tumeona ukiongea na wadau mbalimbali hili jambo na lenyewe iwe ni sehemu ya kufanya maamuzi magumu ili tuweze kuwa na viwanda vyta madawa hapa Tanzania na hii itasaidia, hizi pesa nyngi zinaenda nje lakini zingebaki ndani zingeweza kuboresha huduma za afya na ninaamini tutapiga hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala la Bima ya Afya, hili suala ni jambo ambalo ni muhimu Watanzania hawawezi kuwa na pesa ya kujitibu, lakini tunapokuwa na bima ya afya itasaidia. Niiombe sana Serikali iongeze nguvu na waendelee kuwashamasisha Watanzania kila mmoja awe na bima ya afya, hii itasaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Taska Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Majala na Mheshimiwa Ruth Mollel ajiandae.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na rehema kwa kutupa uhai, sisi wote hapa Bungeni ni wazima na tunasikiliza Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo napenda kumpongeza Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Ndugulile kwa kazi nzuri wanayoifanya. Napenda kuwapongeza Mawaziri wote kwa

kazi nzuri wanazozifanya kutumikia Taifa hili. Napenda kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anazozifanya za kuwanyanya wanyonge na kuleta heshima ya kazi ndani ya Taifa hili. Zamani kazi ya Serikali ilikuwa inadharaulika na Manesi hawa walikuwa na lugha mbaya lakini sasa hivi wana lugha nzuri, Mheshimiwa John Pombe Magufuli usi-*change gear* ongeza *gearnyingine*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo napenda niende kwenye Mkoa wangu wa Katavi, napenda nishukuru kwa pesa tulizopata kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya mkoa, naomba muuangalie kwa jicho la pekee mkoa huu kwa sababu mkoa huu ni mpya, naomba mtuongezee pesa kwa sababu sisi ndiyo tunaanza kujenga hospitali. Mkoa huo ni mpya, miundombinu ni mibovu, kwa hiyo, watu wote wa Mkoa wa Katavi wanasubiri Hospitali ya Mkoa iweze kuisha ili iweze kuwasaidia maana yake Hospitali ya Rufaa iko mbali Mkoa wa Mbeya ni kilometra 500 kutoka Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo hitaji lingine la Mkoa wa Katavi tunaomba gari la chanjo kwa Manispaa ya Mpanda. Manispaa ya Mpanda haina gari la chanjo, Halmashauri zingine zipo, kwa hiyo, inawafanya watoto pale wadogo wale wanaozaliwa kwenye Manispaa ya Mpanda waweze kukosa huduma ya chanjo. Namuomba Mheshimiwa Waziri utupatia gari hilo la chanjo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lingine ni kile kituo cha afya ambacho kilikuwa kinafanyiwa marekebisho pale kwenye Hospitali ya Wilaya ya Mpanda kiweze kufunguliwa, ninazo taarifa kwamba Mheshimiwa Ndugulile ulikwenda Kakuni ukakagua ile shule ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo amejenga pale Kakuni, ametupatia sisi wananchi wa Mkoa wa Katavi ifunguliwe iwe kituo cha afya.

Nimuombe basi Mheshimiwa Dkt. Ndugulile kwa sababu ulikwenda pale Kakuni na ukaiona hiyo shule, ufanye ucharaka wa kukamilisha hili jambo ili kituo hicho cha afya

kiweze kufunguliwa na kile kituo cha afya cha zamani kiweze kutumika kwa akina mama wa Mpanda pamoja na watoto kwa maana ya kuwa kliniki ya watoto. Naomba hilo Mheshimiwa Ndugulile kwa sababu jambo hili unalifahamu na Kakuni ulifika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Pinda, Waziri Mkuu Mstaafu kwa kutupatia hiyo shule ambayo alikuwa ameijenga kijiji ni kwake, ahsante sana kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Katavi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lingine la wananchi wa Mkoa wa Katavi kuhusu afya, tunaomba ile Hospitali ya Inyonga bado haijapewa hati ya kuwa Hospitali ya Wilaya, tunaomba ipewe hati ili iweze kutoa huduma kwa wananchi wa Mlele.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lingine kwa sababu dakika ni tano naenda u upesi, ombi lingine la wananchi wa Mkoa wa Katavi wazee wa Mkoa wa Katavi wanaomba sana wapewe bima ya afya. Sasa hivi wale wazee huwa wanapigwa picha wanapewa vitambulisho wanakwenda kutibiwa kwenye dirisha la wazee lakini wanapokosa zile dawa pale hospitali hawawezi kuzipata zile dawa kwa sababu hawana bima ya afya. Nimeangalia pale Manispaa ya Mpanda mmewapatia shilingi milioni saba, kwa ajili ya wazee wa Manispaa ya Mpanda na wao waliomba shilingi milioni 17, lakini mimi nasemea wazee wote wa Mkoa wa Katavi muwaangalie kwa jicho la pekee. Mkoa ni mpya ndiyo unaanza, una mahitaji mengi na wale wazee wa kule hawajafaidika na hii bima ya afya, nawaombea wazee wangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuiomba Wizara ya Afya ninaomba Mkoa wa Katavi mtupatie wadau wa afya. Tunaye mdau mmoja anaitwa *Water Rid* yeye ndio yuko Mkoa wa Katavi anatusaidia saidia tunamshukuru sana, tunaomba mnapopata wadau wa afya wengine huko Wizara ya Afya

muwalete Mkoani kwetu Katavi ili waweze kutusaidia kwenye sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri wa Afya pia nizungumze suala dogo kuhusu usafi ambalo limezungumziwa pia na mwenzangu aliyepita Mheshimiwa...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Taska Mbogo muda wako umekwisha.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja *hundred percent.* (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kunti Majala atafuatiwa na Mheshimiwa Ruth Mollel ama aliyeleta jina lake hapa atakayebadilishwa naye, halafu Mheshimiwa Alex Gashaza ajiandae.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi siku ya leo niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ya Afya na ninaomba nianze tu na suala zima la upungufu wa wahudumu wa Wizara ya Afya na naomba nilisemee kwa Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Dodoma ni Mkoa ambao umekwenda sasa kupata ongezeko kubwa sana la wageni kutoka nje na tuna Hospitali ya Rufaa kwa maana ya Hospitali ya Mkoa wa Dodoma, lakini pia tuna Hospitali ya Benjamin na hospitali zingine za taasisi, lakini kumekuwa na changamoto kubwa sana ya foleni ama msongamano kwenye hospitali hizi. Nilikuwa nataka Mheshimiwa Waziri ukija naomba utuambie wananchi wa Dodoma msongamano huu, mkakati wako ni nini wa kuepusha msongamano kwani watumishi kwa maana wageni wengi ambao wameingia ni watumishi wa Serikali na mara nyingi

wanatumia kupata *appointment* na madaktari wanapofika pale hospitalini hawapangi foleni. Wenyeji wa Mkoa wa Dodoma wanapanga foleni Mheshimiwa Waziri mpaka siku tatu mtu hawezi kumuona daktari, kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri utakapokuja uweze kuniambia suala hilo linatatuliwaje kwa udharura wa ongezeko la watu katika Mkoa wetu wa Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kusemea suala zima ni sera ya Serikali kwamba kila mkoa unatakiwa kuwa na Hospitali ya Mkoa, Wilaya kuwa na Hospitali ya Wilaya, lakini pili kata kuwa na vituo vya afya na vijiji kuwa na zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wamekuwa wakisimama hapa wanalamikia suala zima la hospitali za Wilaya na vituo vya afya. Mkoa wangu wa Dodoma una Wilaya saba, Wilaya tatu hatuna hospitali. Tumekuwa tukiomba fedha mara kadha wa kadha na fedha hizo hazitoki. Sasa Mheshimiwa Waziri suala la ongezeko la watu hapa Mkoa wa Dodoma linakwenda pia kuleta changamoto kubwa kwa sababu wananchi wa Wilaya za pembezoni zote wanapokosa huduma huko kwenye Wilaya zao wanakuja hapa Makao Makuu kwa maana ya Hospitali ya Mkoa wa Dodoma. Sasa leo Wilaya hizi hazina hospitali za Wilaya, lakini bado kuna msongamano mkubwa, naomba utuambie Mheshimiwa Waziri hizi Wilaya tatu nini hatma yake kwenye bajeti hii ya fedha ya mwaka huu 2018/2019. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Chemba ina kata 26. Kati ya kata 26 ni kata nne tu ndiyo ina vituo vya afya, lakini tuna kituo cha afya Kituo cha Hamai, kituo hiki nilikisemea Bunge liliopita ama kikao cha bajeti kilichopita. Hiki ndiyo kituo kinachotumika kama Hospitali ya Wilaya ya Chemba, lakini cha kustaajabisha na cha kusikitisha kituo hiki kina watumishi 16, kituo hiki hakina maji, kituo hiki hakina *x-ray machine*, kituo hiki hakina gari la wagonjwa. Kituo hiki acha tu kwamba kinahudumia kama kinakuwa kina-*take charge* ile ya wagonjwa wa Wilaya ya Chemba, lakini pia

kinahudumia Wilaya ya Kiteto, kinahudumia Wilaya ya Chamwino, kinahudumia Wilaya ya Kondoa. Hivi vitu hebu tunaombeni muwe mnatuona na watu wengine huku, msiwe mnagawana gawana tu hizi fedha halafu watu wengine mnatusahau. Mngeacha hata kutujengea ule uwanja wa Chato kwa shilingi bilioni 42 mkatuletea hizi fedha zingeweza kutusaidia kujenga hizi hospitali zetu za Wilaya ikaweza kusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hii shilingi trilioni 1.5 ambayo inapigwa pigwa chenga na Serikali mimi naamini ipo mahali, mlikuwa mnatikisa kiberiti, sasa tunaomba muitoe hadharini ije iende ikatekeleze shughuli za maendeleo kwa kutoa huduma ya afya, kwani tunaamini Mama Salma amesema kwamba bila afya hakuna uchumi. Mnatangaza Serikali ya viwanda, Serikali ya viwanda Watanzania wagonjwa hawana dawa, hakuna wahudumu, Tanzania ya viwanda iko wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninaomba sana kwa jinsi mnavyojinabu Serikali sikivu tunaomba usikivu huo uende kwenye shilingi trilioni 1.5 ikatulee madawa na kulipa mishahara ya watumishi katika Taifa letu ili Watanzania waweze kwenda kuendelea. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha. Mheshimiwa Anna Gidarya atafuatiwa na Mheshimiwa Alex Gashaza, Mheshimiwa Zainabu Nuhu Mwamwindi ajiandae.

MHE. ANNA J. GIDARYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mimi naomba nijikite kwenye hoja iliyoko mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja iliyoko mezani inaonesha kwamba Watanzania ni jinsi gani akili zetu zinachezewa. Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2018 inaonesha ni trilioni 1.7 lakini ya mwaka huu ni shilingi 886,236,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, unawezaje kuhudumia Watanzania kwa bajeti hii, nchi ambayo watu wake hawana

afya nzuri, hawana lishe bora, ni nchi ambayo watu wake kiuchumi na kiafya hakutakuwa na nguvu kazi ya Taifa hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajinasibu kwamba wanafanya mambo mazuri, ni kweli upande mwininge kuna mambo yanaenda sawa. Kuna mambo hayaendi sawa, kwenye Idara ya Afya kuna mambo ambayo tunaona ni kama mchezo wa kuigiza kila mwaka. *Issue* ya watumishi kwenye hii idara ni *issue* ambayo imezoleka, Wabunge wanaleta maswali ya msingi, majibu ya Mawaziri inaonyesha ni kutuchezea akili za Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye kitabu cha Kamati, TWaweza wameleta takwimu inaonesha kwamba kila baada ya dakika 12 mtoto mmoja wa Kitanzania anapoteza maisha kwa sababu ya kukosa lishe. Ukienda tena zaidi wanasema mpaka masaa ya jioni ni watoto 35 wanakufa kutokana na lishe duni, sasa tunajiuliza hii bajeti mmezunguza kwa nini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni idara nyeti, hakuna msomi anayesoma kama hana lishe bora. Hakuna mtu ye yote anayeweza kwenda kwenye Serikali ya viwanda kama hana lishe bora. Tusiletane maigizo ambayo yanaweza yakaleta hasira kwa Watanzania, tunahitaji Watanzania wenyе afya njema, tunahitaji Watanzania wenyе akili ambazo zina afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna habari ya matibabu bure kwa wazee. Nakubaliana ni kweli kuwe na matibabu bure kwa wazee lakini Serikali haikuangalia ni wapi mtu anapokuwa na magonjwa ya kudumu. Unapokuwa kijana kuna magonjwa si nyemelezi, lakini umri unavyozidi kukua na unapozidi kuzeeka mwili unapoteza nguvu. Kuna watu wanaumwa magonjwa ya figo, kuna watu wanaumwa magonjwa ya tezidume, haya mambo yote yana-*compare* kwenye uzee, kwenye umri mkubwa, lakini suala la matibabu bure kwa wazee ni *paracetamol*/kwenye vituo vya afya. Kwa namna moja au nyingine tunawapoteza wazee wengi kwa sababu ya huu mwamvuli wa matibabu bure.

Tunaomba sasa mje na mkakati mwingine namna ya kuokoa maisha ya wazee wa Kitanzania ambao wamefikia umri mkubwa na wana mashambulizi ya magonjwa ya kudumu ni mengi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye zahanati zetu kuanzia ngazi ya vituo, zahanati zimejengwa kwa mahitaji ya mtu kama mimi ambaye sina mahitaji maalum. Hawa watu wenye mahitaji maalum hawajawekewa kipaumbele kwenye zahanati zetu, ninategemea Waziri atakapokuja hapa atuambie ana mkakati gani wa kujenga maeneo katika zahanati yetu kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo lingine ambalo ni eneo nyeti, matumizi ya madawa ya kupunguza makali ya VVU, matumizi haya mna...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Anna Gidarya muda wako umekwisha, ahsante sana. Mheshimiwa Alex Gashaza atafuatiwa na Mheshimiwa Zainab Nuhu Mwamwindi, Mheshimiwa Martha Umbulla ajiandae.

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara ya Afya. Niungane na Wabunge waliotangulia kuponzeza jitihada zinazofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, lakini pia kazi kubwa wanayoifanya Waziri na Naibu Waziri na watendaji wao wa Wizara katika kuboresha afya za Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo mengi yamefanyika katika Jimbo langu la Ngara hasa katika kuboresha afya za wananchi wa Ngara ikiwa ni pamoja na kuboresha vituo vya afya Musagamba Mabawe, lakini pia hata upatikanaji wa dawa kabla ya hapo wananchi wa

Jimbo la Ngara walikuwa wanaenda kutibiwa Burundi haya wa kata za mipakani lakini leo imekuwa ni *vice versa* kwamba kuna wanaotoka upande mwingine kutaka kuja kupata huduma upande wetu. Kwa hiyo, napongeza Serikali na Wizara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizo bado zipo changamoto, tuna vituo vinne katika Wilaya ya Ngara kati ya kata 22, lakini kipo Kituo cha Afya Lukole ambacho kituo hiki ni mionganoni mwa hivyo vituo vinne. Hiki kituo kilikuwa katika Kambi ya Wakimbizi ya Lukole wakati wakiwepo wakimbizi wa Burundi, majengo yaliyojengwa katika kituo kile ni majengo ambayo mengi yalijengwa kwa tofali za tope kwa hiyo siyo majengo ya kudumu lakini ni kituo ambacho kinahudumia watu zaidi ya elfu ishirini na tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Mheshimiwa Waziri Ummy, Naibu Waziri Dkt. Ndugulile mmeefanya kazi kubwa kwangu, lakini niombe hili nalo tuliangalie kwa macho mawili kwamba hiki kituo nacho tuweze kukiboresha ili kiwe kwenye hadhi kwa sababu kinatoa huduma ka wananchi wa Jimbo la Ngara hata Jimbo jirani la Bihalamuro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa watumishi upo kwa kiasi kikubwa kwenye sekta hii ya afya, kuanzia kwenye hospitali ya Nyamiaga, vituo hivyo vinne na kwenye zahanati. Niombe kwamba sasa kwa watumishi hawa ambaao wanaenda kuajiriwa, watumishi 16,000 kwenye bajeti ya mwaka huu, idara ya afya basi mtufikirie.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado pia kuna baadhi ya watumishi waathirika hususan katika Hospitali ya Murugwanza, Dada yangu jana aliongelea na mimi nalisisitiza hili kwa sababu wapo watumishi 49 ambaao wakati wa uhakiki wa vyeti siyo makosa yao, waliondolewa kwenye *payroll* wakati hawakuwa na kosa na bado wakarudishwa. Wengine wanadai miezi kumi, wengine wanadai *arrears* za mishahara yao miezi sita, saba kwa namna tofauti, niombe hilo liweze kushughulikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono mpango wa bima ya afya kwa watu wote, hii inaweza kuwa ndiyo suluhisho kwa ajili ya kuondoa *double standard* na kuwahudumia watu kwa usawa. Ni nia njema ya Serikali na niombe hili lifanyiwe haraka na Wabunge tupo tayari kwa ajili ya kuendelea kuhamasisha ili mpango huu uanze. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipo Kituo cha Afya katika Kata ya Nyakisasa, kituo hiki kilianzishwa kwa nguvu za wananchi, lakini pia kwa kutumia Mfuko wa Jimbo; yapo majengo ambayo ambayo hayajaweza kutosheleza kuwa kituo cha afya, lakini tunaamini ikiwekwa nguvu kidogo kituo kile kinaweza kikafunguliwa kulingana na jirografia ya hali ya Ngara, kituo hiki ni muhimu na tunakihitaji. Niombe Mheshimiwa Waziri utakapokuja ulififikirie hilo katika vituo ambavyo unaweza ukaviongezea fedha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwenye upande wa lishe. Lishe katika hali ya kawaida inaonesha kwa mujibu wa takwimu kwamba Tanzania tuna lishe duni ni watatu Afrika, lakini ni wa kumi duniani, unaweza ukaona ni jinsi gani ambavyo kuna changamoto hiyo. Pamoja na kwamba Taasisi ya Chakula na Lishe (*TFNC*) wameonesha ni jinsi gani ambavyo wamefanya jitihada katika *ku-control* hata vifo vya watoto chini ya miaka mitano vinavyotokana na udumavu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri kwamba twende zaidi tujaribu kushirikiana hata na Wizara ya Kilimo kuona ni namna gani tunavyoweza kuhamasisha baadhi ya mazao ambayo yanaongeza lishe. Kwenye ukurasa ule wa 89 kwenye kitabu hiki cha hotuba ya Waziri wameonesha ni jinsi gani ambavyo wanajaribu kutoa chanjo kwa asilimia kubwa kwa watoto chini ya miaka mitano kwa matone ya Vitaminini A.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipo vyakula lishe kama viazi lishe ambavyo vina Vitaminini A nyingi ya kutosha ambavyo tukihamasisha ulimaji wa viazi lishe (*orange sweet potato*) vinaweza vika-cover eneo ambalo tunatumia

gharama kubwa kwa ajili kuwachanja watoto hawa kwa matone ya Vitamini A. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Zainabu Nuhu Mwamwindi, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Umbulla na Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma ajiandae.

MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi na mimi leo niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Afya, Wizara nyeti, Wizara ambayo kwa kweli imeshika uhai wa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Wabunge wenzangu kwa kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa namna ambavyo amejitoa muhanga kwa ajili ya Watanzania. Pia nimpongeze mama yetu Mama Samia Suluhu na yeye kwa kumsaidia kwa nafasi yake ya Makamu wa Rais. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa namna ambavyo kwa kweli wanafanya kazi na macho yetu yanaona na masikio tunasikia yale ambayo wamekuwa wanayafanya katika maeneo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee sana ninaomba nimpongeze sana mwanangu Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana Mheshimiwa Ummey Mwalimu na kweli wewe ni mwalimu, lakini niseme tu nitakuwa sijajitenda haki kama sitakupongeza kwa namna ambavyo kwa kweli umethubutu katika Wizara hii kama mama. Niseme tu kweli kwamba hujatuangusha sisi wanawake wenzio na tunazidi kukutia nguvu kwamba changamoto za kawaida kama binadamu na pale unapokosea Mungu anaona kwamba

umekosea kwa bahati mbaya lakini nia na dhamira yako ya kweli katika nafasi hii tunaiona na tuseme tu Mheshimiwa Rais hajakosea kukupa nafasi. Pia nimpongeze Naibu Waziri na pia niwapongeze watendaji wote wa Wizara yako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM) ni mpango ambaao umeelekezwa na Serikali kwamba kila kijiji kiwe na zahanati, kila kata iwe na kituo cha afya na kila Wilaya iwe na Hospitali ya Wilaya. Zahanati ya Kalenga kwa yejote ambaye ameshafika Kalenga, na kwa namna ninavyoifahamu Kalenga zahanati ile ni kongwe, imejengwa kabla ya uhuru na haikujengwa *purposely* kwamba iwe zahanati kwa ajili ya kutoa huduma ya afya, ilikuwa ni shule ya msingi ambayo mimi kwa umri wangu nimesoma darasa la kwanza mpaka la nne, halafu shule ile ikahamishiwa baada ya Serikali kufuta shule za *middle school* ikahamia kwenye shule iliyokuwa inaitwa *Kalenga Upper Primary School* na ikawa zahanati ya kijiji cha Kalenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kalenga ni kijiji ambacho kina historia na ni kijiji ambacho viongozi wetu wakuu akiwemo aliyekuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Chifu Adam Sapi Mkwawa amezaliwa pale na amezikwa pale, lakini pia ni kijiji ambacho kina makumbusho ya Taifa letu. Kijiji kile kwa sasa ni kijiji mji na idadi iliyokuwepo wakati ule na sasa, idadi ya watu imeongezeka kuliko mara tano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zahanati ile kwanza majengo yake yalifanya kuchapiwa tu, kubadilishwa iwe zahanati lakini haina sifa wala hadhi ya kuitwa zahanati ya kijiji cha Kalenga. Kwa sababu dakika tano kwangu ni chache, mengine nitatoa kwa maandishi, nikuombe Mheshimiwa Waziri mwanangu Ummy ushirikiane na Wizara ya TAMISEMI angalau uitazame kwa jicho la huruma,

wananchi wa Kalenga wana utayari wa kujenga kituo cha afya, wana eneo lao ambalo limezidi ekari 12 ambalo halina gharama ya Serikali kulipa fidia lakini pia wapo tayari wao kama wao kutumia nguvu zao kuweza kusimamisha kuanza kujenga pia wanaomba serikali pale watakapokwama iweze kuwasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee sana katika Majimbo magumu ambayo ninayafahamu mimi ni Jimbo la Kilolo. Jimbo la Kilolo kuna shida, wao kutohana na miundombinu ya kwao pale wamekubaliana katika kila kata, vijiji vitatu viunganike vijenge kituo cha afya kimoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwamwindi muda wako umekwisha.

MHE. ZAINAB N. MWAMWINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Martha Umbulla atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma; Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla King ajiandae.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi. Kwanza mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu anayetupa zawadi ya uhai kwa wote humu ndani na kuendelea na shughuli zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sitatenda haki bila kuishukuru Serikali yetu kwa kuweka kipaumbele katika Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba inaboresha maisha ya Watanzania walio wengi. Kipekee pia na mimi nimpongeze sana Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, kwa kweli mdogo wangu na mwanangu umeweka alama katika nchi yetu, hongera sana. Pia nimpongeze Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara yako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mengi mazuri

ambayo yamefanywa na Serikali yetu, ninaomba kushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa tatizo la vifo vyatya akina mama wajawazito na watoto ni tatizo sugu katika nchi yetu, miaka nenda rudi tumekuwa tukipewa takwimu za kupanda na kushuka kuhusu tatizo hili ambalo limeshindikana kabisa kuisha. Namuomba Mheshimiwa Waziri kama ambavyo tunaona anaweka alama, tunamuomba ahakikishe kwamba suala hili la vifo ambavyo siyo vya lazima vya akina mama wajawazito naomba alitafutie ufumbuzi. Kwa kuwa sekta ya afya ni sekta mtambuka, naishauri Serikali itenye bajeti kwa kila wizara kuhakikisha kwamba suala hili la vifo vya wanawake wajawazito kila mwaka tunaloambiwa na kwa kuwa changamoto zake zinafahamika zinaweza kutatuliwa, ziweze kufutwa kama ambavyo nchi yetu imeondoa tatizo la ndui katika nchi hii na hili tatizo liwe historia. Naiomba kila Wizara itenye bajeti ili kutatua tatizo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kuna tatizo sugu la malaria, malaria inaua Watanzania walio wengi kuliko ugonjwa wowote hapa nchini. Ninaiomba Serikali kwa kusaidiana na fedha na wafadhili wengi ambao wanatoa fedha katika eneo hili nalo hilo eneo liweze kuangaliwa kwa sababu changamoto zake zinajulikana, zinatatulika na lenyewe liweze kufutwa ili nchi yetu iwe salama kwa ugonjwa wa malaria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie haraka haraka usambazaji wa dawa kwa asilimia zaidi ya 80 katika maeneo ya vijiji. Naipongeza Serikali kwa hilo, lakini inasikitisha pia kuona juhudhi ya Serikali kubwa kwa kiasi hicho maeneo ya pembezoni hususan Mkoa wa Manyara, Hospitali ya Mkoa ya Mrara, Hospitali za Wilaya na vituo vya afya havina dawa za kutosha wananchi bado wanaambiwa wakanunue madawa pemberi. Tunaoimba hili nalo ulivalie njuga uhakikishe kwamba kama kuna hujuma ya aina yoyote, wahusika wote waweze kuchukuliwa hatua hadharani ili iwe fundisho kwa sababu tatizo hili Serikali imekwishalimaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia huduma za Madaktari Bingwa kwa sababu nimeona kwenye kitabu cha Waziri ameizungumzia, kwanza nimshukuru kwa hilo. Huduma za Madaktari Bingwa inahitajika kwa sababu magonjwa sugu yapo vijijini, nitoe mfano wa ndugu yangu ambaye alipata *mild stroke* huko Kambi ya Simba - Karatu na badala ya kupewa huduma ya Uduktari Bingwa pale alipo akasafirishwa umbali wote huo zaidi ya kilometra 200 kwenda KCMC kumbe angeweza kushauriwa kwamba na hatujui kwamba aweze kupumzishwa, apewe huduma ya kwanza na baada ya hapo aweze kusafirishwa kwenda kupata huduma. Sasa hilo lilipoteza maisha na ninaomba kwamba Serikali iweze kuliona hili, imekwishaliona lakini iweze kuweka msisitizo kupeleka huduma bingwa katika maeneo ya vijijini. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuzungumzia pia suala zima la Wizara ya Afya kuweza kutenganishwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Michango mingi humu ndani ambayo tumeisikia, katika watu kumi pengine ni mtu mmoja amezungumzia masuala ya wanawake. Mimi nilikuwa natoa ushauri Wizara ya Afya ni Wizara kubwa sana na inameza kabisa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto. Ninaomba Serikali ione ni namna gani inaweza kutenganisha Wizara hizi mbili ili huduma hizi za masuala ya wanawake yaweze kusambaa na ipate upana mrefu wa kuweza kushughulikiwa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru na ninaomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia 100, nitachangia kwa maandishi. (Makof)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla King na Mheshimiwa Shaabani Shekilindi ajiandae.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza kwa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano lakini pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Kiukweli Wizara hii ya Afya ina mambo mengi sana na wenzetu Waziri na Naibu wake wanafanya kazi kubwa sana, lakini mwisho wa siku tukubaliane tu hizi changamoto za afya hazitakaa zije ziishe kwa ukamilifu wake, hata zikiisha bado zitazaliwa zingine kutokana na vyakula tunayokula, *life style* tunayoishi na mabadaliko ya tabianchi. Kwa hiyo, kila siku kwenye Wizara ya Afya changamoto zitakuwepo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa dakika ni tano itoshe kuwapongeza wenzetu kwa kazi nzuri wanayoifanya Serikali ya Awamu ya Tano hasa kwa kujitahidi ama kuweza kuokoa fedha kwa wagonjwa walikuwa wanaenda kupata matibabu ya moyo nje ya nchi. Ukiangalia hapa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri inasema wameweza kupunguza ilikuwa kutoka wagonjwa 43 mpaka wagonjwa 12 kwa mwaka 2016/2017; hiyo ni pongezi kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ninachopenda kuwapongeza kwa lile la kuanzisha chanjo ya saratani kwa mabinti wa miaka 14, wamefanya kazi kubwa sana. Pengine hapa nataka niiombe Serikali yangu iangalie sasa mabinti *above 14* yaani huo umri wa wao ambao wameuchukua sasa wanaozidi umri huo, Serikali ina mkakati nao gani? Niiliwa tu napenda kusaidiwa katika hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho ningependa kukizungumzia kwenye dakika hizi tano, napenda kuiomba Serikali na niliwahi kuuliza swalijuu ya sera ya matibabu bure kwa wajawazito, hili bado nalionna kama kidogo tuna changamoto nalo, pengine Serikali sasa ione namna bora ya kufanya mapitio upya ya hii sera, kama itabidi viro baadhi ya vitu tutahitajika kuvitolea ufanuzi. Hivi bure kwa wajawazito kwenye kila kitu au kuna baadhi ya vitu bure na kuna baadhi ya vitu vingine wananchi inabidi wachangie?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema hii tungeiweka vizuri kwa sababu hofu yangu wapiga kura na wananchi wetu wengi wanalalamikia kwamba *once* wako wajawazito wanapoenda hospitalini wanatozwa ama kuwa-*charged*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe tu mfano, vidoge vile vya uchungu wanaviita ama dripu, yenyewe ile, nikijitolea mfano hata mimi mwenyewe binafsi, nililipia kwa *cash* ingawaje nina kadi ya *NHIF* ni kadi ya Bunge ambayo naamini katika kadi ambazo ziko vizuri ni kadi za *NHIF* za Wabunge, lakini ilikuwa hai-*cover* vidonge tu vya uchungu. Kwa hiyo, mimi naiomba sana Serikali ikae iangalie vizuri sera, ipitie upya Sera ya Matibabu Bure kwa Wajawazito. Pia utakuta mama mjamzito ambaye anapata *miscarriage* anasafishwa kwa kati ya shilingi 300,000 mpaka 500,000. Kwa hiyo, nafikiri tunahitaji kuifafanua vizuri zaidi hii sera ili isituchonganishe na wananchi kipi ni bure, kipi tunatakiwa kukilipia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho ninapenda kukizungumza kiko kwenye ukurasa wa 17, juu ya afya ya uzazi, mama na mtoto. Kiukweli Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu na Naibu wake wanajitahidi kwa kiasi kikubwa sana kupambana kupunguza vifo vya mama na mtoto. Ila kuna kitu kimoja kinanisumbua siyo peke yangu, naona tuko watu wengi tu, pengine leo mngetusaidia kikitolea ufanuzi ili kiweze kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanamama anapokuwa mjamzito anapo-*attend* kliniki ni lazima, sijui kama ni lazima ama ni utaratibu wa kuwa anafanya *ultra sound* ili kuangalia maendeleo ya mtoto. Nikikumbuka mwenyewe aliyekuwa akinifanyia alikuwa anasema unaona mtoto wako huyu anaendelea vizuri, mapigo ya moyo, vidole vyake hivi vitano, hana mgongowazi, walikuwa wanasema hivyo. Ila kuna tatizo, wanashindwa kuangalia kama nitakosea kitaalamu mtanirekebisha, Mheshimiwa Dkt. Ummy na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, kuna kitu kinaitwa *coding* ama wanasema kitanzu, sijui kwa nini lile linashindwa kuangaliwa kipindi kile mama anapo-*attend* kliniki, kiasi kwamba...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha muda wa
Mzungumzaji)*

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla King atafuatiwa na Mheshimiwa Shaabani Shekilindi na Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke ajiandae.

MHE. PROF. NORMAN A. S. KING: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kuwapongeza Mawaziri wenye dhamana, dada yangu Mheshimiwa Ummy pamoja na rafiki yangu Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya kwenye Wizara hili. Katika kufasili kwa usahihi matamshi na matarajio ya Rais wetu waliweza kuandaa kongamano au mukutano kwa ajili ya kupata wawekezaji tarehe 4 Aprili ambapo na mimi nilhudhuria, nawapongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka, jambo la kwanza, pamoja na jitihada nzuri za Serikali za kununua vifaa na hasa Hospitali zetu za Muhimbili pamoja na Mloganzila, naomba sana Serikali ijikite kusomesha madaktari hawa nje ya nchi, nasisitiza Madaktari Bingwa wasome nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ya India kwa mfano na Hospitali zake za Apollo, idadi kubwa ya madaktari wake, *actually asilimia 94* ya madaktari ambao tunawaona kwenye Hospitali za Apollo India, hawajasoma India. Kwa hiyo, ni muhimu sana na sisi tujenge uwezo kwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, ninaomba sana, pamoja na kwamba Serikali inaweza ikapata shida kwenye taulo za kike, lakini utafiti uliofanywa kwenye Wilaya ya Makete wanafunzi wa Wilaya ya Makete hasa darasa la sita na la saba na sekondari wengi wao ni yatima kwa sababu *orphanage rate* kwa maana ya Tanzania

hii Makete tunaongoza. Wanahitaji kuangaliwa kipekee ili taulo za kike waweze kupewa watoto hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vituo vya afya; ninaipongeza Serikali kwa kazi nzuri ya vituo vya afya, lakini naomba sana Wilaya zile ikiwemo Makete, ambazo zina mtandao wa barabara au wa eneo kubwa zipewe upendeleo wa vituo vya afya. Kwa mfano, Tarafa ya Ukwama inahitaji kituo cha afya na gari la wagonjwa, Tarafa ya Bulongwa, vivyo hivyo Tarafa ya Ikuo, kitu cha afya na *ambulance*, kwa sababu inachukua karibu kilometra 105 kutoka kwenye kata hizi kwenda Makao Makuu ya Wilaya. Jambo hili likifanyika mtakuwa mmefasili kwa usahihi matatizo wanayoyapata wananchi wa Wilaya ya Makete na Watanzania wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, itoshe kusema tu kwamba kazi nzuri inayoendelea kufanywa sasa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya kuendelea kuongeza bajeti Wizara ya Afya ni kazi kubwa na nzuri ambayo wananchi wa Makete tutaendelea kuiunga mkono kwa nguvu zote. Na kwa hili, kipekee kabisa nimpongeze sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na timu ya wasaidizi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niongelee kidogo Hospitali ya Misheni ya Ikonda. Makete tunayo Hospitali ya Ikonda, hospitali hii inahudumia mikoa takribani nane Iakini Serikali inapaswa kutia jicho la kipekee na kuwapa ahueni na hasa malipo ya Madaktari Maalum amba wanatoka Ujerumani na Italia kwa ajili ya kwenda kuhudumia wananchi wa Wilaya ya Makete na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili, tumeandika barua mara nyingi kwa maana ya Hospitali ya Ikonda na mimi kama mwakilishi wao kwa Waziri kuombia *favourna* hasa ya madaktari hao, wasiwe wanatozwa fedha kwa sababu wanakuja kuhudumia Watanzania hawa na kwa kweli hata malipo yanayotozwa Watanzania kwenye hospitali hii ni malipo madogo sana. Niombe sana Waziri

aweze kuiangalia Hospitali ya Ikonda ya Misheni kwa jicho la kipekee ili kuendelea kuwasaidia Watanzania zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia umealikwa Mheshimiwa Waziri ili utembelee Hospitali ya Ikonda ukajionee mwenyewe. Pale tuna kituo kikubwa cha viungo bandia ambavyo huwezi kupata eneo lingine lolote Tanzania hii, tunaomba sana utenge muda utembelee ili uone shida za wananchi wa Makete.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, Mungu ibariki Serikali ya CCM. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Shaabani Shekilindi, atafuati na Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis ajiandae.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Wizara hii ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kunijalia afya na nguvu na mimi niweze kuchangia katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kazi kubwa anayoifanya kwani mwenye macho haambiwi tazama. Pia nimshukuru Waziri wangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Ndugulile na watendaji wote, kwani kazi wanayoifanya Watanzania hakika wanaiona. Mimi naamini hakuna cha kuwalipa ila Mwenyezi Mungu mwenyewe ndio atajua cha kuwalipa ninyi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye vituo vya afya. Kwanza nimshukuru Waziri, Serikali yangu tukufu kwa kunitengea shilingi milioni 700 kwa ajili ya Kituo cha Afya Mlola, sasa hivi naamini mambo ni mazuri kabisa, tumetengewa shilingi milioni 700 kwa maana hiyo

shilingi milioni 400 kwa ajili ya majengo na milioni 300 kwa ajili ya vifaa tiba, kwa hiyo naishukuru Serikali yangu Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Lushoto, Halmashauri ya Lushoto, Jimbo la Lushoto lina kituo cha afya kimoja tu ambacho kiko Mlola. Kwa hiyo, kituo kile hakitoshelezi kabisa mahitaji ya wananchi. Kwa hiyo, niiombe sasa Serikali yangu kwa kuwa wananchi wa Gare, wananchi wa Ngwelo wamejitalidi wenyewe wamejenga vituo vya afya mpaka kufikia mtambaa wa panya na majengo mengine yamepauliwa, niiombe Serikali sasa safari hii itengete pesa za kutosha kwa ajili ya kumalizia vituo vile kwa maana ya Kituo cha Gare na Kituo cha Ngwelo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hayo, hospitali yetu ya Wilaya imeelemewa. Wilaya ya Lushoto ina takribani Majimbo matatu, Halmashauri mbili, kwa maana ina wakazi zaidi ya 600,000, *ultra sound* na *x-ray* ya Lushoto ni ndogo sana haikidhi mahitaji. Kwa hiyo, tunakosa wananchi wengi sana pale, wanapoteza maisha kwa sababu ya *x-ray* ile ni ndogo sana, ikihudumia watu watano tu inakufa. Kwa hiyo, niiombe Serikali yangu tukufu na sikivu ipeleke *x-ray* yenye uwezo ili kuweza kuhudumia wananchi wale, hususan kuokoa maisha ya mama na mtoto pamoja na wananchi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, gari la wagonjwa niiombe Serikali, Mheshimiwa Ummy anajua kwamba Wilaya ya Lushoto jiografia yake ni mbaya sana, ni ya milima na mabonde. Kwa hiyo, chondechonde, kwa kweli hali ni mbaya. Juzi nikiwa niko Jimboni nilishuhudia vifo vya akina mama watatu wamekufa kwa ajili ya kifafa cha mimba kwa sababu ya kukosa usafiri kufika katika Hospitali ya Wilaya. Kwa hiyo, nimuombe dada yangu Mheshimiwa Ummy, naomba *Land Cruiser*, siyo vile vigari vidogo maana naamini anajua barabara za kwetu, nimuombe atupatitie *Land Cruiser* ili kuweza kuhudumia hususan wananchi wa Mlola, Makanya, Bwelo, Mlalo, Mbwei, Malibwi pamoja na Kwai. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala zima la

walemavu. Kule kwetu ni vijiji mno kiasi kwamba walemavu hawapati huduma. Kwa hiyo, niiombe Serikali sasa ipeleke hususan vifaa kwa walemavu hususan walioko vijiji, hasa kule Lushoto maeneo ya Makanya, Mavului, Manolo pamoja na Mbwei, kwani ukiangalia hali halisi ilivyo takwimu zinazoletwa na wataalam kutoka Halmashauri ni potofu siyo sahihi, kwa hiyo niiombe Serikali yangu sasa ipeleke vifaa vya kutosha hususan vya walemavu katika maeneo yale ya Lushoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke atafuatiwa na Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis na kama dakika zitakuwa bado zipo Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ajiandae.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Ummy kwa hotuba yake nzuri, nimpongeze Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Afya. Nampongeza sana Mheshimiwa Ummy kwa sababu ni ukweli usiofichika kwa jinsi anavyofanya kazi kubwa ya kuhakikisha vifo vya akina mama na watoto vinamalizika, ninampongeza sana. Tumeendalea kuona anavyofanya kazi katika nchi yetu ya Tanzania, anavyofanya ziara katika maeneo mbalimbali, kwa kweli ziara zake anazozifanya zinazaa matunda, tunampongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweza kushuhudia jinsi *theatres* zinavyojengwa, vituo vya afya, wodi za wazazi zinavyojengwa, sasa baada ya juhudhi hizo kinachofuata sasa tunaomba ahakikishe wanapatikana wataalam wa kuweza kufanya shughuli hiyo ya kuwasaidia akina mama kwa sababu maeneo mengi hakuna madaktari, hakuna waganga wa upasuaji. Kwa hiyo, tunaomba wataalam hao baada ya kuwa *theatres* zimejengwa, baada ya kuwa wodi

zimejengwa, waweze kupatikana wataalam wa upasuaji. Tusipofanya hivyo akina mama wengi watapoteza maisha kwa sababu maeneo hayo wasipopelekwa wataalam watakuwa wanafanya upasuaji watu wasiokuwa na ujuzi matokeo yake badala ya kunusuru maisha ya akina mama wataweza kufa kwa wingi.

Kwa hiyo, ninaiomba Serikali ihakikishe madaktari na wataalam wanapelekwa katika *theatres* hizo zinazojengwa pamoja na wodi hizo zinazojengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie Mkoa wa Kigoma; Mkoa wa Kigoma karibu asilimia 65 hatuna watumishi kabisa. Ninaomba basi kwa sababu muda mrefu Mkoa wa Kigoma kutokana na miundombini haikuwa mizuri barabara tulikuwa hatuna, reli ilikuwa inasuasua, watumishi wallkuwa wakipangiwa Kigoma hawaendi, lakini sasa baada ya Mkoa wa Kigoma kuanza kufunguka tunaomba wataalam waweze kupelekwa Kigoma ili tuweze kupata watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika Hospitali ya Kasulu tuna madaktari wanne na mahitaji ya madaktari ni 23, kwa hiyo tuna upungufu wa madaktari 19. Lakini wapo Madaktari Wasaidizi, mahitaji ni 35 lakini tunao wanne, pungufu 31 na ma-nurse pamoja na wauguzi kwa kweli hawatoshi, tunaomba mtusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Kibondo kama nilivyoeleza wiki iliyopita wakati nauliza swalii la nyongeza. Mkoa wetu wa Kigoma kuna wakimbizi, wakimbizi wanaotoka katika maeneo mbalimbali ya makambi ya wakimbizi wengine wanapelekwa katika Hospitali ya Kibondo, kwa hiyo, tunahitaji watumishi waweze kuongezwa katika Hospitali ya Kibondo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Kakonko ni Wilaya mpya hakuna Hospitali ya Wilaya na wagonjwa ni wengi kwa sababu Wilaya ile inapakanwa na Mkoa wa Kagera, wapo wagonjwa wengine wanaotoka mkoa wa jirani kuja kutibiwaa

katika kituo kile cha Kakonko, tunaomba Serikali ihakikishe Hospitali ya Wilaya ya Kakonko inamalizika haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hilo la hospitali liliopo Kibondo na Kakonko ni hivyo hivyo. Katika Kituo cha Mtendeli cha Wakimbizi, wakimbizi wanatoka kuja kutibiwa katika Kituo cha Afya cha Kakonko, kwa hiyo, naiomba Serikali ihakikishe Hospitali ya Wilaya ya Kakonko inajengwa haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Mama Ummey Mwalimu, Waziri, Naibu Waziri wake pamoja na watendaji wake wote, Katibu Mkuu na Wakurugenzi kwa kitabu kizuri walichotuletea ambapo wameelezea utekelezaji wa nyuma na utekelezaji kwa mwaka 2018/2019 sasa unalinganisha na unaiona faraja katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie na pia kutoa pongezi nyingine juu ya kinga ya saratani. Kwa kweli, hii kinga ya vijana wetu wale wa miaka tisa mpaka 14 ni nzuri, lakini hii kinga inayotolewa je, vijana wetu wamepewa elimu? Unakwenda kumpeleka kwenye kinga anapata kinga ye ye anajua ana kinga, lakini hizo kinga unazompa umpe na elimu namna ya kuweza kujikinga na ile kinga aliyokuwa nayo na elimu hii bado sijaiona na hata kwenye hiki kitabu chako sijaiona, ningeomba hili mliangalie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni la ugonjwa wa fistula. Fistula anapata wa mjini, anapata wa vijijini na ukiangalia utakuta hospitali inayoshughulikia siyo hospitali ya Serikali, ni hospitali ambayo imekubali kujitolea na kutoa huduma za bure kwa anayetibiwa hata kama yuko kijijini, nauli mpaka anaweza kufika akatibiwa. Sasa mimi

ninashangaa kwa nini Serikali na ninyi msingeingia hamu mkaona hili jambo muweze kulitekeleza kama Serikali, mkaapeleka vituo katika Mikoa. Kumtoa mtu kijjini kuja mjini kutibiwa ndiyo mtakuta baadhi ya wananchi hawawezi kuja hawesi kuiacha familia yake akaja huku wakati anajua anakuja kupata matibabu, lakini kama na Mikoani mngeweka vituo ambavyo vikaweza kutibu fistula ambayo inatibika, ingekuwa vizuri zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye suala lingine ambalo ilikuwa linazungumzwa mara nydingi na kwenye hiki kitabu suaona. Walikuwa wanazungumza kuna *kit bag* ina vifaa au zana mama anapokwenda kuzaa anakuwa navyo. Hata Dar es Salaam wakati wa pasaka Mheshimiwa Makonda alivitumia kama yeye alitoa msaada kwa akina mama na ambapo ilisemekana vinauzwa, sikumbuki kama ile *kit bag* moja ni shillingi 20,000 au kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini msingefanya vikawa bure mkaviweka hospitali kwa anayekwenda kujifungua akifika ana uhakika kwamba atapata zana za kutosha ambazo zimetolewa na Serikali.

Kwa hiyo, inavyoonesha hizi *kit bags* syo mbaya, mimi naona hata mtakapokuwa katika ushirikiano baina ya Bara na Visiwani ingawa Visiwani kule inatolewa matibabu ni bure, ni Sera ya Zanzibar, lakini na ninyi pia mngeipeleka hii elimu wa kuwa na *kit bags* kama zile wakaweza kuwawekea akina mama wakati wanakwenda kujifungua wakapata wepesi na kuwa na uhakika kuna kitu kinaweza kunisaidia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 21, namba 23 ilikuwa inaelezea ujenzi wa vituo vya afya ambapo ilikuwa TAMISEMI ishirikiane na Wizara ya Afya muweze kujenga vituo vya afya vya vijiji, Wilaya na Kata, lakini hadi hii leo mnazungumzia tu mnaboresha vya zamani vya zamani tunajua viro, tunataka vipya vijengwe na ni muda mrefu havijajengwa. (*Makofî*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na haya mengine yaliyobakia nitayaleta kwa maandishi. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunawashukuru kwa michango, lakini nitaje majina machache yatakayochangia mchana kabla ya mtoa hoja wetu kuhitimisha hoja yake. Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli, Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga, Mheshimiwa Janeth Masaburi, Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Hussein Bashe, Mheshimiwa Rashid Chuachua na kama muda utaturuhusu tutaendelea na Mheshimiwa Mashimba Ndaki na Mheshimiwa Daniel Mtuka.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni leo.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

NAIBU SPIKA: Tukae Waheshimiwa. Katibu.

NDG. ATHUMAN HUSSEIN – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya,
Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa
Mwaka wa Fedha 2018/2019**

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na mjadala, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma atafuatiwa na Mheshimiwa Joram Ismail Hongoli na Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga ajiandae.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii.

Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mungu na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara ya Afya, napenda kutoa shukrani kwa Serikali yetu ya Awamu ya Tano kwa mambo mazuri inayotufanyia Mkoa wa Morogoro. Imetupatia fedha kwa vituo vitano ambavyo ni Gairo, Mtimbira, Kidodi, Mkuyuni, Kibati na Rupiro. Kwa upande wa Mtimbira tumepeata shilingi bilioni 500 kwa ujenzi pamoja na ukarabati na vituo vingine vilivyosalia tumepeata shilingi bilioni 400 kwa kila kituo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri Ifakara Mji, Ifakara hawana Hospitali ya Wilaya na mara kwa mara wanatumia kibaoni Kituo cha Afya Kibaoni kama hospitali yao ya Wilaya. Maombi yalishaletwa ya kukipandisha kituo hiki kiwe Hospitali ya Wilaya. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aweze kuona kuna haja ya kuipandisha hadhi na kuwa Hospitali ya Wilaya kwa sababu wanakihitaji hasa akina mama na watoto ambaao mpaka sasa hivi majengo yapo, lakini kinachokosekana hakuna wodi ya watoto njiti ambaao wanazaliwa kabla ya muda wao na wanachanganywa pamoja na watoto ambaao wanaumwa, namna hii wanaweza wakapata maradhi kutokana na mchanganyiko huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwininge naomba pia kwa upande wa hospitali ya Rufaa ya Mkoa ambayo mara nydingi tumekuwa tunaomba *x-ray* pamoja na chumba pekee cha upasuaji wa mifupa, nyote mnajua kuwa Mkoa wa Morogoro unapokea watu wengi ambaao wanapa ajali, pia tunaomba gari la wagonjwa tuweze kuongezewa gari lingine kwa sababu Manispaa yetu ina kata 29 pamoja na Wilaya zingine ambazo hazina hospitali na zinatumia Hospitali hii ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezea hapo kuna Wilaya ambazo hazina hospitali kwa mfano Gairo, Kilombero

nilivyosema pamoja na Morogoro Manispaa. Kwa hiyo, naomba sana kuwa tuweze kujengewa hospitali hizi kusudi kupunguza mrundikano wa wagonjwa kwenye Hospitali yetu ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bima ya Afya ni mpango wa Serikali kuwa kila mmoja aweze kutumia bima ya afya. Kwa hiyo, mkakati uliowekwa na Serikali wa kuona kuwa kila mmoja aweze kutumia Bima ya Afya kuangaliwa kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kuhusu suala la lishe, kwa ukweli kwenye upande wa nchi yetu ya Tanzania bado lishe inahitajika kwa wingi, bado tuna udumavu, bado tuna ukondevu na ninasema kuwa tuna *malnutrition* ambayo imepitiliza. Naomba hii mikakati ya ambayo wameiweka waweze kultimiza na naomba kwa sababu suala la lishe ni mtambuka waweze kushirikiana pamoja na Wizara ya Kilimo kwa sababu unaweza ukatumia vyakula na ukapata vitaminini pamoja na *minerals*.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa wataalam wa Maendeleo ya Jamii. Ni ukweli usiopingika kuwa wataalam wa Maendeleo ya Jamii ndiyo wanaosukuma maendeleo kwenye Mikoa yetu, kwenye kata zetu na kwenye vijiji vyetu, uliangalie suala hili ili kusudi tuweze kuwa na wataalam wa Maendeleo ya Jamii kwenye kila kijiji na kwenye kila kata kusudi tuweze kusukuma maendeleo ambayo ndiyo yanatakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuongelea uwezeshaji wa wanawake, kuna asilima tano ambayo pamoja na TAMISEMI naomba muweze kushirikiana na TAMISEMI ili kusudi hawa Maendeleo ya Jamii ndiyo wanaosukuma maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema kuwa naunga mkono hoja na Mwenyezi Mungu akubariki kwa kunipatia nafasi hii na nawapenda sana. Ahsanteni sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa kwa kutupenda. Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli atafuatiwa na Mheshimiwa Joel Mwaka Makanya na Mheshimiwa Susan Lyimo ajiandae.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii. Nianze kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Wazri kazi kubwa ambazo wanazifanya kwa ajili ya kuboresha afya za Watanzania nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda hautoshi nichangie kidogo juu ya afya na usafi wa mazingira. Naipongeza Serikali kwa kuanzisha hii kampeni ya usafi wa mazingira na kuhakikisha kwamba Watanzania wanatumia vyoo bora. Ni dhahiri kwamba kama inavyooneshwaa kwenye taarifa matumizi ya vyoo bora imeongezeka toka 1,996,413 mwezi Juni, 2017 na mpaka hadi sasa hivi kuna vyoo milioni 2,414, 094 ilipofika Desemba. Nipongeza sana ni dhahiri kwamba tunapoboresha vyoo ni kwamba tunapunguza magonjwa ambayo yanababishwa na uchafu. Kwa hiyo, ninapongeza kwa kufanya hivyo maana yake tunapunguza gharama za kutibu haya magonjwa ambayo yanatokana na kukosa vyoo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmshauri ya Wilaya ya Njombe imekuwa ikiongoza katika usafi huu wa vyoo na mazingira bora toka mwaka 2013, ilikuwa ya kwanza mwaka 2014 kijiji cha Wagenyi kilikuwa cha kwanza na Halmashauri ilikuwa ya kwanza, mwaka 2015 kijiji cha Image kilikuwa kijiji cha pili na Halmashauri ilikuwa ya pili, mwaka 2016 kijiji cha Wanginyi kilikuwa cha kwanza, Matiganjola kikawa cha pili Sovi cha tatu na Halmashauri yangu ilikuwa ya kwanza ninaishukuru Serikali ilitupatia zawadi ya gari *Land Cruiser*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2017 kijiji changu ambako mimi natoka ninakoishi kijiji cha Kanikere kiliongoza nchi hii na kuwa cha kwanza, lakini kijiji cha pili kilikuwa kijiji cha Nambara cha kutoka Mara, kijiji cha tatu kilikuwa kijiji

cha Lyalalo kutoka Jimbo la Lupembe, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe na kijiji cha nne kilikuwa cha Image.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nijue vizuri Waziri utakaposimama utueleze vizuri maana yake nilikuwa napiga hesabu hapa, hesabu ndogo tu ilitumika hapa ukipiga hesabu utakuta kwamba Halmashauri ambaye ilitakiwa iwe ya kwanza ni Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, maana kuna vijiji vitatu viro namba moja, namba tatu na namba nne lakini cha kushangaza tukaambiwa kwamba sisi ni namba mbili Halmashauri ambayo ina kijiji kimekuwa namba moja. Sasa nataka nipate ufanuzi ni kwa nini Halmashauri tena haikuwa ya kwanza wakati kuna vijiji namba moja, kijiji namba tatu, kijiji namba nne kinatoka Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, lakini kijiji cha Nambara ambacho kipo Meru kilikuwa cha pili na Halmashauri ikawa ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika *simple arithmetics* naona kama kidogo inagoma, basi utanisaidia mwishoni kutoa ufanuzi ilikuwaje na hesabu zilipigwaje Halmashauri yangu ikawa ya pili badala ya kuwa wa kwanza. (*Makofii*)

Pia ninaipongeza Serikali kwa kuja na mpango huu wa hasa huduma ya *CHF* kuhakikisha kwamba tunatoka kwenye *CHF* ambapo mwananchi alikuwa anakatia kwenye kituo cha afya au zahanati hapo na anatakiwa kutiwa kwenye eneo lake husika tu na kuna maeneo mengine tunaenda mbali tukawa tunatibiwa kwenye Kata kwenye Halmashauri moja ndani ya Halmashauri anaweza akatibiwa sehemu yoyote ile, lakini sasa hivi Serikali imeenda mbali zaidi kuhakikisha kwamba kwa mpango huu unoitwa *ICHF* sasa wananchi wataweza kutumia hiyo *CHF* iliyoboresha kutibiwa ndani ya Mkoa kwa maana wataweza kutibiwa mpaka kwenye Hospitali ya Rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hatua kubwa sana naipongeza sana Serikali, naamini kwamba kupitia mpango huu wananchi wetu hasa ambao wanaishi maeneo ya vijiji ambao kwao tiba imekuwa ni changamoto kubwa, hasa

wanapotoka nje ya Halmashauri sasa watapata matibabu kirahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru Serikali na niunge mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga atafuatiwa na Mheshimiwa Susan Lyimo; Mheshimiwa Bonna Kaluwa ajiandae.

MHE. JOEL M. MAKANYAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nashukuru sana kunipa nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii ya Afya, na mimi nianze kwa kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara ya Afya kwa kazi nzuri na kubwa wanayoifanya, tumeona hata katika uwasilishaji wa bajeti yao hotuba yao ilivyosheheni mambo yaliyo ya muhimu sana kwa wananchi wa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijikite kwanza kabisa kusema Watanzania tunayo kazi kubwa sana mbele yetu, kazi hii tumedhamiria kwamba tuondoke hapa tulipo kwenye ulimwengu wa tatu, nchi maskini, tuingie angalau kwenye nchi yenye uchumi wa kati. Ili tuweze kufanikiwa katika hili kama afya zetu zitakuwa mgogoro hatutaweza kufika huko salama, tutakuwa tunasuasua sana na itatuchukua miaka mingi kufika kwenye nchi ya uchumi wa kati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nichukue nafsi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu katika maadhisho ya siku ya usafi wa mazingira na ujenzi wa vyoo bora kimkoa Dodoma yalifanyika katika Kata ya Aneti kijiji cha Umekwa katika Jimbo langu la Chilonwa. Namshukuru sana kwamba alishiriki pamoja na kushiriki aliweza kutoa ahadi mbalimbali kwamba atasaidia kumalizia ujenzi wa chumba cha upasuaji pale kwenye Kituo cha Afya cha Aneti nakushukuru sana Mheshimiwa Ummy kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile aliahidi kutupatia

madaktari katika Zahanati za Aneti, Chinene pamoja Umekwa katika Kata hiyo ya Aneti. Kama vile haitoshi kwa sababu ya *speed* kali tunayokwenda nayo hadi sasa tunavyoongea katika kijiji cha Aneti tayari tumeshapewa daktari mmoja, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia uliahidi kuipatia shule ya msingi Umekwa shilingi 400,000 kwa ajili ujenzi wa vyoo bora pale shulenii, nashukuru sana kwa haya mambo mazito unayotufanya. Nisimalize bila kukushukuru sana wewe pamoja na Wizara yako kwa kutuangalia Chamwino kwa jicho la huruma sana kwamba ultupatia fedha kwa ya ajili ya kuboresha pale kituo cha afya cha Chamwino shilingi milioni 500, lakini pia ukutupatia fedha kwa ajili ya kuboresha zahanati ya Mpunguzi shilingi milioni 700 na juzi pia umetupatia tena fedha kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Chamwino shilingi bilioni 1.5, tunakushukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nimalize kwa kukuomba Mheshimiwa Waziri tuna mahitaji mengi sana ya afya katika Jimbo la Chilonwa, nakuomba sana uliangalie kwa huruma sana kijiji cha Kwahemu ambapo wananchi wameanza ujenzi wa zahanati, lakini wamefika njiani tukisaidiana wote pamoja na Mbunge, Diwani na nani tunasuasua, tunaomba sana utuangalie pale kama unaweza kutusaidia angalau tuweze kumalizia ile zahanati, kijiji hicho kiko ndani sana, kiasi kwamba kusafiri toka pale kwenda Aneti inakuwa shida sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache nashukuru sana, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Susan Lyimo atafuatiwa na Mheshimiwa Bonna Kaluwa, Mheshimiwa Rashid Shangazi ajiandae.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Naibu Spika,

nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ili na mimi niweze kuchangia hoja hii muhimu sana ya Wizara ya Afya, kwa sababu wote tunaamini kwamba hakuna Taifa lolote linaweza kuendelea bila afya na hata viwanda tunavyotaka kwenda kuvijenga kama Watanzania watakuwa na afya mgogoro ni matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Wabunge kazi yetu kubwa ni kuishauri Serikali, lakini jambo ambalo linasikitisha sana kazi kubwa pia ya kwetu ni kupidisha bajeti/ kuidhinisha bajeti, tukiamini kwamba bajeti tunayoipitisha inaenda kufanya kazi yake vizuri. Lakini ni jambo la kusikitisha sana kama tunaweza kupidisha bajeti ya maendeleo mwaka jana tulipitisha shilingi bilioni 785 lakini cha ajabu fedha za ndani ukiangalia ni asilimia 17 tu zimeweza kwenda. Kati ya hizo ni shilingi bilioni 64 tu ndani zimeweza kwenda sawa na asilimia 17.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo tunawezaje kusema kweli afya zetu zitaboreka. Katika hilo tunawezaje kwenda kusema kwamba hospitali zetu zinaboreshw, vifaatiba vinanunuliwa, haiwezekani na wala hailingii akilini. Kwa hiyo, naona saa nyingine kwamba hakuna hata sababu ya kupidisha bajeti kama bajeti tunazopitisha hazitoki hela zinakuwa kwenye makaratsi, lakini uhalisia hakuna, yet Bunge linatumia fedha nyingi Wabunge wake kwenda kukagua miradi, miradi ambayo hakuna hata shilingi moja tumeweka, nadhani hata hao watendaji wanatuona sisi ni watu wa ajabu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nitakuja kuomba mwongozo kuna sababu gani kweli ya Wabunge kukaa hapa miezi mitatu, tunapisha bajeti ambayo kiuhalisia haiendi kufanya hiyo kazi wala hela hazitoki, hizi hela huwa zinakwenda wapi? Kwa sababu kama *TRA* wanakusanya..., tunajua kwamba tunatumia *recurrent* bajeti, lakini haiwezekani hela za ndani ziende asilimia 17.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala nzima la afya ya mama na jana Mheshimiwa Kangi Lugola alisema

kwamba tuwe na llani za CCM, nimejaribu kwenda kusoma llani ya CCM. Moja ya mambo ni kupunguza vifo vya watoto soma Ibara ya 85, lakini tunashangaa kama llani inasema ni kupunguza vifo na vifo vinaendelea vya akina mama maana yake hatuna sababu ya kusoma llani ya CCM labda tusome ya Vyama vingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija pia kwenye fedha zilizotengwa mwaka jana zilitengwa shilingi bilioni kumi na mbili na milioni mia moja, mwaka huu wameongeza shilingi milioni mia moja lakini hawajatuambia zile shilingi bilioni kumi na mbili za mwaka jana zilienda chache sana. Ukiendelea kuangalia haya mambo najua Mawaziri wanajitahidi sana lakini wanafanyaje kazi kama hakuna pesa. Kwa hiyo, haya mambo kwa kweli ni kuyaangalia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaongelea wanawake wengi wanavyofariki, lakini sijajua nchi hii tumerogwa na nani, mimi naamini aliyetuloga ameshakufa na huko alikozikwa hatujui twende tukafanye matambiko. Leo Tanzania asilimia 70 ya Watanzania ni wakulima lakini tunaambiwa kila dakika 12 mtoto mmoja anafariki kwa sababu ya lishe. Nimepiga mahesabu kama mtoto mmoja anakufa ndani ya dakika 12 ina maana kwa sasa moja wanakufa watoto watano, kwa mwezi mmoja watoto 3,600, kwa mwaka watoto 43,000 kwa uhai wa Bunge miaka mitano ni watoto 219,000. Hili ni janga la Taifa na ninadhani lazima kuwe na mkakati maalum wa kuhakikisha kwamba watoto wanawekewa lishe. (*Makofi*)

(Hapa kengele ya kwanza illilia)

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mimi nina dakika kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, twende kwenye suala la Wazee najua halijazungumzwa kwa sababu Wizara hii ni kubwa. Mimi nina *declare interest* kwamba ni Makamu Mwenyekiti wa Wazee Taifa wa Chama changu, kwa maana hiyo nina kila sababu ya kuzungumzia matatizo makubwa ya wazee.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Serikali ituambie mwaka 2003 walipitisha Sera ya Wazee, kila nikisimama kuhusiana na masuala ya wazee nazungumzia huwezi kuwa na sera kama hatuna sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2017 walikuwa na mkakati wa kufuatilia mauaji ya wazee, kama tungekuwa na Sheria ya Wazee maana yake ni kwamba haya mambo yangekuwa yamewekwa na vifo nya wazee vingepungua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunajua kwamba ni wazee watarajiwa, lakini wazee wa Taifa hili wameendelea kuishi kwa matatizo makubwa. Mlizungumzia kwenye ilani yenu kwamba wazee watapatiwa bima na kwamba watakuwa wanatibiwa bure kwenye vituo nya afya. Ninalosoma, Ilani ya Chama cha Mapinduzi Ibara ya 85(h) inasema; "Kuimarisha huduma za matibabu ya wazee nchini kwa kuwapatia vitambulisho na kuwatungia sheria matibabu yao ya bure ili waweze kutibiwa bure katika vituo vyote bila usumbufu wowote."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa kiasi gani mmetekeleza hili? Wazee wanapata matatizo makubwa sana, wazee wanadharaulika hawana hata hivyo vitambulisho, kama wanavyo ni wachache sana. Hii ndiyo Ilani yenu ya 2010/2015 hamjaitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, walisema kwenye ilani yao kwamba watanunua magari 10 kwa vituo 10 nya wazee; mtuambie ni vituo vingapi nya wazee hapa nchini vimepata magari?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nzungumzie kuhusu suala la matatizo ya afya ya akili (*Generalize Anxiety Disorders*). Kwa Jiji la Dar es salaam mwaka jana watu 150 mpaka 200 walikuwa wana-report kwenye vituo kwamba wana matatizo ya afya ya akili, hiyo ni kwa Dar es Salaam, ina maana tatizo hili linaendelea kukua kutokana na hali ngumu ya maisha, kutokana na wasiwasi, hawajui kesho yao

itakuaje. Hata hivyo hatuna wataalam wanaoshughulika na afya ya akili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba tuna hospitali kubwa ya Mirembe, tumewahi kwenda kutembelea pamoja na Kamati yangu matatizo ni makubwa sana, watalaan ni wachache sana. Hata hivyo pamoja na kwamba watalaan hawa wachache bado Serikali hajaona umuhimu na ndio sababu tumeona kwamba tuna tatizo kubwa la watalaan wa afya mabingwa. Tuna upungufu wa takribani mabingwa 500, na hatujaona mkakati wowote wa Serikali kuhakikisha kwamba tulikuwa na mabingwa hawa ili waweze kusaidia watu wetu. Leo tunapita barabarani tunaona watu wanatembea hawajielewi, Serikali ina mkakati gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hili suala la kwenda kutibiwa nje, na kwenda kutibiwa nje kuna *process* ndefu kama ambavyo hata Mheshimiwa Spika amesema hata wengine tumewahi kwenda nje. Hainiingii akilini, juzi nimemsikia Mheshimiwa Waziri wa Afya akizungumza na nitaomba baadae atupe majibu wkaati aki-*wind up*; anasema kwamba lazima uhakiki ufanyike, mimi nakubaliana naye. Hata hivyo anaposema yawezekana watu wengine wamekwenda tu kufanya *plastic surgery*; kubadili maumbile au kuongeza maumbile au kufanya vyovyote vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata shida sana, kwamba inawezekana hawa wanaokwenda kufanya hivyo hawakupita katika utaraibu wa kawaida, ni vigogo. Mimi ninaamini wananchi wa Tanzania mpaka upate kibali cha kwenda nje ni *hassle* kubwa sana, lazima jopo la madaktari likae, waangalie, wajue ni ugonjwa gani. Sasa mimi ninaposikia Waziri anasema wengine wamekwenda kufanya mambo mengine ambayo ni kinyume mimi nashindwa kuelewa, na nitaomba aje atuambie ni kwa sababu gani na wizara yake imefanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia. Ni jambo la kusikitisha kwamba Fungu 53 ambalo

ndilo la maendeleo ya jamii limepewa shilingi bilioni 4.9 tu; na mimi nadhani huku ndiko kwenye maafisa ustawi wa jamii nashani na ndiyo sababu hawa maafisa ustawi wa jamii imeshindikana sasa kazi hizo wapelekwe kwa Makonda kule Dar es Salaam na matokeo yake ndiyo haya. Kwamba wizara imeshindwa kufanyakazi yake vizuri inamkabidhi kazi hiyo Makonda na Makonda hana watalaaam. Kwa hiyo, ninaomba sana Wizara hii fungu namba 53 lipewe fedha ili watoto wetu waweze kuthaminiwa ...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha saa ile pale Mheshimiwa muda wako umekwisha kihalali kabisa.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Mheshimiwa Bonnah Kaluwa atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Hussein Bashe ajiandae.

MHE. BONNAH M. KALUWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipanafasi hii. Kwanza naomba nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa ambayo inafanya hususani kweye mambo ya usambazaji wa dawa, lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy kwa kazi kubwa ambayo anaifanya, sisi wote Watanzania tunaiona, tunakupongeza sana na kama mwanamke tunajivunia wewe kuwa hapo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Naibu Waziri wa Afya kwa kazi kubwa wanayoifanya ambapo wanazunguka na kuangalia ni sehemu gani kuna changamoto, lakini pia na kuendelea kutatua hizo changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, naomba sasa niongee changamoto ambazo zinalikabili Jimbo langu. Jimbo langu mwaka 2016/2017 liliikuwa lina watu 773,000; Jimbo langu lina kata 13 lakini mpaka sasa

hivi Jimbo langu halina kituo cha afya. Najua haya mambo yako TAMISEMI Mheshimiwa Ummy, lakini naliongelea kwako kwa sababu wewe ndiye unayeangalia sera, na sera yetu ya afya inasema kila kata iwe na kituo cha afya na kila kijiji kiwe na zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi watu wa mijini hatuna kijiji, tuna mitaa. Kwa hiyo, nilikuwa nakuomba sana Mheshimiwa Ummy, Jimbo la Segerea, nilisimama mwaka 2016 na 2017 nikiongelea usimamizi wa sera, tunahitaji tupate kituo cha afya. Kutoka kata ya Kisukulu mpaka Amana ni kilomita tisa, kwa hiyo, wananchi wanapata shida sana. Unaweza ukaangalia kwamba labda kwa sababu sisi tunakaa mijini ndiyo maana; labda kwa sababu kuna hospitali nyingi ambapo wananchi wanaweza kutibiwa, lakini ujue kwamba tuna changamoto moja kwamba mtu anapotoka sehemu ya mbali kwenda Amana kwanza kuna foleni ya magari, lakini pia kuna changamoto nyingine ni za mrundikano wa watu kwa sababu watu wote wanakwenda Amana, ni kwa sababu hatuna kituo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na Mheshimiwa Waziri mimi katika Jimbo langu, mfano, kama ukiongelea kata ya Vingunguti ina watu 200,000 na mpaka sasa hivi haina kituo cha afya wala zahanati yake pia haina miundombinu mizuri. (*Makof*)

Kwa hiyo, nilikuwa nakuomba Mheshimiwa Ummy, Mheshimiwa Waziri na Wizara yote ya Afya muangalie vizuri Jimbo la Segerea, msimamie hizo sera ili tuweze kupata kituo cha afya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nimeshafanya na Naibu Waziri tumekwenda kata ya Segerea, tukaenda kata ya Mnyamani. Halmashaauri ya Manispaa ya Ilala imeshatoa fidia kwa nyumba ambazo zilikuwa zinaizunguka Hospitali ya *Plan International*/kwa ajili ya kupanua kile kituo ili kiweze kuwa kituo cha afya. Tumeshafanya hivyo, Mkurugenzi tayari ameshatoa hela sasa tunawasubiri ninyi Wizara ili muweze kutuboreshea sasa na kukipandisha hadhi kiwe kituo ili

wananchi wanaokaa Jimbo la Segerea wasiweze kwenda Amana au wasiwe kwenda sehemu zingine waweze kuishia pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nilitaka kuongelea suala la *delivery kits* ambalo wajumbe wengine waliweza kuliongelea. Mambo ya uzazi ni mambo ya baraka lakini pia ni mambo ya maumbile na pia ni mambo ya majaliwa. Kwa hiyo, nilitaka niongee na Mheshimiwa Waziri, na kwa sababu Mheshimiwa Waziri ni mwanamke najua atalifanya kazi. Kuna watu wengine ambao wako vijijini akina mama wenzetu hawawezi kununua kwa shilingi 22,000 au shilingi 25,000. Sasa nilitaka niiombe Serikali waangalie wanaweza kuwasaidiaje akina mama wenzetu ambao wako kijjini ambao hawawezi kutoa hizo fedha ili waweze kupata hiyo *delivery kits*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri uweze kunaangalia. Tunajua kwamba lazima na sisi wananchi lazima tuweze kuchangia kiogo katika Serikali lakini pia lazima tuangalie na wananchi wenzetu ambao wanakaa nje ya mijini kwa sababu sisi wa Mijini pengine tunaweza tukawa tuna hizo pesa za kutoa ili tuweze kuangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Rashid Shangazi atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Bashe, Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua ajiandae.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nitoe pongezi kwa dada yangu Mheshimiwa Ummy kwa kazi kubwa anayoifanya, kazi inaonekana, chapa mwendo tuko pamoja na wewe. Lakini shukrani za pekee nizitoe mimi kama Mbunge wa Jimbo la Mlalo kwa msaada mkubwa wa mabati ulichotupatia katika kituo chetu Mwangoi, tunashukuru sana. Nitoe pia pongezi kwa Mheshimiwa Naibu Spika kama Balozi

wa Afya katika Jimbo la Mlalo, umefanya mambo makubwa sana, Mwenyezi Mungu aendeleee kukubariki na ile wodi ambayo tumeipa jina lako sasa tuko katika hatua za usafi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa haraka sana nichangie katika hoja iliyopo mbele ya Bunge lako Tukufu, nikianza katika ukurasa wa 112, vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2018/2019, kipengele namba mbili, kuimarisha huduma ya kinga dhidi ya magonjwa yanayotokana na kutokuzingatia kanuni za usafi na usafi wa mazingira kama magonjwa ya kuhara, kuhara damu, kipindipindu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ipo kampeni inayoendelea sasa hivi ya "usichukulie poa nyumba ni choo" hapa kuna jambo la msingi saa ambalo Wizara inatakiwa ilifanyie kazi. Nimefanya utafiti mdogo katika Jimbo langu nimegundua kwamba watoto wengi wa shule ndio ambao wanaugua ugonjwa wa *UTI* na sababu kubwa inayosababisha tatizo hili ni ukosefu wa vyoo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninaitaka sasa Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI watengeneze mkakati mahsus wa kuhakikisha kwamba shule zetu za msingi na sekondari zinakuwa na vyoo bora kabisa. Inawezekana kabisa kila mwaka tunasema bajeti ya Wizara ni kubwa, haiongezeki lakini inawezekana tukawa tunahitaji bajeti kubwa kwa kuwaaminisha kwamba Watanzania ni wagonjwa sana kumbe tatizo siyo ugonjwa labda tukipata elimu inawezekana bajeti hii ikapungua kabisa wala hatuhitaji kuwa na mabilioni mengi katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba sana hii kampani ya "usichukulie poa maisha ni choo" tuiendeleze na hata kule kwa wenzetu Wasukuma kule Mwanza tunaona nyumba ziko milimani kule na hatujui hata vyoo wanachimbia maeneo gani, naamini katika hili tutapunguza fedha nyingi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye *reportya CAG* amezungumzia deni la Wizara ya Afya katika hospitali zile za nje hasa kule India. Niombe Wizara ilifanyie kazi eneo hili. Wapo Watanzania wengi sana ambao wanahitaji rufaa za kwenda kupata matibabu nje, lakini wanashindwa kwenda kwa sababu tunadaiwa fedha kule.

Kwa hiyo, nikuombe dada yangu Ummy, wewe ni shahidi kuna mgonjwa mmoja nilikuomba angalau umsaidie alikuwa ameshapata kibali na alikuwa ameshapata kibali na alikuwa yuko tayari hata kujilipia nauli tatizo lilikuwa fedha za matibabu na natumia nafasi hii kukwambia kwamba Mwenyezi Mungu yule mgonjwa amempenda zaidi. Kwa hiyo, huoni kwamba ni Watanzania wengi wanapoteza uhai kwa kukosa fursa hii? Kwa hiyo, nawaomba sana Wizara isimamie hili ili liweze kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizingumzia ni suala la Kituo cha Saratani cha *Ocean Road*; wanafanyakazi nzuri sana lakini kwa kweli kuna msongmanao mkubwa. Nitoe rai kwa Wizara hii; hebu tutengeneze mkakati wa kuwa na hospitali kwa kanda, tunaweza tukaanza Kanda ya Ziwa pale Bungando, tukaenda Mbeya angalau pale hospitali ya Rufaa ya Mbeya tukatengeneza vituo vya saratani ili tupunguze ule msongamano pale Dar es Salaam. Wananchi wengi wanapata shida sana kwa kwenda mpaka Dar es Salaam kupata hii huduma ambayo sasa hivi sasa saratani imekuwa ni ugonjwa wa kawaida sana kwa ndugu zetu hawa.

Mheshimiwa naibu Spika, lingine nizungumzie huduma za hospitali katika Hospitali yetu ya Rufaa ya Mkoa Bombo pale Tanga, najua Mheshimiwa Waziri wewe ni mwenyeji vizuri pale, lakini siyo wakati wote unapata muda wa kuembelea pale. Huduma zetu bado zinahitaji kuboreshwa sana. Tunaye Daktari Bingwa nadhani ni mmoja tu, kwa hiyo bado tunahitaji tupate Madaktari Bingwa wa kutosha. Kama unavyojua jiongojia ya Mkoa wetu wananchi ni wengi sana wanaohitahi huduma katika hospitali hii, kwa hiyo, nikuombe sana na hili nalo ulizingatie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, ahsante sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua kama nafasi yetu itaruhusu atafuata Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa. Jambo la kwanza nitumie fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nzega kuishukuru Serikali kwa dhati kabisa kwa *support ambayo imetupa* katika *improvement* ya Kituo cha Afya cha Zogolo, lakini vilevile mpango uliopo kwa ajili ya vituo vya afya vya Mbogwe na Migua. Pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, na nikushukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Ummy kwa kazi kubwa unayoifanya kuhakikisha kwamba akina mama wanajifungua wakiwa salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilitaka nishauri mambo mawili madogo. *Improvement* tunayoifanya katika *referral hospital*, kwa mfano kama Muhimbili Serikali imafanya kazi kubwa sana ya ku-*improve* hospitali yetu ya Muhimbili na dhamira ya Wizara kuhakikisha kwamba akina mama wanajifungua salama nilitaka niiombe Serikali Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Afya na Wizara ya Mzee Mkuchika kutumia takwimu za *TASAF*, zile kaya maskini, ili tuweze ku-*establish* akina mama wanaotoka katika kaya maskini kabisa kuona au kuja na mpango wa namna gani wanaweza kupata zile *delivery kits* ili wasiweze kukumbana na lile zoezi la kuwa wanalipa shillingi 20,000 ama kwenda kununua kwa sababu kuna kaya ambazo ni maskini na kwa takwimu zetu kuna asilimia kama 28 mpaka 30 ya Watanzania ambao wako katika umasikini wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo nilitaka niiombe Wizara, *MSD* tunatenga fedha za dawa nyingi lakini bado kuna tatizo la *out of stock*. Nikitolea mfano katika Wiaya ya Nzega na Mheshimiwa Waziri wewe mwenyewe ulilionia katika ziara yako hivi juzi tulivyokwenda wote, mtu ana

bima, anafika katika dirisha anakosa dawa, ina-*discourage* watu kujiunga katika *National Health Insurance*. Mfano, jambo la pili ambalo ni la kusikitisha, tunaamini *MSD* wako katika mfumo ambao unawafanya waombaji wa dawa kuweza kupata *feedback* haraka ya kujua kwamba dawa hakuna lakini kupata ile barua ya kuwaruhusu kwamba *we are out of stock*, hatuna dawa kwenda kununua dawa katika *vendors* ambao mmewaruhusu inachukua *ages*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo hapa mkononi nina barua ilioandikwa na Daktari wa Hospitali ya Wilaya Nzega tarehe 27 Februari, aliomba idadi ya dawa tofauti 100. Kati ya hizo 100 akakosa 48, ile barua ya kumruhusu ili aende kwa *vendors* ili aweze kwenda kununua hizo dawa 48 tofauti mpaka leo hawajapata. Matokeo yake inaonekana kwamba fedha tunazotenga, wananchi wanaokwenda kupata dawa katika viuto vyetu vya afya ama hospitali zetu wanakuwa hawapati dawa kwa sababu ya *inefficiency*ya taasisi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nilitaka niiombe Serikali, tunatenga fedha kama Bunge na zile dawa muhimu ukiangalia bajeti ya mwaka jn ni *almost* asilimia 100 hazina wametoa fedha zake lakini zile dawa kuzipata kwa wakati katika vituo vya afya ni changamoto. Mimi niwa-*challenge* Serikali, tafuteni *solution*ya *MSD*na *delivery system* katika vituo vyetu vya afya kuhakikisha kwamba kinachoombwa kinapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi teknolojia imekua mtua anaweza akaomba kutokea ofisini kwake akajua *stock* iliyopo na ambayo haipo, *system* ikamruhusu kwenda kuomba katika *vendors* waliopo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *otherwise* mimi nitumie nafasi hii kuwashukuru sana na naunga mkono hoja, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua atafuatiwa na Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

MHE. MOHAMED R. CHUACHUA: Mheshimiwa Nabu Spika, ahsante sana kwa kupata nafasi hii ya mimi kuchangia angalau dakika tano. Nataka niseme tu kwamba naipongeza sana Serikali, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake inayoonesha kwamba tumepiga maendeleo makubwa sana katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo ningependa kuzungumza ni kuishukuru tena pia Serikali kwa kunipatia uhakika wa kupata fedha kwa ajili ya kujenga kituo kimoja cha afya cha mionganoni mwa kata zangu, kwangu mimi hili ni jambo kubwa sana katika kuboresha afya za wananchi wetu wa Masasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niongelee pia suala la Hospitali ya Kanda ya Rufaa. Ni muda mrefu sasa Serikali imekuwa ikizungumza na ikiwa na utaratibu wa kutaka kujenga Hospitali ya Kanda ya Rufaa katika Mkoa wa Mtwara, lakini kwa bahati mbaya sana jambo hili linakwenda taratibu mno. Tunasikia kwamba *NHI/F* wamepewa dhamana ya kutaka kumalizia hospitali hiyo, lakini mpaka sasa hatujui kwa sababu hatuoni kinachofanyika. Tungependa kusikia kauli ya Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja yake, ni kwa vipi wamejipanga kukamilisha Hospitali hii ya Kanda ambayo itakuwa inahudumia mikoa ya Ruvuma, Lindi pamoja na Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lakini nizungumze kidogo kuhusu suala la Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Wabunge wa Mtwara wamezungumza jambo hili na sisi katika jambo hili ni wa moja sana nataka kusema mionganoni mwa mambo ambayo ni magumu na ni mazito sana kwetu kuyatolea maelezo ni hali ya hospitali yetu ya mkoa. Hospitali hii ina hali mbaya sana kwa upande wa watumishi natoa tu mfano; kwa mfano tunatakiwa na Madaktari Bingwa 24 lakini tunao Madaktari Bingwa wawili tu, tunatakiwa tuwe na madaktari wa kawaida 30 tunao saba, Madaktari Masaidizi (*AMO Assitant Medical Officers*) tunatakiwa tuwe nao 23 tunao wanane tu, *nursing officer* wanatakiwa wawe 37 tunao wanne.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna upungufu wa ma-nurse wengi kwa sababu wanatakiwa wawe 131 tunao 44 tu. Hali ya hospitali hii ni mbaya na inajhitaji jicho la kipekee la Serikali ili kuhakikisha kwamba hospitali hii inaimarishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatukuishia hapo tu katika changamoto za hospitali hii kuna miundombinu chakavu sana. Tuna matatizo ya vifaa tiba, kwa mfano tunayo *x-ray* zeefu na ni ya kizamani sana na inaharibika mara kwa mara, tungependa Serikali sasa itupati *digital x-ray* ili tuweze kutoa huduma kwa wananchi wetu kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifika katika chumba cha upasuaji hata mashine ile ya kuchemshia vifaa nayo imezeeka sana, lakini pia inaharibika mara kwa mara na inakwamisha sana shughuli za hospitali. Mashine ya kufulia nguo pamoja na mashuka ya wagonjwa ni mbovu na imezeeka sana, tungependa Serikali iangalie mambo haya. Kwa bahati mbaya sana tunalo gari moja tu la kusadfirisha wagonjwa na gari hilo nalo limezeeka sana, tunasikia kwamba Serikali ina mpango wa kutenga fedha kwa ajili ya kununua gari lingeni la wagonjwa yaani *ambulance*, tungependa Serikali ikamilishe jambo hili haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Mji wangu wa Masasi hatujapata bado fedha kiasi fulani cha fedha katika mfuko wa afya. Tilitengewa shilingi millioni 187 tumepata shilingi milioni 76 tu. Tunaimani Serikali sasa inapaswa kuhakikisha kwamba fedha hizi zinakwenda haraka iwezekananvyo ili tuweze kupata nasi fursa ya kununua dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumze kidogo kuhusu huduma ya tumaini la mama; hii ni huduma nzuri na naipongeza sana Serikali kwa hatua iliyofikia. Hata hivyo nataka niseme kitu kimoja tu, kabla Serikali haijaanza jambo hili katika jimbo langu mimi nilikuwa natumia mfuko wa jimbo kununua *package* hizi kwa ajili ya akina mama kujifungulia. Hata hivyo hata baada ya Serikali kuanzisha utaratibu huu bado ninalazimika kutenga baadhi ya fedha kutoka kwenye mfuko wa jimbo kwa ajili ya kununua vifaa vy'a akina mama

kujifungulia kwa sababu huduma ya tumaini la mama haitoi vifaaa vyote tunaomba sasa Serikali kwa sababu huu ni mpangao ambao umeamua kuianzisha kwanza mpango huu uwe endelevu, lakini pili u-*accommodate* vifaa vyote ambavyo vinahitajika kwa ajili ya akina mama. (*Makofî*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Chuachua muda wako umekwisha, Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Afya.

Kwanza niwashukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na Naibu wake kwa kutupeleka mbele kwenye suala la afya kwenye nchi yetu. Wakati tunaanza Bunge hili kulikuwa na kelele za upatikanaji wa dawa, dawa zilikuwa hazipatikani kwenye zahanati, vituo vya afya na hata hospitali zetu, lakini leo tuna asilimia kama 80.

Pia kulikuwa na kelele za upatikanaji wa dawa za chanjo wakati tunaanza Bunge hili leo hatusikii kelele hizo zikiwapo, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake. Kiwango cha chanjo kwenye nchi yetu kimepanda mpaka asilimia 90 na kwa Afrika kama taarifa yao ilivyosema tuko watatu baada ya Rwanda na Zambia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwapongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa ujenzi wa miundombinu pamoja na upatikanaji wa vifaa na vifaa tiba. Niwashukuru sana kwa ajili ya kuniletea vifaatiba kwenye kituo changu cha afya cha Malampaka, tumepata vifaatiba vizuri vya kisasa vingi vinatosheleza pia tumepata pesa za kutosha kuweza kujenga wodi pamoja na majengo mengine, tunawashukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la upungufu wa watumishi wa afya sasa hivi kwenye nchi yetu ni mkubwa. Taarifa ya kamati inasema tuna upungufu wa asilimia 48, hiki ni kiwango kikubwa sana na hiki kinaenda mpaka kwenye maeneo yetu. Mkoa wa Simiyu tuna wataalam wenyewe ujuzi ambao wanaweza wakahudumia wagonjwa wachache sana. Kwa taarifa nilizonazo ni kwamba mwaka 2012 wakati mkoa unaanza tulikuwa na wataalam wenyewe ujuzi asilimia 2.6, lakini mwaka 2016 wameongezeka kidogo asilimia 4.8. Sasa ukijaribu kuangalia kiwango hiki ni kidogo sana. kwa Wilaya yangu ya Maswa ina upungufu wa watumishi wa afya 525, uhitaji ni 726 na walioopo ni 201 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo upungufu huu ni mkubwa Sana na nilkuwa nasihi kwamba Serikali sasa langalle tatizo hili kama tatizo kubwa linaloikumba nchi yetu na lishughulikiwe kwa pamoja Wizara ya Utumishi, Wizara ya Afya pamoja na Wizara ya TAMISEMI. Vinginevyo lishughulikiwe kama ambavyo tumeshughulikia tatizo la upatikanaji wa walimu kwa shule zetu. Suala hili lazima lifanyiwe hivyo vinginevyo watu wetu tutakuwa wanaangamia kwa sababu ya kukosa huduma kwenye vituo hivi ambavyo tuna bidii kubwa ya kuviboresha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala lingine ambalo halijazungumzwa kabisa; kuhusu uzazi wa mpango. Uzazi wa mpango sijaona hata kwenye hotuba ya Kamati hata hotuba ya Mheshimiwa Waziri mwenyewe. Hata hivyo najaribu kuangalia kwa mbele kwamba idadi ya watu inaongezeka kwa kasi sana. Nchini mwetu sasa inakadiriba kuwa na watu kama milioni 58 na tunavyoendelea mpaka mwaka 2022 pengine tutakuwa watu milioni sitini na kitu; na kwa kuangalia vizuri watoto watu walio chini ya umri wa miaka 15 kwenye nchi yetu ni nusu ya Watanzania. Sasa utaona Watanzania hawa watu wazima wanahudumia watu wengi kiasi gani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofî*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mungu na kumtakia rehema, kiongozi wa umma, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na wasaidizi wao ukiwemo wewe Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wasaidizi wenu kwa kazi nzuri mnayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa imefanyika na inaendelea kufanyika. Pamoja na juhudini nzuri na kubwa ambazo zimekwishafanyika kama ujenzi wa Hospitali ya Mloganzila, upatikanaji wa vifaa na dawa, magari ya kubeba wagonjwa na dawa, lakini ukweli changamoto hasa kwa sisi wenye majimbo ya vijiji tumeendelea kupata taabu na changamoto nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri yetu ya Chalinze, hitaji la wauguzi na waganga kwa ajili ya kutoa huduma za kitabibu imeendelea kuwa changamoto. Mfano, katika Kituo cha Afya Kibindu kuna daktari mmoja tu; ye ye asikilize mgonjwa, achome sindano, agawe dawa na hata pia atoe ushauri nasaha. Hapo sizungumzii wakati anatibu mgonjwa wa malaria au surua akaja mama mjamzito anayehitaji kujifungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudini kubwa, bado tunahitaji kubwa la waganga hasa katika vituo vya afya Kibindu, Miono, Msata, Lugoba, Vigwaza, Ubena na maeneo mengine yanayofanana na shida hii ya Halmashauri yetu ya Chalinze.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudini kubwa zinazofanyika na zinazofanywa na Halmashauri yetu ya Chalinze ya kujenga nyumba za waganga, natumia nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kutupatia fedha kiasi cha fedha halali shilingi milioni 750 kwa ujenzi wa vituo vya afya Lugoba na Kibindu. Licha ya juhudini hizo, ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Chalinze umeendelea kusucasua. Juhudi za Serikali ya Halmashauri ya wilaya ya Chalinze kumalizia zinazofanyika.

Mfano pesa kiasi milioni 50 zimetengwa, lakini ukweli nguvu hii inahitaji mkono wa Serikali kumalizia mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa hospitali hii kutapunguza rufaa zinazokwenda Kibaha na Bagamoyo hivyo kupunguza wingi au Lundo la wagonjwa katika hospitali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni tumeshuhudia zoezi lilioendelea pale Dar es Salaam ambalo kwa ukweli kabisa kumekuwa na uvunjifu mkubwa wa maadili na sheria ambazo zimesababisha hata heshima za watu kuvunjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine zoezi hili limeibua changamoto ya kuonesha kuwa kuna walakini katika taasisi zetu za kiutendaji. Hapa nakusudia Taasisi au Idara ya Ustawi wa Jamili. Taasisi hii illikuwa wapi kufanya haya? Je, mfumo gani wanatumia kufanya kazi? Je, kwa nini hawatoi elimu kwa wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Chalinze, miaka 13 iliyopita tulikubaliana kujenga shule za sekondari za kata. Katika makubaliano hayo, ujenzi wa mabweni kwa ajili ya kuwalaza vijana wetu wa kike na wa kiume ulikubaliwa. Matatizo makubwa hasa kwa watoto wa kike wanaoishi kwenye mabweni yamekuwapo kipindi wanapoingia kwenye siku zao za hedhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ombi kwa Serikali, kutokana na hali ngumu za maisha za wazazi wetu na hali ya malezi, niombe Serikali ikubali kuondoa kodi kwenye taulo hizi ili kuwezesha lengo la milenia la kumuelimisha mtoto wa kike kutimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Chalinze kijiografia ni jimbo pana sana na hata wakati mwingine huchukua umbali mrefu sana toka *point* moja ya Halmashauri kwenda *point* nyingine. Umbali huo umekuwa ni kero hasa kutokana na mapungufu ya magari ya kubebea wagonjwa kuwatoa zahanati au nyumbani/vijijini hadi kwenye hospitali

au kituo cha afya. Pamoja na hili hakuna gari la chanjo la Wilaya. Tunaomba gari la wagonjwa kwa Kituo cha Afya Lugoba na Kwaruhombo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kumkumbusha Mheshimiwa Waziri, ombi la Halmashauri kuhusu kuongezewa waganga ili kupambana na mapungufu yaliyopo sasa limeendelea kuwapo. Kwa sasa watumishi waliopo ni asilimia 30 ya mahitaji halisi. Kwa taarifa hadi sasa zipo zahanati ambazo zinaongozwa na wahudumu wa afya na hili limesababisha kushindikana kufunguliwa kwa zahanati mpya zilizojengwa huko Magulumatari, Talawanda na Buyuni Vigwaza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja tukafanye kazi sasa kutatua kero za afya Tanzania na hasa Chalinze.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na mimi niweze kuchangia kwenye bajeti ya Wizara hii ya Afya na Maendeleo ya Jamii. Kwanza kabisa naunga mkono mapendekezo ya Kamati maana na mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa kabisa ni upungufu na uchakavu wa zahanati na katika jimbo zima la Mikumi lenye kata 15 lina vituo vya afya viwili tu; yaani Kituo cha Afya cha Ulaya na Kituo cha Afya cha Kidodi ambacho tunashukuru sana tulipokea shilingi milioni 400 kwa ajili ya kukitanua na kukiboresha ili kiweze kuokoa maisha ya mama zetu na watoto pia kufanya upasuaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vituo viwili tu vya afya kwenye jimbo zima la Mikumi havitutoshii, Kituo cha Afya cha Ulaya kina hali mbaya sana, kimechakaa sana lakini pia kina upungufu mkubwa sana wa watumishi wa afya, wananchi wanateseka sana, wengi wanakimbilia hapo lakini kusema ukweli huduma zimekuwa mbaya sana na kuumiza sana wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zahanati zetu katika Jimbo la Mikumi zina hali mbaya sana na mimi kama Mbunge nimeshirikiana bega kwa bega na wananchi wenzangu wa Kata ya Malolo (vijiji vya Chabi na Mgogozi) kujenga zahanati mbili na tupo kwenye umalizaji, lakini pia kwenye Kata ya Masanze zahanati ya Kijiji cha Dodoma lsanga niliezeka kwa Mfuko wa Jimbo pia. Zahanati ya Kijiji cha Muungano na Nyali ambapo nimezikarabati pia kwa kupitia Mfuko wa Jimbo mwaka 2016/2017 lakini bado tuna changamoto kubwa sana kwenye Jimbo la Mikumi na tunaomba sana Mheshimiwa Waziri aweze kutusaidia kuunga mkono jitihada hizi za wananchi wa Jimbo la Mikumi.

Lakini pia Mji Mdogo wa Mikumi ambao kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 inaonesha kuwa kuna idadi ya watu wapatao 21,113 lakini Zahanati ya Mikumi imechakaa sana na ina uwezo mdogo sana wa kuhudumila wananchi hawa ambao wengi ni akina mama. Hivyo tunaomba sana Mheshimiwa Waziri na Serikali iweze kuboresha na kutanua ujenzi wa Zahanati ya Mikumi kuwa Kituo cha Afya ili kuondokana na adha ya huduma ya afya wanayoipata wakazi wa Mji Mdogo wa Mikumi; lakini pia Serikali iweze kusaidia ukarabati wa Zahanati za Uleling'ombe, Zombo, Kisanga, Tindiga, Vidunda, Mhenda, Ruhembe na Mabwerebwere na pia jiografia ya Jimbo la Mikumi ni mbaya sana hivyo tunaomba sana Serikali iweze kutusaidia magari ya wagonjwa ili tuweze kuokoa maisha ya akina mama na watoto ambao wengi sana wanapoteza maisha kwa sababu ya ukosefu wa *ambulance* na usafiri wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mji Mdogo wa Mikumi una hopsitali ya taasisi ya dini ya *St. Kizito* ambayo imekuwa ikitoa msaada mkubwa sana kwa wananchi wa mji wa kitalii wa Mikumi, lakini pia watu wa mataifa mbalimbali wanatumia barabara kuu ya Tanzania mpaka Zambia mpaka Afrika Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na umuhimu wa hospitali hii ya *St. Kizito*, Serikali ilikuwa inatoa ruzuku na kulipa mishahara ya baadhi ya watumishi, lakini katika hali

ya kusikitisha hospitali hii haijapata ruzuku hii kwa miaka kadhaa mfululizo na nilipokwenda kuzungumza nao walisema walikuwa wanapewa shilingi milioni 60 kwa mwaka ambazo kwanza zilikuwa hazitoshi. Lakini pia kwa sasa hawajazipata kwa miaka mitatu mfululizo, lakini pia kuna tetesi kuwa Serikali imeamua kusitisha mikataba na hospitali hizi muhimu za taasisi za kidini ambazo kwenye Wilaya yetu ya Kilosa zipo mbili yaani *St. Kizito* na Hospitali ya Berega ambayo ipo pia kwenye Wilaya yetu ya Kilosa. Tunaomba sana majibu ya Mheshimiwa Waziri ili tujuwe wameamua kuvunja mikataba yao na hospitali hizi za taasisi za kidini? Na kama jibu ni hilo Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi wa Wilaya ya Kilosa hasa Jimbo la Mikumi ambao wengi ni maskini na gharama za huduma ya afya zimekuwa kubwa sana na wameshindwa kuzimudu kutokana na taasisi hizo kutoza pesa nydingi kwa wananchi ili ziweze kujilendesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna upungufu mkubwa sana wa Maafisa Maendeleo kwenye kata zetu nydingi za Jimbo la Mikumi, lakini pia kwa masikitiko makubwa sana nifikishe malalamiko makubwa sana kwa Afisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Kilosa kwa kufanya kazi zake kisiaza zaidi na kushindwa kushirikiana na taasisi zinazotaka kuja Wilayani Kilosa hasa Jimboni kwangu Mikumi kwa kushindwa kutoa vibali kwa taasisi hizo zinazotaka kuja kutoa elimu kwa wananchi hasa vijana, akina mama na wazee ili waweze kujunga kwenye vikundi na kushirikiana na Ofisi ya Mbunge na Serikali ya Wilaya ili waweze kujiletea maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taasisi isiyokuwa ya Kiserikali ambayo inaitwa *Tanzania Bora Initiative* ambayo ilioneshwa nia njema ya kuja kutoa elimu na kuwaunganisha vijana kwenye Jimbo la Mikumi na Handeni na walifuata taratibu zote za Kiserikali ili waweze kusaidia wananchi wa maeneo hayo, lakini katika hali ya kusikitisha Afisa Maendeleo ya Wilaya ya Kilosa mpaka sasa anawapiga chenga kuwapa kibali cha kufanya kazi hii njema ya kuwafanya wananchi wajiunge pamoja na kujiletea maendeleo, tena kwa

kushirikiana na Serikali bila sababu za msingi na wamefuatilia kibali hicho cha kuja kufanya shughuli hizo muhimu kwa wananchi wa Wilaya ya Kilosa, Jimboni Mikumi ili waweze kushirikiana na Serikali yao kujiletea maendeleo yao. Ahsante sana.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kuhusu uhaba mkubwa wa watumishi wa afya; kutokana na jiografia ya Visima vya Ukerewe upatikanaji wa watumishi ni tatizo kubwa na hivyo kusababisha vifo vya mara kwa mara hasa mama wajawazito na watoto. Muda mfupi Kituo cha Afya cha Buisya kitakamilika lakini hakina wataalam wa kutosha ili kituo hiki kiwe na ufanisi. Watumishi sita pekee kwa kituo kama hiki ni jambo lisilo na afya. Hivyo, tunaomba watumishi wa afya wenye utaalam kwa ajili ya Kituo cha Afya Buisya na Ukerewe nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya afya kwa wazee; pamoja na Sera ya Afya kwa Wazee kutaka vitambulisho kutolewa bure kwa wazee bado wazee (hasa Wilayani Ukerewe) wamekuwa wanatozwa shilingi 1,000 ili kupata vitambulisho hivyo. Naomba Serikali itoe maelekezo/ kauli katika hili jambo ili kuepusha manyanyaso kwa wazee hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uimarishaji wa Hospitali ya Wilaya; kwa kuwa Hospitali ya Wilaya ya Nansio (Ukerewe) ndiyo Hospitali ya Rufaa kwa Visiwa vya Ukerewe lakini hospitali hii ina upungufu mkubwa wa madaktari pamoja na vifaatiba jambo ambalo limekuwa linaathiri sana utoaji wa huduma kwa wananchi wa visiwa hivi vya Ukerewe. Naomba hospitali hii iangaliwe kwa namna ya pekee kuhakikisha kuwa afya ya wananchi wa Visiwa vya Ukerewe inawekewa mazingira salama.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala la ukarabati wa zahanati na vituo vya afya. Ni jambo zuri la Serikali kujenga zahanati kila kijiji na vituo vya afya kila kata. Lakini viro vituo vilivyopo ambavyo ni chakavu na havina wahudumu wa afya na vifaa. Ushauri,

Serikali ingeviimarisha vile vilivyopo kwanza na kuhakikisha kuna vifaa, madaktari na manesi na dawa na hii kwa kiasi kikubwa itapunguza sana msongamano kwenye ngazi za juu Wilaya hadi Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu magonjwa yasiyoambukiza (*NCD*), pamekuwa na ongezeko kubwa sana la magonjwa yasiyoambukiza kama ugonjwa wa sukari ya kupanda na kushuka, shinikizo la damu ya kupanda na kushuka, magonjwa ya moyo na kadhalika. Magonjwa haya mengi yanachangiwa zaidi na mtindo wa maisha, vyakula tunavyokula na kutofanya mazoezi ya mwili. Inasemekana karibu asilimia 10 ya wananchi wana uzito uliopitiliza (*obesity*).

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri, elimu itolewe zaidi na Wizara ishirikiane na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ili barabara zinapojengwa wahakikishe wanajenga *pavement* ya wapita kwa miguu au kuendesha baiskeli, hili ni zoezi zuri sana. Wafanyakazi badala ya kwenda na magari kazini wanaweza kutembea na pia ofisi zote zinaweza kuwa na chumba cha kufanya mazoezi kwa kufanya mazoezi; kwa kufanya hivi Serikali itaokoa kwa kiasi kikubwa fedha kwa ajili ya matibabu. Pia pawepo na vipimo vya kupima sukari na shinikizo la damu kwenye maofisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ugonjwa hauna muda, mama mjamzito akija kujifungua anaweza pata uchungu muda wowote. Sehemu za vijijini wanawake wengi wanapoteza maisha kutowana na umbali wa kufika hospitali ya ngazi za juu. Je, kwa nini zahanati zisifanye kazi kwa muda unaozidi masaa nane? Sababu hizi ndizo zilizopo karibu na wananchi au pawepo na gari (*ambulance*) masaa 24 itakayosaidia kuwakimbiza wagonjwa kwenye kituo cha afya au ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upandikizaji wa figo; napenda kuipongeza Serikali kwa jitihada hizi kubwa na kuweza kuwasaidia watu wengi waweze kupata huduma hii ambayo ni ghali sana. Swali langu ni kwmaba kwa kuwa mtu akishapandikizwa figo ni lazima atumie dawa kwa

maisha yake yote na dawa hizo ni ghali sana, je, Serikali imejipangaje kuhakikisha wagonjwa hawa watazipata dawa hizo kwa sababu sio kila mgonjwa atakuwa na uwezo wa kununua dawa hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona wagonjwa wengi wanaomba msaada wa matibabu kupitia magazeti, televisheni na wengine wamepewa barua kutoka Ofisi za Serikali kutoka kwa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mkoa kuwaombea misaada ya matibabu, je, ni jukumu la Serikali kuruhusu wagonjwa hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tatizo la vifo nya akina mama vitokanavyo na uzazi ni kubwa sana hapa nchini na badala ya kupungua vinaongezeka. Kuna haja ya kuliangalia suala hili kwa umuhimu sana na kuhakikisha vifaa na wakunga wanakuwepo wa kutosha; na upungufu wa wataalam naamini unachangia vifo hivi.

Mwisho kabisa niwapongeze Waziri na Naibu Mawaziri wanavyojitahidi katika sekta hii, lakini tukumbuke wote sisi ni wazee wa kesho, kambi za wazee mfano iliyopo Moshi Manispaa (Njoro) ipo katika hali mbaya, malazi sio mazuri hata vyoo vyao sio vizuri. Naomba Serikali iende ikakague kituo hicho ili waweze kuwasaidia wazee.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kuanzia kwa Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Makamu wa Rais na Waziri wetu mama yetu mpendwa Ummy Mwalimu, Naibu Waziri Mheshimiwa Faustine Ndugulile na watendaji wote wa Wizara na ngazi zote kwa kutatua changamoto ya upungufu wa miundombinu ya majengo, dawa, vifaatiba na rasilimali watumishi kwa ujumla; kuendelea kuboresha sera yetu ya afya nchini na kusimamia utekelezaji wa llani ya CCM 2015 hadi 2020.

Aidha, naungana na Watanzania wenye nia njema pamoja na wananchi wa Jimbo langu la Mbulu Mjini kwa

maombi na mapenzi makubwa kwa Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kutoa ushauri wangu kwa Serikali kuhusu bajeti inayowasilishwa ya Wizara hii kwanza, kuendelea kutoa nafasi kubwa ya ajira kwa sekta hii ya afya kuitia mipango yetu ya ikama kila mwaka. Pili, kuongeza uwezekano wa mashine za *x-ray* katika Hospitali za Wilaya na vituo vya afya ili kuleta tija zaidi, tatu, kusimamia matumizi ya mashine za kielektroniki katika vituo vya afya, zahanati, hospitali za wilaya, rufaa kote nchini ili kuongeza mapato na nne, kusimamia mpango wa kila Mtanzania anaetaka Bima ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika tano, kufufua bodi za afya za zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya kulingana na muda wa ukomo wao wa uteuzi; sita, kuendelea kuhamasisha kliniki ya wanaume na wajawazito ili kujenga ushawishi wa uzazi wa mpango; saba, kuitaka *MSD* kutumia dawa zenye muda mrefu katika hospitali zetu; nane, kuona na kutathmini mpango wa *PPP* katika hospitali binafsi unanufaisha jamii au wapokee huduma kwa kiasi gani badala ya kuboresha hospitali zetu, hata hivyo, mpango huu wa ubia wa sekta binafsi haumpunguzii mpokea huduma gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kuna madeni makubwa ya malipo ya masaa ya ziada katika Halmashauri za Mji wa Mbulu, hospitali hiyo iliyokuwa ya Wilaya hapo awali inakabiliwa na upungufu wa watumishi hivyo basi naomba sana *OC* inayotolewa itumike kwa vigezo vya bajeti kinyume na matumizi mengine.

Pia naomba Serikali ione umuhimu wa kuona inafanya maandalizi ya watumishi wapya kwa vituo vya afya vya Daudi, Thawi na Dongobeshi kwani mahitaji hayo mapya ya miundombinu yanaweza kufanya majengo hayo yasitoe huduma. Kwa sasa hospitali ya Wilaya ya Mbulu iliyoko Mbulu Mjini inatoa huduma asilimia 30 kwa wananchi wa Jimbo la Babati Vijijini, Mbulu Vijijini na Karatu hivyo kupewa mgao

wa dawa kwa kuangalia takwimu za sensa ya mwaka 2012 haitakidhi haja ya huduma bora. Hata hivyo Halmashauri ya Mji ya Mbulu kupitia Baraza la Madiwani walishatuma taarifa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa idadi ya watoto walemaruvu ni kubwa, Serikali ione kila Halmashauri inateua shule moja ya msingi na sekondari na kufanya marekebisho ya miundombinu yake ili kundi hili lipate elimu kwa maisha ya baadae katika jamii yetu na kizazi kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa katika Hospitali ya Wilaya, baadhi ya vifaatiba havipewi vipaumbele mfano shule, blanketi, vifaa vya matibabu ya macho na meno kitendo kinachofanya wataalam hao kutokutoa huduma na katika vikao vya Baraza la Madiwani ukihoji wakati wa bajeti kauli ni kwamba ukomo wa bajeti hauruhusu, mfano ni Hospitali ya Wilaya ya Mbulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho Mheshimiwa Waziri wa Afya nimemuomba atembelee Hospitali ya Wilaya ya Mbulu kwa kuwa ni mali ya Serikali na kwa kuwa tayari mwaka jana alitembelea Hospitali ya Rufaa ya Hydom na kituo cha afya katika mwezi wa Juni. Pia ziara hii ni ahadi yake, Mungu akitujaalia hasa siku ya Jumamosi moja ili Jumapili Mheshimiwa awahi kwenye majukumu yake. Katika ziara hiyo aweze kutembelea Tarafa ya Nambis ambako tarafa hiyo haina kituo cha afya hata kimoja na ina akina mama wengi sana kwa maelezo nitatoa maelezo zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ninawatachia kazi njema na majukumu mema katika kutumikia Wizara hii muhimu sana kwa mustakabali wa maisha yetu na Taifa kwa ujumla. Ahsante sana.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na pongezi kwa Waziri wetu Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri sana ambayo wamekuwa wakiifanya kwa ajili ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Mkoa wa Iringa ina eneo finyu sana kutokana na muingiliano wa Gereza Kuu la Iringa na kusababisha Madaktari wetu Bingwa kuishi nje ya hospitali. Tunaomba kwa sababu Serikali ni moja, Gereza liondoke kupisha hospitali ili hata kuweza kujenga majengo mengine ya huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wetu wa Iringa una upungufu wa wafanyakazi asilimia 60. Changamoto hii inasababisha matatizo makubwa sana mpaka katika Hospitali za Wilaya. Pia tuna changamoto Hospitali ya Mkoa haina Daktari Bingwa wa Watoto. Tunaomba Serikali iangalie kwa uzito mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu dawa *MSD*; niipongeze Serikali kwa upatikanaji wa dawa na nipongeze kwa kuleta moja kwa moja katika vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bima ya Afya, tunaiomba Serikali suala la wazee, huduma ya wazee dawa ni ghali sana zipo nje ya mfumo wa bima yao, wanapata shida sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie watoto yatima walio katika vituo wanapata shida sana hawana bima ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango gani wa kuweka madawati katika vyuo vikuu. Nilipata bahati ya kukutana na Serikali za Wanafunzi wa Vyuo Vikuu. Wanafunzi wanachangia pesa lakini haziwasilishwi Bima ya Afya kwa wakati kwa ajili ya kupatiwa kadi za matibabu. Naomba Wizara ilichukue hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tatizo la ugonjwa wa saratani; niipongeza Serikali kwa kuanza kutoa chanjo kwa mabinti zetu kuanzia miaka tisa hadi 15; hii ni hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata ufanuzi je, watoto wa kiume hawana haja ya chanjo hii? Huwa naona kuna kansa ya mabusha. Je, inawezekana chanjo hii wakapatiwa wanawake wenye umri wa zaidi ya miaka 15? Nimeona nchi nyingine wanapatiwa. Ni imani hata mkiweka malipo kwa ajili hiyo au bima ziweze kulipia chanjo hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo kubwa sana kwa wagonjwa wa saratani katika Mkoa wa Iringa kwenda Hospitali ya *Ocean Road* Dar es Salaam ni kwa nini Serikali isiweke *centre* za haya matibabu kikanda au matibabu yasogezwe Dodoma ili iwe rahisi kufikiwa na kupunguza gharama kwa sababu kina mama wanapata shida sana hata kimaisha wapokwenda Dar es Salaam kwa ajili ya matibabu hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma ya matibabu ya moyo na figo; pongezi kubwa sana huduma hiyo imetupa moyo sana kuwa imeweza kupunguza hata gharama za matibabu ya nje ya nchi. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa maoni yangu juu ya hoja ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna upungufu mkubwa wa wataalam wa sekta ya afya karibu zahanati, vituo vya afya na hata hospitali za mjini na vijiji. Hili jambo ni kubwa naomba Serikali ilifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mahusiano makubwa ya TAMISEMI na Wizara ya Afya hivyo ni maoni yangu kuwa kuwe na chombo cha pamoja kushughulikia *allocation* ya watumishi wa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shida ya wazee kupata matibabu kwa kutumia bima au utambulisho kwa wazee.

Hili jambo naomba lifanyiwe kazi ili wazee wasipate shida pindi wanapougua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shida kubwa ya gari la wagonjwa katika hospitali, vituo vya afya llala na hasa Jimbo la Ukonga. Naomba nipate gari la wagonjwa walau lihudumie Ukonga tu ili kuwa na uharaka wa usafiri pindi tupatapo wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali za kuboresha huduma za afya nchi nzima. Wilaya yetu ya Mbogwe tumebahatiha kupatiwa jumla ya shilingi milioni 800. Kituo cha Afya Masumbwe kimepatiwa shilingi milioni nne na Kituo cha Afya Iboya shilingi milioni 400; fedha hizi zimetengwa mahususi kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya upasuaji, nyumba za waganga, nyumba kwa ajili ya maabara na famasia na majengo kwa ajili ya kuhifadhi maiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza Serikali kwa mikakati yake pia ya usambazaji wa dawa muhimu za binadamu kuititia *MSD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu ya Awamu ya Tano inafanya kazi kubwa sana katika kuhakikisha kuwa tunapata magari kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa (*ambulances*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kutupatia magari ya kubebea wagonjwa katika vituo vyetu viwili vya afya vya Iboya na Masumbwe. Hongera sana Serikali kwa kazi nzuri. Aidha, nashauri Serikali iendelee na mkakati wake wa kuunga mkono jitihada za wananchi kujenga na kumalizia majengo ya vituo vya afya na zahanati

katika vijiji na kata mbalimbali Wilayani Mbogwe. Wilaya ya Mbogwe inakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na Hospitali ya Wilaya. Naomba sana Serikali itoe fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali hii ya Wilaya ili kusaidia utoaji wa huduma za afya zinazotolewa na vituo vya afya na zahanati Wilayani Mbogwe ili kupunguza utegemezi wa wagonjwa wa Wilaya yetu kutibiwa katika Hospitali za Wilaya za Bukombe, Kahama na Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua Serikali yetu inafanya kazi kubwa sana kuhakikisha afya za Watanzania walio wengi zinaboreshwu. Ninaamini wazi kuwa siku za usoni Taifa letu la Tanzania litakuwa likitoa huduma bora zaidi katika ukanda huu wa Afrika Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali zetu za Jakaya Kikwete, Hospitali ya Taifa ya Rufaa ya Muhimbili zimepata sifa kutohana na utoaji wa huduma bora kabisa za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ya viwanda itajengwa na Watanzania wenye afya bora na kwa hakika Wizara ya Afya imejipanga vyema kuhakikisha nchi yetu inakuwa na Watanzania walio na afya bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Serikali iendelee kutoa kipaumbele katika kutoa fedha kwa wakati ili kuhakikisha miradi ya maendeleo katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto za uhaba wa watumishi, vifaatiba na madawa zinapaswa kushughulikiwa ili kuhakikisha huduma za afya zinapatikana karibu kabisa na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuipa kipaumbele sekta ya afya na kuendelea kuboreshwa kila wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongozi sana kwa mafanikio ambayo yanasaidia wananchi wa Tanzania kupunguza gharama za matibabu hasa nchi za nje. Mafanikio haya ni kama vile huduma za kupandikiza figo Muhimbili na *Benjamin Mkapa Hospital*; chanjo muhimu kwa watoto, chanjo ya saratani ya mlango wa kizazi kwa wasichana; upatikanaji wa dawa kwa kiwango kikubwa; dawa mpya ya kifua kikuu kwa watoto na ununuzi wa vifaatiba, mashine na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudhi hizi zinalenga kuendelea kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata huduma za afya kwa wakati na ubora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongozi pia kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya pamoja na Naibu Waziri wake na timu yote ya wataalamu kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kusimamia na kutekeleza majukumu yao na kuhakikisha huduma za afya zinawafikia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kutoa ushauri kwa Wizara hii ili kuweza kuendelea kutoa huduma bora; kuendelea kutoa elimu kwa jamii ili wawe na tabia ya kupima afya zao na kugundua matatizo kabla hayajawa sugu na kuwasababishia vifo, gharama kubwa za matibabu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu zaidi itolewe kupima tezi dume, saratani, ugonjwa wa ini, magonjwa yasiyoambukizwa (*non-communicable diseases*).

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza juhudhi za Serikali kuwa na Bima ya Afya kwa kila mwanachi. Hivyo ili kuondoa changamoto ya msongamano wa wagonjwa kumuona daktari na kufanya vipimo ni vema sasa Serikali ikaendelea kuajiri madaktari na wasaidizi wengi wa afya ili kuondoa adha hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitengo cha Tiba Asili ni cha muda mrefu, lakini bado hatujaona ripoti inayoonesha

mafanikio ya upatikanaji wa dawa zilizothibitishwa na kitengo hiki ili zisambazwe kwenye maduka ya dawa. Hii itasaidia kupunguza matumizi ya dawa zenyе kemikali ambazo si nzuri sana kiafya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea kuboresha Hospitali za Rufaa za Mikoa kwa kuweka mashine za kisasa kama vile *MRI*, *X-ray (Digital)*; *CT-SCAN* na kadhalika, lakini pia kuajiri Madaktari Bingwa ili kupunguza msongamano wa wagonjwa katika Hospitali ya Muhimbili na kupunguza gharama za usafiri na malazi kwa mgonjwa na ndugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kuna wanawake wengi wanaojifungua watoto zaidi ya mmoja. Wapo hadi wanaojifungua watoto watano. Wote tunafahamu ugumu wa kulea mapacha au idadi kubwa hiyo ya watoto watatu, wanne, watano na kadhalika. Ili kuokoa maisha ya watoto hawa pamoja na mzazi, kunahitajika matunzo ya hali ya juu ukizingatia familia hizi vipato vyao ni vidogo kukidhi kulea watoto wanne (kwa mfano) kwa wakati mmoja. Je, Wizara ina mpango mkakati gani katika kusaidia familia hizi kulea hawa watoto angalau katika kipindi cha mwaka mmoja wa kwanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wa mitaani na mimba za utotoni ni tatizo linaloendelea kukua katika nchi yetu. Sababu za watoto wa mitaani na mimba za utotoni zipo nyingi, lakini sababu mojawapo ni baba wa watoto hawa kukataa kutoa malezi na matunzo, hivyo kupelekea mama zao kushindwa kuwapa mahitaji ya msingi ikiwemo elimu, afya, chakula na kadhalika. Hali hii husababisha watoto hawa wajitafutie riziki kwa njia mbalimbali zikiwemo kuombaomba mtaani, kujiingiza katika mapenzi wakiwa na umri mdogo na kutumia ngono zembe na kadhalika.

Je, Serikali sasa, ina mpango mkakati gani wa kuhakikisha baba wa watoto hawa wanawajibika kulea watoto wao, maana hivi karibuni tumeshuhudia akina mama walivyofurika kwenda ofisini kwa Mheshimiwa *RC* wa Dar es Salaam kupeleka malalamiko yao. Hali hii imeonesha/

kudhihirisha kuwa kuna tatizo katika vyombo vya maamuzi ikiwemo Mahakama na Ustawi wa Jamii katika kuwawajibisha akina baba hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia na ninaomba kuwasilisha.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja, naomba nitoe mchango wangu kwa kuanza na suala la ukosefu wa gari la wagonjwa. Katika Halmashauri yangu ina vituo vya afya vya Serikali ambavyo ni Mtowisa, Laela, Miwepa, Mpui na Msanda Muungano. Vituo hivi havina gari la wagonjwa isipokuwa ni juzi tu Serikali ilitupatia gari la wagonjwa aina ya P-Suzuki gari ambalo kulingana na mazingira ya jimbo langu tuliamua kulipeleka Kituo cha Afya Laela. Hivyo tunaomba kwa kuanzia tena tupatiwe gari la Kituo cha Afya Milepa kituo ambacho kina msongamano wa wagonjwa na kina hudumia kata saba na kiko katika mazingira magumu kimiundombinu. Pili, ikiwezekana na Kituo cha Afya Mpui nacho kipatiwe gari la wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upanuzi wa vituo vya afya, tunashukuru Serikali kutupatia shiligi milioni 400 kwa ajili ya upanuzi wa kituo na kazi inaendelea vizuri, tatizo litakalobaki katika kituo cha afya hicho cha Milepa ni gari la wagonjwa. Tunaomba kutokana na jiografia ilivyo katika jimbo langu, naomba sana tupatiwe fedha kwa ajili ya upanuzi wa kituo cha afya Mpui.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upungufu wa watumishi wa Wizara ya Afya katika Halmashauri yangu yapata asilimia 67 kwa maana ya waganga, wahudumu, wauguzi, manesi na kadhalika. Tunaomba Serikali ipeleke watumishi wa kutosha. Kwa upande wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, tunashukuru sana Serikali kututengea shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kujenga Hospitali ya Wilaya katika Wilaya ya Sumbawanga ambapo Halmashauri tayari ilishahamasisha wananchi kupitia Mkuu wa Wilaya Dkt. Haule akilishirikiana na viongozi wengine Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa

Madiwani. Hadi sasa tumeshafyatua tofali 400,000; pia kutenga eneo hekari 30, tunasubiri fedha zije tuanze kazi ya ujenzi, tunashukuru sana na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jimbo langu tunavyo vituo vya afya vinavyoendelea kujengwa kwa kushirikiana na wananchi kwa nguvu kazi na michango mbalimbali. Tunaomba Serikali itupatie fedha za kumaliza ujenzi wa vituo hivyo ambavyo ni Muze, Illemba, Kaoze, Kipeta na Kalambanzite.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama sera ya Chama cha Mapinduzi inavyoelekeza kuwa na ujenzi wa zahanati kila kijiji wananchi waliitikia wito huo kwa dhati na kuanza kazi hiyo. Tunazo zahanati yapata nane ambazo zimefikia katika hatua ya mwishoni ili ziweze kusajiliwa na kuanza kutoa huduma, na ni kutokana na nguvu za wananchi, michango na kushirikiana na Mbunge wao kupitia Mfuko wa Jimbo ambazo ni zahanati ya Maleza, Mpona, Ilanga, Mumba, Jangwani, Kizumbi, Kazi na Mtapenda. Tunaomba Serikali kuunga mkono kwa kutoa fedha ili kumalizia zahanati hizo haraka ili ziweze kutoa huduma haraka kwa wananchi, ikiwa ni pamoja na kutowakatisha wananchi hao tamaa. Zipo pia zahanati za wananchi ambazo ni kama zifuatavyo; Ngingo, Kawila, Ilambo, Ndelema, Mshani, Sikaungu. Zipo pia zahanati ambazo zilisha anza kutoa huduma, tunaomba Serikali itoe fedha za kuboresha kwa kumalizia majengi zahanati hizo ni Kisa, Msia, Sakalilo, Kisa, Lyapona, Illemba, Kinambo.

MHE. NAJMA MURTAZA. GIGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa jinsi anavyokuwezesha Mheshimiwa Waziri (mwanamke mwenzetu) kufanya kazi zake kwa ujasiri na uweledi unaothibitisha kuwa wanawake tunaweza kabisa.

Mheshimiwa Waziri hoja yangu inajikita moja kwa moja kwenye hotuba yako kwenye ukurasa wa 101 hadi 107 na ukurasa wa 109 hadi 110. Umekiri kabisa kuwa ukatili dhidi ya watoto bado ni tatizo kubwa hapa nchini, na mimi ninakiri

pia kwa kauli yako hii. Matukio ya ukatili dhidi ya watoto yameongezeka kwa asilimia 28 kutoka mwaka 2016 hadi kufikia mwaka 2017, ninaamini kabisa elimu sahihi kuhusu vitendo hivi ikiwafikia Watanzania walio wengi na kuweza kutoa taarifa za matukio ya ukatili dhidi ya watoto, asilimia hii inaweza kuzidi hadi kufikia asilimia 60 au zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sichoki na wala siyachoka kutoa ushauri wa kuangalia adhabu mbadala kwa makatili wazoefu wanaoharibu maisha ya watoto wetu ambaao ni Taifa letu la kesho.

Mheshimiwa Waziri inasikitisha sana kuona kuwa haki za binadamu zinapewa kipaumbele kwa hawa makatili wa watoto wetu na hasa wabakaji watoto wa kike na wanaolawiti watoto wakiume, mbali na kutumikia kifungo kwa miaka 30 makatili hawa sugu (ambao wanathibitika kuwa wazoefu katika kuwaharibu watoto wetu) wafikiriwe adhabu mbadala ya kuhasiwa uume wao ili iwe funzo kwa wengine na kuwaokoa watoto wetu kutohana na janga hili ambalo tukizidi kuwaonea huruma kwa kisingizio cha haki za binadamu tutaliangamiza Taifa la kesho kwani hili janga mwisho wa siku litakuwa janga la kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Ibara ya 30 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaeleza wazi kwamba haki na uhuru wa binadamu ambavyo misingi yake imenorodheshwa katika Katiba hii havitatumwa na mtu mmoja kwa maana ambavyo itasababisha kuingiliana kati au kukatizwa kwa haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya umma; kuhakikisha kwamba haki na uhuru wa watu wengine au maslahi haviathiriwi na matumizi mabaya ya uhuru wa haki za watu bibafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali kuwa ibara hii ya Katiba ikionekana kuvunjwa kwa namna yoyote kwa mujibu wa ibara 30 mtu anaweza kufungua shauri katika Mahakama Kuu. Hili suala la kufungua shauri katika mahakama zetu bado inaonekana siyo muafaka sana kwa maslahi ya watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakushukuru Mheshimiwa Waziri ukiwa kama mwanamama mwenzangu ulitafakari na kukaa na timu yako kutafakari zaidi suala la kuleta muswada wa sheria ya kuwashai wabakaji sugu wa watoto wa kiume na wa kike, tukizingatia ibara hizo hapo juu za Katiba yetu zinaturuhusu kutunga sheria katika jambo la aina hii, tuache kabisa kisingizio cha kuvunja haki za binadamu wakati hawa wabakaji wanaendelea kuvunja haki za binadamu wadogo.

Naomba sana Wizara yako ijaribu kutafiti na kuona uwezekano wa kutungwa sheria hii ya adhabu ya kuhasi kwa kulinganisha na nchi nydingine ambazo tayari zina hukumu za aina hii. Mfano Mheshimiwa Mary Karoro Okurut, Waziri wa Jinsia Kazi na Maendeleo wa Uganda anaunga mkono suala hili la kuwashai wabakaji hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai ili niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii.

Naomba nianze kuwapongeza Mawaziri wote wawili na watumishi wote wanaohudumu kwenye Wizara hii. Sina budi kushukuru kwa kile kidogo nilicho jaliwa kupata kwenye jimbo langu la Liwakle kwa kunipatia watumishi wanee, Mungu awabariki sana.

Sasa naomba kuchangia/kugusia suala la wazee nchini. Imekuwa ni jambo la muda sasa tangu Serikali iahidi kuleta sheria ya wazee humu Bungeni. Kwani pamoja na matamko mengi juu ya wazee kama vile makazi bora kwa wazee, matibabu bure kwa wazee na kadharika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo haya hayawezi kukamilika bila kwanza kuwatambua hao wazee ni akina nani kwa mujibu wa sheria. Hivyo ni bora sasa sheria hiyo

ikaletwa ili tuweze kuwatambua hao wazee. Pamoja na juhudhi kubwa inayofanywa na Serikali ya kuboresha miundombinu ya afya juhudhi hizi zinaweza zisileté matunda tarajiwa kwa kuwepo na tatizo la uhaba wa watumishi kwenye Wizara halitatatuliwa. Kwa kuwa sehemu kubwa ya watumishi hawa wanashughulikia afya ya watu, hivyo weledi mkubwa unahitajika, hivyo watumishi wachache kuhudumia watu wengi kunawaondolea umakini na kukosa ufanisi, kwa mfano katika Hospitali ya Wilaya ya Liwale ina watumishi wachache sana hospitali ina wodi za *grade II*, kwa saa za usiku wodi hizi zote zina huduma na wauguzi wasaidizi, ni zahanati nne tu ndio zinahudumiwa na *clinical officers* wasaidizi. Jambo hili ni bayá sana kwani ikitokea akiwa likizo zahanati husika hufungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Liwale iko mbali sana na Hospitali ya Rufaa ya Sokoine, Lindi. Jambo hili limefanya umuhimu wa kuwa na gari kwani umbali uliopo ni zaidi ya kilometra 300. Hospitali pekee ya karibu ni ya Ndanda iliyoko Masasi, Mkoani Mtwara, kwa sababu hizo uhitaji wa vifaa bora na Madaktari Bingwa ni muhimu sana kwa hospitali ambayo haina usafiri na haina Madaktari Bingwa ni hatari ya wagonjwa kufia njiani ni kubwa sana wakati wakielekea Ndanda kwa kutumia magari ya abiria. Naomba jambo hili lingepewa msukumo wa kipekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, maduka ya *MSD* yameongezeka kuwa msaada mkubwa sana katika idara hii ya afya, hivi imefikia wakati sasa maduka hayo sasa yangetapikana katika Mikoa a Wilaya zote nchini hasa kwenye zile Wilaya ambazo ziko mbali na Makao Makuu ya Mikoa ambako kuna maduka hayo, lakini vilevile pale ambapo maduka hayo yapo basi ni bora dawa zote muhimu zikapatikana ikiwa ni pamoja na vitendea kazi vingine yaani vifaatiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bima ya Afya imeonesha kuwa na manufaa makubwa kwa jamii. Changamoto pekee katika utekelezaji wa jambo hili ni elimu duni katika jamii juu

ya uchangiaji na uandikishaji wake. Lakini jambo lingine ni tatizo kwenye Halmashauri zetu ni juu ya uchangiaji wa *CHF*, pamoja na jamii kuendelea kupewa elimu . Lakini mchango wa fedha za kutoka Serikali hazipatikani kwa maana ya tele kwa tele, jambo hili linalea mkanganyio mkubwa kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa zahanati na nyumba za watumishi sasa jambo hili linaachwa kwenye Halmashauri. Lakini mkumbuke kuwa Halmashauri hizo kwa sasa zina mzigo mkubwa sana. Mfano ujenzi wa maabara za shule za sekondari, nyumba za walimu, vyoo vyaa shule na walimu na majengo mengine. Hivyo ni bora Serikali ikaona upo umuhimu wa kuzisaidia Halmashauri kujenga zahanati kila kijiji na kituo cha afya kila kata kama Sera ya Taifa inayotaka ujenzi wa vituo vyaa afya na zahanati ukiachwa chini ya Halmashauri, kwenye Halmashauri zenye mapato kidogo jamii itaendelea kuteseka maana Serikali ya Awamu ya Tano mara zote wanasema hakuna miradi mipya itakayoanzisha mpaka Halmashauri husika yaani Serikali kazi yake ni *ku-support* tu nguvu za wananchi mahali ambapo wananchi hawana uwezo, patabaki kuwa nyuma kimaendeleo ya kiafya. Na sera ya kuwa na kituo cha afya kila kata haitafikiwa kwani Halmashauri zetu nyingi zina uwezo mdogo na zina mzigo mkubwa sana ikiwa ni pamoja na matamko ya mara kwa mara ya kutoka Serikali Kuu.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, upelekaji wa fedha za maendeleo katika Hospitali za Mikoa imekuwa wa kusua jambo ambalo linakwamisha shughuliza za utoaji wa huduma katika maeneo mbalimbali hapa nchini kwa kuwa mahitaji ya fedha za maendeleo ni mkubwa katika sekta na maeneo mbalimbali, hivyo basi naishauri Serikali kuliko kugawa fedha za miradi ya maendeleo kwa mtawanyiko wa nchi nzima bila kuonesha matokeo ya haraka na miradi kubaki viperor. Nashauri fedha za miradi ya maendeleo kila mwaka ipelekwe kikanda kwa kuangalia na kutanguliza maeneo yenye mahitaji makubwa zaidi. Hata hivyo ugawaji huu uendane na takwimu zinaonesha uhitaji upo kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upungufu wa watumishi katika sekta ya afya, sekta hii inakabiliana na upungufu wa asilimia 49 ya watumishi wa afya katika mwaka a fedha 2016/2017; changamoto hii imekuwa ya muda mrefu hasa maeneo ya vijijiini jambo ambalo linapelekea wananchi kukosa huduma na hasa tukilinganisha idadi ya ongezeko la watu nchini. Naishauri Serikali kuhakikisha inaweka mkakati wa haraka wa kuhakikisha inakabiliana na changamoto hii kwani idadi ya watu nayo inaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu chakula na lishe, tatizo la udumavu nchini ni kubwa kutohana na lishe duni kwa watoto na wajawazito, udumavu huu kwa watoto ambao ndiyo Taifa la kesho maana yake tutatengeneza Taifa la udumavu. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na *REPOA* takribani watoto milioni 2.4 wana udumavu; takwimu hii ni kubwa na watoto hawa wengi ni wale walio katika kaya maskini za vijijiini. Hivyo basi, Serikali ituambie ina mkakati gani wa kuiwezesha Taasisi ya Chakula na Lishe kifedha na kuweka mikakati ya haraka ya kukabiliana na hali hii ya lishe duni unaosababisha udumavu kwa watoto hapa chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uzazi wa mpango, uwekezaji wa Serikali katika mpango wa uzazi ni jambo la muhimu sana kwani jambo hili limekuwa haliwekewi fedha za kutosha, umuhimu na uhusiano wa mpango wa uzazi na mkakati wa kupunguza vifo vya wanawake wajawazito; uzazi vina mahusiano ya karibu, hata hivyo kukiwepo na uzazi wa mpango ndivyo ambavyo tunaweza kupanga mipango bora ya maendeleo. Nashauri Serikali ihakikishe upatikanaji wa madawa, vifaa vya uzazi wa mpango katika maeneo yote ya utoaji wa huduma ya afya nchini. Serikali iongeze bajeti na kutoa fedha zilizoainishwa za fungu hili. Pia kuwa na huduma na vituo vya afya ya uzazi kwa vijana nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pensheni kwa wazee; wazee wa nchi hii wamekuwa wakipewa matumaini ya kupatiwa pensheni bila mafanikio yoyote. Je Serikali ina

mpango kati wa haraka wa kutoa pensheni kwa wazee nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, uwakilishi na usawa wa kijinsia, kwa mujibu wa takwimu za *Employments and Earns Report* ya mwaka 2015 nafasi za wanawake walioshika nyadhifa mbalimbali ni asilimia 15 tu ya idadi ya waajiri, wateuliwa na wachaguliwa wote nchini. Idadi hii ni ndogo sana. Hivyo basi Wizara iwjajibike kuona ongezeko la usawa wa kijinsia katika nafasi mbalimbali unaongezeka zaidi, nawasilisha.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mungu kwa kunipa uzima siku ya leo ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na changamoto; kumekuwa na changamoto kubwa sana katika sekta ya afya katika Mkoa wangu wa Ruvuma. Elimu ya uzazi wa mpango bado inahitaji kufikishwa vijijini, vituo vya afya vingi havina maji, vituo vya afya havina magari ya wagonjwa jumbo ambalo limekuwa likisababisha vifo vingi vya akina mama na watoto. Wahudumu katika vituo vya afya, manesi na madaktari ni tatizo kubwa.

Kumekuwa na tabia ya baadhi ya wazazi kushirikiana na watu ambao wanawapa mimba wanafunzi kuwafichcha wahalifu ambao wamewapa mimba watoto ambao ni wanafunzi. Je, Serikali imeshachukua hatua gani kwa wazazi ambao wanajihusisha na tabia hiyo ya kumdidimiza ntoto wa kike? Je, ni madume wangapi ambao wamefungwa kwa kosa la kumpa mimba mwanafunzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, taa za kufanya *operation* nazo ni shida, mashine za *oxygen* hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbinga Mji kuna changamoto ya upungufu wa wodi za wagonjwa hususani wodi za akina mama (wodi ya wazazi), tunaomba Wizara itusaidie kuongeza wodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ni kuhusu mikopo ya akina mama. Wanawake wamekuwa na hitaji kubwa la mikopo lakini hawapati ipasavyo, ipo mikopo inayotolewa na Halmashauri mbalimbali, lakini bado haitoshi. Je, Wizara ina mpango gani wa kuwawezesha wanawake?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na vitendo vyakikatili ambavyo wamefanyiwa wanawake na watoto, hivi karibuni kuna mtoto ambaye anatembezwa kwenye mtandao ambaye ameshuhudia baba yake akiwachinja wadogo zake mapacha wawili. Napenda kujua kama Wizara inajua jambo hili na kama inajua imechukua hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Wilaya ya Tunduru ina tatizo la kitanda cha upasuaji. Tunaomba Wizara ichukue hatua za haraka ili kuokoa maisha ya wananchi wa Wilaya ya Tunduru.

MHE. MARIA N. KANGOYE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi. Nitumie fursa hii kuikumbusha Ofisi ya Waziri Mkuu juu ya ahadi yake ya shilingi milioni 10 aliyotoa kwa ajili ya zahanati ya Maligisu alivyokuwa kwenye ziara Wilayani humo.

Aidha, nichukue nafasi hii pia kumkumbusha Waziri wa Afya ahadi yake ya kuongeza vitendea kazi katika Hospitali ya Sengerema, wagonjwa wanapata shida sana pale wanapolazwa ukizingatia hospitali hii inahudumia wananchi wengi wa Wilayani hapo pamoja na mikoa mingine kama Geita na Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa kazi nzuri ifanyikayo na uongozi wa Awamu ya Tano chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli. Pia Waziri na Naibu Waziri wa Afya na timu yao nzima nawapongeza kwa kujitoa na kujituma kwa dhati katika nafasi zao kiutendaji kazi,

wameonesha uweledi na uzalendo kwa dhati ya huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa tuna wananchi takribani milioni 55, Serikali inajitahidi sana kwa upatikanaji wa dawa kwa uponyaji wa maradhi kadhaa. Kufuatana na hotuba inadhihirisha mapungufu ya rasilimali watu yaani watumishi na maandalizi yao yanachukua muda mrefu. Tunaomba Serikali kujipanga kwa kuwasambaza wataalam waliopo ambao wamerundikana kwenye mijji ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya. Vijijini tumekuwa na upungufu mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili Serikali kuangalia stahiki za wataalam wa afya ili waendelee kutoa huduma kwenye zahanati za Serikali, kwani tunawasomesha kwa pesa nyingi lakini wanakosa ajira na stahiki bora wanakwenda kwa watu binafsi au hata nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia suala zima la mapungufu makubwa ya rasilimali watu yaani watumishi wa maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii. Mheshimiwa Waziri tunakuomba sana upigie jicho la pekee na kutatua mapugnufu ya maafisa maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii kwani watu hawa ni wa muhimu ndani ya maeneo yetu. Wananchi wetu wanahitaji kupatiwa uwelewa na ufahamu wa maendeleo yao, hasa kina mama ndio chachu wa kila kitu ndani ya Kaya, Kijiji, Wilaya, Mkoa hadi Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa matumizi ya bima ya afya ni pamoa na kuinua uchumi na kuachana na umaskini. Katika Mkoa wa Rukwa, Maafisa Maendeleo ya Jamii tuna mahitaji ya 158 tulionao ni 50 tu; katika Halmashauri ya Sumbawanga mahitaji ni 39 waliopo 15 kwa pungufu ya 24; Nkasi mahitaji ni 34 waliopo 10 kwa pungufu 24; Manispaa mahitaji ni 33 waliopo 13 kwa pungufu ya 20 na Kalambo mahitaji ni 29 waliopo 13 kwa pungufu ya 16.

Mheshimiwa Naibu Spika, maafisa ustawi wa jamii ni wachache sana tena sana ukizingatia uhitaji kwao ndani ya jamii katika suala zima la kukinga. Unahitajika uelewa huu awali kwa wananchi wetu kuliko tiba ni ghamama kubwa. Hali halisi kwa mkoa wetu kwa maafisa ustawi wa jamii ni mkoa mmoja, Kalambo mmoja, Sumbawanga wawili, Manispaa watatu, hospitali ya mkoa wanne. Ifahamike mkoa wa Rukwa una kata 97 na mitaa 172 tu na Ziwa Tanganyika na Ziwa Rukwa. Tunahitaji kuiomba Serikali kuona umuhimu wa kutoa ajira kwa watumishi wa kada hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaombwa Wizara kuona namna ya kuwasaidia na kuwatatalia Idara ya Maendeleo ya Jamii changamoto zifuatazo; usafiri (magari, pikipiki), vifaa vyua uandishi (*stationary*), uhaba wa fedha za mikopo za Mfuko wa *WDF* toka mapato ya ndani (Wizara kulitolea maombi kwenye Serikali na ufuatiliaji wa karibu kwa maslahi ya watumishi hawa).

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaombwa Serikali kuona umuhimu wa kutoa taulo kwa watoto wetu mashulenii kwani tunazo pamba za kutosha kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa pamba hapa nchini, tuna kila namna ya kuzalisha taulo hizi na wanafunzi wa kike waweze kujistiri katika kipindi cha miaka nane kabla ya kwenda chuo angalau tuwawezeshe Watanzania hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi hotuba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri na wafanyakazi wake wote kwa utayarishaji na uwasilishaji mzuri wa hotuba hii katika Bunge hili. Katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni uboreshwaji wa Hospitali za Rufaa za Mikoa. Takwimu zinaonesha kuwa ajali nyingi za magari zinatokea katika sehemu za mikoani kuliko mijini ambako ziko hospitali nzuri zenyе vifaa lakini Hospitali za Rufaa za Mikoa inaonekana zina upungufu wa baadhi ya vifaa vya kukabili ajali hizo zinapotokea na kulazimika wagonjwa kusafirishwa kupelekwa Dar es Salaam. Mfano wa hivi juzi ambao Waheshimiwa Wabunge sita walipata ajali na kukimbizwa katika Hospitali ya Mkoa wa Morogoro ilibidi wasafirishwe kupelekwa Dar es Salaam kwa matibabu zaidi baada ya kukosekana *CT Scan* ambayo ingeweza kuwachunguza na kuonekana matatizo yao pale Morogoro, hii inawatokezea Waheshimiwa Wabunge, lakini je, ajali hii kama ingekuwa ya wananchi wa kawaida ingekuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Wizara na Serikali kuendeleza juhudzi za kuziimarisha hospitali hizi kwa kujipatia vitendea kazi vya kisasa ili kuweza kukabili matokeo haya na mengineo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu udhibiti wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza; napenda kuipongeza Wizara hii kwa kuendelea kusambaza elimujuu ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza, Wizara inajitahidi sana kueneza elimu katika mikoa yote ya Tanzania. Ushauri wangu katika suala hili ni kuomba Wizara iongeze ujuzi wa elimu hii katika maeneo ya vijijini ambako hawawezi kupata elimu hii kwa kutumia njia za vyombo vya habari kama vile *tv* na magazeti. Ni vyema Wizara ikawa na timu maalum ambayo itaweza kwenda moja kwa moja vijijini ambako itaweza kuwaelimisha wanavijiji

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia Wizara kwa kugusia vitu vichache, lakini muhimu sana. Ni kweli kwamba Tanzania tumeingia Mkataba wa Abuja (*Abuja Declaration*) ya kutenga walau 15% ya bajeti yote kwenye afya, lakini miaka yote tumekuwa

tukitenga fedha chini ya 10% na bado hatutekelezi hata hii asilimia ndogo tuliyotenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuizungumzia kwa takwimu sehemu mojawapo ya bajeti ya afya ambayo ni kuzuia vifo vya mama na mtoto, lakini katika bajeti ya mwaka 2017/2018 kwenye mradi wa kupunguza vifo vya akina mama zilitengwa jumla ya shilingi bilioni 12 ambazo zote ni fedha za ndani; kwenye ukurasa wa 179 kwenye jedwali la mchanganuo wa fedha za miradi ya maendeleo halijaonesha mchanganuo ni kiasi gani ambacho kilipokelewa katika kutekeleza mradi huu ikizingatiwa kwenda 2017/2018 fedha za ndani ambazo zilipaswa kutekeleza miradi ya maendeleo kwa Wizara hii ilikuwa 42.8% ya fedha za ndani na zilizopelekewa zilikuwa 19% tu ya fedha iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka unaokuja wa fedha 2018/2019 mradi wa kupunguza vifo vya akina mama vinavyotokana na uzazi umeongezewa bajeti kwa 0.82% na hivyo kufikia shilingi bilioni 12.2 tu. Je, Wizara imezingatia masuala au vigezo gani katika ongezeko hilo ukilinganisha na ukubwa wa tatizo la vifo vya akina mama vinavyotokana na uzazi nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwa mwaka wa fedha 2018/2019 mradi wa kupunguza vifo vya akina mama vinavyotokana na uzazi umetengewa shilingi bilioni 12.2 na katika malengo ya utekelezaji wake kwa mwaka 2018/2019 karibu 50% ya kiasi chote kilichotengwa imeelekezwa katika kukamilisha malipo ya mchangwa Serikali katika *First Health Rehabilitation Project* uliokuwa wa ukarabati mkubwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Kutokana na mradi huu kuchukua fedha nydingi ambazo ni takribani shilingi bilioni sita karibu 50% kutoka kwenye kiasi kilichotengwa kwa mradi wa kupunguza vifo vya akina mama vitokanavyo na uzazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kujua mradi huu wa *First Health Rehabilitation* umesaidia au utasaidia kwa

kiwango gani kupunguza vifo vya akina mama ukilinganisha na kiasi kikubwa cha pesa zilizoelekezwa huko?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwagine kwa mwaka wa fedha 2018/2019 bajeti ya miradi ya maendeleo imeshuka kutoka kiasi cha shilingi bilioni 785.8 (785,805,952,000) kwa mwaka 2017/2018 mpaka shilingi 561,813,998,998 kwa mwaka 2018/2019 ambayo ni sawa na 28.50%. Nataka njue Wizara ina maelezo gani kuhusu punguzo hili ukiangalia kwamba kutoka bajeti ya mwaka 2017/2018 ni 49% kati ya bajeti iliyopangwa ndio zilizopelekewa katika kutekeleza miradi ya maendeleo hii inamaanisha kuna miradi mingi bado hajiateakelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kujua Serikali imejipangaje katika kutekeleza miradi iliyopangwa kwa mwaka uliopita na kuendeleza miradi iliyopangwa kwa mwaka huu kwa punguzo hili la bajeti ya miradi ya maendeleo?

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya maendeleo kwa mwaka 2018/2019 imepunguza utegemezi wa fedha za nje katika bajeti ya mradi wa maendeleo yenye kiasi cha shilingi 561,813,998,998 fedha toka vyanzo vya nje ni shilingi 184,959,998,998; je, Wizara imejipangaje katika ukusanyaji wa mapato ya fedha za ndani ili kukamilisha utekelezaji wa mradi wa maendeleo kwa kuzingatia mwaka 2017/2018 fedha za ndani zilizokusanywa kutoka bajeti ya maendeleo iliyopokelewa ni shilingi 385,771,297,343 zilikuwa ni shilingi 64,756,206 sawa na 19% na fedha za nje zilikuwa shilingi 34,015,208,137.12 sawa na 71% zilizoidhinishwa. Hii ina maana kwamba fedha maendeleo zinatoka nje.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watumishi wote wa Wizara kwa hotuba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia maeneo yafuatayo nikianza na kuongezeka kwa madai na kutokuwepo kwa ukusanyaji wa madeni kwa Hospitali yetu

ya Muhimbili kwa mujibu wa taarifa ya CAG ya tarehe 30 Juni, 2016 yalifika shilingi bilioni 30.8 ilikillinganishwa na mwaka uliopita ya shilingi bilioni 17 sawa na ongezeko la asilimia 45. Hali hii si nzuri hata kidogo na hii inaashiria kwamba uongozi wa Hospitali ya Muhimbili hausimamii vyema eneo hili, je, tatizo ni Kitengo cha Fedha? Wizara lazima ihakikishe madeni yote yanakusanywa kwa sababu fedha ndio ikakayosaidia kuimarisha huduma za afya ukizingatia hii ni hospitali inayotegemewa na Watanzania wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo lipo tatizo la madai ya bima za afya yaliyokataliwa ya shilingi bilioni 1.86; kiasi hiki kimekataliwa kulipwa na makampuni ya bima eti kwa sababu ukaguzi ulibaini, mfano NH/Filikataa madai ya shilingi milioni 241.97 ya Hospitali ya Muhimbili ikidai ni madai ya madawa ambayo NH/F ilibaini hayakutolewa kwa waganga. Udanganyifu huu ulifanywa na watumishi je, hatua zipi zimechukuliwa na Serikali kwa watumishi hawa? Mheshimiwa Waziri naomba majibu ya kina juu ya mapungufu ambayo kwa hakika hayapaswi kufungiwa macho hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukarabati wa vyuo vya CD/S na fedha za maendeleo; changamoto ya kukarabati vyuo vya maendeleo (CD/S) ni suala linalopaswa kutupiwa macho sana, nipongeze juhudhi ambazo Wizara mmeonesha kufanya ukarabati kwa baadhi ya vyuo hivi, vyuo hivi ni muhimu sana, vimesaidia vijana wetu kuzalisha wataalam katika sekta ya ujenzi na ufundi, kuna umuhimu mkubwa kwa Wizara kuhakikisha inaweka msisitizo wa kufuatilia fedha za maendeleo kukarabati vyuo hivi kwani itasaidia kupunguza tatizo la ajira nchini. Waasisi wa nchi hawakufanya makosa kuvianzisha vyuo hivi, nikuombe Mheshimiwa Waziri na uongozi mzima wa Wizara jitahidi pia mtoe mafunzo ya kutosha kwa walimu (*lectures*) ili watu kuongeza ujuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la kupandisha Kituo cha Afya Songe kuwa Hospitali ya Wilaya; niipongeze Serikali kuititia Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kutupatia kiasi cha shilingi

milioni 500 kukarabati kituo chetu cha afya Songe. Wizara ya Afya ndio wenyе dhamana ya Hospitali za Wilaya, kituo hiki kina sifa zote za kupandishwa kuwa Hospitali ya Wilaya baada ya ukarabati huu kwa sababu tumepatiwa pia shilingi milioni 220 kwa ajili ya vifaatiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, jithada hizi zinatoa fursa kwa kituo chetu kuwa na sifa zote za kuwa Hospitali ya Wilaya, nimuombe Mheshimiwa Waziri atume timu kwenda Wilayani Kilindi kufanya tathimini ya kitaalamu na wakiridhika kituo hiki kipandishwe hadhi, Wanakilindi wanauhitaji mkubwa wa Hospitali ya Wilaya tunayo Hospitali ya Rufaa ya KKKT lakini yapo malalamiko makubwa kwa gharama kubwa na huduma dhaifu inayotolewa na hospitali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na pongezi kwa Wizara inafanya mageuzi makubwa katika sekta na hivyo kuboresha huduma za afya kwa upana wake. Hongera kwa timu nzima ya Wizara ikiongozwa na Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na wataalam wote na wasaidizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Tunduru na Jimbo la Tunduru Kaskazini, katika Hospitali ya Wilaya chumba cha upasuaji tunaomba *replacement* na *improvement* ya vifaa hususan *operation beds/tables* ikiwa ni pamoja na ukarabati wa chumba chenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhaba wa wataalam, nafahamu changamoto hii iko karibu katika maeneo yote nchini, naomba Wilaya ya Tunduru itazamwe kama eneo la pembezoni na lilliosahaulika kwa miaka mingi (*disadvantaged*). Tunaomba apatikane *DMO* kwani aliye po anakaimu nafasi hiyo. Pia kuna uhaba mkubwa katika vituo vyा afya na zahanati hususan Kituo cha Afya cha Matemanga na Nakapanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Matemanga kilitengewa fedha kiasi cha shilingi milioni 500 kwa madhumuni ya ukarabati na uboreshaji wa vifaa. Fedha hizo hatujaletewa hadi leo na taarifa za awali nilizonazo, fedha hizo zimepelekwa eneo lingine. Sio muhimu sana kupata/kujua sababu ya kuwa *diverted* fedha hizo, lakini ninaomba tupatiwe fedha kama ilivyopangwa awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna mahitaji ya gari la wagonjwa; nimesikiliza hotuba iliyosomwa na Mheshimiwa Waziri wa Afya, hongera kwa kutenga fedha kwa ajili ya magari ya wagonjwa (*ambulance*)¹⁷. Ombi langu ni kupewa angalau gari moja kwa Tunduru Kaskazini ambako Hospitali ya Wilaya iko. Izingatiwe pia kwamba (*location*) mahali Hospitali ya Wilaya ilipo inasababisha baadhi ya wanaohitaji huduma za rufaa kutoka katika zahanati wanatoka umbali wa kufikia hadi kilometra takribani 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kituo cha Afya Nakapanya, tumekamilisha ujenzi wa jengo la upasuaji katika kituo hiki. Ombi ni kupatiwa vifaa vya upasuaji na vingine vinavyoendana na hivyo. Ahsante.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Wizara ya Afya namshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kufanya ziara katika jimbo langu na kujionea changamoto.

Nashukuru kwa kupewa gari la wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Kirando na kuokoa vifo vya hasa akina mama. Pia nashukuru sana kwa kupewa pesa mwaka huu kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ya Nkasi kwa kuwa tuna miaka 40 hatuna Hospitali ya Wilaya, shukrani sana kwa Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tuna vituo vya afya viwili tu, naomba kujengewa kituo cha afya katika Kata ya Kabwe na Korongwe maana kata hizo ziko mbali na Makao Makuu ya Wilaya na wakazi ni wengi, pia usafiri ni mbaya sana na hata hivyo, nilipeleka gari la wagonjwa

nililopewa na Rais wetu ili lisaidie katika kata hizo mbili, hilo gari limekuwa ukombozi mkubwa sana tena sana, ni ukombozi sana kwa wagonjwa wa kata hizo mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana tena sana Mheshimiwa Rais Magufuli kwa msaada na ukombozi kwa hilo gari. Pia shukurani sana kwa Waziri Ummy Mwalimu na Naibu Waziri Dkt. Ndugulile kwa jitihada zao.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, alipokuja Halmashauri ya Mbozi alielezwa changamoto nydingi za Wizara hii. Mojawapo ya changamoto hizo ni ukosefu wa magari ya wagonjwa katika vituo vya afya na hospitali; Kituo cha Afya cha Itaka kinahudumia Kata nne za Itaka, Nambinzo, Bara na Halungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alipofanya ziara Mkoa wa Songwe aliahidi kuwapatia gari la wagonjwa wananchi wa Mbozi ili lisaidie Kituo cha Afya cha Itaka kutokana na kituo hiki kuhudumia wagonjwa wengi. Litakuwa jambo jema endapo Waziri wa Afya atatimiza ahadi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali ya Awamu ya Nne ilijenga Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete Ilyopo Hospitali ya Muhimbili, sio jambo baya, ni jema, ila tatizo ni kwamba taasisi hii muhimu haina baadhi ya vitendea kazi. Serikali inunue vitendea kazi (vifaatiba) ili kuendelea kupunguza tatizo la wagonjwa, hasa wenye magonjwa makubwa kama ya moyo kwenda kutibiwa nje ya nchi. Fedha zote zinazoidhinishwa wakati wa bajeti kwa ajili ya taasisi hii muhimu ni vema zitolewe zote na kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Wilaya ya Mbozi ina changamoto nydingi zinazohitaji utatuzi, mfano, kuna *OPD* ndogo, hakuna wodi ya wazazi, hakuna maji hivyo ni vema Serikali ikatatua kero hizi ili wananchi wanufaiké.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upungufu wa watumishi wa afya; Wilaya ya Mbozi ina upungufu wa watumishi wa Idara ya Afya; zaidi ya watumishi 600 wanahitajika. Upungufu huu unazikabili hospitali zote mbili, Hospitali ya Wilaya ya Mbozi na Hospitali ya *Mbozi Mission*. Hospitali ya *Mbozi Mission* inaendeshwa kwa PPP hivyo watumishi wanaotakiwa kuajiriwa na Serikali ni wachache sana. Naishauri Serikali kuajiri watumishi katika hospitali hii, pia Vituo vya Afya vya Isanga, Itaka, lyula na zahanati havina watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI: Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana kwa kazi mnazozifanya, tunaziona, kazana sana. Nashauri katika hospitali nyingi za vijijini hazina vitendea kazi vya kutosha, viongezwe; pili, wafanyakazi ni shida, unakuta wako wawili kazi zinawawia nyingi, wanachoka, hivyo basi lifanyie kazi suala hili waajiriwe wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu dawa, baadhi ya dawa nyingine hatuzipati, hasa zile muhimu; fuatilia suala hili, tunaambiwa hazipo tununue katika maduka ya dawa ya watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, wazee sehemu nyingine hawajapatiwa vyeti vya kutibiwa bure, wasaidie wazee; kama Kata ya Kanyangereko, Maruku, Nyakato na nyingine nyingi.

MHE. STELLA A. IKUPA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana pamoa na Naibu wake kwa kuchapa kazi na jinsi wanavyojitoa kuhakikisha afya za Watanzania zinakuwa salama (ulizima wa nguvu kazi ya Taifa letu). Pili, niwapongeze watendaji wote wa Wizara hii wanaowasaidia Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi; utambuzi wa watu wenye ulemavu wenye vipato duni ili waweze kupatiwa vitambulisho kwa ajili ya matbabu tofauti na ilivyo sasa ambapo mtu mwenye ulemavu mpaka apatiwe barua ya utambulisho. Madhara ya barua ya utambulisho ni pale mtu mwenye ulemavu anapouqua ghafla usiku ama akapatwa na ugonjwa akiwa nje ya eneo linalomtambua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kuwa Wizara iliangalie hili na ikiwezekana zoezi hili liende sambamba na zoezi linaloendelea sasa la kuwapatia vitambulisho wazee.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema jambo tajwa hapo juu, naunga mkono hoja hii ya hotuba Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

MHE. SHAMSIA A. MTAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kujenga hospitali ya kisasa ya Benjamin Mkapa iliyopo Dodoma, lakini napenda kuishauri Serikali kwamba hospitali ile ina upungufu mkubwa wa madaktari pamoja na wauguzi. Hivyo basi Serikali iangalie hospitali ile kwa ukaribu mkubwa kwani inahudumia wananchi wa maeneo mengisana kama vile *UDOM* ambapo wanafunzi takribani wote wanatibiwa pale, Wabunge na wananchi wa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na ongezeko kubwa la udhalilishaji wa wanawake na watoto. Naishauri Serikali iweze kutoa mafunzo pale akina mama wanapokuja kliniki ni namna gani inapotokea kubakwa kwa mtoto wake. Katika hatua ya awali kitu gani afanye ili ushahidi wa awali uweze kupatikana. Mara nydingi ushahidi huu hukosekana kwa vile huwasafisha kwa kuwakosha wakiona wanaweka vizuri kumbe wanapoteza ushahidi.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya kwa juhudzi zake za kupeleka Madaktari Bingwa katika mikoa ya pembezoni kwa huduma za kibingwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi walikuwa wakishinda kufuatilia huduma hizi Muhimbili jambo ambalo limeleta fara kubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na ongezeko kubwa la maradhi ya kisukari mpaka kwa watoto wadogo jambo ambalo limeleta hofu sana kwa wananchi wetu. Hivyo naishauri Serikali ifanye utafiti tuweze kujua sababu au chanzo cha maradhi hayo. Inawezekana pengine kuna vitu ambavyo vinasababisha ongezeko la kasi lilioljitokeza la maradhi haya ya kisukari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikia Mheshimiwa Waziri wa Afya akisema katika hotuba yake kwamba kuna kitengo cha matibabu ya kupandikiza figo kwa wagonjwa walio na matatizo ya figo. Hivyo basi naipongeza Serikali pamoja na Waziri wa Afya kwa mafanikio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kujua mgonjwa anapopata tatizo hili anapata wapi figo hizi kwa ajili ya kupandikiza? Anakuja na mtu wake ambaye atatoa figo au ananunua? Naomba Serikali watupatie majibu ili tuelewe kwa sababu hili jambo limetufanya tupate faraja kubwa.

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa zoezi zima la uwezeshaji vituo vya afya kuweza kutoa huduma za upasuaji, jengo la mama na mtoto na maabara. Hii itapunguza kwa kiasi kikubwa wazee, akina mama na watoto kutembea umbali mrefu kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Ludewa tunashukuru kwa kupewa shilingi milioni 500 kwa Kituo cha Afya Mlangali na shilingi milioni 400 kwa Kituo cha Afya Manda na madawa shilingi milioni 300. Kwa sasa Wilaya ya Ludewa kuititia nguvu za wananchi na wadau mbalimbali tunajenga vituo vya afya 17 ambavyo tunaweza kujenga mpaka ngazi ya uezekaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo tunaiomba Serikali kuunga mkono jitihada za wananchi katika kutekeleza llani

ya Uchaguzi ya CCM (2015-2020) katika ngazi ya umalizaji majengo hayo pamoja na zahanati 22 zinazojengwa katika vijiji mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tatizo la dawa limekuwa ni sugu katika baadhi ya zahanati bila kusahau watumishi katika zahanati na vituo vya afya. Ikumbukwe jiografia ya Halmashauri ya Ludewa kimiundombinu si mizuri kwani tuna vijiji 15 havifiki kwa mawasiliano ya barabara yaani huko vilipo vijiji hivyo havijawahih ona gari toka kuumbwa kwa ulimwengu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa inaomba kupatiwa magari (*ambulance*) walau mawili ili kutoa huduma ya usafiri pindi itokeapo dharura ya mgonjwa anapozidiwa na anapopewa rufaa kwani miundombinu ni mbali toka sehemu moja kwenda nyingine ukizingatia hakuna huduma ya mawasiliano kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja iliyoko mezani leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto nyingi sana kwenye Wizara ya Afya na kila mara imekuwa ikipangiwa bajeti ndogo sana kulinganisha na mahitaji. Sasa hivi kumekuwa na mkanganyiko mkubwa sana kati ya Wizara ya Afya na TAMISEMI. Kwa nini Serikali ili amua kuchanganya kazi za Wizara hizi mbili? Kwa mfano, inapofikia suala la majengo ni jukumu la TAMISEMI, halafu watumishi ni wa Wizara ya Afya. Ningependekeza masuala haya yote ya ajira na majengo yanetakiwa kuwa chini ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine linahusu Jimbo moja kwa moja; wakati wa ziara ya Waziri Mkuu aliahidi kuleta gari la wagonjwa kwenye Zahanati ya Chiwale, napenda kufahamu ahadi kama imekufikia na utekelezaji wake utafanyika lini ukizingatia kwamba Jimbo la Ndanda

lina kituo cha afya kimoja tu, kati ya Kata 16, hili lifanyike kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni juu ya majengo; pamekuwa na sintofahamu kubwa sana juu ya aina ya majengo yanatotakiwa. Wananchi wanahitaji majengo ya kuweza kupatiwa huduma, lakini Serikali imetengeneza ramani ambazo kwa hali ya wananchi wetu ambao tumewataka weweze kukamilisha majengo haya mpaka hatua ya lenta ndipo Serikali itayapokea, lakini suala hili limekuwa gumu sana kutekelezwa kwa sababu ya uwezo mdogo wa wananchi pamoja na kukatishwa tamaa na hali ya kutokukamilishwa kwa majengo ambayo wananchi tayari wameshakamilisha majengo hayo. Pamoja na kuangalia miaka ya mbele, basi Serikali sasa ikubali angalau kukamilisha majengo ya zamani (maboma).

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ugonjwa wa tezi dume umeonekana kuongezeka sana nchini. Tatizo kubwa ni *operation* zinazofanyika, lazima mgonjwa afanyiwe mara mbili. Aidha, hata wanaofanyiwa *operation* wengi wanakufa.

Ushauri wangu madaktari waongezewe ujuzi nje ya nchi na ikibidi vifaatiba vyta kisasa vipatikane kuokoa wanaume hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira ya watumishi sekta ya afya; Mkoaa wa Kigoma una upungufu wa watumishi ya afya wapatao asilimia 70 hali ambayo inatishia uhai wa watu wa Kigoma. Aidha, nchi nzima kuna upungufu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu Serikali ichukue hatua za makusudi kuajiri watumishi hao ila kila zahanati iwe na CO/CA, vituo vyta afya viwe na daktari mmoja na CO_s, hii itasaidia kupunguza vifo vyta akina mama wajawazito na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la matibabu ya wazee; sera ya wazee kutibiwa bure bado inasuasua sana kwani sehemu nyingi wazee hawa hawapati matibabu bure. Aidha, vitambulisho vimekuwa shida kupatikana. Ni vyema vitambulisho vikatolewa kwa wazee hawa wenye umri wa miaka 60+.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kuwa Wizara iwasiliane na TAMISEMI ili wazee wote wapewe vitambulisho ili wapate matibabu bure. **NB:** Vitambulisho vitolewe bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya *Engender Health* na *Bloomberg*; miradi hii iko Mkoa wa Kigoma na inatarajiwa kufikia ukomo/mwisho Aprili, 2019. Huduma nyingi zinazofanyika Mkoani na Wilaya zote ni huduma ya mama, baba na mtoto. Mfano, vituo vitano kila Wilaya vilivyojengwa vimewekewa vifaatiba vyaa kisasa lakini hakuna wataalam wa vituo hivyo hasa Jimbo la Buyungu (Kakonko). Ni aibu kwa Serikali yetu kupewa msaada wa majengo na mfadhibili kisha Serikali inashindwa kuweka/kuajiri wataalam wenye ujuzi wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ushauri wangu kuwa vituo hivi vipewe vipaumbele na Wizara itafute ufadhili utakaosaidia miradi hii iendelee kutoa huduma (*sustainability*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kinga ni bora kuliko tiba; Wizara ya Afya ijiimarishe kwenye kampeni ya kinga ili iepuke kutumia fedha nyingi za tiba. Kampeni ya kutumia tv, redio, michezo/maonesho/sanaa na kadhalika, vipindi kama chakula bora (kuleni chakula bora, mboga, samaki, maziwa na kadhalika), kampeni ya kunawa mikono baada ya kutoka chooni, kuchemsha maji; mabwana na mabibi afya wafanye kazi kukaguza usafi majumbani (karo, vyoo safi na kadhalika).

MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima wa afya zetu na

tunaendelea na harakati zetu vizuri. Pia ninapenda nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwako wewe kwa namna unavyosimamia Bunge hili kwa umakini na umahiri mkubwa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichangie Wizara hii ya Afya kwa mambo yafuatayo; malaria, UKIMWI, maradhi ya figo na maradhi yasiyo ya kuambukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba malaria yameshuka nchini kwa kiasi cha afadhali, lakini kwa namna Serikali ilivyojisahau uwezekano wa kurudi tena kwa kasi upo. Hivyo basi ni vyema Serikali ikafikiria tena namna ya kupambana na malaria. Ni vyema Watanzania wakawekwa mbali na malaria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Taifa linaelewa sana jinsi athari za UKIMWI zinavyoweza kupunguza nguvukazi ya Taifa, ni vyema Serikali ingeongeza juhudu zaidi katika kuwaelimisha watu wetu. Lakini pia hizi dawa za ARV ni vyema ikawa ni rahisi zaidi kupatikana katika kila eneo la nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nitoe pongezi kwa Wizara kuhusiana na kadhia hii, Taifa limeweza kulipa fedha nydingi sana kwa kuwatibu watu wetu nchini. Kwa namna ya pekee, ninapenda niishauri Serikali iendelee kufunza zaidi wataalam wa fani hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba niishauri Serikali kutoa taaluma ya kutosha kuhusiana na vipi Watanzania wataweza kujilinda na maradhi haya, yakiwemo *pressure*, sukari na kadhalika. Kwa kasi ya kutisha maradhi haya yanajitokeza kwa watu wetu na pia namna ya kuwatibu haijakuwa maridhawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala hili la vifaatiba, bado kabisa Taifa letu lina tatizo kubwa sana. Ukienda hospitali zote za rufaa utawakuta wagonjwa wengi wamepanga mistari wakiwa wanashubiri kupata huduma

za *x-rays*, *CT-scan*, *ultra sound* na vifaa vingine. Mimi ninadhani huu sasa ndiyo wakati wa kuacha porojo na kufanya kazi kubwa ya kujenga afya zetu kwa kuvitafuta vifaa hivi na kuvieneza katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usambazaji wa dawa; hapa napo pana uzembe mkubwa. Hivi inakuwaje Serikali inanunua au inatengeneza dawa kwa maslahi ya Watanzania wakati wa kuzisambaza dawa hizi eti kuna maeneo hazifiki, zinapelekwa wapi na nani? Ninaomba hapa Waziri atakapofanya majumuisho atoe majibu ya swali hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na utumishi wa Wizara, ni ukweli usiofichika kwamba Wizara hii ina uhaba mkubwa wa watumishi, yawezekana ndiyo maana utendaji wa Wizara hii unasuasua, siyo mzuri, malalamiko ni mengi, wagonjwa wanarundikana mahospitalini, watabibu ni haba. Ni vyema Serikali ikafikiria vizuri na ikaajiri vijana kwa lengo la kuziba hii mianya.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhaba wa hospitali; bado kabisa hospitali ni haba sana kulingana na ukubwa wa nchi yetu. Tanzania ya sasa inahitaji hospitali kama za Muhimbili angalau 10 katika Mikoa yote mikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayoendelea kufanyika. Nashukuru kwa mgao wa magari ya *ambulance*, mgao wa Madaktari Bingwa na watumishi. Pamoja na pongezi hizi, naomba kutoa ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, matibabu ya *cancer* - Bugando; zipo taarifa kwamba zaidi ya asilimia 30 ya wagonjwa wa *cancer - Ocean Road* wanatoka Kanda ya Ziwa. Kutokana na takwimu hizo ni vyema Serikali ikaongeza bajeti ya vifaatiba kwa hospitali hii ili kupunguza msongamano wa wagonjwa wanaotoka Kanda ya Ziwa kwenda Dar es Salaam jambo ambalo litapunguza gharama

na usumbufu lakini pia litasaidia kupunguza gharama kubwa kwa mgonjwa inayotolewa hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Hospitali ya Rufaa ya Geita; kwanza naipongeza Serikali kwa kutenga fedha za ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Geita. Hivi sasa wananchi wa Mji wa Geita wanapata taabu sana kwa kukosa hospitali ya *level* ya Halmashauri ya Wilaya kwa kuwa hospitali yetu ya Wilaya/Mji ndiyo Hospitali ya Mkoa kwa sasa.

Naiomba Serikali kuhakikisha ujenzi wa Hospitali ya Mkoa ambayo ipo Mjini Geita na inasuasua kutokana na uhaba wa fedha. Naitaka Wizara kutofautisha inapozungumza kuhusu Hospitali ya Mkoa inamaanisha hospitali ipi kati ya Hospitali ya Geita Mjini na Hospitali ya Chato. Ni vizuri kutofautisha ili kutoa uelewa mpana wa wananchi kufahamu ni kipi kipaumbele cha Wizara kati ya hizi hospitali mbili za Mkoa ndani ya Mkoa mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upungufu wa watumishi; kwa muda mrefu Hospitali ya Mkoa wa Geita inaendelea kutokuwa na Madaktari Bingwa, hadi leo kuna Daktari Bingwa mmoja tu ambae ni *surgeon*, wale ambao Wizara iliwapeleka wote hawajafika. Pia kuna upungufu mkubwa wa manesi, wataalam wa kada za maabara, usingizi na madaktari wa kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana *TFDA* kwa kuendelea kusimamia viwango vya chakula kwa Watanzania. *TFDA* wanatoza ada kwenye kila leseni ya *bar*, *grocery* na migahawa ya shilingi 100,000 kwa mwaka. Ada hii ambayo ambayo ni sharti ya mfanyabiashara kupata leseni katika Halmashauri zetu, kwa ujumla hakuna kazi ambayo *TFDA* wanafanya kwenye *bar* kwa kuwa vinywaji vyote vinavyouzwa *bar* au *grocery* ni vya kununua na havitengenezwi na muuzaji. Hata kama lengo ni mamlaka hii kukusanya fedha ili iweze kujientesha, busara ingetumika angalau shilingi 20,000 kwa hoteli kubwa zenye *barna* shilingi 10,000 kwa *grocery* au *bar* za mitaani kwa kuwa ada hizi zinaongeza gharama kwa wananchi bila sababu yoyote.

Naiomba Serikali ifahamu pamoja na ada ya *TFDA* kuna ada ya leseni, ushuru, *TRA*, michango ya mwenge, majengo, ukaguzi wa watu wa afya, usafi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha za madeni ya watumishi; Jimbo langu kuna watumishi wengi Hospitali ya Mkao ambao zamani walikuwa *DC* wana madeni makubwa na ya muda mrefu. Naiomba Wizara kulipa madeni yote kwa kuwa yameleta usumbufu mkubwa.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naanza kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri ya matumaini makubwa kwa Watanzania. Pia naipongeza Wizara ya Afya kwa juhudzi zake za kuhakikisha kuwa Watanzania wanakuwa na afya bora wakiwemo wananchi wa Nyang'hwale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kama Mbunge kwa Wizara hii ni kuhakikisha pesa zinakwenda kwa wakati katika hospitali, vituo vya afya na zahanati zetu. Wizara imepanga kutoa chanjo kwa watoto wa kike ya saratani ya shingo ya kizazi. Kikubwa elimu itolewe huko vijiji ni ili wananchi waondokane na hofu ya chanjo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu; Kituo cha Afya Kharumwa kina upungufu wa wataalam wa afya, vifaatiba, *X-ray* na kadhalika, pia dawa hazitoshi, wodi hazitoshi na zilizopo ni ndogo sana zina vitanda vinane kwa wanaume na wodi ya mama na mtoto ina vitanda 20 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Nyang'hwale vitambulisho vya wazee bado hawajapewa, kwa hiyo hawapati haki yao ya matibabu bure. Je, ni lini watapewa vitambulisho vyao?

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua kali zichukuliwe kwa watu wanaonajisi na kubaka watoto wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kutoa gari la

wagonjwa Kituo cha Afya Kharumwa. Wananchi wanawapongeza sana na wanaomba kwa Mungu muendelee na moyo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri ni lini Kituo cha Afya Kharumwa kitapandishwa na kuwa Hospitali ya Wilaya? Hadi sasa inaitwa Hospitali ya Nyang'hwale lakini haijapata hati hadi leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja bajeti hii ya Wizara.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, Dar es Salaam ina wakazi takribani milioni tano na Wizara ilikuwa na azma ya kuimarisha Hospitali za Temeke, Ilala na Mwananyamala ili kusogeza huduma za kibingwa kwa jamii na kupunguza msongamano kwenye Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili. Lengo hilo la kuimarisha hospitali kwenye Wilaya hizo halijafanikiwa na hivyo msongamano wa wagonjwa umeendelea kuwa kero. Naishauri Serikali kuimarisha hospitali hizo ili kusogeza huduma kwa jamii na kupunguza msongamano wa wagonjwa kwenye Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi kubwa ya kupeleka wataalam wa fani mbalimbali kwenye vituo vyta afya na *dispensaries*, bado upungufu ni mkubwa na umeongezeka zaidi baada ya kufukuza watumishi wenye vyeti *fake*, wengi wao wakiwa wataalam wa afya. Ni muhimu sasa kwa Serikali kupeleka wataalam wa kutosha ili kupunguza *ratio* ya wagonjwa kwa wataalam wa afya. Kama *WHO standard* ni daktari 1:10,000 lakini kwa Tanzania ni daktari 1:25,000, uwiano huu ni mkubwa sana na inafanya madaktari kulipua kazi bila ya kutumia muda wa kutosha kumsikiliza mgonjwa, kumpa ushauri nasaha na mwishowe tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali itekeleze mkakati maalum wa kutoa mafunzo kwa watumishi wa afya

na kuhakikisha wanapunguza kazi kwenye maeneo mbalimbali. Serikali ianzishe mkakati wa kutoa motisha kwa watumishi wanaopangwa maeneo magumu yasiyokuwa na miundombinu rafiki.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, hali mbaya ya Hospitali ya Wilaya ya Ulanga, majengo ni chakavu na machache. Wataalam (wahudumu wa afya) wapo wachache na wasio na sifa, gari la wagonjwa lipo moja ambalo nililikarabati mimi Mbunge na mahitaji ni makubwa sana; upatikanaji wa dawa bado hauridhishi kutokana na kuchelewa usambazaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NHIF* bado kumekuwa na ugumu kwa baadhi ya mashirika ya umma kujunga kama takwa la kisheria. Mfano *BOT* mpaka sasa hawajajiunga.

MHE. ZAINAB M. AMIRI: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Ummy A. Mwalimu (Mbunge) pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile (Mbunge) kwa juhudini kubwa wanazofanya katika kutekeleza majukumu yao kwa weledi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iondoe malipo katika hospitali za Serikali kwa maiti ambazo zimehifadhi wa katika vyumba vyaya kuhifadhi maiti kwa kuwa wakati wa uhai wao walikuwa wanachangia Pato la Taifa kwa kulipa kodi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wote walio chini ya miaka mitano wapate huduma za afya bure kama ilivyo kwa wazee.

Mheshimiwa Naibu Spika, dawa za ugonjwa wa saratani ni ghali mmo, hivyo nashauri Serikali ipunguze bei ya dawa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kwa wale wagonjwa wasio na uwezo wa matibabu ya moyo hususani

watoto, Serikali iweze kugharamia matibabu hayo. Kuna baadhi ya chanjo za watoto ambazo wakati wanachanjwa huwaletea homa kali sana. Nashauri Serikali ifanye maboresho kwa chanjo hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, akina mama wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano waendapo kliniki kuchunguzwa afya zao nashauri Serikali itoe vyakula vya lishe kama ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya usafishaji figo ni gharama sana. Hivyo naishauri Serikali ipunguze gharama za tiba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iweke *stand by generators* katika hospitali zote za Wilaya ili kuweza kusaidia wagonjwa na wauguzi umeme unapokatika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali nyingi majengo yake ni chakavu, ukarabati ufanyike katika hospitali hizo, naishauri Serikali iweke nyavu za kuzuia mbu katika wodi za Hospitali ya Muhimbili na ukarabati wa vyoo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iboreshe miundombinu ya hospitali zetu hususani upatikanaji wa huduma ya maji katika hospitali zetu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, madaktari na wauguzi waongezwe mishahara na posho ili waweze kufanya kazi kwa weledi na kuondoa tatizo la rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iboreshe kambi za wazee, kujenga/kukarabati nyumba zao, chakula cha kutosha na kuwapatia vifaa muhimu katika kambi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, namuomba Mwenyezi Mungu awape afya njema na umri mrefu Waheshimiwa Ummy A. Mwalimu (Waziri) na Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile (Naibu Waziri) ili waweze kutekeleza majukumu yao ya kila siku katika Wizara hii ambayo kimsingi

ni tegemeo la Watanzania wote hususani katika masuala ya afya.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hotuba Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na upungufu wa vituo vya afya; Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ina jumla ya kata 39 lakini tuna vituo vya afya vitano tu na zahanati 57 kati ya vijiji 167. Hali hii inadhoofisha utoaji wa huduma ya afya kwa akina mama na watoto. Akina mama wajawazito wanalazimika kutembea umbali wa zaidi ya kilometra 10 kufuata huduma za afya. Hivyo, tunaomba Serikali itupie jicho Wilaya hii ya Tunduru kutohana na uchache wa vituo vya afya na zahanati. Jitihada za Halmashauri ya Wilaya zinagonga mwamba kutohana na ukubwa wa eneo pamoja na makusanyo madogo ya mapato ya ndani. Hata hivyo, kuna upungufu mkubwa wa watumishi katika sekta ya afya; zahanati nyingi zina wahudumu si zaidi ya wawili, nyingine zina mhudumu mmoja tu, jambo ambalo linadhoofisha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi ya muda mrefu ya Rais wa Awamu ya Nne Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete mwaka 2014 alitoa ahadi ya kujenga kituo cha afya katika Kijiji cha Nalasi chenye wakazi zaidi ya 50,000 katika mgawanyo wa vijiji vinne. Jambo hili limekuwa ni kero kubwa sana, wananchi walijitolea kufyatua tofali na Halmashauri ilitoa shilingi 80,000,000 mwaka 2015 lakini fedha hizo zilliishia kujenga *foundation* tu, pamoja na uwepo wa matofali yale mpaka leo hakuna kilichoendelea. Halmashauri imejitahidi kutenga shilingi milioni 100 kila mwaka lakini upatikanaji wa fedha umekuwa mgumu sana. Hivyo ninaiomba Serikali kutekeleza ahadi hii ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ahadi ya muda mrefu ya gari la wagonjwa; Rais wa Awamu ya Nne alitoa ahadi ya kutoa gari katika Kituo cha Afya Mchoteka mwaka 2014 lakini hadi hivi leo ahadi hiyo haijatekelezwa. Ninaomba

Serikali kuona umuhimu wa kutekeleza ahadi hii kwani kituo hiki cha afya kipo umbali wa kilometra 80 kutoka ilipo Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Mtina kimejengwa mwaka 1970, majengo yake ni machakavu na hakuna wodi ya akina mama na watoto; haina maabara wala *theater* (chumba cha upasuaji) na kituo hiki kinahudumia Kata nne; Lukumbule, Mchesi, Tumemado na Kata ya Mtina yenyewe; zaidi ya wananchi 80,000 wanahudumiwa katika kituo hiki. Hivyo, ninaiomba Serikali kutoa fedha kuongeza huduma za afya kama ilivyo katika vituo vingine vilivyoongezewa majengo ili kutoa huduma ya malazi, upasuaji na huduma ya maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Tunduru Kusini kuna Hospitali ya *Mission* ya Mbesa ambayo inategemewa takribani na wananchi zaidi ya 200,000. Rais wa Awamu ya Nne alitoa ahadi ya kuifanya hospitali hii kuwa Hospitali Teule ya Wilaya lakini mpaka leo ahadi hiyo hajatekelezwa pamoja na kwamba Halmashauri inapeleka watumishi katika hospitali ile ili kusaidia kutoa huduma kwa wananchi kama ilivyo katika hospitali nyingine teule zilizopo maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Wilaya ina gari bovu sana la wagonjwa na ukizingatia Wilaya ile ni kubwa sana, hivyo, tunaomba gari la wagonjwa.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri Wizara itathmini miradi yote iliyokuwa imefadhiliwa na Benki ya Dunia kuboresha baadhi ya zahanati kwa kujenga wodi za wazazi na *theater* ili kuboresha afya ya mama na mtoto.

Moja ya zahanati hizo ni Zahanati ya Itumba katika Jimbo la Igunga ambayo ilipewa mradi wa kujenga na kuboresha *theater* na wodi. Mradi huo ulimalizika bila kukamilishwa kwa majengo (miundombinu) hayo kwa miaka mitatu sasa. Naomba Serikali ikamilishe mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naiomba Serikali pia ikiboreshe Kituo cha Afya cha Igurubi ambacho uhudumia kata sita za Tarafa ya Igurubi za Kiningu, Igurubi, Kininginila, Mwameshimba, Itunduru na Isakamaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutoa pongezi za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Tano na Wizara ya Afya kwa kazi nzuri ya kuboresha huduma za afya. Pamoja na changamoto hizo, napenda kutoa maoni yangu kuhusu changamoto zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Kituo cha Afya Mjmwema - Songea Mjini; kituo hiki cha afya kinafanya kazi kama Hospitali ya Wilaya, hivyo basi kufanya kazi kubwa kuliko uwezo wake. Kituo hiki cha afya kinakabiliwa na changamoto zifuatazo; ukosefu wa wodi ya wanawake na wanaume, ukosefu wa *x-ray*, *MR*/na vifaa tiba vingine, ukosefu wa gari la wagonjwa (*ambulance*) na uchakavu wa majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Songea una jumla ya wakazi 230,000 lakini hakuna Hospitali ya Wilaya. Tunahitaji Hospitali ya Wilaya ili kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vya afya; Wilaya ya Songea Mjini yenye jumla ya wakazi 230,000 na kata 21 haina Hospitali ya Wilaya. Tunahitaji vituo vya afya angalau vitatu katika Kata za Ruvuma, Ndilima Litembo na Mletele.

MHE. MARTIN M. MSUHA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Afya kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya katika kuhudumia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza ni uhaba wa vituo vya kutolea huduma za afya; Halmashauri ya Mbinga ina jumla ya kata 29, tarafa tano na vijiji 121, lakini kuna zahanati 42 tu na vituo vya afya viwili hivyo kufanya upungufu wa zahanati 79 na uhaba wa vituo vya afya 27. Pamoja na upungufu huo wa vituo vya afya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga haikuletewa fedha za upanuzi/ujenzi wa vituo vya afya kama ilivyofanyika kwenye Halmashauri zingine. Hivyo basi niiombe Wizara iweze kutuletea fedha za upanuzi wa vituo vya afya vifuatavyo; Kituo cha Afya Mapera, Kituo cha Afya Kindimba Chini na Kituo cha Afya Matiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhaba wa watumishi; kwa idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya tulizonazo *Mbinga DC* tuna mahitaji ya watumishi 324 wa kada mbalimbali za afya lakini waliopo ni 112 tu hivyo kufanya upungufu wa watumishi 212. Serikali ifikirie kwa haraka walau kutupatia watumishi 22 wanaohitajika ili vituo/zahanati mpya nne zilizokamilika hivi karibuni ziweze kufunguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo la *NACP/NTLP Joint Office; Programme za NACP/NTLP* walikuwa na mradi wa ujenzi wa ofisi ya pamoja iliyopo Luthuli nyuma ya Ofisi za *WHO*. Jengo hilo lilikuwa linajengwa kwa ufadhilli wa *Global Fund*. Tangu mwaka 2013 *Global Fund* waliachcha kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi huo hivyo jengo hilo la ghorofa tatu limekwama na limeanza kuchakaa. Niiombe Wizara iangalie uwezekano wa kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha jengo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Hospitali ya Mloganzila, niipongeze Serikali kwa ujenzi wa hospitali hiyo. Niiombe Serikali kuipa jicho la pekee hospitali hiyo kwa maana ya kupeleka watumishi wa kutosha. Wananchi wamekwishaanza kutoa malalamiko kuwa ukipelekwa Mloganzila basi unapelekwa pahali ambapo hapana usalama na uhakika wa tiba, vifo ni vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Waziri Ummy pamoja na Naibu Waziri wake pamoja na timu yote kwa ujumla kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuwatumikia Watanzania bila kuchoka. Mwenyezi Mungu atawalipa ujira wao huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Lushoto kuna Kituo cha Afya kimoja tu ambacho kipo Mlola na kituo kinahudumia zaidi ya kata nane, na hii imepelekea mrundikano wa wagonjwa. Hivyo basi niiombe Serikali yangu tukufu ipandishe hadhi Zahanati ya Makanya kuwa Kituo cha Afya kwani hii itapunguza mrundikano wa wagonjwa na kuokoa vifo vyaa wananchi hasa vifo vyaa mama na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto kubwa sana ya gari la wagonjwa katika Kituo cha Afya Mlola. Niiombe Serikali yangu katika bajeti hii mtutengene pesa kwa ajili ya kununua gari la wagonjwa kwani tunapoteza wananchi wengi hasa akina mama wajawazito pale wanapohitaji usafiri kwenda katika Hospitali ya Wilaya na kama unavyojuu miundombinu yetu ya barabara sio mizuri kabisa. Kwa hiyo kunahitajika gari la wagonjwa ambalo ni kwa ajili ya kubebea wagonjwa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kuwa Jimbo la Lushoto kuna kituo cha afya kimoja lakini wananchi wamejitolea na kuanza kujenga vituo vyaa afya viwili ambavyo ni Kituo cha Afya Gare na Kituo cha Afya Ngwelo. Hivyo basi, naomba safari hii Serikali ivitengee pesa ambazo zitatosha kumalizia vituo hivyo ili kupunguza msongamano katika Hospitali ya Wilaya na ni pamoja na kuendelea kuokoa vifo vyaa mama na mtoto ukizingatia vituo hivi vipo mbali na Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo changamoto za vifaatiba katika Hospitali ya Wilaya ya Lushoto ambavyo ni *ultra sound, x-ray machine* ni ndogo haina uwezo. Kwa hiyo,

inaharibika mara kwa mara hii imepelekea wagonjwa wengi kukosa huduma na kupata usumbufu wa kwenda na kurudi na ukizingatia wagonjwa wengi wanatoka mbali. Kwa hiyo, niiombe Serikali ipeleke vifaa hivyo ili kuokoa vifo vya wananchi ambavyo vinaweza kuzuilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la watumishi katika kada ya afya, niiombe Serikali ipeleke watumishi wa kutosha katika zahanati zetu pamoja na vituo vya afya pamoja na Hospitali ya Wilaya. Wananchi wengi wamejenga zahanati kwa nguvu zao mpaka nyingine zimeisha, lakini watumishi ni shida mpaka zahanati hizi kuelekea kuwa magofu na hii inapelekea kuwavunja nguvu na kuwakatisha tamaa. Naomba Serikali iajiri watumishi haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiofichika kuwa katika vituo vyetu vya afya na katika hospitali zetu za wilaya chanjo ya kichaa cha mbwa ni gharama, na siyo gharama tu pia haipatikani. Kwa hiyo, niiombe Serikali ipeleke chanjo hiyo ya kichaa cha mbwa katika hospitali zetu pamoja na vituo vya afya mpaka kwenye zahanati ili kuokoa wananchi wanaopata ajali ya kung'atwa na mbwa. Tumekosa na kupoteza wananchi wengi waliopata ajali hizo za kung'atwa na mbwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, dawa muhimu hazifiki kwenye zahanati zetu vituo vya afya pamoja na hospitali ya wilaya, kwa mfano dawa za kisukari hizi ndio kabisa. Mimi kama Mbunge nimepata malalamiko mengi sana hasa kwa wale wazee amba wanatibiwa bure. Niishauri na kuiomba Serikali yangu ipeleke dawa hizi muhimu hasa katika zahanati, vituo vya afya na katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti inayopitishwa na Bunge ipelekwe kwenye maeneo husika na muda muafaka ili kuondoa changamoto wanazokutana nazo wananchi katika maeneo mbalimbali nchini hasa maeneo ya vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na ongezeko kubwa la watoto wa mtaani Serikali iongeze maeneo ambayo watu watapewa msaada pale inapobidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapungufu ya Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri zetu ni jambo ambalo limekuwa changamoto katika huduma mbalimbali za kijamii kulingana na uchache wa watumishi katika maeneo mbalimbali nchini. Pia upungufu wa Madaktari Bingwa katika Hospitali ya Rufaa katika Mkoa wa Rukwa na hospitali hili inazidiwa na wagonjwa kwa kuwa hatuna Hospitali ya Wilaya hata moja katika Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu dirisha maalum kwa ajili ya wazee; hospitali nyingi hazina dirisha maalum kwa ajili ya wazee na maeneo ambayo wamejitahidi kuweka dirisha kwa ajili ya wazee hakuna huduma. Nashauri Serikali kufatilia suala hili kwani wazee wetu wanapata taabu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu afya ya akili; Serikali iwekeze kwenye utafiti kujua nini kinasababisha suala hili kuendelea kwani idadi ya waathirika wa akili inazidi kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Serikali ikawekeza kwenye lishe kwani tuisipowekeza kwenye lishe tunakwenda kuzalisha watoto wenyewe udumavu wa akili.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja. Naipongeza Serikali ya CCM katika juhudzi za makusudi za kuwasaidia wananchi hasa wanawake na watoto kupata afya bora na huduma nyinginezo za kijamii. Naishukuru na kuipongeza Serikali kwa hatua iliyochukua kuanzisha matibabu ya kupandikiza figo

na upasuaji wa moyo hapa nchini. Pia naipongeza Serikali kwa kuanzisha chanjo ya saratani ya mlango wa kizazi kwa wasichana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri, naiomba Serikali iangalie namna ya kupunguza bei ya vifaa vya kujifungulia kwa mama wajawazito ili akina mama wasio na uwezo waweze kumudu gharama za vifaa hivyo. Serikali ijenge vituo vya kuwasaidia vijana walioathirika na madawa ya kulevyta na bangi ili warudi katika hali yao ya kawaida na waungane na wananchi wenzao katika ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *mayoma* kwa akina mama yanazidi kuwa tatizo kwa wanawake ni vyema ufanyike utafiti juu ya ukubwa wa tatizo hilo na baadae elimu itolewe kwa wanawake waende hospitali kabla ya matatizo hayajawa makubwa na kusababisha madhara mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naipongeza Wizara na viongozi wote wa Wizara kwa juhudhi kubwa wanazofanya katika kuvisimamia Wizara na utekelezaji wa majukumu yote kwa bidii, waendelee na moyo huo. Pamoja na Madaktari Bingwa akiwepo Dkt. Janabi, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu kwa hotuba yake nzuri na yenye kuleta matumaini. Tatizo la *x-ray* na Hospitali ya Wilaya ya Mafia limeingia katika hatua nzuri kuelekea kumalizika baada ya Serikali kutupatia mtaalamu wa mionzi (*Radiology*) na kufuatia mazungumzo yangu na Naibu Waziri Mheshimiwa Faustine Ndugulile tumekubaliana kuuwa tarehe 23 Aprili ataleta mtaalam sambamba na mtaalam wa kampuni iliyoleta *x-ray* hiyo ambao mimi Mbunge nawajibika kuwalipia gharama za safari zao kutoka India mpaka Mafia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema hili kwa sababu mara ya kwanza mwaka 2016 nilliingia gharama ya kuwaleta wataalam hao kwa gharama kubwa kuwaflikisha Mafia na Wizara yako Mheshimiwa Waziri iliweka katazo la kufanya *x-ray* zamani iliyotolewa na kampuni ya Philips ambayo ndio yenye mkataba na Wizara kutengeneza mashine za *x-ray*. Mheshimiwa Waziri wataalam wale walikaa Mafia kwa wiki tatu huku mimi binafsi nikishughulikia vibali nya kufunga mashine bila ya mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo furaha kukufahamisha kuwa baada ya mjadala mrefu uliopelekea kujengwa kwa chumba kipywa cha *x-raysasa* Wizara imeridhia kufungwa kwa *x-ray* Mafia na Naibu Waziri amenihakikishia atatumua mtaalam wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalizo ninalotaka kultoa hapa ni mnaingia gharama kwa mara ya pili kuwaleta wataalam kutoka India kuja kufunga *x-ray* ile. Ninaomba Wizara itekeleze ahadi yao hii ya kutoa ushirikiano ili *x-ray* ile ifungwe Mafia. Ni ukweli usio na shaka ikishindikana kufungwa mara hii sitapata na sitakuwa na uwezo wa kugharamia gharama hizi ambazo kwa kweli ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hospitali ya Wilaya ya Mafia gari la wagonjwa (*ambulance*)hi kuukuu na hufanya kazi kwa taabu sana na linaharibika mara kwa mara. Hivyo tunaiomba Wizara itufikirie kupata *ambulance* mpya. Sambamba na hilo Kisiwa cha Mafia kimezungukwa na visiwa vidogo vidogo vinne yaani Jibondo, Bwejuu, Chile na Juani. Kwa namna ya kipekee tunaiomba Wizara itusaidie kupata *ambulance boats* ili kusaidia dharura zinapotokea iwe rahisi kuwa wagonjwa kukimbizwa Hospitali ya Wilaya.

Mwisho tunaishukuru Serikali kwa ahadi ya shilingi milioni 500 za kujenga Kituo cha Afya Kirongwe. Tunaomba tuharakishiwe kupata fedha hizo ili ujenzi uanze mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naunga mkono hoja.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu hongera kwa kazi nzuri unayofanya wewe na Naibu wako na watendaji wako. Ni kazi iliyotukuka hadi mmewezesha Namtumbo tutarajie kuwa na huduma za upasuaji kuititia Kituo cha Afya cha Namkumbo kinachotarajiwa kukamilika kujengwa tarehe 31 Mei, 2018. Ahsante ninyi ndio mlitafuta fedha za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Namtumbo ni Wilaya kubwa nawaomba mtutafutie fedha zaidi kwa ajili ya kuendeleza nguvu za wananchi kuititia Halmashauri yao ya Namtumbo kukamilisha ujenzi wa vituo vya afya vingine viwili vya Lusewa na Mtakanini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Lusewa kiliahidiwa kukamilishwa na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne pamoja na Makamu wa Rais wa Awamu ya Tano. Ni vyema ahadi hiyo ikatekelezwa ili wananchi wa Lusewa na Tarafa nzima ya Sasawala waache kuwabeba akina mama wajawazito wanaoshindwa kuzalishwa na waganga wa kienyeji kupakiwa kwenye balskeli ndani ya matenga au machakacha kupelekwa Kiuma (Tunduru); Mbesa (Tunduru) au Songea umbali wa kilometra 72, 95 na 150; Mtawalia na ni wazi huwa hawafikishwi katika maeneo hayo yenye huduma ya upasuaji na huishia kugeuza safari, mama akibadilishwa jina kwa kuanzia na marehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha Mtakanini kiliombwa na Marehemu Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa kwa Rais wa Awamu ya Tatu na Rais huyo Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kukubali ombi hilo mbele ya familia na wanakijiji wote wa Mtakanini na ikakubaliwa kuwa ndio kiwe Kituo cha Afya cha Kata ya Msindo. Aidha, kituo hicho kitahudumia kata tatu, Kata za Msindo, Hanga na Namabengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa George Mkuchika dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile dakika 15, Mheshimiwa mto a hoja atafuati.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja, pili nataka kueleza kwamba hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, Kamati inayosimamia Wizara hiyo pamoja na wachangiaji wengi wameelezea umuhimu wa kupatikana haraka iwezekanavyo watumishi wa Idara ya Afya. Wameeleza kuwepo kwa upungufu katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kutoa taarifa na kuwaondoa mashaka Waheshimiwa Wabunge kwamba kama mnavyokumbuka mwezi Oktoba, 2016 Serikali ilifanya zoezi la uhakiki, katika uhakiki ule walipatikana jumla watu 14,000 wa kada mbalimbali ambao waligundulika kujipatia kazi kwa vyeti vya kughushi. Kati yao walikuwemo watumishi 3,310 kutoka katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa uhakiki huo Serikali ilisitisha ajira kwa maana ya kujiridhisha tuna watumishi wangapi. Napenda niliarifu Bunge lako tukufu kwamba zoezi lile limekamilika na kazi ya kwanza iliyofanywa na Wizara yangu ilikuwa ni kuziba pengo la wale watu ambao walionekana wameondolewa katika utumishi wa umma. Kwa hiyo, ilitoa kibali kuajiri watumishi mbadala 2,500 ili kufidia upungufu uliotokana na watumishi wa kada ya afya kuondolewa; kwa hiyo hao zoezi hilo linaendelea. Pamoja na hayo katika mwaka wa fedha 2017/2018 kama mtakumbuka Bunge hili lilipitisha ajira ya watumishi 52,436 zikiwemo nafasi za ajira za watumishi wa kada ya afya 14,104 sawa na aslimia 26.9 ya nafasi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili zoezi la watu 52,000 tutakapokuwa tunaajiri asilimia 26 sawasawa na watu 14,000 watakuwa wametoka sekta ya afya. Pia katika bajeti mlionipitishia juzi, na ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge

Serikali imetenga nafasi zingine za ajira 49,536. Ukichanganya wale 49,000 na 52,000 tutaajiri watumishi inafika karibu laki. Sasa ajira ya watumishi wa kada ya afya katika hao laki moja ni 16,205 sawa na asilimia 32.7 watakuwa ni watumishi wa sekta ya afya. Kwa hiyo utaona kwamba Serikali tumejipanga. Hata hivyo msisitizo wa Serikali kwa sasa ni kuhakikisha huduma za afya hazikwami kwa namna yoyote ile na hivyo ninawataka waajiri wote katika Serikali za mitaa kufanya uwahishaji wa matumizi kada za afya pamoja na kada nyiningine kwa kuwatoa watumishi wa kada hizi sehemu mbalimbali ambapo wapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nataka kusisitiza watu wengi, Waheshimiwa Wabunge wengi walipokuwa wanachangia hapa ndani walikuwa wanaeleza kwamba ziko zahanati zimefungwa, kuna vituo vya afya vimefungwa kwa kukosa watumishi. Mimi nataka kuliambia Bunge lako tukufu, nilishatoa maagizo na leo narudia tena, Serikali ya CCM haitoruhusu kituo cha afya kifungwe kwa sababu ya kukosa watumishi. Nilishasema ikitokezea mahala pengine amefariki maana si lazima iwe kwa sababu ya kufukuzwa, iwe kwa sababu yoyote ile Serikali ya CCM haitaruhusu kituo cha afya kifungwe kwa sababu ya kukosa mtumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nkipata taarifa katika Wizara yangu haraka haraka pale walipo wengi nitahamisha mtu nitapeleka wakati zoezi la kuajiri linaendelea naomba nilieleze Bunge lako Tukufu kuanzia leo yoyote ambaye aliongea humu ndani ambaye ana uhakika kuna zahanati haina mtumishi imefungwa; kuna kituo cha afya kimefungwa huduma zinakosekana niletewe taarifa hiyo wakati Bunge hili linaendelea nitapeleka watu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.
(*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mkuchika, naona wiki hii una habari njema nydingi sana na hii ni habari njema sana. Waheshimiwa Wabunge, tumpelekee orodha Mheshimiwa Mkuchika ili atupelekee wahudumu wa afya

kwenye vituo vyetu. Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile kwa dakika 15.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naanza kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi kwa rehema yako kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu ili niweze kuta hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Katika kipindi hiki cha utendaji wa kazi nikiwa kama Naibu Waziri nimepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Shukurani za pekee kabisa nazielekeza kwa Mheshimiwa Dkt. Ummy Mwalimu namuita daktari, Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ujuzi wake na ubobezi katika sekta ya afya na kwa ushirikianoa ambao amenipa katika kutkeleza majukumu yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha napenda kuwashukuru Makatibu Wakuu Dkt. Mpoki Ulisubisya pamoja na Sihaba Nkinga kwa mchango wao kwa kuwezesha utekelezaji wa majukumu yangu. Vilevile nawashukuru Profesa Mohamed Bakari - Mganga Mkuu wa Serikali, na pia nachukua fursa hii kuwashukuru watendaji wa wizara taasisi za Wizara pamoja na Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Waganga Wafawidhi wa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati; Vyuo vya Mafunzo vilivyo chini ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile natoa shukurani zangu kwa ushirikiano ambao wameendelea kutupa katika sekta ya afya maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii na wananchi wote kwa ushirikiano.

Mwisho natoa shukurani zangu za dhati kwa watoa huduma wote katika sekta ya afya kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameendelea kuitoa na uzalendo wao. Sifa tunazipata sisi Mawaziri lakini kazi kubwa zinafanyika huko chini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijielekeze katika kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge na la kwanza nitajiekeza katika hoja ambazo Wabunge wengi wamechangia kuhusiana na masuala ya miundombinu katika sekta ya afya. Serikali imekuwa inafanya kazi kubwa sana kuboresha zahanati, vituo vya afya na hospitali kwa mujibu wa Mpango wetu wa Maendeleo ya Afya ya Msingi ambapo zinazeleza kwamba kila kijiji kitakuwa na zahanati na kila kata itakuwa na kituo cha afya. Tumeboresha kwa kiasi kikubwa sana vituo vya afya na Waheshimiwa Wabunge wengi humu ndani mtakuwa mashuhuda kwamba vituo vingi vya sasa hivi vimeboresha, zaidi 208 .

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya TAMISEMI ambayo tumeipitisha hivi karibuni tunesema kwamba tutajenga Hospitali za Wilaya 67; katika mapendeleko ambayo tunaleta katika Bunge lako tukufu hilli baada ya Serikali kutukabidhi Hospitali za Rufaa za Mikoa tutaanza ujenzi wa hospitali sita za rufaa za mikoa pamoja na kuboresha hopsitali nydingine za rufaa katika maeneo ya afya ya mama, mtoto na huduma za dharura. Kwa hiyo, tumeendelea pamoja na hilo kuboresha huduma mbalimbali katika Hospitali zetu za Kikanda, Hospitali zetu Maalum na Hospitali za Rufaa za Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambasamba na kuboresha masuala ya miundombinu tumejielekeza katika kuboresha ubora wa huduma za afya. Moja ya jambo ambalo tumeweza kulifanya kama Serikali ni kuanzisha mfumo wa *starrating* ambao unaweka viwango vya ubora katika utoaji wa huduma na kwa kiasi kikubwa tumeweza kufanikiwa sana. Tuliweza kufanya tathimini ya awali ambapo zaidi ya asilimia 33 ya vituo vya kutoa huduma ya afya vilikuwa na viwango vya nyota sifuri; lakini baada ya kuja kufanya tathimini na maboresho makubwa viwango vile vimepungua sna kwenda chini ya asilimia 10 ni mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunaka tujielekeze zaidi kwenda mbali zaidi, tutatoa viwango vya ubora katika utoaji huduma. Sambasamba na hilo tunataka tuanzishe

utaratibu wa kutoa leseni kwa vituo vyetu nya utoaji huduma nya afya ambavyo sasa badala mtu kuwa kutoa huduma tu pasipokuwa na kuzingatia viwango nya ubora tutaanza kutoa leseni na leseni hii inahuishwa na viwango nya ubora ambavyo anavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo ilibuka kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge ni kwamba ni nani mwenye mamlaka ya kupandisha hadhi vituo nya afya na zahanati. Niseme tu, kwa mujibu wa *instrument* tulio nayo Wizara ya Afya ndio mamlaka pekee ambayo ina mamlaka kisheria ya kupandisha hadhi zahanati na vituo nya afya; na hii inaendana sambamba kabisa na majukumu ambayo Wizara ya Afya inayo. Wizara ya Afya itasimamia sera, masuala yote ya viwango na miongozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo Wizara ya Afya itasimamia Wizara zote za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Kanda, Hospitali Maalum na Hospitali za Taifa. Wenzetu Ofisi ya Rais, TAMISEMI majukumu yao ni kusimamia utekelezaji wa sera, viwango na miongozo inayotolewa na Wizara ya Afya, lakini sambamba na hilo watasimamia Zahanati, Vituo nya Afya na Hospitali za Wilaya; huo ndio mgawanyo wa majukumu ambao tunao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze kidogo katika suala la dawa, na hoja zimekuwepo nyingi na Waheshimiwa Wabunge wamechangia sana. Niseme tu kwamba katika awamu hii ya tano bajeti ya dawa imeongezeka kutoka bilioni 31 mwaka 2015/2016 kufika bilioni 269 katika mwaka huu wa fedha na mwakani tutakuwa na bilioni 270. Tumekwenda mbali zaidi kuimarisha mifumo yetu, takribani kama wiki tatu/nne tulikuwa tunazindua magari mapya 181, na mfumo ambao tunautumia ni kuhakikisha kwamba dawa tunazipeleka mpaka katika kituo cha kutoa huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambasamba na hilo tumeweka mwongozo wa utoaji wa huduma na hili nilitaka nilisisitiza. Tumeweka mwongozo wa kutoa huduma za afya za dawa, tunasema dawa gani itatolewa wapi kwa ngazi

gani kwa ugonjwa gani. Kwa sababu tulikuwa tunapata changamoto katika hospitali kubwa kwamba kampuni za dawa zilikuwa zinaenda kwa watoa huduma, wanawaambia andika dawa hii na utakapokuwa umeandika dawa hii ikawa inanunuliwa kwa wingi na sisi tutakuwa tunakupa *commission*. Na hii wakati ikasababisha zile dawa zisiwe zinapatikana pale kwa sababu tu wale wafanyabiashara walikuwa ndio wanatoa mwongozo wa jinsi gani ya dawa kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tumeweka mwongozo wa kutoa dawa ambao sasa utatoa mwongozo dawa gani inatumika wapi na katika aina gani ya ugonjwa. Lakini sambamba na hilo, tumekwenda mbali kuweka *label* katika dawa zetu. Kwa hiyo, ninaamini mifumo hii ambayo tunaendelea kuiboresha itahakikisha kwamba dawa tunazipata kwa kiasi cha kutosha. Hata hivyo nitoe rai, na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa sababu wengi wameniuliza mbona dawa fulani haipatikani. Kuna dawa zipo katika ngazi tofauti tofauti, hatutegemei tukakuta dawa kwa mfano *insulin* katika zahanati, hatuvezi tukazikuta zile. Zile dawa ziko katika ngazi tofauti kwa sababu dawa zile zinategemea na aina ya utaalam ya wale ambao wanatakiwa kuzitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunatambua kwamba magonjwa yasiyoambukizwa yanazidi kuongezeka na sisi tutakuwa tunapitia miongozo yetu mara kwa mara kuangalia wapi tunahitaji kuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuja na hoja nyingine ya masuala ya *CT Scan* na *MRI* katika hospitali za Rufaa za Mikoa. Kwa sasa hivi kwa mujibu wa miongozo yetu, huduma hizi haziwezi zikapatikana katika Hospitali za Rufaa za Mikoa. Ngazi ambazo *CT Scan* na *MRI* zinaweza zikaanzia, kwa mujibu wa miongozo yetu ni katika ngazi ya Rufaa za Kanda. Hata hivyo kadri nchi yetu inavyozidi kuongezeka na huduma zinazidi kuboreshwa tutafanya mapitio kuangalia kama tunaweza sasa tukaruhusu teknolojia hizi zikaweza kutumika katika ngazi hii kwa sababu changamoto hii si suala tu la

kuwa na vifaa hivi ni suala vilevile kuwa na wataalam ambao wanaweza kusimamia vifaa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lilikuwa ni suala la rasilimali watu. Tunakiri kwamba tumekuwa na changamoto kubwa ya rasilimali watu na nimshukuru sana Mheshimiwa Mkuchika, ameainisha vizuri sana kwamba katika mgao utakaokuja na sisi tutapata mgao katika watumishi wa afya. Naamini katika hili litatusaidia sana kupunguza changamoto ya watumishi ambayo tunayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo lilikuwa limeongelewa na hili nataka niwapongeze watoa huduma kwa kweli kwa kiasi kikubwa sana, kelele za wananchi kuhusu utoaji wa huduma zimepungua sana. Lugha za matusi na masuala ya rushwa kwa watumishi wa afya tumepongua sana; na hii niwashukuru sana na kuyapongeza mabaraza ya kitaaluma na maadili ambayo yako chini ya Wizara ya Afya. Tumezidi kuyaboresha na tumeendelea kuhakikisha kwamba tunafanya mabadiliko ya kisheria kuhakikisha kwamba taaluma hizi tunazisimamia vizuri. Moja ya mikakati ambayo tumeiweka ni kuhakikisha kwamba sasa kada zetu zote tunatoa leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, msije mkashangaa, tumepitisha Sheria ya Madaktari ambayo itahitaji hata mimi Naibu Waziri ambaye nimesimama hapa ni daktari, baada ya muda mtakuwa na mimi mnaniiona *dispensary*pale natoa huduma au Hospitali ya Benjamin Mkapa ili kuhakikisha kwamba tunapata mafunzo endelevu kuhakikisha kwamba na mimi ili niendelee kuitwa daktari na ku-*practice* kama daktari ninakuwa na leseni yangu na ninapata mafunzo endelevu na yote hii ni mikakati ya Serikali kuhakikisha kwamba watoa huduma wote wanakuwa... muda umekwisha?

NAIBU SPIKA: Endelea.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa

nijielekeze sasa katika ngazi ya maendeleo ya jamii. Kuna hoja kama mbili/tatu ambazo nazo ziliguswa sana na Waheshimiwa Wabunge na moja ilikuwa suala la *NGO's*, kwamba kuna *NGO's* nydingi hapa nchini. Nydingi ni *NGO* za Kimataifa lakini zimejisajili kama *NGO* za hapa nchini. Sambamba na hilo kuna fedha nydingi ambazo zinakuja kwenye *NGOs* na hazijulikani zinakwenda wapi. Tatu, ilikuwa ni kwamba kuna baadhi ya *NGO's* zimekiuka majukumu yao ya kikatiba na kuanza kujiingiza katika mambo mengine ikiwa ni pamoja na siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia idara yetu ya *NGO* tumefanya tathmini ya *NGOs* zote, kuangalia usajili wao, kuangalia mifumo yao ya fedha, kuangalia wanafanya shughuli gani, kuangalia kama je wanawasilisha taarifa muhimu zote ambazo zinatakiwa kwa mujibu wa sheria na tumekuta *NGOs* nydingi ambazo zimekuwa zinakiuka masharti haya na baadhi tumeshazifuta na nydingine zimepewa maonyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tumewekeza nguvu kubwa sana kuhakikisha kwamba sasa tunazisimamia vizuri hizi *NGOs* ili ziweze kutimiza majukumu yake. Hatuna shida na *NGO's*; ni wadau wakubwa sana wa Serikali na sisi kama Serikali tuna-*appreciate* sana kazi kubwa na nzuri ambayo wanaendelea kuifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine la mwisho ambalo nilitaka nigusie ilikuwa ni suala la wazee. Sisi kama Serikali kupitia Sera ya Afya ya mwaka 2007 tunatambua umuhimu wa wazee na katika sera yetu imesema kwamba wazee watapewa matibabu bure. Mheshimiwa Waziri amekuwa kinara katika hili kuhakikisha kwamba tunatenga madirisha ya wazee na wazee wetu wanapata vitambulisho vya kuweza kuwatambua na kuweza kupata matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakiri kwamba tumekuwa na changamoto kidogo katika utekelezaji wa hili, lakini na sisi tutaongeza juhudzi zaidi kuhakikisha kwamba tunasimamia kwa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuja hoja ambayo ilikuwa *raised* hapa kuhusiana na Sheria ya Wazee. Tuna Sera ya Wazee ya mwaka 2003, sasa hivi tunaifanyia mapitio na baada ya hapo tutaitleta kwa ajili ya kuleta hiyo rasimu ya sheria ili iendane na mazingira ya sasa ya hali ya wazee tuliokuwa nao hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, mimi nikushukuru sana na niwashukuru watoa hoja wote kwa michango mizuri ambayo wameweza kuitoa katika bajeti yetu. Sisi tunaamini kwamba michango hii itatusaidia sana kuboresha utendaji wetu wa kazi. Nawashukuru sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, mtoha hoja.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama hapa, nianze kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia hoja yangu ya kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2018/2019. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo na Huduma ya Jamii, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba ambaye amewasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu utekekelezaji wa kazi za Wizara kwa mwaka 2017/2018 pamoja na bajeti ambayo tunaipendekeza Bunge lako Tukufu kuipitisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawashukuru Kamati kwa kututia moyo, kwa kupongeza Wizara yangu na kwa niaba ya wafanyakazi wote wa sekta ya afya katika ngazi zote nchini Tanzania na maendeo ya jamii kwa niaba yao napenda kupokea pongezi hizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa majibu ya hoja mbalimbali ambazo zimewasilishwa na Waheshimiwa Wabunge niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi; na kwa sababu kanuni zinanibana kuwataja niseme tu kwamba hoja yangu imechangiwa na Wabunge 117, kati ya hao Wabunge 73 wamechangia kwa kuzungumza na Wabunge 44 wamechangia kwa maandishi. Aidha, Waheshimiwa Wabunge nane wamechangia kuhusu sekta ya afya wakati wa mjadala wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa ufanuzi, niseme kwamba tumepokea maoni, ushauri na mapendekeo ya Kamati na Waheshimiwa Wabunge kuhusu kuboresha huduma za afya. Vilevile tumepokea pongezi zenu na mimi ninasema pongezi hizo zirudi kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli ambaye kwa dhamira yake ya dhati ameamua kuwekeza kwenye afya ya Watanzania; na hii ni kutokana na kuamini kwamba hatuwezi kujenga Tanzania ya viwanda bila kuwa na Watanzania wenye afya bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli ambaye ametoa kipaumbele katika sekta ya afya. Kabla hajaingia madarakani tunaona kwamba bajeti ya sekta ya afya imeongezeka. Wakati hajaingia madarakani ilikuwa shilingi trillioni 1.8, mwaka wa kwanza wa Mheshimiwa Magufuli imepanda mpaka shilingi trillioni 1.9 na mwaka wa pili wa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli bajeti ya Sekta ya Afya imepanda mpaka shilingi trillioni 2.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kwamba Wizara ya Fedha wanaendelea kufanya tathmini na uchambuzi wa bajeti ya mwaka 2018/2019. Sina shaka hata kidogo kwamba sekta ya afya itaendelea kuwa kipaumbele kati ya vipaumbele vitatu vya Serikali ya Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu changamoto za sekta ya afya katika nchi yetu ni nydingi, hasa katika mazingira ambayo tuna idadi kubwa ya wanawake ambaao wanazaa watoto wengi. Kiwango cha uzazi ni asilimia 5.1. Vilevile tuna mzigo wa magonjwa, zamani tulikuwa na magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama kipindupindu, *TB*, *HIV* lakini sasa hivi tunabeba mzigo wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza ikiwemo kisukari, magonjwa ya moyo na saratani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na changamoto hizi, sekta ya afya katika kipindi cha miaka miwili na nusu ya Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli imepata mafanikio makubwa sana. Tumeona leo katika historia ya nchi yetu Tanzania tumeanza kupandikiza figo katika Hospitali yetu ya Muhimbili na hospitali yetu ya Benjamin Mkapa. Lakini tumeona watoto wanaozaliwa na matatizo ya kusikia wakiweza kupandikiziwa vifaa vya kuongeza usikivu katika Hospitali yetu ya Muhimbili wakati zamani miaka miwili na nusu iliyopita huduma hizi zilikuwa hazipatikani katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kaka yangu James Mbatia aliongelea kuhusu *Medical Tourism in Tanzania*. Nataka kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge ndani ya Magufuli *Medical Tourism* Tanzania itawezekana na itawezekana kwa kipindi kifupi tu. Tunamaliza kufunga mitambo ya *LINAC* katika Hospitali yetu ya *Ocean Road* ambayo ni mionzi ya kisasa kwa ajili ya tiba ya saratani. Tunakaribia kununua kifaa cha *Pet Scan*, hakipo Kenya, hakipo Uganda, hakipo Zambia, hakipo Malawi. Kwa hiyo, watu wa kutoka nchi za Afrika watakuja Tanzania kwa sababu ya uwekezaji mkubwa ambaao anaufanya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ya Mheshimiwa Rais ni mengi, lakini nimalize tu kwa kusema tumeona uwekezaji mkubwa katika afya ya mtoto, asilimia 97 ya watoto wote Tanzania wanapata chanjo, na sisi tumejidhatiti tutamfikia

kila mtoto popote alipo ili kuhakikisha anapata chanjo ili kuweza kumkinga na magonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa nijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge na nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ufanuzi ambaao ameutoea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na hoja kubwa za Kamati. Kamati imezungumzia kuhusu makubaliano ya Abuja ambayo yalifanyika mwa 2001 ambapo nchi za Afrika zilikubaliana kutenga asilimia 15 ya bajeti zao za nchi katika ajili ya kutatua changamoto za sekta ya afya. Suala la *Abuja Declaration* ni dhamira si kwamba ni kitu kina-*bind*, kinabana nchi wanachama, ni dhamira ya nchi za Afrika kuwekeza kwenye sekta ya afya. Hata hivyo kama nilivyosema tumeona uwekezaji ambaao Serikali ya Awamu ya Tano imekuwa ukifanya katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, tumefanya utafiti, ni nchi moja tu ya Afrika ambayo bajeti yake ni asilimia 15 ya bajeti ya nchi. Kwa sababu kama nilivyosema changamoto za nchi za Afrika ni nyingi, kuna masuala ya maji, barabara, kilimo, na maji. Kwa hiyo muhimu kile kidogo ambacho tunakipata muhimu kwetu sisi sekta ya afya ni kuhakikisha kwamba kinatumika kikamilifu bila kupotea katika mambo ambayo hayana tija kwa Watanzania hasa Watanzania wanyonge. Kwa hiyo, nashukuru maoni ya Kamati kwamba haijafika lakini ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba tunafikia asilimia 15 ya bajeti nzima ya Serikali katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeongea suala la kwamba bajeti ya Wizaya ya Afya kwa mwaka 2018/2019 imepungua ukilinganisha na ya mwaka 2018/2019.

Waheshimiwa Wabunge, mwaka jana wakati nawasilisha bajeti hapa mlini-*challengekwamba* Mheshimiwa Waziri bajeti yako kwa kiasi fulani inategemea wafadhli wa nje, je, wafadhili wa nje wakijitoa mtatatua vipi changamoto za sekta ya afya?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kilichotokea bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka huu kwa fedha za ndani imeongezeka kutoka billioni 628 mwaka jana hadi billioni 681. Punguzo tunaloliona ni fedha za nje na hii ni kuonesha dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli ya kutaka kupunguza utegemezi kwa wadau wa maendeleo katika kutatua changamoto za watanzania ambao wao ndio wamempa ridhaa ya kumchagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ukiangalia *domestic allocation* zimepanda, lakini kwenye *forex* zimeshuka, na ni kwa sababu tunataka kuanza kujipima wenyewe leo *donor* akijitoa tutaweza kutatua changamoto zetu kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo limeongeleta na Kamati ni suala la kwamba inashauri Serikali kutoa fedha zote zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kama ambavyo Bunge lako tukufu liliidhinisha. Serikali hii ni sikivu na kwa sababu bado hatujamaliza mwaka wa fedha wa 2017/2018 tunaamini kwamba tutaweza kupata fedha kutoka Wizara ya fedha na mipango kwa ajili ya kutekeleza miradi ambayo tumejiwekeea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ambalo Kamati ya Bunge imelizungumzia, suala la lishe, kwamba lishe sio suala la wizara ya afya pekee bali ni suala mtambuka na Serikali ichukue hatua za makusudi za kupunguza janga la lishe. Tunapokea ushauri na maoni ya Kamati kuhusu suala hili, na mimi nikiwa Waziri mwenye dhamana nimefarijika sana kuona Kamati ya Bunge na Wabunge wote wanatoa kipaumbele katika suala la lishe. Kwa kweli suala la lishe na mimi nakubaliana nanyi si suala la mchezo kwa sababu kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2015/2016 kiwango cha udumavu kwa watoto wetu ni asilimia 34. Of course tumepeiga hatua ukiangalia kutoka mwaka 2010 ilikuwa ni asilimia 42.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini maana ya watoto kuwa na udumavu ni nini, tunawekeza katika ujenzi wa Tanzania ya viwanda, tunakosa watoto ambao wanawenza

wakawa na ubunifu, udadisi lakini ambao wanaweza wakawa na afya bora kwa ajili ya kutatua changamoto za kujenga Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama Serikali tumechukua mikakati na hatua mbalimbali chini ya uratibu wa Mheshimiwa Waziri Mkuu na yeye mwenyewe alisimamia kikao cha kwanza cha wadau wa masuala ya lishe kutoka wizara zote ambapo sasa tunatekeleza mpango jumuishi wa kitaifa wa utekelezaji wa masuala ya lishe kwa kipindi cha 2016/2017 mpaka 2020/2021. Mpango huu umeweka vipaumbele mbalimbali ambavyo Mikoa pamoja na Halmashauri zitatekeleza katika kuinua hali ya kiwango cha lishe nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimshukuru sana Waziri wa Fedha Dkt. Mpango, hayupo hapa, lakini baada ya kuona tatizo la lishe aliahidi na ameyatekeleza. Katika Wizara ya Fedha sasa hivi kuna Afisa mahususi ambaye anahusika na masuala ya lishe, yeye kazi yake ni kuangalia bajeti zote hizi ni kiasi gani masuala ya lishe yamepewa kipaumbele. Pia tumepeleka maafisa lishe sasa hivi wako katika mikoa, wako katika halamashauri pia wako katika ngazi mbalimbali za wizara mtambuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumezindua pia mpango wa kuhamasisha mabadilko ya tabia mlongoni mwa jamii ijlikanayo kama Mkoba wa siku 1000 za mwanzo, kwa sababu kwa mujibu wa wataalam wa afya siku 1000 za mwanzo za mtoto ndizo siku muhimu katika maisha yake. Pia tumeongeza idadi ya viwanda vinavyoongeza virutubishi, tunasema *food fortification* kutoka viwanda 13 hadi viwanda 21. Sasa hivi viwanda ambavyo vinazalisha ngano, mafuta ya kula, unga wa mahindi na chumvi lazima viwe na virutubisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ambayo tunaipata na mimi nikiri, kwa sababu wanakobia unga katika *lower level* kwenye vijiji na mitaa, kwa hiyo, kidogo kuwabana kwamba ule unga ambao wanazalisha uwe na

virutubisho inakuwa ngumu. Lakini kubwa ambalo tumeliona ni kutoa elimu ya lishe katika jamii kwa sababu hata ukiangalia mikoa ambayo ina viwango vikubwa vy a udumavu unakuta ni mikoa ambayo ina uzalishaji mkubwa wa chakula. Kwa mfano, tukiangalia Rukwa wana udumavu asilimia 56 wakati ndio wazalishaji wakubwa wa chakula. Tukiangalia Njombe, Ruvuma, Iringa, Katavi na Mbeya. Kwa hiyo, sisi tumeona ni suala la elimu kwa jamii hasa kwa siku zile ambazo mama anajiandaa kubeba ujauzito.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa ambalo tutaendelea nalo pia ni kuhimiza uzalishaji na matumizi ya mazao lishe katika mahindi, viazi vitamu, maharage na mihogo; lakini ambalo sasa nataka kulifanya baada ya kuwasikiliza Waheshimiwa Wabunge ni kufanya tafiti ya kitaalam ili kubaini sababu au chanzo cha hali ya lishe nchini. Kwa sababu nimesema Rukwa, Katavi, Iringa, Njombe wanazalisha chakula kwa nini tuna udumavu. Kwa hiyo nataka kupata majibu ya kisayansi kuhusu hali ya viwango vy a utapiamlo katika baadhi ya mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala kubwa ambalo limeongelewa na Wabunge wote, Wabunge wanawake na wanaume ni suala la huduma za mama na mtoto. Tunawashukuru sana Kamati kwa kupongeza jitihada ambazo Serikali inafanya katika kuhakikisha kwamba tunaboresha huduma za afya ya mama na mtoto ikiwemo huduma za upasuaji wa dharura.

Waheshimiwa Wabunge wameniuliza Mheshimiwa Waziri kwamba vifo vitokanavyo na uzazi vinaongezeka tumetoka kwenye 432 mwaka 2015/2016 vimefika mpaka vifo 556.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunatoa majibu haya Disemba, 2016 tulitaka kubishana, tulibishana kidogo tukasema tumekoneksi wapi, pamoja na jitihada zote ambazo Serikali imefanya kwa nini vifo vy a akina mama wajawazito vimeongezeka? Baada ya kutafakari tukaamua hakuna maana ya kubishana, awe amekufa mwanamke mmoja

bado kwetu sisi ana umuhimu mkubwa sana. Kwa hiyo, tukajikita katika kuchukua hatua za kuboresha huduma ya mama na mtoto na ndiyo maana sasa hivi tukaandika andiko na tukapata fedha kwa ajili ya kuboresha vituo vya afya ili viweze kutoa huduma za uzazi za dharura ikiwemo upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Watanzania wanataka kumuhukumu Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli mumuhukumu kwa jitihada ambazo amezifanya katika kuboresha huduma za upasuaji za dharura. Mwaka jana ni asilimia 21 tu ya vituo vya afya vya Serikali vinavyoweza kufanya upasuaji, lakini tutakapofika Disemba tutakuwa na asilimia 53 ya vituo vya afya vya Serikali vitakavyoweza kufanya upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ambayo iko mbele yangu sasa kama sekta ni kuhakikisha tunakuwa na wataalam, watumishi wenye ujuzi ambao wataweza kuwahudumia akina mama wajawazito ambao watapata matatizo ya uzazi wa dharura. Tumeshaanza kuwafundisha wauguzi katika masuala ya utaalamu wa usingizi ambao tutawasambaza katika vituo hivi ambavyo vinajengwa *theatre*. Tumesambaza *ambulance* 50 katika mikoa mbalimbali pamoja na kuimarisha huduma za damu salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hatua inayokuja sasa hivi kama nilivosema ni kuimarisha huduma za uzazi wa mpango. Kwa sababu wataalam wamenifundisha Wizara ya Afya kwamba endapo tutakuwa na idadi kubwa ya wanawake wanaotumia uzazi wa mpango tutaweza kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kwa asilimia 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge tuhimize matumizi ya uzazi wa mpango kwa wanawake kwa sababu sasa hivi ni asilimia 32 tu ya wanawake nchini Tanzania ambao wanatumia huduma za kisasa za uzazi wa mpango. Pia tutaendelea na jitihada za kuimarisha huduma wakati wa ujauzito na hapa tunahitaji lengo letu wanawake wajawazito angalau

wahudhurie kliniki mara nne kama wataalam wanavyoshauri. Sasa hivi wanawake wanahudhuria kliniki mara nne ni asilimia 51.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo eneo ambalo tutaliboresha pia pale ambapo mama mjamzito anaenda kliniki tunataka apate huduma bora badala tu ya kupoteza muda wake. Tunawaambia wenzetu mama mjamzito anatoka kilometra 20, 30 hata 40 anafika kwenye kituo hapimwi wingi wa damu, hapimwi maambukizi aliyokuwa nayo, hapewi huduma mtoto amekaa vizuri, kwa hiyo, tunatoka kwenye miundombinu tunaenda kwenye ubora wa huduma. Tunataka kuona huduma bora kwa akina mama wajawazito. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa mama na mimi nimeingia *labour* mara mbili, nataka kuwaahidi Waheshimiwa Wabunge na Watanzania tutahakikisha huduma kwa mama mjamzito zinaendelea kuboreka.

Mheshimiwa Naibu Spika, limejitokeza suala la *delivery pack* kwamba zinauzwa, na pia tutoe ufanuzi kwamba matibabu kwa wajawazito je, ni bure au si bure?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Afya na mimi nimeuwa nikilisisitiza hivi si hili kwamba matibabu kwa wajawazito, huduma kwa wajawazito ni bure kuanzia wakati anapohudhuria kliniki mara tu baada ya kujigundua ni mjamzito, lakini pia wakati wa uzazi na wiki sita baada ya kujifungua. Kwa hiyo suala la kwamba akina mama wajawazito wanatozwa fedha za kumwona daktari nalikemea mara moja, na niwatake watoa huduma za afya zote Waganga Wakuu wa Mikoa kusimamia agizo hili, kusimamia sera hii. Ni marufuku kum-charge mama mjamzito fedha pale ambapo amekwenda katika kituo cha kutoa huduma za afya kwa ajili ya kupata fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *delivery pack*, Waheshimiwa Wabunge mama mjamzito hatoi fedha ya kumwona daktari, hatoi fedha ya dawa, hatoi fedha

anapo jifungua wala hatoi fedha ya kufanyiwa upasuaji. Kwa hiyo *delivery packs* zitaendelea kuwepo kaatika vituo vya kutoa huduma za afya kwa kuzingati rasilimali fedha ambayo Serikali au kituo kinacho. Nimeongea hapa, kwa mwaka tunakuwa na wajawazito milioni mbili *delivery pack* 21,000. Waheshimiwa Wabunge, naomba mnisaidie shilingi bilioni 40 ambazo kila mwaka tutazitenga kwa ajili ya kutoa *delivery pack*. Sisi tulichokifanya pale ambapo kuna fedha za Serikali na mama mjamzito ataenda atakuta vifaa hivi atapewa bure. Sasa suala la *delivery pack* ni suala la mama mjamzito kuijandaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzazi si dharura ni miezi tisa, uzazi ni miezi tisa, kwa hiyo, ni sawa sawa na mama anavyojiandaa kununua nguo ya mtoto, kununua kanga, akiikuta *delivery park* kwenye kituo atasema *Alhamdulillah*, asipoikuta inakuwa ni sehemu ya maandalizi. Hata hivyo nataka kuendelea kuwaahidi, tunaelekea kwenye Bima ya Afya kwa kila mtu (*Universal Health Coverage*). Kundi ambalo tutaanza nalo pale ambalo tutatoa Bima ya Afya, kwa sababu tume sema akina mama wajawazito huduma ni bure tutawapatia huko mbeleni, kwa hiyo, ndio kundi ambalo tutalipa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ina maana tunaweza tukaangalia utaratibu wa kupata kadi za bima ya afya ili waweze kupata huduma bila vikwazo vya fedha. Tumeanza kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani, huduma hii tunaiita Tumaini la Mama, inafanyika katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Tanga na Mbeya. Msije mkasema Tanga nimeikuta hata kabla sijawa Waziri, kwa hiyo, ni eneo ambalo tumeanza nalo, lakini tunaamini kwamba tutaweza kuboresha huduma hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lili lohusu masuala ya afya ya mama na mtoto ni suala la chanjo ya kuwakinga wasichana na saratani ya mlango wa kizazi. Nafurahi kuona kwamba Waheshimiwa Wabunge mmelipokea vizuri na wengi mmetusisitiza kwamba tukatoe elimu kwa jamii na sisi tutaenda kutoa elimu kwa jamii.

Tunaomba Wabunge, hasa Wabunge wenzangu wanawake, kumuuguza mgonjwa mmoja wa saratani ya mlango wa kizazi tunatumia shilingi milioni tano, hatujahesabu gharama familia ambayo inaingia katika kumuuguza mgonjwa yule. Nadhani tutakuja kufanya semina muone, endapo tutawachanja wasichana na chanjo hii ya saratani ya mlango wa kizazi ndani ya miaka 10 saratani ya mlango wa kizazi itakuwa historia katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe rai tena kwa wazazi na walezi wenzangu, tuwapeleke binti zetu kupata chanjo hii. Mimi mwenyewe binti yangu ana miaka 13. Tumeanza na miaka 14 kwa sababu chanjo hizi mahitaji ni makubwa sana. Waziri wa Afya wa Nigeria kwa mwaka anahitaji dozi milioni 20, mimi nikiwachanja mabinti wote wa miaka tisa mpaka 14 nahitaji dozi kama milioni 3.9. Kwa hiyo, mzalishaji amesema nitaweza kuwapa dozi za wasichana 600,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tumeona badala ya kusubiri mpaka mwakani na Mheshimiwa Kiteto Koshuma umeongea vizuri, watoto wetu wanaanza utundu mapema. Tunaweza tukasema tusubiri mwakani tuwachanje wote miaka tisa mpaka 14 hawa 14 kuna asilimia fulani tutawapoteza. Kwa hiyo, timesema tuanze na miaka hii 14 halafu sasa mwakani tutawatoa wasichana wote na Mheshimiwa Angella Kairuki ameniahidi na yeye watoto wake amewachanja tena amewachanja dozi tatu.

Kwa hiyo, akina mama Wabunge nitaomba tutoke mbele, tuwashawishi wanawake wenzetu kwamba chanjo hii ni salama. Chanjo hii itapigwa dozi mara moja kwenye sindano halafu baada ya miezi sita itarudia. Sambamba na hayo tutaongeza jitihada pia za kuwapima na kutoa huduma za matibabu ya awali kwa wanawake wajawazito.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia iliongelea suala la Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na ambao wameshauri kwamba tuufanyie marekebisho pamoja na kuja na vifurushi vyta bima. Ushauri huu tunaupokea na mimi mwenyewe nimekuwa nikwa-*challenge* Bima ya Afya, kwamba kwa nini

msifanye kama kampuni za simu, jipimie, unajipimia. kwamba unataka huduma za afya mpaka Muhimbili, unataka huduma za afya mpaka Hospitali ya Bombo Tanga au unataka huduma za afya mpaka ufile KCMC.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimefurahi kwamba ndani ya siku chache tutazindua vifurushi mbalimbali ili wananchi wajipimie katika kupata huduma za matibabu. Pia tumeona kuna bima ya afya, total afya kadi 50,400 kwa mtoto matibabu mwaka mzima mpaka Muhimbili, mpaka *MO*/mpaka *JKC*. Kwa hiyo, tumekubaliana badala ya kusubiri mzazi aliye shilingi 50,400 kwa mara moja nimewaelekeza *NHIF*waweke utaratibu, mzazi leo ana shilingi 5000 anachangia, ana shilingi 10,000 anachangia, baada ya miezi fulani tumeweke utaratibu wa miezi mitatu kadi itakuwa imekamilika mnampa bima ya afya mtoto anakuwa na uhakika wa matibabu kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilikuwa Nzega kwa Mheshimiwa Bashe, tukawaauliza boda boda kuna bima ya afya ya kikundi tunaita kikoa, kwa nini hamkati? Wakaniambia Waziri shilingi 78,600 hatuwezi, lakini ukiniambia nitoe shilingi 2,000 kila siku nitaweza kuchangia shilingi 2,000. Kwa hiyo tumeona kwamba inawezekana kuongeza idadi ya Watanzania watakaokuwa na bima ya afya lakini lazima pia na sisi tuwe wabunifu. Kwa hiyo, tunaupokea ushauri wako Mheshimiwa Peter Serukamba pamoja na Wabunge wote ambao mmeutoa katika kuongeza idadi ya Watanzania ambao wana Bima ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumejiongeza, tunafanya mazungumzo na vyama vyaya ushirika, Wabunge wa Mikoa ya Kusini mmezungumzia suala la korosho. Kwa hiyo, tayari tunasema wakati mkulima anauza korosho basi pale pale aweze pia kukatwa na Bima ya Afya.

Kwa hiyo tumechukua hili zao la korosho, pamba pamoja na kahawa, na vyama vyaya ushirika vimeshakubali, kwamba pale ambapo wananchi wanapewa fedha zao watakatwa pia ili kupata Bima ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge matibabu ni gharama na matibabu ni gharama narudia tena tukisema kila mzigo ubebe Serikali hatuwezi kufika, tutakuwa tunajidanganya. Kama wapiga kura wetu wanaweza kununua vocha ya simu shilingi 500 kila siku siamini kwamba wanashindwa kuchangia shilingi 500 hiyo hiyo ili waweze kupata Bima ya Afya.

Kwa hiyo, tutaendelea pia kuhamasisha ili wananchi waone kwamba kuwa na Bima ya Afya unakuwa na ukahika wa kupata matibabu kabla ya kuugua. Mtu maskini akiumwa leo atauza baskeli yake, atauza shamba, atauza vitu alivyokuwa navyo, lakini mwenye Bima ya Afya atawenza kupata huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Kamati pia ilikuwa ni mapambano dhidi ya UKIMWI, kwamba upatikanaji wa fedha za Serikali kwa ajili ya ununuzi wa dawa za kufubaza UKIMWI tunategemea wenzetu kutoka nje. Tumepokea changamoto hii na nitumie fursa hii kuwatoa hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista tumeanzisha *extra fund* ambayo itawenza sasa kugharamia huduma mbalimbali zinazolenga UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Jenista nakushukuru sana uliweza kunipa *cheque* ya milioni 260 ili tuweze kununua dawa kwa ajili ya magonjwa nyemelezi kwa wenye matatizo ya UKIMWI. Kwa hiyo, suala hili ninamini kabisa kwamba ndani ya muda mchache; na sasa hivi pia, kama nilivyosema tunakamilisha mkakati wa kugharamia huduma za afya (*financing for health sector*). Kwa hiyo katika mkakati huu pia tumebainisha maeneo ambayo tunaweza tukapata vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kugharamia huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilikuwa naongea na Waziri mwenzangu wa *South Africa*, wao katika kila asilimia fulani ya fedha ambayo ni kwa ajili ya sukari inaenda kwa ajili ya kugharamia pia changamoto za sekta ya afya. Juzi

tulikuwa pia na watu wa Ghana na wenyewe wametupa nao uzoefu wao kwamba asilimia mbili ya VAT pia inaenda kugharamia huduma za afya. Kwa hiyo, tutaendelea kufanya mashauriano na wenzetu Hazina ili kuona ni kiasi gani basi; Mheshimiwa Bashe amezungumza wale watu maskini ambao kwa mujibu wa takwimu za *World Bank* ni asilimia kama 28 ya Watanzania ndio maskini sana. Kwa hiyo, tutaangalia ni kiasi gani sasa tutaweza kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia changamoto za afya ikiwemo masuala ya UKIMWI na *HIV*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ambalo pia limeongeleta na Waheshimiwa Wabunge hasa Mheshimiwa Lubeleje ni suala la afya ya mazingira. Nimpongeze sana Mheshimiwa Lubeleje kwamba hawa Mabwana Afya wamewekwa katika maeneo ambayo si sahihi. Mheshimiwa Lubeleje nimepokea hoja yako na ndiyo maana ukialangalia hotuba yangu ya bajeti ya mwaka jana na mwaka huu. Mwaka huu baada ya chanjo eneo la pili ambalo nimeliweka ni suala la afya na usafi wa mazingira. Kwa sababu tunapoteza fedha nydingi sana katika kutibu magonjwa ya kuhara kipindupindu na minyoo na magonjwa mengine ilhali tungeweza kuyaepuka pale ambapo Watanzania watazingatia kanuni za usafi wa mazingira pamoja na usafi wa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni kweli kaka yangu Shangazi tutaendelea pia na kampeni yetu ya usichukulie poa nyumba ni choo na lengo la kampeni hii ni kutaka kubadilisha mtazamo na mwamko wa Watanzania kuhusu usafi wa mazingira ikiwemo vyoo bora. Watanzania wana nyumba nzuri, utamwona ana *tv screen* inchi sijui hamsini na ngapi, nenda kaangalie choo chake, nenda kaangalie vyoo katika *stand* zetu, nenda kaangalie vyoo katika vituo vyetu vya kutoa huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwangu mimi baada ya suala la chanjo kwa watoto suala la afya na usafi wa mazingira ndicho kipaumbele cha pili. Kwa hiyo, natuma salamu kwa Mabwana Afya wote katika Halmashauri na

mikoa, haitakuwa *business as usual* maana Mabwana Afya wetu muda mwingi wanapoteza kwenda kukagua *butcheries* na mahoteli kwa sababu wanapata fedha. Kwa hiyo tumeambizana tutakaa chini na tutatoa miongozo, tunataka waende kwenye kaya na kuhamasisha masuala ya afya na usafi wa mazingira badala ya kujikita kwenda kukagua *butcheries* na hoteli kwa sababu pia kuna kasilimia fulani wanaweza kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Lubeleje pia tumeangalia suala la kada ile ya kama ulivyosema *environment health officers* na *assistant*, kwa hiyo tutalijadili Wizarani, na tumeamua kwamba baada ya kulijadili tutakuja na mapendekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ambalo pia linahusu kuhusu afya ya mazingira na hilli nimpongeze sana mdogo wangu Mheshimiwa Maria Kangoye amezungumzia suala la hedhi salama. Tunakubaliana, ndiyo kipaumbele pia kama kweli tunataka kuimarisha usafi na afya ya mazingira. Kwa hiyo, suala hili la hedhi salama hasa kwa wasichana na wanawake wa vijijini tunalipa kipaumbele. Sisi kubwa ambalo tutalifanya ni kuongea na wenzetu wa Wizara ya Fedha kama ulivyosema kuweza kuwaomba tutoe kodi katika taulo za wanawake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini hili litawezekana, kwa sababu tusidanganyane tutatoa taulo za kike kwa sasa hivi kwa watoto wangapi, kila mwaka tunaongeza Watanzania wapya milioni mbili, na ninyi mnafahamu asilimia 51 ya wananchi ni wanawake. Kwa hiyo hili suala tunalichukua, lakini tutaendelea kuimarisha tu mazingira kwenye shule zetu pamoja na vituo vyta kutoa huduma za afya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, limeongelewa pia suala la ongezeko la magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambalo Waheshimiwa wameongea, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete pia dada yangu Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa. Pamoja na utoaji elimu ya afya kwa jamii pamoja na kupima

magonjwa tutaendelea, na ndio maana tunaimarisha pia kitengo chetu cha elimu ya afya kwa umma. Mheshimiwa Rita Kabati alizungumzia mpango wa kutoa chanjo ya *HPV* kwa watoto wa kiume pia kwa watoto ambao wana umri zaidi ya miaka 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeipokea hoja hii, lakini kwetu sisi tumeangalia kundi au rika ambalo ndilo liko kwenye hatari. Kwa hiyo, nchi zenye uwezo zinatoa chanjo hii kwa wavulana, zinatoa chanjo hii kwa wasichana wa zaidi ya miaka 15, sisi tunajikuna pale ambapo tunaweza. Kwa hiyo, tumeona tuenze na umri huu wa miaka tisa hadi miaka 18.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maendeleo ya jamii, kuna hoja imetolewa kuhusu mimba za utotoni ikiwemo mikakati gania ambayo tunafanya, tunaendelea kutoa elimu kwa wasichana, wazazi na walezi kutoa elimu ya *sexual and reproductive health education* (elimu ya uzazi na afya ya uzazi kwa wasichana) na nimeongea na Mheshimiwa Profesa Ndalichako tunaangalia pia, *curriculum* (mitaala yetu) ili sasa katika shule zetu tuwe na walimu, lakini pia tuwe na somo ambalo hawatafanya mitihani, lakini watoto watajua A, B, C, *my right my protection*, angalao wajue *my body my protection*. Kwa hiyo, ni eneo ambalo tunaona linaweza kutusaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Mwenyekiti Najma, amezungumza kuwahasi watu ambao wanabaka na kulawiti watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimelitafakari suala hili, nikaangalia Sheria ya Makosa ya Kujamiihana ambayo imeingizwa katika Sheria ya Kanuni za Adhabu, tumeweka adhabu kali miaka 30, kuanzia miaka 30 mpaka kifungo cha maisha kwa mtu ambaye atakutwa amebaka. Mimi naona adhabu hii ni kali kwa kiasi fulani. Kwa hiyo, sisi tujikite katika kuelimisha jamii ikiwemo wasichana na wazazi kutimiza wajibu wao kwa malezi, lakini na watoto wa kike pia kujitambua na kujilinda na kuwajengea uwezo watoto kutoa taarifa pale ambapo wanafanyiwa vietndo vyta ukatili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dalaly Kafumu amezungumzia masuala ya vituo vya afya na Wabunge wengi, kwamba, kuboresha vituo vya afya. Mheshimiwa Naibu Waziri amelijibu suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, ujenzi wa miundombinu ya afya, zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya upo chini ya Serikali za Mitaa, TAMISEMI. Sisi kazi yetu ni kusimamia sera kuhakikisha kwamba kuna miundombinu ya kutoa huduma za afya. Hata hivyo pale ambapo tunaona kuna changamoto. Kama nilivyosema tumekuja na hoja ya uzazi salama, kwa hiyo, sisi tukaamua tutafute fedha za kuboresha vituo vya afya, ili viweze kutoa huduma za uzazi za dharura. Kwa hiyo, ni eneo ambalo..., kwa mfano, tunataka kuja na mpango wa kuboresha huduma ili tuweze kuwahudumia wagonjwa wa kifua kikuu, wagonjwa wa UKIMWI, lakini pia na ugonjwa wa malaria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mama Mheshimiwa Riziki Lulida sijakusahau, balozi wa malaria katika Bunge hili. Malaria ni changamoto na ninafurahi kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge tarehe 25 Aprili tunaenda Kasulu na moja ya shughuli ambayo tutaifanya ni kuzindua hali ya malaria nchini Tanzania. Habari njema ni kwamba kiwango cha malaria kimepungua na tutatoa takwimu. Tutaendelea pia kujikita katika afua za kuzuwa badala ya kusubiri kutibу. Ni kweli tunatumia fedha nyigi sana kwa ajili ya kuwatibu watu malaria wakati tungeweza kutumia viuadudu vile ambavyo vinazalishwa Kibaha kwa ajili ya kuuwa mazalia ya mbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge kwa hiyo nimemua katika fedha za dawa ambazo tunazipeleka kwenye Halmashauri tutakata baadhi ya fedha kwa ajili ya kununua viuadudu vya kuuwa mazalia ya mbu. Kwa sababu badala ya kusubiri wanunue wenyewe hawanunui, kwa hiyo, tutawakata kwenye fedha za dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kuhusu mapambano ya *VVUna* UKIMWI, Mheshimiwa Mama Salma

Kikwete kwamba suala la dawa za kufubaza *VVU* hazipatikani kwa wakati, Mheshimiwa Mama Salma tutafuatilia, lakini kati ya eneo ambalo kwa kweil tuna uhakika wa kupata dawa ni suala pia la dawa za *ARV* na tunawashukuru sana wadau wetu ambao wanatupa fedha katika kutoa *ARV* ambao ni *Global Fund* pamoja na *PEFA* wa Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala pia la ongezeko la UKIMWI Dodoma, Mheshimiwa Fatma Toufiq. Ni kweli, hata mimi Tanga maambukizi kwa mujibu wa takwimu za *THIMS* yameongezeka kutoka *2.4 percent* mpaka asilimia tano. Kwa hiyo pia tutafanya tathmini kwenye hii mikoa ikiwemo Tanga na Dodoma, ni kwa nini maambukizi ya *VVU* na UKIMWI yameongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kupigiliwa kengele, lakini kwa kweli, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa maoni na ushauri, na tutajibu hoja zenu kwa maandishi. Kipekee nirudie tena kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Faustine Ndugulile, kwa sababu wote mnafahamu hata kabla hajawa Naibu Waziri alikuwa ni mmoja wa washauri wangu katika kutatua sekta ya afya. Kwa hiyo, ninamshukuru sana kwa ushirikiano mzuri ambao ananipatia, vile vile nawashukuru sana wataalam wote, madaktari, wauguzi wote wanaotoa huduma katika vituo vyenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuwa mkali sana ninapoona hatutoi *consideration*, tunafanya vitendo vya kuwaumiza watoa huduma za afya. Sisemi kwamba, wote ni wazuri, wapo wabaya, lakini ni wachache...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, wale wazuri lazima tuwape heshima yao, lazima tuwathamini. Kwa mfano wauguzi, kazi ya wauguzi wanne inafanywa na muuguzi mmoja na yeye ni binadamu anachoka. Kwa hiyo,

nitaomba sana viongozi wenzangu wa Serikali tuwaheshimu na kuwathamini madaktari na wauguzi kwa sababu wanatoa huduma za afya na wanatibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Rais, Katibu Mkuu Mpoki na Mama Sihaba Nkinga na Mganga Mkuu wa Serikali na wote Profesa Janabi anatuletea heshima kubwa sana katika nchi yetu na Mwenyezi Mungu ninaamini *Medical Tourism* itaanza Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Tutaendelea na utaratibu wetu, Katibu!

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

**Fungu 52 – Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia,
Wazee na Watoto – Afya**

Kif. 6001 – *Amana Regional Referral Hospital – Dsm.....Sh. 811,216,919/=*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ninayo orodha hapa.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kif. 6002 – *Bombo Reg. Ref. Hosp.–Tanga....Sh. 659,882,729/=*
Kif. 6003 – *Dodoma Reg. Ref. Hosp.....Sh. 798,869,206/=*
Kif. 6004 – *Geita Reg. Ref. Hosp.Sh. 539,774,150/=*

Kif. 6005 – *Iringa Reg. Ref. Hosp.*Sh. 478,128,301/=
Kif. 6006 – *Kagera Reg. Ref. Hosp.*.....Sh. 706,184,277/=
Kif. 6007 – *Katavi Reg. Ref. Hosp*Sh. 451,610,032/=
Kif. 6008 – *Ligula Reg. Ref. Hosp.-Mtwara.... Sh. 463,980,739/=*

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kif. 6009 – *Manyara Reg. Ref. Hosp.*.....Sh. 501,482,176/=

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Mimi langu ni dogo tu Mheshimiwa Waziri; kwanza nikushukuru kwa fedha ambazo umetupa katika kumalizia Hospitali yetu ya Mkoa wa Manyara, zimetusaidia sana na ujenzi unaendelea.

Sasa wagonjwa wanavyofika katika hiyo hospitali wamekuwa wakipata shida vile ambavyo hawako kwenye *groups* katika bima ya afya, na umetoka kulizungumzia na *concern* yao kubwa ni kwamba, kwa nini mimi peke yangu nisilipe ile bima ya shilingi 76,000 nifikatibwa, badala yake nalazimika mpaka niwe kwenye *group?* Naomba tu ufanuzi kwa hilo, lakini nashukuru sana kwa fedha ambazo mmekuwa mkiendelea kutupa katika hospitali yetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nalionia kama la kisera, lakini nashukuru kwa mwongozo wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama tulivyosema kwamba tunafanya mapitio ya vifurushi mbalimbali vya Bima ya Afya na ndio maana tunataka kwenda kwenye hiyo *approach* ya jipimie au kwenda kwenye *ICHF*. Kwa hiyo, naomba kabla ya miezi miwili tutakuwa tayari tumeshatoa muelekeo mpya, nashukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kif. 6010 – *Mara Reg. Ref. Hosp*.....Sh. 581,575,067/=
Kif. 6011 – *Maweni Reg. Ref. Hosp.-Kigoma*..Sh. 528,745,632/=
Kif. 6012 – *Mawenzi Reg. Ref. Hosp-K/Njaro*..Sh. 618,844,731/=
Kif. 6013 – *Mbeya Reg. Ref. Hosp*.....Sh. 644,684,169/=
Kif. 6014 – *Morogoro Reg. Ref. Hosp*.....Sh. 742,167,199/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kif. 6015 – *Mt. Meru Reg. Ref. Hosp.-Arusha*...Sh. 647,706,196/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Amina Mollel.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika Hospitali yetu ya *Mount Meru* ninafurahi sana na ninashukuru kwa ukarabati unaoendelea. Hivi sasa Serikali katika mkakati wake wa kuboresha vituo vya afya naipongeza Serikali kwa ukarabati huu wa vituo vya afya na hasa ujenzi wa vituo vipyta vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini madaktari na *clinical officers* wanaofanya kazi katika vituo vya afya pamoja na zahanati madai yao makubwa ni kwamba utaratibu uliopo wa bima ya afya kwa madaktari ambao wanafanya kazi katika hopsitali za wilaya na mkoa wao ile *consultation fees* wanalipwa shilingi 15,000, lakini hawa wanaofanya kazi katika vituo vya afya pamoja na zahanati wanalipwa shilingi 2,000. Na ukizingatia sasa hivi utaratibu wa Serikali ni kuhakikisha kwamba hivi vituo vya afya vinafanya *operation* na ni kweli kabisa, zoezi hilo limeshaanza.

Sasa je, hatuoni kwamba tunawa-*demoralise* hawa madaktari ambao wanakwenda kwenye vituo hivi vya afya, ambao walipokuwa huku mwanzo wanalipwa ile *consultation fee* shilingi 15,000 lakini hivi sasa imekuwa ni shilingi 2,000. Naomba tu ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Afya.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Amina Mollel kwa swali lake zuri. Ni kweli, zamani tunaita haya malipo, *reimbursement* za Bima za Afya yalikuwa yanaangalia ngazi ya kituo kama ni zahanati, kituo cha afya, hospitali au, lakini ndani ya mwaka mmoja tumefanya mabadiliko. Tumeyafanya kwa lengo kwamba tunataka katika, kama unavyosema vituo vya afya tuwe na madaktari. Kwa hiyo, tunakoendelea kama mtu ana sifa zinazofanana mmoja yuko Kituo cha Afya cha Nkasi, lakini na mwingine yuko Muhimbili, kwa sababu sasa hivi wa Muhimbili analipwa sana kuliko wa Nkasi, lakini wana sifa zinazofanana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo tunalirekebisha kwa sababu, lengo letu tunataka mtu awe Nkasi, awe Arusha, awe Muhimbili, *as long as* wana sifa zinazofanana wote walipwe viwango sawa vya kumuona mgonjwa na sisi hii tunaamini kwamba ndiyo itasukuma sasa Madaktari Bingwa kwenda kufanya kazi katika mikoa na katika maeneo ya vijijini. Kwa hiyo Mheshimiwa Amina angalia, imepanda kidogo lakini bado tunafanya *acturial study* kwa sababu kule chini pia ndiko ambakoo wagonjwa wengi wapo. Hata hivyo tumeiongeza kutoka shilingi 2,000 mpaka kwenye shilingi 10,000 hivi, ahsante.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukumbushane tu, maswali ya kisera yanesubiri Fungu la Mshahara wa Waziri. Wakati huu hivi vifungu unaomba ufanuzi kwenye fedha zilizotengwa, unatutajia kabisa ni wapi unapotaka ufanuzi. Kwa hiyo, tuisimame kwenye vifungu kuuliza maswali ya jumla au masuala ya jumla, unauliza fedha zilizotengwa wapi unataka ufanuzi. Ufanuzi wa mambo ya jumla tunasubiri saa ya mshahara wa Waziri, maswali ya kisera, nadhani hapo tutakuwa tunaenda vizuri.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kif. 6016 – *M/nyamala Reg. Ref. Hosp-Dsm*.Sh. 1,285,228,841/=
Kif. 6017 – *Njombe Reg. Ref. Hosp.*Sh. 465,697,853/=
Kif. 6018 – *Sekou Toure Reg. Ref. Hosp-MZ* ...Sh. 607,847,790/=
Kif. 6019 – *Shinyanga Reg. Ref. Hosp*Sh. 525,426,776/=
Kif. 6020 – *Simiyu Reg. Ref. Hosp*Sh.464,967,054/=
Kif. 6021 – *Singida Reg. Ref. Hosp.*Sh. 454,989,036/=
Kif. 6022 – *Sokoine Reg. Ref. Hosp. – Lindi* ...Sh. 479,796,008/=
Kif. 6023 – *Songea Reg. Ref. Hosp.-Ruvuma*...Sh. 641,469,231/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kif. 6024 – *Songwe Reg. Ref. Hosp.*Sh. 485,476,554/=

MWENYEKITI: Fungu la ngapi unauliza Mheshimiwa?

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Sub-Vote 6024, *Songwe Regional Referral Hospital*.

MWENYEKITI: Karibu Mheshimiwa.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona imetengwa shilingi milioni 485.4, sasa tulikuwa tunataka kujua tu kwamba, ni lini wametangaza Mkoa wa Songwe kuwa na Hospitali ya Rufaa, kwa sababu, hatuna hospitali ya rufaa; na juzi tulikuwa na kikao cha mwisho cha RCC jambo hili hatujalisikia, tuna Hopitali ya Wilaya tu pale Songwe, sasa hizi, tunaomba ufanuzi kwenye fungu hili.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba Hospitali sasahivi ile ya Mbozi ndio tunaitumia kama Hospitali Teule ya Mkao wa Songwe. Kama utakumbuka katika kitabu chetu cha bajeti ukurasa wa 115, katika moja Mkao wa Songwe ni mmoja ambao na sisi tunafikiria kujenga Hospitali za Mikoa, samahani ukurasa wa 118, ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa, mmojawapo ni mkoa wa Songwe na tunategemea shilingi bilioni 30 kwa kazi hiyo.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 6025 – *Sumbawanga Regional*

Referral Hospital – RukwaSh.542,928,319/=

Kif.6026-*Tabora Regional Referral*

HospitalSh. 530,322,459/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 6027 – *Temeke Regional Referral Hospital*

– Dar es SalaamSh.1,069,620,701/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sungura.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kifungu kidogo cha 21113 - *Personal Allowances* katika *Temeke Regional Referral Hospital*, nimeona imekuwa *amount* kubwa sana uki-*compare* na *amount* zilizoko hospitali nyingine, imeenda mara mbili mpaka mara tatu. Kwa nini imekuwa hivyo, *what is so special* katika Hospitali ya *Temeke Referral?* (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Sabreena aangalie ukurasa wa 137 wa hotuba yetu. Mzigo ambao Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Temeke inaubeba ni mkubwa na nikikupa mfano tu Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Temeke ina vitanda 294 lakini wagonjwa wanaowaona ni 138,000 ukilinganisha na Tabora Hospitali ya Kitete wana vitanda vinavyolingana lakini wao wanaona wagonjwa 24,000. Kwa hiyo, unaona mzigo wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Temeke ni mkubwa. (*Makof!*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nifafanue tu kwamba wakati mwingine mnapoona madaktari wengi Temeke, Amana na Mwananyamala siyo kwamba tunawapendelea lakini pia ni kutokana pia na mzigo mkubwa wa kuwaona wagonjwa ambao wanao. (*Makofii*)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 6028 – *Tumbi Kibaha Regional Referral Hospital* – Pwani.....Sh.534,337,851/=

MWENYEKITI: Kabla sijawaita Wabunge waliosimama, Waheshimiwa Wabunge hasa upande wa Serikali mkumbuke kuitikia kama mnataka haya makadirio Bunge lipitishe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niulize swalii ambalo linafanana kidogo na la Mheshimiwa Sungura, isipokuwa katika Hospitali yetu ya Tumbi ambayo inafahamika kwamba ni hospitali inayobeba mzigo mkubwa sana, hasa ukizingatia kwamba inasaidia Mkoa wa mzima wa Pwani lakini hakuna fungu kwa ajili ya *training* ya watu wetu, hakuna fungu la *communication* wala *routine maintenance* ya vitu vyetu.

Nataka nimulize tu Mheshimiwa Waziri hii ni kwa bahati mbaya wameviruka vitu hivi au ni ndiyo utaratibu wa kwamba tusipate *training* kwa watu wetu? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii tumeweza kuiweka na kuacha hivyo vifungu vingine kutokana na ukomo wa bajeti, lakini Wizara mama itaendelea kusimamia masuala ya mafunzo kwa watoa huduma wote katika ngazi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ridhiwani kwenye kifungu hiki unasimama mara moja tu. Mheshimiwa Maftaha.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Na mimi naomba nipate ufanuzi kwa sababu Hospitali hii ya Tumbi naifahamu sana. Kwenye *sub-vote 22014 - Hospitality Supplies and Services* imewekwa shilingi 600,000 tu na hii ni hospitali kubwa sana, wanafanya kazi za kuhudumia wagonjwa ambapo wengine wanatoka Dar es Salaam na Mikoa ya Kusini. Naomba nipate ufanuzi kwa nini hii pesa imekuwa ndogo wakati hospitali hii inafanya kazi kubwa sana kwa Watanzania? Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kinachoonekana ni kwamba tumepata ukomo wa bajeti lakini tukumbuke kwamba hospitali hizi bado nazo zinafanya makusanyo yake ya ndani pamoja na bima ya afya ambazo kwa kiasi kikubwa itaweza ku-cover zile *deficit* nyingine ambazo zipo katika hospitali hizo.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1001 – *Administration Human Resources Management*.....Sh. 8,081,010,335/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki ndicho chenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

Nimeletewa orodha hapa na vyama tulivyonavyo humu ndani japokuwa majina yamezidi, lakini tutaanza na Mheshimiwa Oscar Mukasa.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri na timu nzima kwa kazi nzuri ambayo inaonekana na hakuna shaka kwenye hilo lakini wanasesma mzigo mzito mpe Mnyamwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikiliza hotuba ya Waziri na michango ya Wabunge wengi, lakini hata ukiangalia *votes* hapa, nimehesabu vifungu vipo 61 kwenye *votes* zote mbili, lakini zinazoongelea kinga ni mbili tu. Tukienda na *trend* hii kwa miaka 10 *automatically* hata bila Mheshimiwa Rais kubadilisha itakuwa Wizara ya Tiba badala ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano wa lishe ambao ameusema vizuri. Mapendekezo yangu naomba tipeleke Maafisa Maendeleo ya Jamii vijiji, ndiyo iwe *action* yetu ya kwanza na kama hatuwezi kuwapeleka kwa haraka tutumie Watendaji wa Vijiji, wakaelimishe tuanze safari ya kubadilisha kutoka kwenye tiba tu twende kwenye kinga. Nitatoa mfano kwa nini nimechukua lishe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko kwetu nakotoka na sehemu nyingi Tanzania watu wanaona fahari (*prestige*) kula unga uliokobolewa halafu kuku wanapewa yale makapi, kwa hiyo kuku ndiyo anakula lishe bora; Watanzania wanakula makapi kwa sababu kule kwenye kukobolewa hakuna kitu. Najua utekelezaji wake ni jambo mtambuka lakini sisi tunaonjea na Serikali hapa, naomba Watendaji wa Vijiji kwenye hadidu za rejea za kazi zao na hili linaweza likaanza sasa hivi, iwe ni kutazama namna gani ya kuelimisha na tuweke hata vipimo, hatuwezi kukubali kijiji ambacho una asilimia 60 ya watoto ni *stunted* halafu tunasema tuna Mtendaji wa Kijiji, Mtendaji wa Kata au Mkurugenzi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakusudia kushika shilingi kama sitapata maelezo ya namna ya kutekeleza hilo, tuanze sasa pamoa na kusubiri. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ufanuzi.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nimpongeze sana Mheshimiwa Oscar Mukasa kwa swali lake zuri na huo ndiyo mwelekeo wa sekta afya kwamba sasa hivi tunataka kujikita pia kwenye kinga badala ya kujikita sana kwenye tiba.

Mheshimiwa Oscar nitaomba usitoe shilingi kwa sababu ukiangalia mipango ambayo tumeiweka pale Wizarani, sasa hivi nimemwandikia Waziri wa Utumishi, Mheshimiwa Mkuchika, tunataka kuja na kada mpya rasmi inaitwa *Community Health Workers*, hawa sasa ndiyo watakuwa sungusungu wa afya, Ethiopia wanawaita *Healthy Army* (wanajeshi wa afya) ambao watacaa kwenye ngazi ya kijiji, wao hawatakuwa kwenye hospitali. Kazi yao kubwa itakuwa ni kuhamasisha kwenye vijiji masuala ya lishe, wajawazito kujifungulia vituo vya afya, masuala ya HIV na malaria. Kwa hiyo, nasubiri hatua moja tu Mheshimiwa Mkuchika akamilishe ili tuweze sasa iwe kada rasmi ya afya. Kwa hiyo, tutakuwa na watumishi wa afya katika vituo lakini tutakuwa na watumishi wa afya katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Oscar nimepata wadau tutaanza na mikoa nane katika kila kijiji ya Katavi, Rukwa, Songwe, Mbeya, Tabora, mikoa ambayo ina idadi kubwa ya vifo. Kwa sababu pia *Community Development Officers* pia wako Wizarani, tumeliongea juzi pia tunapitia *job description* zao, kwa kiswahili sijui ni nini, ili kuwaongezea majukumu kwamba pamoja na kazi watakazofanya itakuwa pia ni kuhamasisha wananchi kuzingatia masuala ya kinga badala ya tiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunasema afya ni mtaji. Kwa hiyo, tutaenda sana kuwataka Watanzania wawekeze kwenye afya zao kwa kufanya mazoezi, kupunguza pombe kwa sababu hata unywaji wa pombe kupita kiasi unaleta madhara katika afya na kufanya mazoezi mara kwa mara. Namshukuru sana Mheshimiwa Oscar na namwomba asitoe shilingi kusudi nikimaliza nikambane Mheshimiwa Mkuchika anipitishie barua yangu ambayo nimemwomba tupitishe wahudumu wa afya ngazi ya jamii. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Jamani walimu wa kiswahili watuletee *dictionary* (kamusи) humu ndani. Mheshimiwa Mukasa naona umesimama tena. (*Kicheko*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Waziri nardhishwa sana na *political will* uliyonayo ambayo ni muhimu sana, lakini nachosema wakati tunajandaa kwa mambo ambayo ni wazi hayawezhi kuanza kesho na inawezekana yakachukua muda kidogo hayo maandalizi, kuna mahali ambapo tunaweza tukapatumia hiyo kazi ikaanza wakati tunasubiri hiyo mbinu ya kufanya kwa muda mrefu kwa uendelevu. *Definition ya science* kwa ufupi ni *do simple things well*, mambo madogo tu yafanye vizuri ndiyo *science*. Una Watendaji wa Vijiji pale, hebu tuongeze kwenye hiyo hadidu yao rejea ya kazi hii kazi ianze mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuambia kwa nini kuna uharaka. Sasa hivi tunasifia hapa wote nikiwemo mimi kwamba tunaongeza bajeti ya dawa, ni jambo zuri sana, lakini hiyo nayo lazima ifikie *plateau* mahali, ukiongeza zaidi ukienda miaka mitano, kama nilivyosema itageuka kuwa ni Wizara ya Tiba tu sasa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mukasa, malizia sekunde mbili.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri sawa mipango ni mizuri lakini kuna namna tunaweza kuanza sasa, naomba tuanze sasa. Sitashika shilingi lakini naomba ultafakari hilo. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa sababu kashairudisha shilingi yake, labda tuanze na *canteen* Waheshimiwa Wabunge waache kula ugali uliokobolewa, tuanzie hapo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nataka kupata ufanuzi kwa Mheshimiwa Waziri na kiukweli nakusudia kushika shilingi kama hatanipa majibu sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Afya anatembelea baadhi ya maeneo na kimsingi sisi Wabunge huwa tunawaalika Mawaziri ambao tunaona kuna umuhimu kwenye majimbo yetu. Aliwahi kuja kwenye jimbo letu kule Geita akaona uhitaji wa wananchi wa Jimbo la Geita Vijiji ambao wanatembea kilometra 100 mpaka kilometra 97 kuipata hospitali ya wilaya. Yeye mwenyewe kama mama kwa huruma yake na aliangalia hata *population* ya watu ni kubwa akaridhia mwenyewe kupandisha Kituo cha Afya cha Nzela kuwa Hospitali ya Wilaya ya Geita ambayo haina Hospitali ya Wilaya mpaka sasa. Baada ya mwezi mmoja kama Mkoa na Wilaya tulikamilisha taratibu na Mheshimiwa Waziri akaipandisha hospitali ile kwa kutupa barua kutoka Wizara ya Afya, lakini TAMISEMI inasuasua kukubaliana na maamuzi ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Afya kisera ndiyo anayepandisha vituo vya afya, ndiye anayeshughulika na afya halisi kimsingi, lakini TAMISEMI nao wana maamuzi kwenye maamuzi ya Waziri wa Afya. Sisi wananchi wa Geita ambao hospitali yetu ilipandishwa, nataka nipate majibu ya msingi nakusudia kutoa shilingi, nani hasa anayehusika kupandisha hizo hospitali au kushughulika na hilo suala la afya? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri ukae kidogo ili twende vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, maswali yanayoulizwa hapa ni ya kisera na siyo kila mtu aulize kuhusu jambo lake yeye, ama jambo lake yeye au eneo lake, ni sera. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri hapa alikuwa amesimama atuelezee jambo hilo kisera lakini naomba wale wanaoendelea kuitwa majina hapa mbele wazungumzie sera. Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kisera mwenye mamlaka ya kupandisha hadhi zahanati, kituo cha afya au hospitali yoyote ni Waziri wa Afya, Maendeleo ya

Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Atafanya hivyo baada ya vigezo vyote kukidhi kuanzia ngazi ya wilaya, mkoa inakuja wizarani na akishaandika barua hatakiwi mtu mwingine yejote kwenda kuihoji barua hiyo kwa sababu mamlaka ya kisheria yako chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Musukuma ili uzungumze lazima uitwe, sasa zungumza nimekuita. (*Kicheko*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na kwa kweli nimefurahishwa na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri na kwa uchapaji kazi wa Waziri wa Afya sina sababu ya kuendelea kushika shilingi. Naomba sasa ile mifano niliyoitoa iko kwa Wabunge wengi, niliweka tu mfano kwa kujenga hoja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nimesikia jibu lako na mimi nitafuatilia, nashukuru. (*Makofu/Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Musukuma. Mheshimiwa James Mbatia.

Waheshimiwa Wabunge nimeletewa jina la Mheshimiwa James Mbatia kwa nafasi ya CHADEMA ili baadae watu wasije kuanza kuandika ujumbe hapa mbele. Nimeletewa kwa niaba kambi hii hapa, kwa hiyo, atakuwa amebaki mmoja wa CUF. Ahsante sana.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwenye mchango wangu nilizungumzia kuhusu suala la vifaa tiba, kwa mfano, *MRI*, *CT-Scan* na vifaa vingine katika hospitali zetu na hasa ngazi ya mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mgonjwa akiwa Jimbo la Ruangwa Vijijini amepatwa na *brain hemorrhage* mpaka afike Muhimbili hali ni tete labda imeharibika, tumekuwa tukipoteza uhai wa Watanzania

walio wengi. Ni-*declare interest*, Januari nilimpoteza shangazi yangu yuko KCMC mashine imeharibika anaambiwa apelekwe Selian Arusha na namna ya kumpeleka na huku amepata *brain hemorrhage* akapoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua hawa wataalam ni shida kuwapata lakini wako wale ambao tumewa-*train* humu ndani, wataalam wa mionzi hawa, tunawapa *incentives* gani wasiende nje, wengi wanafanya kazi nje na pia *specialization* zao. Dunia ya leo ni kijiji, kama hatuna wa kutosha humu ndani kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri alisema pia siyo zile mashine tu hatuna watalaam wa kutosha, kwa nini tusi-*solicit* au tusitafute wataalam duniani kwa ajili ya uhai wa Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Wizara hii iseme na *iji-commit* kwamba umuhimu wa hospitali zetu na hasa Mikoa ya Kusini pia wa kuweza kupata huduma hii kwa sababu ni haki ya msingi ya kila Mtanzania kwenye kupata huduma hii na hivi vifaa tiba ni tatizo nchi nzima. Kama Serikali haitatoa majibu ya kutosha na hasa *specialization* pia niko tayari kutoa shilingi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua na amejenga hoja yake vizuri sana lakini kama nilivyosema wakati nahitimisha hoja kwamba katika sekta ya afya tumeweka miongozo ya aina ya huduma ambazo zinapatikana katika ngazi mbalimbali. Katika ngazi ya sasa hivi huduma za *MR/na CT-Scan* zinapatikana katika ngazi ya kanda. Sambamba na hilo kwa sasa hatuna *capacity* kwa maana ya wataalam wa kuweza kuhudumia huduma hizi katika ngazi hizo ambazo tunazo kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Serikali imepokea Hospitali za Rufaa za Mikoa na moja ya kada za kipaumbele tumeelekeza katika Madaktari Bingwa katika ngazi ya *radiology* na katika mwaka huu wa fedha tumepeleka

madaktari 125 ikiwa ni pamoja na madaktari wa *radiology*. Pia tunaenda mbali, katika Hospitali zetu za Rufaa za Mikoa tunataka tuweke mashine za *radiology* za kisasa (*digital x-rays*) ambapo sasa hivi badala kuwa *x-ray* kwa sababu kwa sasa hivi tunaishi katika *global village*, dunia sasa hivi imekuwa ni kijiji, moja ya mkakati ambao tunataka kuufanya tutaweka chumba kimoja pale Dar es Salaam badala ya madaktari wetu kuzunguka kutoka hospitali moja kwenda nyagine kwenda kusoma *x-ray*, *MR/na ST-Scan* kwa kutumia Mkongo wetu wa Taifa *x-ray* zote nchi nzima zitakuwa *reported* sehemu moja zitasomwa na ndani ya muda mfupi majibu yanarejeshwa iwe Ruangwa, Katalamba, Nsimbo au sehemu yoyote katika nchi yetu. Wakati huo huo tunaendelea na mkakati wetu wa kusomesha madaktari na kadri uwezo utakavyozidi kuongezeka tutaanza sasa kushusha teknolojia hizi katika ngazi ya mkoa. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa James Mbatia.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu iliyotoa Serikali hapa kupitia kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Hili ni suala la kitibabu na kitaalam nakubali kabisa lakini nakumbuka majibu ya Serikali mwaka jana kwenye vifaatiba hivi hivi ilikuwa ni *kuji-commit* lakini nimesema matatizo ya kibajeti na kadhalika, sasa uhai wa mwanadamu hauna thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningombwa wenzangu wachangie hoja hii kwa msingi tu kwamba ni namna gani tunafanya maamuzi kama Bunge ili haki hii ya msingi ya Watanzania, hospitali za kanda tu zilizopo hazitoshelezi na pia hospitali za kanda zilizopo leo hii vifaa vyenyewe vingine viko hoi bin taabani na havifanyi kazi, sasa tufanye nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi ili Wabunge wenzangu wanisaidie sikuridhika na majibu, naomba kutoa hoja. (*Makof!*)

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono. Wachangiaji nitachukua majina, Mheshimiwa Marwa, Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Bashe, upande wa Serikali hakuna, sawa. Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na hoja ya Mheshimiwa Francis Mbatia, ni kweli kabisa anachokisema. Ukiongea na wahudumu, wataalam, waganga ama madaktari wengi wanalamika sana kuhusu upungufu wa vifaatiba. Kwa mfano, ukienda kwenye hospitali nyingi sana za Wilaya, Hospitali za Mikoa hazina *CT-Scan*. Kwa hiyo, nadhani hoja anayoisema ni hoja ya msingi sana kuhusu vifaatiba, ukizingatia kwamba ukiangalia kwenye vitabu humu hakuna. Sasa ni vizuri Serikali ije na mkakati wa kutuambia mna mkakati gani wa kununua *CT-Scan* kwa kila Hospitali ya Wilaya? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mbatia kwa kuzingatia yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kupata tiba mahsus ya kukutibu ugonjwa wako kama hujafanyiwa *proper diagnosis*, la kwanza.

La pili, tuangalie aina ya magonjwa yaliyoongezeka sasa hivi, tukiaangalia pia na suala Waheshimiwa Wabunge wengi wameongelea afya ya mama na mtoto, tunahitaji huduma za *ultra-sound*. Sasa kama huna wataalam hawa wa *radiology* au *expert* wa kusoma hizi *imaging tools*, hamna *tools*, hamna wataalam unaweza ukawa umejitahidi kuleta dawa za kutosha, lakini kama dawa haijilikani inaenda kutibu nani na ugonjwa gani bado tuko kwenye tatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ameutoa Mheshimiwa, una mgonjwa amepata *hemorrhage* yuko

vijijini, ile hekaheka tu ya kumsafirisha kilometa 500 anaenda Hospitali ya Rufaa ni kumuua lakini tungekuwa tuna hizi *basics*, *CT-Scan*, *x-rays*, *ultra-sound machines* unaweza kutoa huduma Wilayani au kwenye kata husika ni *basics*. Siongelei mashine za *MRI*, najua ni *very expensive* na zitaenda kwenye kanda lakini kuna *basics* za kawaida. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna uhaba mkubwa wa hawa *expert* ambao wanakupa tiba ambayo inaenda kukuponyesha. Kwa nini Serikali isiangalie kwa jicho la ziada hawa wachache walionao tusiwape malipo stahiki ya kuwawezesha na kuweka mfuko maalum wa kuwaajiri hao *radiologist?* Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. Mheshimiwa Jitu Soni.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi pia naunga mkono suala ambalo amesema Mheshimiwa Mbatia ni jambo muhimu sana. Mimi nilenge namna ya kutoa ushauri na namna ya kufikia huko. Ningeshauri Serikali kwa sababu leo hii inafanya kazi nzuri sana na Naibu Waziri ameeleza masuala ya *tele-medicine*, hongereni na hiyo pongezi iende kwa timu nzima ya Wizara ya Afya kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa sababu vifaatiba hivi akileta mtu binafsi, kuna watu ambao wako nje wakitoa hata kwenye hospitali zetu hata kama vituo vya afya na zahanati za Serikali vikija hapa nchini vinatozwa kodi. Mngehakikisha kwamba vifaa vyote kwa mtu ye yeyote iwe kwa mtu binafsi, vifaa vyote vya tiba na inahusiana pia na walemauvu kama *wheel chairs*, *walking sticks*, mambo ya macho lakini na hizi *x-rays* na vyote mngeondoa kodi ili *private sector* isaidiane na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kwenye suala la kodi, mashirika au makampuni mengi yanapenda kuchangia lakini akichangia tu milioni tano au kumi anapigwa 30% *income tax*. Mngeweka *social corporate responsibility*

kwamba akichangia asilimia fulani, mpange isiwe kubwa, kwamba kwenye kampuni yoyote basi asilimia 10 iwe *allowed expense* kuchangia kwenye sekta ya afya hatatozwa kodi ya mapato, watu wengi zaidi pia watachangia kwenye sekta ya afya, mtapata hela nyangi ambayo itasaidia Serikali kwenda na mpango huo kwa sababu idadi ya vituo nya afya, zahanati, Hospitali za Wilaya tunazotakiwa kujenga ni nyangi na naamini kabisa bajeti hiyo hatuna. Kwa hiyo, tukilenga kuondoa hilo suala la kodi kwa muda mfupi kama ni miaka mitatu vifaa hivyo vitakuja kwa wingi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Jitu Soni. Mheshimiwa Hussein Bashe.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi naungana mkono na hoja ya Mheshimiwa Mbatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *speciality, equipment* na *health system* ni lazima tuje na mpango mpya. Kama alivyoongea Mheshimiwa Jitu suala la *incentive* ya kodi, lakini kwa nini Serikali isianze kutafakari *PPP* kwenye hizi Hospitali zetu za Mikoa na Wilaya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Serikali imeamua kuwakabidhi Wizara ya Afya na katika dua ninayoomba kwa Mwenyezi Mungu kila siku mkabidhiwe na Hospitali za Wilaya yaani hii ni dua naomba. *Improvement* mnayofanya katika *basic health system* huku kwenye kata bila kuhakikisha tunapata *equipment* za uhakika katika mikoa tafakarini na mjadiliane ndani ya Serikali, *private sector* iingie na tuwe na *incentive package* ambayo itapunguza gharama za huduma hii watakapoleta hawa wawekezaji kwenye hospitali zetu za mikoa ili *MRI* na *CT-Scan* zipatikane ili kupunguza mzigo wa Serikali kuwaza kununua kila siku.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile ameongea suala la *digital x-rays* lakini *in a next two, three, four, five years* zitapitwa na wakati. Zikipitwa na wakati Serikali itanza kuwaza tena kutafuta fedha kununua nyingine kutokana na mabadiliko ya teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakubaliana ni lazima tulitafakari hili wazo alilosema Mheshimiwa Mbatia kwa mapana yake na ku-*incorporate private sector* kwenye *health system.* (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Jenista Mhagama.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi sana kuona kwamba Waheshimiwa Wabunge kwa namna moja wanakubaliana na mkakati wa Mheshimiwa Waziri na Serikali wa kuboresha huduma ya afya, lakini *concern* hapa kubwa ni kuchangia mawazo mbadala ambayo yatasaidia Serikali na Wizara kufanya kazi hiyo vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukilitizama jambo lenyewe wote tunaungana mkono na Mheshimiwa Mbatia lakini tunachokisema sasa turudishe kazi hiyo kwa Wizara ya Afya kwa maana ya kwamba Wizara ya Afya ianze kutafakari suala la msingi alilolisema Bashe la *PPP*, Wizara ya Afya ianze kutafakari jambo hili ndani ya Serikali la kufuta kodi katika vifaa tiba ili viweze kuongezeka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kukisema hapa ni kwamba Waheshimiwa Wabunge tumuamini Waziri wetu na tuiamini Serikali. Tumeshafanya kazi nzuri sana katika kupandikiza figo, kwa muda mfupi Serikali imefanikiwa hilo. Kwa muda mfupi tumeanza kazi ya kusafisha figo ndani ya nchi yetu ya Tanzania, imeshaanza kufanyika. Kwa muda mfupi tumeshaanza kupandikiza vifaa vya kusikia kwa watoto ndani ya nchi yetu, ni hatua kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Waziri amesema tumeanza na hospitali za kanda, tutakwenda hospitali za mikoa, tutakwenda mpaka hospitali za wilaya na Mheshimiwa Bashe anafikiri ni lazima uko mfumo wa afya ukae vizuri. Nimuombe sana kaka yangu Mheshimiwa James Mbatia kwa kazi kubwa ambayo imeshaanza kufanyika ndani ya nchi yetu kwenye tiba, sina shaka hata jambo hili lenye msingi tukimuachia Mheshimiwa Waziri na Serikali litasimamiwa vizuri na baada ya muda mfupi tutafika huko tunakokwenda. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana tumuamini Mheshimiwa Waziri. Kaka yangu Mheshimiwa James muachie mshahara wake Mheshimiwa Waziri akafanyie kazi ndani ya Serikali ushauri wa Waheshimiwa Wabunge uliotolewa leo tufike huko tunakotakiwa kufika. Tumeshaona mwanga wa kutosha, tunakokwenda nadhani mwanga ni mkubwa zaidi kuliko tulikotoka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba shilingi ya Mheshimiwa Waziri iachiwe na mshahara wake uwe salama. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia katika hoja hii na hoja ya Mheshimiwa Mbatia.

Kimsingi kama alivyosema Mheshimiwa Jenista Mhagama kwamba wote tunaonekana tuna dhamira ya dhati tuboreshe sekta ya afya na sisi kama Serikali tunaikubali na tumeshaanza. Katika vituo vya afya hivi ambavyo tumeviboresha kwa kuweka miundombinu na tukasema kwamba tutatenga shilingi milioni 200 mpaka shilingi milioni 300 huduma ya *ultra-sound* tutaziweka katika vituo hivyo. Sambamba na hilo, tunanunua mashine za *x-ray* kama nilivyosema *digital x-rays* na tutatumia mfumo wa *tele-medicine* kuziunganisha katika ngazi hizi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee hoja moja ambayo Mheshimiwa Bashe ametoka kuisema na ndiyo mtazamo wetu. Sasa hivi gharama tunazotumia kununua vifaa, gharama ambazo tunatumia kutengeneza vifaa vikiharibika na Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Dau amekuwa analia kwa muda mrefu sana mashine zimeharibika miaka sita, gharama ambazo tunazitumia kutengeneza mashine zetu, dunia ya sasa imeshahama huko, dunia ya sasa hivi inaongelea kuweka vifaa na kununua huduma. Tuna watengenezaji wa vifaa, sisi kama nchi tunawaambia Watanzania milioni moja wanahitaji kupiga *x-ray*, tunawaambia wale watengenezaji wa hizi *technology* wanakuja wanaweka mashine zao pale, gharama za kuziweka pale ni za kwao, gharama za *ku-maintain* ni za kwao, gharama ya teknolojia kubadilika ni za kwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huo ndiyo mtazamo ambao sasa hivi tunakwenda nao kama Serikali na mimi niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge mturudishie shilingi yetu ili tuweze kwenda kujipanga vizuri katika mwelekeo huu ambao nimetoka kuusema. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mtoa hoja, Mheshimiwa Mbatia.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana Waheshimiwa Wabunge walioniunga mkono na pia upande wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imeji-*commit* kwenye suala hili sitapenda tupige kura isipokuwa niishauri Serikali suala la kuwa na *big investors* ambalo nililisema hata asubuhi ubia, mashirika ya dini na sekta binafsi katika kuhakikisha wanaisaidia jamii ya Watanzania kwenye sekta ya afya utiliwe mkazo. Kwa sababu majibu yao hayakuwepo bayana wakati wanajibu nasema sasa kwamba nairudisha shilingi ili wakafanye kazi yao. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Maftaha Nachuma.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nchi hii miaka ya 1970 ilileta sera ya *decentralization of services* kwa maana ya kupeleka huduma karibu na wananchi. Sera hii ya kupeleka huduma karibu na wananchi lengo lake ni kupunguza gharama za huduma hizi kwa wananchi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwenye ilani ya chama kinachotawala, kwa sababu ni ukweli usiopingika kwamba nchi hii tunaenda na mfumo wa *majority rule* kwamba wale waliopata kura nyingi ndiyo ilani yao inatawala nchi, hilo ni ukweli kabisa. Kwa hiyo, naomba kusema kwamba katika sekta hii ya afya kumetamkwa sera ya kwamba kanda zote Tanzania ziweze kujengwa hospitali za kanda lakini wilaya zote kuweze kuwa na Hospitali za Wilaya.

Naomba nipate ufanuzi wa kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri hapa utekelezaji wa sera hii ya kwamba kila Wilaya kuwe na Hospitali ya Wilaya na kila Kanda kuwe na Hospitali ya Kanda imetekelezwa kwa namna gani na kwa kiwango kipi mpaka leo na hasa ukizingatia hilli liliwekwa katika llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 na zilizopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufanuzi na nakusudia kushika shilingi kama sitapata maelezo ya kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 104 nitaongeza nusu saa ili Kamati iweze kumaliza kazi zake. Mheshimiwa Naibu Waziri, ufanuzi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba kuna Wilaya mpya na kuna Wilaya nyingine zilizokuwepo, lakini hazina Hospitali za Wilaya. Ndiyo maana katika bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, hii ambayo tumeipitisha hivi karibuni tumeweka Hospitali za Wilaya 67 ambazo tutaanza kuzijenga. Sambamba na hilo, sisi kama

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Wizara ambao tunasimamia Hospitali za Rufaa za Mikoa tumejielekeza kujenga Hospitali za Rufaa mpya sita katika ngazi ya mikoa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba tuna huduma za ubingwa ambazo zinapaswa kuwa katika kanda. Moja ya kanda ni Kanda ya Kusini ambapo tunahitaji kujenga hospitali yetu ya kanda. Katika bajeti hii ukiangalia katika ukurasa wa 118 tumetenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Hospitali hii ya Kanda ya Kusini. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maftaha.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nishukuru kwa jibu la Mheshimiwa Nailbu Waziri, lakini kumekuwa na changamoto kubwa sana kwa wananchi wa Mikoa ya Kusini kwa maana ya Mtwara, Lindi na Ruvuma pale ambapo tunapata taabu sana kusafiri umbali mrefu kwenda kufuata tiba hizi katika Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili kwa sababu kule Kusini hatuna Hospitali ya Kanda. Hospitali hizi maeneo mengine tayari zimeshakamilika na wananchi wanapata huduma hizi, lakini Wizara kila mwaka tumekuwa tunaongea ndani ya Bunge hili kwamba wananchi wa kusini wanatembea umbali mrefu sana pale wanavyopewa *referral* kwenda Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa niombe Mheshimiwa Waziri anieleze maelezo ya kina kwamba kwa nini ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Kusini ambapo hilo jengo limeanza kujengwa takribani miaka 10 na zaidi iliyopita mpaka leo halijakamilika. Kila mwaka tunaambiwa pesa inatengwa, pesa inatengwa lakini hiyo pesa ingine haifiki na msisitizo wake unakuwa mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulimpeleka Mheshimiwa Waziri pale, dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu akaangalia *progress* ya lile jengo ambalo linajengwa *OPD* mpaka leo halijakamilika. Naomba nipate ufanuzi na

niombe Waheshimiwa Wabunge nitoe hoja ili muweze kuniunga mkono tuweze kujadili suala hili.

MWENYEKITI: Hoja hajuaungwa mkono Mheshimiwa. Kwa hiyo, tunaendelea na Mheshimiwa Richard Mbogo.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Eneo ambalo napenda kupata maelezo ya kina au *commitment* ya Serikali ni kuhusiana na hii Wizara ya Afya. Tunatambua kwamba tuna uzuiaji (*prevention*) na tuna tiba (*curing*) lakini bajeti hii ukiichunguza kwa kina tumejikita zaidi kwenye tiba kuliko kuzuia. Bajeti hii kiujumla katika hizi bilioni zilizotengwa ni takribani kama asilimia tatu ya bajeti nzima ya Serikali tofauti na Azimio la Abuja ambalo lilikuwa linatuhitaji bajeti ya Wizara ya Afya iwe asilimia 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitaji maelezo ya kina kutoka upande wa Serikali na hoja ni kwamba tuangalie katika vyanzo vyetu vya mapato na katika vyanzo vya mapato vya Serikali tuchague asilimia ngapi tuiweke kwenye zuio kwa ajili ya kushughulika na uzuiaji wa magonjwa (*prevention*)?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lugha nyepesi tufanye *ring-fence*, kwa mfano, unaweza ukasema makusanyo labda ya kodi za majengo uchukue asilimia 10 u-*ring-fence* kwa ajili ya kazi kiujumla za kuzia magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya uwekezaji huu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbogo kengele imegonga.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba maelezo ya Serikali zaidi ya hapo nitaomba suala hili lijadiliwe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ufanuzi.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,

WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana babu yangu Mheshimiwa Richard Mbogo kwa swali lake zuri, lakini lengo ni kuhakikisha kwamba hata wana Nsimbo wanapata huduma bora za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nahitimisha hoja yangu nilieleza kwamba tumekamilisha mkakati wa ugharamiaji wa huduma za afya (*health care financing*) ambao umebainisha maeneo au vyanzo mbalimbali ambavyo vinaweza kutoa rasilimali fedha kwa ajili ya kutatua changamoto za afya. Juzi tulifanya kikao na Kamati ya Bunge na tunaedelea na majadiliano na Wizara ya Fedha ili sasa tuainishe au tubainishe vyanzo ambavyo vitagharamia changamoto za sekta ya afya badala ya kutegemea fedha za wafadhili.

Mheshimiwa Menyekiti, kama nilivyosema nimetoa mfano wa Ghana, wao asilimia 2.5 ya VATinakwenda kwenye Mfuko wa Afya kwa ajili ya kugharamia huduma za afya. Nimetoa mfano wa South Africa wao kuna asilimia ya fedha za sukari na zile tunaita *sin taxes* kwa maana ya kodi za mambo ya dhambi kwa mfano, pombe, sigara, *disco*, kwa hiyo sehemu fulani inakwenda kwenye sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, njambo zuri babu yangu Mheshimiwa Mbogo, naomba usitoe shilingi kwa sababu tunaendelea kushauriana na wenzetu wa Wizara ya Fedha ili kukamilisha vyanzo vya kugharamia huduma za afya nchini ili tuweze kujitosheleza badala ya kusubiri wafadhili. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Richard Mbogo hukusema utashika shilingi, kwa hiyo, nadhani labda unataka kusema jambo kabla hujaahirisha hoja yako.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mweyekiti, nashukuru kwa nafasi. Maelezo aliyotoa Mheshimiwa Waziri ni mazuri, lakini sasa tungeuliza, je, wako tayari kuchukua ushauri huu na kwamba ni lini wataweza kutekeleza?

MWENYEKITI: Hilo swali mnaweza kulijibu sasa? Karibu Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Richard Mbogo na tutaufanyia kazi na naamini tukija kwenye Bunge lijalo tutakuwa na hatua fulani ambayo tumepiga. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Fatma Toufiq.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami naomba kupata maelezo kutoka kwa Serikali kuhusiana na hii Sera ya Wazee ambayo ilitungwa tangu mwaka 2003 lakini mpaka leo hii ni miaka 15 sheria bado haijatungwa. Naomba nipate maelezo kutoka Serikalini. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, uafanuzi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua mchango mkubwa sana ambao wazee wamekuwa wanatoa katika taifa letu. Taifa letu umri wa kuishi nao umeongezeka ni kama sehemu ya mafanikio ya sekta ya afya nchini. Kwa wale ambao wana kumbukumbu miaka ya nyuma ilikuwa ukishafika miaka 45 unakuwa umefikia ukomo wako wa kuishi, lakini sasa hivi wanasema *60 and 70 is the new thirty* kwamba ukifikia miaka 60, 70 sasa hivi ndiyo ujana unapoanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama Serikali na sisi tunawaenzi wazee. Tunatambua kwamba Sera yetu ya Wazee ya mwaka 2003 ambayo tulikuwa nayo kwa kiasi kikubwa imepitwa na wakati sasa hivi ni zaidi ya miaka 15. Hivi tunavyoongea tunafanya mapitiao ya sera hii na baada ya hapo sasa tutakuja na sheria muafaka ikiwa imegusa maeneo na nyanja mbalimbali katika masuala ambayo yanawahu su wazee.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Fatma Toufiq.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru sana kwa maelezo hayo na kwa kuwa wamesema kwamba wanaipitia sera hii basi ifanyike kwa haraka kusudi sasa hii sheria iweze kupatikana ili yale mambo yote kwa ajili ya wazee yaweze kupatiwa ufumbuzi. Nashukuru sana. (*Makof*)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif.1002–*Finance and Accounts*Sh.1,364,149,883/=
Kif.1003 – *Policy and Planning*Sh.1,142,017,824/=
Kif.1004 – *Internal Audit Unit*.....Sh.246,249,568/=
Kif.1005–*Government Communication Unit*. Sh.231,175,476/=
Kif.1006 – *Procurement Management Unit*...Sh.240,044,210/=
Kif.1007 – *Legal Services Unit*.....Sh.109,510,608/=
Kif.1008 – *Information Communication
and Technology*.....Sh.144,775,148/=
Kif.2001 – *Curative Services*Sh. 204,159,291,034/=
Kif.2003 – *Chief Medical Officer*.....Sh.37,047,248,576/=

(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2004 – *Nursing and Midwifery Services
Division*.....Sh. 390,230,691/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu kidogo 22008 ambacho kinahusiana na Idara ya Huduma ya Uuguzi na Ukunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na hata Wabunge wote humu ndani waliochangia wameongelea suala zima la vifo vya uzazi. Mimi naamini kwamba vifo hivi vinatokana pia na hao wauguzi kutokupata mafunzo kwa sababu teknolojia na mazingira yanabadilika.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hiki kifungu nachokizungumzia kinahusu mafunzo ya ndani ya nchi. *Last year walikuwa wamepewa shilingi milioni 27, mwaka huu hawana kitu that means hii Division ya Uuguzi hawaendi kupata mafunzo na hapo hapo tunasema kwamba vifo vya wanawake vinaendelea kuongezeka badala ya hili jambo kuwa furaha kwenye familia inakuwa ni kilio. Ni kwa nini Serikali hajatoa fedha hata kidogo kwa ajili ya kuwapatia waguzi wetu mafunzo japo ndani ya nchi achilia mbali nje ya nchi?*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, ufanuzi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu ambacho amejielekeza Mheshimiwa Susan Lyimo kinaongelea mafunzo kwa watumishi ambao wako Idara ya *Nursing* ndani ya Wizara ya Afya. Mafunzo ya *pre-training* na *post training* kwa *nurses* utayaona katika *training* kwa Idara ya Mafunzo. Katika bajeti yetu tumeelekeza nguvu kuboresha vyuo vyetu pamoja na kugharamia mafunzo kwa kada mbalimbali katika sekta ya afya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ritta Kabati.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi nilikuwa nataka kuhoji kuhusiana na jambo hilo hilo naona limeshajibwa, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sungura.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Niko kwenye kifungu cha 22009 - *Training Foreign.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kabisa kwamba tuna changamoto kubwa sana kwa *nursing* na *mid-wifery* hususani katika *reproductive health* na *menstrual hygiene management*. Pia hawa watu wakipata *training* watatusaidia, kwa mfano, mtu ana diploma anakwenda *advance diploma* ama anakwenda kwenye *nursing degree*, anakwenda kuwa *specialist* na *Ph.D holders*, hawa wasomi

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

hata wakiandika *thesis* au *research* watasaidia Serikali katika kutengeneza sera mbalimbali. Kwa nini tumeweka sifuri hapa badala ya kuweka kiwango chochote ukizingatia kwamba tuna upungufu wa watu ambao wana-*quality skills* katika kutoa huduma? Nashukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, ufanuzi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu la swali hili halitofautiani sana na hili ambalo nimetoka kulieleza hivi punde kwamba *vote* hii inahusiana na watumishi katika Idara ya Wauguzi kupata mafunzo nje ya nchi. Mafunzo yote katika sekta yetu ya afya hususani katika kutoa huduma na wauguzi waliokuwepo kule wanaotoa huduma kwenye hospitali zetu na vituo vyetu vya afya na kwa ambao wako vyuoni, bajeti zake za mafunzo ziko chini ya Idara ya Mafunzo na huko wanapata fursa ya mafunzo mbalimbali. Vilevile tumekuwa tunapata *scholarship* mbalimbali ambapo nako tumekuwa tunawapeleka wauguzi wetu na watumishi wa kada nyinekuweza kwenda kupata mafunzo kuongeza ujuzi waliokuwa nao.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2005 – *Pharmaceutical Services Unit*Sh.185,530,566/=
Kif. 3001 – *Preventive Services*.....Sh.21,147,604,787/=
Kif.3002 – *Health Quality Assurance Division*..Sh.267,721,247/=
Kif.4002 – *Social Welfare*.....Sh.951,708,000/=
Kif.5001- *Human Resource Development*.Sh.11,502,248,051/=

(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

**Fungu 53 – Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii,
Jinsia na Watoto (Maendeleo ya Jamii)**

Kif.1001-*Administration and HR Management*.....Sh.2,527,016,000/=

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kif.1002 - *Finance and Accounts*.....Sh.468,493,600/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning* Sh.883,246,000/=
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit* Sh.392,166,500/=
Kif. 1005–*Government Communication Unit*.....Sh.3,910,618,000/=
Kif. 1006 – *Procurement Management Uni...* Sh.565,523,000/=
Kif. 1007 – *Information, Communication and Technology*.....Sh.479,582,943/=
Kif. 1008 – *Legal Service Unit* Sh.250,972,500/=
Kif. 2001 – *Training and Folk Development College*Sh.952,392,000/=
Kif. 2002 – *Community Development* Sh.8,424,886,457/=
Kif. 3001 – *Gender Development*..... Sh.1,036,337,000/=
Kif. 3002 – *Children Development* Sh.872,025,000/=
Kif. 4001 – *Non-Governmental Organizations* Sh.697,195,000/=
Kif. 5001 – *Social Welfare Division* Sh.5,766,350,000/=

(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

KITABU CHA NNE

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 52 – Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Afya)

Kif. 1003 – *Policy and Planning*Sh.5,906,642,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2001 – *Curative Services* Sh.101,744,590,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo ukurasa wa 115, kifungu cha 5423 - *Mtwara Regional Referral Hospital*.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Naomba ufanuzi kwa sababu nikiangalia bajeti mwaka 2017/2018 ilikuwa shilingi bilioni mbili sasa hivi kuna shilingi bilioni moja. Naomba kupata ufanuzi ni nini kimepungua au kuna kazi ipi imefanywa ambayo sasa hivi inaonekana imeisha mpaka hili fungu likapunguzwa? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Afya.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyeekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Kuchauka na Wabunge wote wa Kanda ya Kusini kwa ajili ya Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini. Mwaka huu tumeweka shilingi bilioni moja badala ya shilingi bilioni mbili ya mwaka jana kama tulivyosema kwamba hospitali hii itajengwa kwa fedha za *NHIF*. Kwa hiyo, hii tumeweka tu kama kulinda kifungu, lakini *NHIF* watajenga kwa ile *model ya BOT (Built Operate and Transfer)*. Kwa hiyo, ndio tutafanya hivyo kwa kutumia hela ya *NHIF*na hii hospitali itaisha haraka kuliko kusubiri hela hii ya kutoka Hazina.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2005 – *Pharmaceutical Services*
Unit Sh. 240,000,000,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 3001 – *Preventive Services* Sh. 205,589,167,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyeekiti, nakushukuru. Napenda kupata ufanuzi kwenye *sub-vote 3001, item 5406*, udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza ambapo inaonekana fedha za ndani za mwaka huu kuna shilingi bilioni 30 na fedha za nje kuna shilingi bilioni 56. Utakumbuka mkakati wa Serikali kwenye huduma hii ya chanjo, afya na uzazi wa mtoto kwenye homa za manjano,

surua na pepopunda mwaka uliopita mliweka shilingi bilioni 33 fedha za ndani (*local*) na pia kukawa na *forex* shilingi bilioni 104. Pamoja na matatizo haya kuongezeka lakini inaonekana kwamba mkakati wenu wa kupambana na matatizo haya ya surua, homa za manjano, fedha za ndani mkaona hazina umuhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi wa kina kwa nini mkapunguza fedha wakati matatizo haya yanaongezeka? Nashukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Afya.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu Mheshimiwa Masoud anasema kwamba tumeweka fedha kidogo kwa ajili ya chanjo na kwa kweli katika jambo ambalo Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli amekuwa akiliangalia ni chanjo za watoto na tunapata fedha za chanjo kutoka Hazina. Kwa hiyo, haya ndiyo mahitaji halisi ya chanjo kwa mwaka huu wa 2018/2019 ambao tunaenda nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia wakati nahitimisha nilisema tunaondoa utegemezi kutoka kwa wafadhili. Kwa hiyo, hii imetusaidia kwamba tunaweka fedha za ndani lakini pia bei ya chanjo imepungua kwa sababu sasa hivi tunanunua dawa, vifaa na vifaatiba pamoja na chanjo kutoka kwa wazalishaji moja kwa moja badala ya kununua kutoka kwa madalali, kwa hiyo na bei ya chanjo pia unakuta imepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa kwa kuamini kwenye chanjo na ni kweli ndiyo maana sasa hivi hatusikii watoto wakiumwa surua, kifaduro, pepopunda, ndui, ni kwa sababu ya uwekezaji mkubwa ambao Serikali ya CCM inafanya katika chanjo. Kwa hiyo, naomba atuunge mkono na amuunge mkono Mheshimiwa Rais ili tuweze kutokomeza magonjwa ya watoto yanayoweza kuzuilika kwa chanjo. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 3002–*Health Quality Assurance Division..* Sh. 400,000,000/=
Kif. 5001–*Human Resource Development..* Sh. 8,119,600,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 53 – Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Maendeleo ya Jamii)

Kif. 1003 – *Policy and Planning* Sh. 0/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2002 – *Community Development*Sh. 550,000,000/=

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu kidogo cha 6030, ukarabati wa vyuo vya maendeleo ya jamii. Nimemsikiliza Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha, ameongelea umuhimu mkubwa wa Maafisa Maendeleo ya Jamii na akasema kwamba wanaanzisha kama kada mpya ili waweze kuajiriwa. Kamati hii imekwenda kwenye vyuo mbalimbali vya Maendeleo ya Jamii vlikwemo Rungemba na kile cha Uyole lakini nchi nzima vyuo hivi viko katika hali mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba kwa hizi fedha walizotenga kidogo namna hii wanategemea vyuo hivi vitaboreshwaje ili waweze kuchukua wanafunzi wengi ambao wataweza sasa kusaidia jamii katika suala zima la maendeleo? Naomba maelezo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, ufanuzi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa mchango wa Mheshimiwa Susan Lyimo.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kwa kweli kada ya maendeleo ya jamii ni muhimu na nyeti sana katika kuamsha ari ya wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni kweli kabisa katika hii shilingi milioni 500 tumelenga kufanya ukarabati kwenye vyuo vitatu vyta maendeleo ya jamii ambavyo ni Chuo cha Mlale, Chuo cha Uyole ambacho Kamati ya Bunge na Mheshimiwa Susan Lyimo walitembelea, lakini vilevile katika Chuo cha Misungwi. Tunafanya hivi kwa awamu kwa sababu badala ya kuwa tunafanya ukarabati mdogomdogo ambao hauna tija, tumeelekeza katika vyuo vitatu ili tufanye ukarabati mkubwa na kuhakikisha kwamba vyuo hivi vinafanya kazi kama ninyi Kamati mlivyokuwa mmetuelekeza katika ziara yenu.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 3001 – *Gender Development* Sh.413,845,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 3002 – *Children Development* Sh.1,200,000,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Amina Mollel.

MHE. AMINA S. MOLELL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika kifungu hiki kwenye *Child Protection and Participation Programme* naona kwamba hakuna fedha zozote zilizotengwa kwa mwaka huu wa fedha unaokuja wa 2018/2019. Tukiangalia kwa hivi sasa watoto wetu hawako salama na tumekuwa tukiona matukio mbalimbali ya unyanyasaji wa watoto, wengine wakichinjwa, sasa nikiangalia hapa hakuna fedha zozote zilizotengwa. Naomba nipate maelezo kutoka kwa Serikali. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Afya.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Amina Mollel kwa kuwa balozi mzuri katika kulinda haki, ustawi na maendeleo ya watoto. Ni kweli, ukiangalia kwenye *sub-vote* 5415 - *Child Protection and Participation Programme*, hatujatenga fedha, lakini *activities* ambazo zilikuwa zinatikelezwa chini ya *subvote* hii tutazitekeleza kwenye *sub-vote* 5414, *Young Child Survival and Development Program*, kwenye randama yetu ataona tumesema ni pamoja na kuraibu uanzishwaji na utendaji wa mabaraza ya watoto lakini pia kuwezesha programu za kuzuia ukatili dhidi ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumeamua tu kuweka zile kazi kwenye *subvote* nyingine. Kwa hiyo, masuala ya kupambana na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto bado yataendelea kuwa kipaumbele cha Serikali ya Awamu ya Tano.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Na mimi naomba nijielekeze kwenye kifungu kidogo 5441 ambacho kinahusiana na *ku-support to social welfare services* (huduma za ustawi wa jamii).

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan Lyimo, ili Taarifa zetu Rasmi za Bunge zikae vizuri, hiki kifungu kisome upya huku mwanzo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Support in Social Welfare...*

MWENYEKITI: Namba.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni 5441.

MWENYEKITI: Ni 5451.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Ndiyo ni 5451.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tunahitaji sana fedha nyingi kwa ajili ya kutoa huduma za ustawi wa jamii. Kwa kweli ukiangalia kuna matatizo makubwa sana kwenye familia, ndoa zinavunjika na watoto wa mitaani, kwa hiyo, *my expectation* ni kwamba hiki kitengo kilitakiwa kipatiwe fedha nyingi ili Wizara hii kuptitia hicho kitengo ifanye kazi za ustawi wa jamii tusije tukakutana na matatizo kama yaliyotokea hivi karibuni wakati Makonda anafanya kazi za *social welfare*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani kuna haja kubwa ya Wizara ku-make sure wale watu wake wa ustawi wa jamii (*psychologists*), wanapewa fedha za kutosha ili waweze kufanya kazi yao Tanzania iwe salama na watoto wetu wawe salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini wametoa fedha kidogo? (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Afya.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Susan Lyimo kwa swali lake kuhusu Idara yetu ya Ustawi wa Jamii. Ukiangalia majukumu ya Maafisa Ustawi wa Jamii kwa kiasi kikubwa yanatekelezwa katika ngazi ya halmashauri na mikoa. Kwa hiyo, hapa hela ambazo tumeziweka ni kwa ajili tu ya *coordination* katika ngazi ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Sheria ya Mtoto Namba 21 ya mwaka 2009, Maafisa Ustawi wa Jamii wako katika kata, halmashauri na mikoani. Kwa hiyo, hapa tunaweka tu hela ya *coordination* na mafunzo lakini sio kwa ajili ya *day to day activities*.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kif. 5001 – Social Welfare Division Sh. 2,750,000,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. ATHUMANI HUSSEIN – KATIBU MEZANI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae, mtoa hoja, taarifa.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,

WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 104(3)(a) na (b), Bunge lako likiwa limekaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi yake ya kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2018/2019. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makof)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Kwa taratibu zetu sasa nitawahoji. *(Makof)*

(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 yalipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Afya almanusura iungwe mkono asilimia 100, kidogo tu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri lakini pia na Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Niwapongeze pia watendaji wa Wizara hii ambao wameweza kazi hii nzuri kuifikia Bunge. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, pia niwashukuru na kuwapongeza sana Kamati ya Bunge ya Huduma ya Jamii kwa kazi nzuri waliyofanya hata wameweza kutushauri kama Bunge Zima kuhusu hoja zao na Mheshimiwa Waziri amepata fursa ya kuzifafanua hapa. Kwa hiyo, tunawashukuru sana Kamati kwa kazi nzuri. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nichukue pia fursa hii kuwashukuru sana ninyi kwa namna mlivyoshiriki mjadala wa hoja hii siku ya jana na leo tunahitimisha. Nichukue fursa hii kuwapongeza wale ambao wameweza kuchangia lakini hata ambao wamechangia kwa maandishi, mmeefanya kazi nzuri. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, niwatakie kila la kheri Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wenu katika utekelezaji wa yale ambayo mmeliahidhi Bunge kwamba mnaenda kuyafanya na Bunge limeidhinisha makadirio hayo ya mapato na matumizi. Tunaamini kwamba mambo yatakuwa mazuri zaidi huko tuendako kama mliviyotuahidi katika ufanuzi, lakini pia katika hotuba yenu mliyoitoa. Tunawatakia kila la kheri kwenye utekelezaji huo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo kutoka kwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Tizeba, anawatangazia kwamba kesho Mheshimiwa Waziri Mkuu ataweka jiwe la msingi kwenye mradi wa ujenzi wa vihenge (*silos*) vya NFRA eneo la Kizota, saa tatu asubuhi. Mwanzo ilikuwa immealikwa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kamati inayohusika na Wizara hii, lakini hili tangazo mbona kama la Wabunge wote?

WAZIRI WA KILIMO: Ni Wajumbe wa Kamati.

NAIBU SPIKA: Sawa, Wajumbe wa Kamati mnakumbushwa mwaliko mliopewa na Mheshimiwa Waziri kwamba hiyo siku imeshafika, ni kesho. (*Makofii*)

WABUNGE FULANI: Ni wote.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri amerekebisha, amesema siyo Wabunge wote, anaalika Kamati pekee. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wa Kamati inayohusika na Wizara ya Kilimo wanaalikwa kesho kwenye uzinduzi wa vihenge ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa mgeni rasmi. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka tarehe 23 Aprili, 2018, siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.11 Usiku Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatatu,
Tarehe 23 Aprili, 2018 Saa Tatu Asubuhi)*